# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 2 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Karibuni tena kwenye shughuli za kikao chetu cha leo na tutaendelea na ratiba yetu kama inavyooneshwa kwenye orodha ya shughuli za Bunge leo.

Lakini ninaomba niwape taarifa kwamba Waziri Mkuu hayupo katika maeneo ya Mji wetu wa Dodoma na hivyo kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu leo hakitakuwepo.

Kwa hiyo, nitamwomba sasa Katibu atuongoze kwa shughuli zitakazotakiwa kufanyika katika siku ya leo. Katibu tuendelee.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema Waziri Mkuu hayupo na kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu hakipo.

Kwa hiyo, tunaanza moja kwa moja na maswali ya kawaida lakini kwa kutokuwepo Waziri Mkuu nimepokea taarifa hapa kutoka Serikalini Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, anakaimu sasa nafasi hiyo ya Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni kwa niaba ya Waziri Mkuu mpaka pale Waziri Mkuu atakaporejea tena katika ukumbi huu wa Bunge kuendelea na shughuli zetu. *(Makofi)*

Na. 130

### Ujenzi wa Zahanati ya Chala-Nkasi

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Ujenzi wa Zahanati ya Chala umekuwa ukisuasua pamoja na kwamba fedha za kukamilisha ujenzi huo zilishatolewa ila hazikusimamiwa vizuri:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha zahanati hiyo?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa ubadhirifu uliofanywa na wasimamizi wa mradi huo?

(c) Je, Serikali ina maelezo gani juu ya fedha zilizoahidiwa na Mheshimiwa Rais mwaka 2008 za kuendeleza ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa zahanati katika Kijiji cha Chala ni moja ya miradi iliyoibuliwa na wananchi na ulianza mwaka 2009 kwa nguvu za wananchi. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Kijiji kilitengewa jumla ya shilingi milioni 8.7 kupitia mfuko wa pamoja wa ukarabati *Joint Rehabilitation Fund.*

Fedha hizi zilitumika kupaua jengo lote, kuweka fremu za milango na madirisha na kupiga lipu katika baadhi ya vyumba. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali imepeleka shilingi milioni 13.7 kupitia fedha za *CDG*, ambapo fedha hizi ni kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati hiyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hatua zilizochukuliwa dhidi ya ubadhirifu uliofanywa na wasimamizi wa mradi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi aliamwamuru mtuhumiwa kulipa kiasi cha shilingi milioni 2.7 ambazo zilipotea kutokana na usimamizi dhaifu wa ujenzi wa mradi huo wa zahanati.

Fedha hizo zimerejeshwa kwenye akaunti ya *General Fund* na kukatiwa stakabadhi Na. 00004101. Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ameandikiwa barua yenye Kumb. Na. CBC.239/265/05 kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Rukwa kumtaka amchukulie hatua Mtumishi aliyesababisha ubadhirifu huo katika kazi. Halmashauri imepanga kutumia fedha zilizorejeshwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa zahanati hiyo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mwaka 2008 Rais alitoa ahadi ya shilingi milioni 2 ikiwa ni mchango wake katika ukamilishaji wa zahanati hiyo alipotembelea Wilaya ya Nkasi. Fedha hizi zimetengwa katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 na zitatumika kununua samani za ofisi.

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana. Naridhika na majibu mazuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Hivi karibuni tumearifiwa kupitia Bunge lako Tukufu kwamba kutakuwepo ajira ya watumishi wa sekta ya afya wapatao 5000.

Je, Serikali inakubaliana na ushauri kuwa katika mgawo wa watumishi hao maeneo yenye upungufu mkubwa nchini kama vile Mkoa wa Rukwa, Wilaya ya Nkasi na Vijiji vya Chala, Wapembe, Kate vizingatiwe katika mgawo huo?

Katika vijiji vyote nchini, Serikali za Vijiji zimejitahidi sana kujenga mazingira rafiki kwa watumishi wa afya kwa kujenga zahanati na nyumba za waganga. Hata hivyo, mazingira magumu ya vijijini imekuwa changamoto ya watumishi hawa kutulia vijijini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka posho ya mazingira maalum kwa watumishi wote wanaoishi vijijini nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la Watumishi 5000 ambao alizungumza Mama Kombani hapa, moja ya maeneo ambayo tunayapa kipaumbele ni maeneo haya ya pembezoni. Mheshimiwa Mipata anafahamu kabisa kwamba mimi nilitembelea katika Jimbo lake la Uchaguzi, yeye na Mheshimiwa Keissy na haya matatizo anayoyasema hapa ni ya kweli.

Kwa hiyo, sisi tuna hakika kabisa kwamba hawa watumishi wanapelekwa katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo ni maeneo ya pembezoni wakati mwingine hata ndugu zetu wanaotoka Kongo wanakwenda kutibiwa katika Zahanati hizi kwa utaratibu uliowekwa kule.

Kwa hiyo hawa watakuwa ni kipaumbele wala asiwe na wasiwasi. Utaratibu kuanzia sasa ni kwamba tunapeleka moja kwa moja hakuna kupitia TAMISEMI tumeshaelewana na wenzetu wa Wizara ya Afya hawa watumishi waende moja kwa moja ili kuondoa huu urasimu ambao Mheshimiwa Mipata anauzungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala hili la kujenga mazingira, hivi ndivyo tunavyofanya na siyo kwa idara hii ya afya tu, tunafanya hivyo hata kwa watumishi wengine wanaotoka elimu na maeneo mengine, tumezitaka Halmashauri zetu na sasa hivi tunazungumza na wenzetu *National Housing* (*NHC)* wanatusaidia katika jambo hili kwa hiyo hakuna tatizo kabisa katika suala hili la kuona kwamba tutafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la posho analolizungumzia hapo, hizi mara nyingi sana zimekuwa (*consolidated*) zimeingizwa kwenye mishahara, lakini ni jambo ambalo pia tumeliangalia.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Kwa kuwa, nilikwisha uliza swali kama hili Bungeni kuhusu Zahanati ya Mang'ula nimeshuhudia mwenyewe kwa macho wanawake na wanaume wanalala wodi moja.

Je, Serikali ina mpango gani kusaidia kituo hiki cha Zahanati ya Mang'ula kipatiwe Wodi ya Wanawake? Jamani ni aibu na ni hatari?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mazingira yanategemeana kwa maana yake kulala chumba kimoja mwanamke na mwanaume ina mazingira, lakini nadhani anachokisema hapa kama nimemwelewa Dada yangu Susan anazungumza ukiingia kwenye zahanati hata kama ni Magereza akina mama wanakaa upande wao na akina baba wanakaa upande wao nadhani ndicho anachosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema ni kwamba kwenye Zahanati hii ya Mang'ula, nadhani nitakachofanya nikishajibu swali hili hapa ninatoka nje. Kwanza nataka nimpate Mkurugenzi anieleze vizuri hii habari kwamba ikoje na udhibiti wake ukoje na utaratibu wake unasimamiwaje kwa sababu inaweza ikatokea na kuzalisha matatizo mengine makubwa sana hapa. Kwa hiyo, naomba nilichukue halafu nitalishughulikia. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ningependa kumwuliza Waziri kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za wananchi zimekuwepo kubwa sana katika ujenzi wa vituo vya Afya na Zahanati. Lakini kumekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi kama alivyojibu mwanzo. Watumishi hawa wanakuwa hawana vivutio kwenda kufanyakazi katika maeneo ya vijijini. Kwanini sasa Serikali isitangaze rasmi leo kupitia Bunge hili kwamba watawalipa kuanzia mwaka huu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mwaka huu tumeanza utaratibu mpya wa kubadilisha jinsi watumishi wa afya wanavyopelekwa katika vituo vya kutolea huduma. Utaratibu wa mwaka huu ni kwamba Mtumishi mwenyewe anapoomba ile ajira ataamua yeye mwenyewe anataka kwenda wapi.

Tatizo la siku za nyuma ni kwamba watumishi walikuwa wanapelekwa maeneo ambayo wao wenyewe wasingependa kwenda. Kwa hiyo, mwaka huu tumewataka wakati wanaomba, kwanza waeleze ni maeneo gani wangependa wachague sehemu tatu. Kwa hivyo ya kwanza watapewa kipaumbele ikishindikana atapewa ya pili au hatimaye atapewa ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mategemeo yetu kwamba kwa utaratibu huo sasa tutaweza kupunguza lile tatizo la mtu ambaye angependa kuwa Rukwa lakini akajikuta amepelekwa labda Liwale na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu suala la motisha kwa wafanyakazi, hili tumelizungumza na wenzetu wa utumishi. Tumekubaliana kwamba iko kila sababu ya kuweka posho ya mazingira magumu lakini kama alivyosema Naibu Waziri ni kwamba siyo kwa watumishi wa Afya peke yake ni kwa watumishi wote wa sekta zote ambao wapo katika mazingira magumu.

Suala hili linafanyiwa kazi, na ni matumaini yetu kwamba tutakuja na maelezo ni jinsi gani ya kuboresha stahili zinazotolewa kwa wafanyakazi ambao wapo katika mazingira magumu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 131

**Utatuzi wa Migomo na Migogoro Vyuoni**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

(a) Je, ni hatua gani imefikiwa katika kuwarejesha wanafunzi waliofukuzwa na waliosimamishwa katika Vyuo Vikuu mbalimbali vya umma ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Afya ya Sayansi Shirikishi *(MUHAS)* na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kutokana na migogoro ya mwaka 2011 na 2012?

(b) Je, ripoti ya Tume ya Rais ya mwaka 2011 ya jinsi ya kuboresha utaratibu wa sasa wa ugharamiaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu imechangia kwa kiwango gani kushughulikia vyanzo vya migogoro ili kupata ufumbuzi endelevu?

(c) Je, ni marekebisho gani yana kusudiwa kufanywa kuhusu waraka wa tarehe 12/6/2009 *(GN.178)* uliofanya mabadiliko kwenye uendeshaji wa Serikali za Wanafunzi katika Vyuo Vikuu na kudaiwa kusababisha migogoro baina ya wanafunzi na Utawala katika baadhi ya Vyuo Vikuu vya Umma nchini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za kinidhamu zilizochukuliwa dhidi ya wahusika wa vurugu katika Vyuo Vikuu ni kama ifuatavyo. Katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanafunzi 99 walibainika kuhusika na vurugu na hivyo kusimamishwa masomo.

Baada ya uchunguzi kukamilika wanafunzi 78 walirudishwa Chuoni na wengine 21 bado wamesimamishwa masomo kutokana na uzito wa ushiriki wao kwenye mgomo na vurugu hizo. Katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) wanafunzi 115 walibainika kushiriki vurugu hizo ambapo kati ya hao wanafunzi 81 walipewa onyo kali, wanafunzi 24 walisimamishwa kwa muda wa mwaka mmoja na walirudishwa chuoni tayari mwezi Desemba, 2012.

Wanafunzi 8 walisimamishwa kwa miaka miwili na watarudishwa Chuoni mwezi Desemba, 2013. Wanafunzi wawili wamefukuzwa chuo kulingana na uzito wa makosa yao.

Katika Chuo Kikuu cha Dodoma wanafunzi 570 walihusika katika vurugu hizo na hivyo kusimamishwa masomo, kati ya hao wanafunzi 563 walirudishwa chuoni na wanafunzi 7 walifukuzwa chuo moja kwa moja.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya Tume ya Rais ya mwaka 2011, Bodi ya Mikopo imeanzisha mfumo wa *Online Loan Application System* (*OLAS*). Tume ya Vyuo Vikuu imeanzisha mfumo wa *Central Admission System* yaani (*CAS*). Mifumo hii imewezesha kuwa na uwazi na uhakika zaidi wa upatikanaji wa takwimu sahihi za wanafunzi waliodahiliwa na wanafunzi waliopata mikopo.

Aidha, kila chuo kimeajiri Afisa Mikopo ambaye ni kiungo kati ya Chuo, wanafunzi na Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Mafanikio haya yote yamepunguza kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa migogoro katika Taasisi za Elimu ya Juu.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yaliyofanywa katika waraka wa Serikali *GN.178* wa tarehe 12 Juni, 2009 yalilenga vifungu sita (6) ambavyo baadhi yake ni utambulisho wa Viongozi wa wanafunzi kama vile Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Spika. Hapo awali majina hayo hayakuruhusiwa kutumika kwenye *GN. 178.* Rekebisho jingine kubwa ni sifa za kitaalam ambazo mgombea uongozi alitakiwa kuwa nazo.

Katika *GN. 178* Mgombea uongozi alitakiwa awe na *G.P.A* ya kuanzia 3.5 lakini baada ya marekebisho hayo Mgombea anatakiwa awe na *G.P.A* kuanzia 2.8.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri ambayo kwa sehemu siyo sahihi kwa sababu idadi ya wanafunzi aliotaja kwa Vyuo mbalimbali ni pungufu ya idadi ambayo mimi nafahamu mpaka sasa wamesimamishwa.

Kuna Vyuo ambavyo hakuvitaja kabisa pamoja na kuwa ni vya Umma kama Mwalimu Nyerere *Memorial*. Takwimu nilizonazo mpaka sasa kuna wanafunzi 80 kwa Vyuo vya Umma hawajarudishwa na wanafunzi zaidi ya 100 kwa Chuo cha *St. John* peke yake ambacho ni cha binafsi.

Kwa kuwa, ripoti ya Tume ya Rais ilibaini kwamba mfumo mbovu wa Bodi ya Mikopo na mfumo mbovu wa uendeshaji wa Vyuo ni moja ya vyanzo vya migogoro hii yote iliyosababisha wanafunzi hao kusimamishwa.

Je, Wizara iko tayari sasa kufuatilia kwenye Vyuo hivi ili kwanza kupata taarifa sahihi na kuweza kuchukua hatua zinazostahili kuhakikisha wanafunzi hawa wanarejeshwa?

Katika sehemu (b) ya swali, imeelezwa kwamba ripoti ya Tume ya Rais imesaidia kupunguza migogoro kwenye Taasisi za Elimu ya Juu, lakini Wabunge wenzangu watakubaliana na mimi kwamba bado kuna migogoro mikubwa ya mikopo kwenye taasisi za elimu ya Juu.

Je, Wizara haioni sasa imefika wakati ile ripoti ya mwaka 2011 iliyotokana na fedha za wananchi isiendelee kufanywa kuwa siri iletwe hapa Bungeni ili Bunge lifanye kazi yake ya kuisimamia Serikali kuwezesha ufumbuzi wa kudumu wa migogoro kwenye elimu ya juu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyika hapa anajaribu kuiambia Serikali kwamba idadi tuliyotoa hapa au takwimu tulizotoa hapa siyo sahihi. Lakini mimi nataka nimhakikishie kwamba sisi ndiyo Serikali na ndiyo tuna takwimu sahihi za hawa wanafunzi tuliokuwa tumewafukuza. Kwenye swali lako la msingi wewe ndiye uliyetaja hivyo Vyuo kwamba Vyuo vya *UDOM, MUHAS* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sasa kama una taarifa zingine tungeomba labda utuletee wewe ili tuweze kufanya masahihisho katika Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la (b) kwamba bado Mheshimiwa Mnyika anaamini kwamba bado kuna migogoro Vyuo Vikuu na akitaka hii taarifa ya Tume ya Rais ije hapa Bungeni. Ninachotaka kusema ni kwamba Tume hii iliundwa na Rais kwa hiyo ni Tume ya Rais. Aliiunda yeye ili imsaidie yeye kuweza kuangalia tatizo la migogoro kwenye Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama utaruhusu Serikali, ilete Taarifa hiyo Bungeni sisi hatuna matatizo, kama Bunge litaridhia. Lakini ilikuwa ni Tume ya Rais, kwa ajili ya kusaidia kuepusha migogoro hii. Ndio maana ikaundwa hiyo mifumo ya *OLAS,* kama nilivyokuwa nimesema, na ile mifumo mingine ya Tume ya Vyuo Vikuu. Kwa hiyo, migogoro Vyuo Vikuu Waheshimiwa Wabunge na nyie mnaweza mkaona kwamba, angalao imepungua kiasi fulani hata migomo kwenye Vyuo Vikuu imepungua sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nitoe wito, bado kuna Wanasiasa ambao bado wanaendelea kuchochea migomo kwenye Vyuo Vikuu vya hawa wanafunzi. Nataka niseme kwamba, kwa kweli, tutakuwa wakali kidogo sasa hivi, tutakapokuwa tunawaona hata baadhi ya Wabunge, wanakwenda Vyuo Vikuu kuwachochea hawa vijana kwa ajili ya kuleta migomo. Hatuwezi kukubaliana tena na hii hali. Mtaendelea kuwachochea, lakini sisi tunaendelea kushika zile Sheria zilizoko kwenye *Chaters* za Vyuo Vikuu kwamba, anayefanya vurugu kutokana na Sheria, tutaendelea kuwafukuza. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza ifahamike tu kwamba, kufanya siasa vyuoni si makosa, hata Museveni Uganda huwa anakwenda kwenye kampeni za Urais kule; mimi mwenyewe nimekuja hapa nikiwa natokea chuoni na nikawashinda watu wazito tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali la msingi. Tumekuwa tunataka Sheria ibadilishwe, mambo ya *Meals-Testing* yabadilishwe, hamtuletei hapa na Rais peke yake hawezi kuachiwa hili jambo. Kwa nini, msilete haya mambo tukayajadili hapa, ili migomo isitokee tena?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mkosamali, ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

**MWENYEKITI:** Ni swali moja, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali moja; kama nilivyosema, Mheshimiwa Mkosamali anasema kufanya siasa Vyuo Vikuu sio kosa. Yeye alikuwa anafanya siasa Chuo Kikuu na ndio maana yuko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kufanya siasa na kuleta vurugu Vyuo Vikuu ni kosa.

Wale wanaokwenda kufanya siasa Vyuo Vikuu kwa kuchochea vijana wafanye vurugu kwa kuleta migomo ya ajabu ajabu tutaendelea kuwachukulia hatua za Kisheria. Kama mtaendelea bado kuwachochea vijana, wale vijana tutaendelea kuwafukuza kama ambavyo tumeanza kuwafukuza sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu labda kuliweka hilo. Kwa sababu, kwa kweli imeonekana baadhi ya wenzetu wanakwenda kufanya siasa Vyuo Vikuu ambazo sio siasa za kiustaarabu. *(Makofi)*

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali, inatambua uwepo wa Serikali za Wanafunzi Vyuoni na inatambua mchango muhimu wa Viongozi wa Serikali za Wanafunzi Vyuoni na inatambua kwamba, ili kutatua mgogoro huwezi ukawaita wanafunzi wote, badala yake unawaita Viongozi wao wawakilishe mawazo ya wenzao.

Inakuwaje Serikali, baada tu ya kukaa na Viongozi wale wa Wanafunzi, huku ikitambua walikuwa wanawawakilisha wanafunzi wenzao, kutokea kuwafukuza walewale Viongozi, ilhali tunatengeneza Viongozi ambao wanajali maslahi ya wale wanaowaongoza?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mwigulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchagua Viongozi hawa kuwawakilisha Viongozi wenzao kwenye upande wa Vyuo Vikuu, kwenye *Chater* za Vyuo Vikuu vyote imeainishwa hivyo na ni kitu cha Kisheria kabisa. Lakini tunachosema ni kwamba, pale inapoonekana Viongozi wale ndio wanakuwa ni chachu ya vurugu na chachu ya ushawishi kwa wenzao, ndipo inapoleta matatizo kama haya, lakini kama wangekuwa wanakwenda kwa agenda, kwa hoja vizuri, kumwita yule Mwadili wa Wanafunzi na wanaongea naye vizuri na mambo yangekuwa yanaendelea kuwa-*solved* vizuri, kama ambavyo sasa hivi Vyuo Vikuu karibu mwaka mmoja kumetulia, wanafunzi wanafuata Sheria na mambo yanakwenda vizuri. Pale Viongozi wanapokuwa wamekiuka ndipo unakuta matatizo kidogo yanatokea na wale viongozi na wenyewe tena wanakuwa kwenye sakata hilo.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa, migogoro mingi inatokana na suala zima la mikopo. Na kwa kuwa, wanafunzi wa vyuo vikuu hawana chanzo kingine zaidi cha mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua pale ambapo inatokea Serikali au Bodi ya Mikopo ndio imezembea kupeleka mikopo hiyo kwa wakati. Ni Sheria gani au ni hatua gani zimewahi kuchukuliwa dhidi ya Serikali? Kwa sababu, tunaona kwamba, wanafunzi tu ndio wanaokuwa wanachukuliwa hatua?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma ni kweli matatizo haya yalikuwa yanatokea kwa sababu Bodi ya Mikopo, kuchelewesha fedha kwa wanafunzi.

Lakini kama nilivyosema kwamba, baada ya Mheshimiwa Rais, kuunda Tume ya kuchunguza mifumo mizima ya Bodi ya Mikopo, ilionekana kwamba, *sometimes* sio Bodi ya Mikopo, lakini matatizo mengine yanatokea hata kwenye Hazina kuchelewesha fedha, lakini hata kwenye mabenki kule fedha zinakopitia.

Lakini vilevile, hata Tume ya Vyuo Vikuu kuchelewesha majina kwa wale wanafunzi wanaokuwa wanadaihiliwa, labda mwaka wa kwanza au matokeo ya wanafunzi wenyewe kucheleweshwa kutoka kwenye Vyuo Vikuu, kwenda Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, matatizo yote haya yalitokana na mifumo ya wanafunzi, Bodi ya Mikopo wenyewe, Wahadhiri wenyewe, *TCU,* na kadhalika. Lakini baada ya Tume ile, mambo mengi.

Kwa kweli, sasa hivi yamerekebishwa. Pale ambapo ilikuwa inaonekana Bodi ya Mikopo Maafisa fulani wamechelewesha pale au labda wametumia fedha vibaya, tumekuwa tukichukua Sheria na ndio maana mtaona hata mwaka jana baadhi ya Maafisa wa Bodi ya Mikopo, tuliwapeleka Mahakamani na kesi zinaendelea. *(Makofi)*

Na. 132

**Mabadiliko ya Matumizi ya Lango Namba Mbili Katika Bandari ya Dar es Salaam**

**MHE. JAKU HASHIM AYUB** aliuliza:-

Kwa miaka mingi, Wananchi wa Zanzibar, wamekuwa wakitumia Lango Namba 2 katika Bandari ya Dar-es-Salaam kwa shughuli za upakuzi wa mizigo yao, lakini shughuli hizo sasa zimehamishiwa kwenye Lango Namba 3, ambalo limewaongezea wasafiri gharama na usumbufu kutokana na umbali liliko Lango Namba Tatu(3):-

(a) Je, Serikali, inaweza kueleza sababu za kuhamisha Lango hilo na ilizingatia vipi usumbufu watakaopata wananchi wengi wanyonge, ambao walikuwa wakitumia eneo hilo kabla ya kuhamishia Lango Namba Tatu?

(b) Mahitaji mengi ya watu wa Tanzania Zanzibar, yametegema bidhaa kutoka soko la Tanzania Bara; kwa kubadili matumizi ya lango Namba 3 na kusababisha usumbufu mkubwa.

Je, usumbufu huo unasaidia vipi kuimarisha Muungano?

(c) Magari yaliyokuwa yakipakia mizigo katika eneo lililozuiwa yanatakiwa pia kutoka kwenye eneo hilo.
Je, eneo hilo sasa linatumika kwa shughuli gani?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayub, Mbunge wa Baraza La Wawakilishi, lenye sehemu *(a), (b)* na *(c)* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Lango Namba 2 la Bandari ya Dar-es-Salaam, limefungwa kwa sababu za kiusalama. Hali hii inatokana na matakwa ya Sheria na Kanuni za Kimataifa za Ulinzi wa Meli na Bandari *(International Ship and Port Facility Security Code (ISPS Code),* zilizoazimiwa kutumika Duniani kote kuanzia mwaka 2004. Sheria hiyo, huzihitaji Bandari kufanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara na Taasisi za Kimataifa za Ulinzi wa Meli na Bandari.

Kutokana na ukaguzi uliofanywa na Taasisi hizo katika Bandari ya Dar-es-Salaam hivi karibuni, iliagizwa kufungwa kwa Lango Namba 2 la Bandari, ili litumike kwa shughuli za kutoa magari Bandarini, baada ya kulipiwa tozo, dharura na uokoaji kwa ruhusa maalum na kwa kuzingatia taratibu za kiusalama pindi inapolazimu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari itahakikisha kuwa Wateja wa Bandari ya Dar-es-Salaam, hawapati adha na usumbufu wowote katika kutumia Lango Namba 3 la Bandari ya Dar-es-Salaam badala ya Lango Namba 2 wakati wanapopatiwa huduma mbalimbali za bandari. Hatua hii imesaidia kuimarisha hali ya usalama ambayo inawafaidia wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hata wageni wanaotumia Bandari yetu ya Dar-es-Salaam.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lililopo katika Lango Namba 2 la Bandari ya Dar-es-Salaam kwa sasa linatumiwa kwa shughuli za kuhudumia magari yanayoshushwa kutoka melini, baada ya kufanyika malipo husika. Aidha, Lango hilo hutumika wakati wa kuhamisha magari kutoka Bandarini, kwenda Bandari kavu.

**MHE. JAKU HASHIM AYUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri mchapakazi, ambaye anafuatilia mafaili, hasubiri mpaka yafike kwenye meza. Naomba kumwuliza maswali madogo mawili tu ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kufunga Geti Namba 2 na kuacha eneo la jirani likitoa shughuli hizohizo haoni ni sawa na kufunga mlango wa mbele kuachia mlango wa nyuma kuwa wazi? Kuna eneo hilo hilo pametolewa hivi sasa, huu usalama uko wapi anaotueleza Mheshimiwa Naibu Waziri? Kuna eneo hilohilo geti Namba 1 kuna mfanyabiashara karuhusiwa, haoni kuwa ni ubaguzi huo?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ..............

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku, umeshauliza Maswali karibu matatu hapo.

**MHE. JAKU HASHIM AYUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni *(a)* tu hilo.

**MWENYEKITI:** Hapana, unatakiwa kuuliza maswali mawili. Katika hilo swali la kwanza, umeshauliza matatu ndani yake.

**MHE. JAKU HASHIM AYUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni moja tu hilo, nionee huruma, ndio kwanza nafika. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku, naomba uketi.

**MHE. JAKU HASHIM AYUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijapata kuuliza swali siku zote mimi. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku, nafikiri tumekuelewa. Sababu yako ya kutokuuliza maswali mara nyingi huku Bungeni, haitoi nafasi uulize maswali 6 unapoingia ndani ya Bunge. Kwa hiyo, kwa maswali hayo sasa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri, aweze kujibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, ya Mheshimiwa Jaku, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Lango Namba 1, bado linaendelea kutumiwa. Na hii ni kutokana na *recommendation* iliyofanywa na wale wakaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Geti Namba 2 kusababisha usumbufu kama alivyousema; uko usumbufu mdogo kwa sababu, kwamba, umbali Geti Namba 3 lilipo ni mkubwa kidogo.

Lakini tuko katika harakati pia kubwa ya kuboresha *movement* ya watu na magari ndani ya Bandari. Mambo yote haya baada ya marekebisho haya, yataangaliwa tena upya na tutakapowaita wakaguzi tena, tutaona kama usumbufu umepungua au umeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa baada ya kupata malalamiko kadhaa kwa watu kubeba mizigo umbali mrefu, nimekwishatoa maelekezo kwa Mamlaka ya Bandari kwamba, magari yanayoingiza mizigo, *Malindi WARF,* pale Bandarini, sasa yaruhusiwe kutumia hilo Geti Namba 2. Magari peke yake na sio watu wanaoingia kwa mguu kuingia na kutoka; magari yanaruhusiwa sasa kuingiza mizigo na kutoa mizigo kupitia Geti hilo hilo Namba 2. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Dar-es-Salaam, abiria wanaokwenda Zanzibar kwa kutumia maboti, huwa wanakaguliwa kwa *screening* ya kisasa, kama ilivyo hii ya hapa Bungeni kwetu. Kwa kuwa, usafiri wa kwenda Zanzibar, sio tu wa kutumia maboti ya abiria, kuna usafiri wa majahazi ambayo yanasafirisha bidhaa na nafaka kutoka Bara kwenda Zanzibar au kutoka Zanzibar kuja Bara.

Je, Serikali, ina mikakati gani ya kufanya *screening* ya mizigo ambayo huchukuliwa na majahazi? Kwa vile, inasemekana huko nyuma, iliwahi kukamatwa *sub-machine gun* katika gunia la mchele?

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Sanya, umehamisha kabisa swali. Sasa sijui hayo majahazi nayo yanaingilia mlango upi?

Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumeanzisha utaratibu wa kuwakagua abiria wote wanaotumia Bandari ya Dar-es-Salaam popote wanapoenda, sio lazima iwe Zanzibar tu. Katika utaratibu huu kulikuwa na manung'uniko ya watu kupanga mstari mrefu sana wakati wa ukaguzi, lakini suala hilo tumelichukulia hatua na sasa limepungua baada ya ku-*introduce metal detectors* badala ya kutumia ile *X-Ray Machine* peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la majahazi na mizigo yao kukaguliwa; majahazi yakipita kwenye maeneo rasmi yatafanyiwa upekuzi na ukaguzi kama kawaida. Lakini majahazi mengi, nafikiri Mheshimiwa Sanya anaelewa kwamba, yanaanzia popote na Mamlaka yetu ya Bandari haiwezi kutawanyika kwenye *stretch* nzima ya Bahari kuanzia Mtwara mpaka Tanga. *(Makofi)*

**MHE. ENG. HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, katika hilo Lango Namba 2 au Lango Namba 3, abiria wanaposafiri wanakuwa na mizigo yao na kuna kituo cha *TRA* ambacho wanatakiwa walipie *VAT* na mbele yake kuna kituo cha Bandari ambacho wanatakiwa walipie *Warfage.*

Kwa kuwa, kuna Sheria ya miaka mingi haijabadilishwa mpaka leo kwamba, abiria anaruhusiwa kuchukua mzigo wa mpaka kilo 20, sawa sawa na kama ilivyo kwenye ndege na kwenye meli hivyo hivyo.

Mheshimiwa mwenyekiti, ni kwa nini sasa, abiria huyu aliyenunua mzigo nje akalipia *VAT,* analipishwa tena pale *TRA* Bandarini? Na ni kwa nini alipie mzigo ule katika hizi meli, aidha za binafsi au za Serikali, wakati zile kilo 20 anaruhusiwa apande bila ya kulipia? Kwa nini Serikali, imenyamaza kimya abiria hawa kunyanyaswa mara mbili, kulipia *VAT* mara mbili na kulipia mzigo bandarini, kitu ambacho Sheria inawaruhusu wapakie mpaka kilo 20 bure?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi hapa lilikuwa kufungwa kwa Geti Namba 2 kwa watumiaji wanaosafiri kwenda Zanzibar. Hili swali analolileta hapa Mheshimiwa Mnyaa, kwanza sio la Wizara ya Uchukuzi ni la Wizara ya Fedha, ambao ndio watozaji wa ushuru ule *VAT* na mambo mengine anayoyataja hapo Bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, nimwombe tu Mheshimiwa alilete kama Swali Rasmi, ili liweze kutafutiwa majibu ambayo yatamtosheleza.

Na. 133

**Kocha wa Taifa Stars Kufundisha Kilimanjaro Stars**

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO K.n.y. MHE. AMINA ABDULLA AMOUR** aliuliza:-

(a) Kwa nini Kocha wa kigeni anayeajiriwa na *TFF* au Serikali, kufundisha Timu ya Taifa *(Taifa Stars)* hufundisha pia Timu ya Tanzania Bara *(Kilimanjaro Stars)?*

(b) Je, ni wachezaji wangapi na *club* wanazochezea kutoka Zanzibar, ambao wanacheza kwenye Timu ya Taifa *(Taifa Stars)?*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa makubaliano Makocha wa Kigeni wanaoajiriwa na *TFF* hufundisha *Taifa Stars* pamoja na Timu ya Taifa ya Tanzania Bara *(Kilimanjaro Stars)* kwa sababu, ni waajiriwa wa *TFF* ambayo, husimamia *Kilimanjaro Stars.* Na pia ni kutokana na utamaduni ambao umekuwepo kwa miaka mingi wa Kocha anayekuwepo kufundisha Timu zote mbili.

Hata hivyo, maoni ya Mheshimiwa Mbunge na ushauri wa Wadau mbalimbali wa kutenganisha majukumu ya Kocha wa *Taifa Stars* na *Kilimanjaro Stars,* yamepokelewa tutayafanyia kazi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kikosi cha Timu ya *Taifa Stars,* hakina wachezaji wanaochezea *club* za Zanzibar, bali kina wachezaji wapatao 5 kutoka Zanzibar ambao wanachezea *club* za Azam, Yanga na Simba.

Hata hivyo, uteuzi wa wachezaji wa *Taifa Stars* hufanywa na Kocha Mkuu kwa kuzingatia uwezo na kiwango cha uchezaji anachoonesha mchezaji wakati akichezea *club* au timu katika michezo mbali mbali. *(Makofi)*

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Baada ya majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba, hakuna wachezaji wanaotoka moja kwa moja kutoka katika vilabu vya Zanzibar. Na kwa kuwa, kauli hii haijengi sura ya utaifa.

Je, ni lini *TFF* itachukua wachezaji kutoka katika vilabu vya Zanzibar kwa kuwaingiza katika Timu ya *Taifa Stars?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, usisome swali lako, ni kinyume na Kanuni.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, ni lini *TFF* itawachukua wachezaji kutoka katika vilabu vya Zanzibar, kuwaingiza katika Timu ya *Taifa Stars?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, Timu ya *Taifa Stars,* imewahi kufanya au kujenga Kambi katika Mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Je, ni mara ngapi Timu ya *Taifa Stars,* imewahi kuweka Kambi Visiwani Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu nimesema kwamba wapo wachezaji wanaotoka Zanzibar lakini kwa sasa wanachezea vilabu Tanzania Bara maana yake hawa ni Wazanzibari. Wachezaji hao ni Mwadini Ally anayechezea Azam lakini pia anachezea Zanzibar Heroes, Aggrey Moris, Mcha Khamis, Nadir Kanavaro na Said Nassoro Choro. Hawa wote ni wa Zanzibari na wanachezea pia timu ya Zanzibar. Kwa hiyo hapa uwakilishi wa kitaifa upo kwa wachezaji hawa watano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nimepokea wazo la kuwa na kambi ya timu ya Taifa huko Zanzibar sijawa na takwimu za uhakika kwamba tumewahi kufanya kambi mara ngapi lakini hilo tumelipokea na tutaelekeza *TFF* katika kuimarisha Muungano waweke kambi pia huko Zanzibar. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Cecilia, Mheshimiwa Ritta na Mheshimiwa Mshama.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante toka Serikali hii ya awamu ya nne imeanza kuajiri makocha wa kigeni.

Je, ni makocha wangapi wazawa wamepata mafunzo ya uhakika ili kuachana na mtindo huu wa kuajiri makocha ya kigeni?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Serikali haijaajiri kocha, Serikali inasaidia kumlipa kocha na katika jibu langu la msingi ni kwamba makubaliano hata mkataba haisini Serikali na kocha inasaini TFF na kocha na Serikali inaendelea kusaidia kulipa makocha.

Lakini nataka niseme tu kwamba ni kwamba makocha hawa wa kigeni wanaajiriwa kutokana na sifa, lakini pia na uwezo. Lakini niseme tu kwamba hata kocha aliyeko sasa mmeweza kuona matokeo yake ni kwamba tunafanya vizuri tumewafunga Morroco na timu nyingine mbalimbali. Kwa hiyo, wako makocha ambao kila kocha wa Taifa anasaidiwa na kocha mzawa katika njia hiyo iwe katika timu ya *Taifa Star* au timu ya vijana makocha wetu wanafaidika na mafunzo wanayopata kwa makocha hawa wa kigeni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kuniona kwa kuwa timu ya wanawake ya Taifa *Twiga Stars* imekuwa ikituwakilisha vizuri sana katika mashindano ya Kimataifa na kutuletea sifa nchi yetu.

Je, ni lini Serikali nayo itaifikiria kuipatia kocha wa kigeni ili iweze kufanya vizuri zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati. Ni kweli nakubaliana naye kwamba timu ya *Twiga Star* imeendelea kufanya vizuri chini ya kocha Ndugu Mkwasa na kwa sasa Serikali imeanza jitihada ya kuleta makocha sasa.

Tuna kocha wa timu ya Taifa mpira wa miguu, tuna kocha wa mpira wa kikapu na hilo tumelipokea kuona kwamba kuna umuhimu wa kuleta kocha, basi tutalifanyia kazi ndani ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza nilikuwa nina swali kwamba lini Taifa au *TFF* itaanzisha *Taifa Stars search* kwa ajili ya kuzunguka Tanzania nzima kuhakikisha kwamba inapata vipaji vya vijana wote ukizingatia Misenyi tulishatoa Ndugu Minziro na sasa hivi kuna kijana ambaye anachezea Uganda lakini hajapata nafasi kuchezea *Taifa Stars?*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Assumpter Mshama, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, kocha huchagua wachezaji kutokana na uwezo wao wanapokuwepo uwanjani lakini vile vile ni kwamba anazunguka Mikoani katika kuangalia vipaji mbalimbali na hivi karibuni amechagua timu ya vijana ya *Taifa Star* ambao watakuwa wakifanya vizuri watakwenda kwenye timu kubwa.

Suala hilo tumelipokea na tutaongeza kasi ya kuona kwamba anapita Mikoani huko na katika ligi mbalimbali kuweza kuibua vipaji vikiwemo huko Misenyi alikosema Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata linaenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na swali hilo linaulizwa na Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 134

**Makao ya Wazee Nchini**

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA** aliuliza:-

Serikali kwa nyakati tofauti ilianzisha makao ya wazee wasiojiweza katika Mikoa mbalimbali nchini katika Mkoa wa Kagera Wilaya ya Bukoba vijijini (Kiilima) kuna makao yaliyokuwa yakiendeshwa na Kanisa Katoliki kabla ya Serikali kuyachukua:-

(a) Je, Serikali inatenga na kupeleka fedha kiasi gani kwa mwezi kwa ajili ya matumizi ya wazee na yatima wanaoishi kwenye makao hayo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati makao ya wazee kiilima?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Elizabeth Batenga sasa nimwombe Naibu Waziri atupatie majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali hili la Mheshimiwa Elizabeth Batenga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Batenga, naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasimamia jumla ya makazi 17 ya wazee nchini yakiwemo makazi ya Kiilima yaliyopo Mkoani Kagera, Wilaya ya Bukoba Vijijini. Makazi haya yana jumla ya wakazi wapatao 30 kati ya wakazi hao wazee wenye ulemavu ni 17 na watoto wao 13 ambao wanasoma.

Aidha yapo makazi mengine 24 yanayosimamiwa na wakala wa hiari. Lengo kuu la Serikali ni kuwa na makazi ni kuhakikisha makundi haya maalum hususan wazee wasiojiweza wanapata huduma za msingi ambazo ni chakula, malazi, matibabu na ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya Kiilima yana jumla ya watumishi saba wanaohudumia makazi hayo, watumishi hao ni wauguzi 4, wapishi 2 na dobi mmoja. Ili kukidhi mahitaji muhimu kwa ajili ya maisha ya wazee Serikali kupitia Wizara ya Afya na ustawi wa Jamii, imeweka utaratibu wa kuhudumia wazee wasiojiweza katika makazi kote nchini.

Utaratibu unahusisha kutenga Bajeti hii ya matumizi ya kawaida kila mwaka kwa ajili ya huduma za uboreshaji wa makazi hayo. Katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi milioni 67, 500,000/= zimetengwa kufanikisha utoaji huduma katika makazi ya Kiilima, kiasi hicho ni sawa na shilingi milioni 5,625,000/= kwa mwezi.

Aidha kulingana na mgao wa fedha zilizopatikana kutoka Hazina kuanzia Julai, 2012 hadi Machi, 2013 Serikali imeshapeleka jumla ya shilingi milioni 24, 211, 486/= kati ya fedha hizo ni shilingi milioni 22, 800,000/= ni gharama za chakula na shilingi milioni 1,350,000/= ni zile za uendeshaji wa Ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilipelekwa kwa miezi ifuatayo:-

Julai mwaka 2012 shilingi milioni 2,484,000/=; Septemba 2012 milioni 8,454,000; Februari 2013 shilingi milioni 1,600,000/=; na Machi, 2013 shilingi milioni 1,281,000/= na Aprili 2013 10, 389,840/=. Fedha zinaendelea kupelekwa kadiri zitakavyokuwa zinapatikana kulingana na uwezo wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha mwaka 2013/2014 Serikali imepanga kufanya ukarabati wa makazi ya wazee wasiojiweza nchini yakiwemo makazi ya Kiilima. Jumla ya shilingi milioni 150 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati huo kupitia Bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Maeneo yanayopewa kipaumbele katika ukarabati huo ni mabweni mawili na kufuatiwa na vyumba vitano vya watumishi pamoja na jiko.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Elizabeth Batenga swali la nyongeza.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa majibu yake mazuri na mchanganua mzuri alioutoa. Kwa kuwa hali tunavyoiona sisi tunaoishi kule ndani ya Makao hayo hayaonyeshi kwamba kuna kiasi hiki cha fedha kinachopelekwa kule.

Je, Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wako tayari kujaribu kufuatilia kuhakikisha kwamba hii fedha inafika na inawanufaisha walengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa kuwa hawa watoto yatima wanaoishi katika Makao haya kwa kweli yaonekana si mahali pao kwa sababu imebidi wagawanyike katika nyumba za wafanyakazi. Kwa hiyo, malezi yao hatuwezi tukayafuatilia zaidi lakini pia kwa kuwa wanasoma na kipindi kinapofika cha kuanza shule inakuwa ni kuhangaika kuwatafutia mahitaji ya shule.

Je, Wizara ipo tayari pia kuwatambua hawa watoto hivyo na kuwatengea mahitaji yao ya kishule?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iko tayari kwenda kuona thamani ya pesa inayotumika katika vituo hivi na tumekuwa tukifuatilia mimi mwenyewe nimeshatembelea kambi kama tatu za wazee na nitaendelea kufuatilia kuweza kuona hali inavyoendelea kutekelezwa kulingana na fedha ambazo zinapelekwa.

Lakini naamini kwamba hali ilivyo kule eneo moja hali hairidhishi kutokana na majengo ambayo kwa hakika kwenye Bajeti yetu ya Miradi ya Maendeleo kama nilivyotoa kwenye jibu la msingi kwamba tumetenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya ukarabati wa majengo na kufanya hali iwe nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watoto wanaosoma kama walivyo watoto wengine katika makambi yote ya wazee bado Serikali imekuwa ikitenga fedha na kuweza kuangalia utaratibu mzuri wa kuweza kuwapatia vifaa muhimu kwa ajili ya masomo na kuwawezesha kupata elimu kama wanavyotakiwa kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante nilikuona Mheshimiwa Selasini .

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana katika hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu mwaka huu tunaomaliza wa fedha 2012/2013 aliahidi kwamba wazee wote nchini watalipwa kiinua mgongo cha shilingi 20,000/=.

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi hii.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya nataka nijibu swali la Mheshimiwa Selasini Mbunge wa Rombo swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo nia ya msingi ya kulipa *pension* kwa wazee kama ilivyoahidi mwaka jana na ndiyo maana katika majibu ya nyongeza yalitolewa hapa na Wizara inayohusika kwamba sasa Serikali imejikita katika kuandaa na utaratibu wa kisera wa namna ya kutekeleza uamuzi huo.

Kwa hiyo, uamuzi wa Serikali imeshafanya na kabla ya kuanza kulipa hizo shilingi 20,000/= au zaidi maandalizi lazima yafanywe kwa hiyo Serikali sasa inafanya maandalizi ya kisera na kanuni na sheria na utaratibu ambao utawezesha uamuzi huo kutekelezwa.

Hili jambo lipo nataka kumhakikishia Mheshimiwa Selasini kwamba hili jambo lipo na Serikali imeamua kulitekeleza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuwa vituo vya wazee pamoja na watoto yatima ni vingi na Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kikiwemo kituo cha Sukamahela, Manyoni; na kwa kuwa hela Serikali inazopeleka ni ndogo.

Je, itakuwa tayari kuongeza kiwango cha pesa kuwatunza hawa wazee kikiwemo kituo cha Sukamahela ili hela hizo ziweze kukidhi angalau mahitaji muhimu kwa hawa wazee?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa Afya mwenyewe.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lazima tukiri kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya huduma kwa vituo hivi vya wazee na watoto yatima hazikidhi mahitaji.

Katika mwaka huu wa fedha tumejaribu kuongeza fedha hizo kwa maana ya hii Bajeti inayokuja na wakati tunajadiliana suala hili na wenzetu wa Kamati ya Huduma za Jamii walitutaka tupunguze maeneo mbalimbali ili kuongeza fungu kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii, tumefanya hivyo na ninamwomba Mheshimiwa avute subira wakati ninawasilisha Bajeti yangu tutamwonyesha ni kiasi gani na maeneo gani tumekata, ili kuongeza kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kuboresha huduma katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kutokana na mkataba wa kimataifa wa Banjul wa mwaka 1986, ambapo nchi yetu iliridhia mwaka 1984 Ibara ya 18(4) inahusiana na haki za binadamu hususani wazee wasiojiweza kuwalinda kulingana na mahitaji yao ya kimwili na kimaadili. Moja haki ya kimwili ya mwanadamu ni kuoa ama kuolewa.

Je, hadi sasa Serikali imeweza kufanya ndoa ngapi za wazee ambao wapo katika makambi hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya waziri wa afya na ustawi wa jamii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa utaratibu wa Serikali hauingilii haki ya maamuzi ya mtu kuamua kuoa au kutooa. Lakini umeweka mazingira wezeshi ya kumwezesha mtu kutambua maamuzi yake hayo ya kuoa au kuolewa.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu sisi kama watoto au kama tuna wazazi wetu ambao bado wanataka kuingia katika maamuzi ya kuoa au kuolewa basi tunaweza tukachukua hatua ya jamii kuchukua hatua kuwasaidia. *(Makofi)*

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwanza niipongeze Serikali kwa mchakato huo wa kuandaa sera na sheria kuwawezesha wazee waweze kupata hiyo *pension.* Lakini kwa vile mwaka jana ndiyo tu Serikali ilikubali kwamba itatoa *pension* kwa wazee ni matarajio ya Watanzania wote kwamba sera hiyo na sheria ingekuwa imeshaletwa hapa Bungeni.

Je, Serikali inatuambia ni lini sera hiyo na sheria itafikishwa hapa Bungeni ili iweze kupitishwa, hawa wazee waanze kupata *pension*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo maelezo ya kujibu kwa uhakika katika Bajeti ya Wizara ya kazi kwa hiyo ningeomba Waheshimiwa Wabunge wasubiri hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, si vizuri sana kwa sababu tutakuwa tunakiuka Kanuni ya kuwahisha shughuli.

Mheshimiwa Waziri wa Kazi atakuja kufafanua ni lini Sheria na Sera zitaletwa hapa Bungeni kwa kujadiliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Swali fupi sana.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Mkoa wa Manyara uanzishwe sasa ni mwaka wa 11 kutoka Mkoa wa Manyara lakini tuna kituo cha wazee pale Magugu katika Wilaya ya Babati hicho kituo bado kina lelewa na Mkoa wa Arusha na Bajeti yake inatengewa chini ya Mkoa wa Arusha ni lini sasa hicho kituo kitarudishwa Mkoa wa Manyara ili kilelewe kwa karibu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ni lini kituo kitarudishwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paulina Gekul, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa taarifa nilizonazo zinaonesha fedha ambazo zimepangwa na kupelekwa katika kipindi cha mwaka huu, Mkoa wa Manyara Kituo cha Magugu zimeshapelekwa shilingi milioni nane kwa ajili ya kutoa huduma katika kambi hiyo. Kwa hiyo, naamini kama ikiwa zinapitia Mkoa wa Arusha, tutafuatilia ili kuweza kuona fedha hizo zinaenda Mkoa wa Manyara kama ilivyo na naamini itakuwa inafanyika hivyo.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri, oneni sasa utaratibu wa kukihamisha kilelewe na Mkoa wa Manyara ambako ndiko kiliko. Mheshimiwa Eugene Mwaiposa, swali la mwisho katika Wizara hii.

**MHE. EUGINE E. MWAIPOSA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashikuru kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa Serikali imeanzisha haya makao ya kuwahudumia wazee; na kwa kuwa katika Mkoa wa Dar es Salaam, wako Wazee wengi ambao wanahitaji sana huduma hizo na wengine wanalala barabarani:-

Je, Serikali inawaelekeza wapi Wazee wa Mkoa wa Dar es Salaam katika suala zima la kupata huduma hiyo ya hifadhi?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri, hakuna Kituo Mkoa wa Dar es Salaam? Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Sera na Uratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugene Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Kisera, jukumu la kuwalea wazee wasiojiweza, siyo wazee tu, watu wasiojiweza, kwanza, ni la Halmashauri; pili, jamii, lakini haiwezi kuwa hawa wazee wote wasiojiweza wanakwenda kwenye makambi. Kwanza, jamii na kwenye familia, mtambuka lazima familia itambue wazee waliko na iweze kuwahudumia. Wale waliopo kwenye vijiji lazima vijiji vyenyewe na Serikali zao zijue namna ya kuwahudumia, lakini Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam anakotoka Mheshimiwa Mbunge, lazima zitambue na zina jukumu la kwanza la kutunza familia na wale wote wasiojiweza.

Kwanza, lazima itambue lakini ihakikishe kwamba, inaweka mkakati wa kuhudumia wale ambao hawajiwezi, siyo wazee tu, hata watoto na watu wengine wasiojiweza. Kwa hiyo, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, jukumu la msingi la kuhudumia jamii isiyojiweza katika maeneo yetu ni la Halmashauri na Halmashauri lazima zitenge bajeti, isipokuwa wale ambao wameshindikana, ambao hawana utambuzi ndiyo Serikali inachukua jukumu ya kuwaweka kwenye Makao ya Wazee.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Nafikiri Dar es Salaam tuna Nyumba ya Wazee Kigamboni kama sikosei. Tunayo Nyumba ya Wazee kwa hiyo, Mheshimiwa Eugene Mwaiposa, unaweza ukawasiliana na Mheshimiwa Waziri. Mkoa wa Dar es Salaam tunayo Nyumba ya Wazee, naamini ipo kule Kigamboni na kule Zanzibar. Kwa kweli hawa wazee ni watu wa kuwatazama, ndiyo *senior citizens* hawa, hivyo tunatakiwa kuwaangalia vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na mnaona leo tumekuwa na maswali ya nyongeza mengi, kwa sababu pia tumeutumia muda wa maswali kwa Wzairi Mkuu, kuwaruhusu Waheshimiwa Wabunge waulize maswali ya kutosha tu kwenye Wizara ambazo zilikuwa na maswali leo. Hata hivyo, Wizara nyingine kama mlivyoona, bado zinakuja na bajeti zao katika ratiba za Bunge; kwa hiyo, hayo maswali mengine tutakuwa na nafasi nzuri kuchangia kwenye Wizara hizo ambazo zinakuja.

Miongoni mwa Wizara hizo ni pamoja na Wizara ya Afya, Wizara ya Kazi na Wizara nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo ya kazi kama ifuatavyo:-

Ndugu Anselm Mrema, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge kwamba, leo tarehe 2 Mei, kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi mara baada ya kipindi cha maswali saa 4.00 asubuhi hii, na kitafanyika katika Ukumbi wa Mheshimiwa Spika, uliopo Ghorofa ya Kwanza, Jengo la Utawala. Nawaomba sana Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge, Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Kamati na kama Wenyeviti wa Kamati hawapo, basi tunaomba Makamu Wenyeviti wawepo. Pia tutaomba sana kuwe na uwakilishi wa kutosha katika kikao hicho saa 4.00 hii asubuhi.

Mheshimiwa Edward Lowassa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Mambo ya Nje, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 227 Jengo la Utawala. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, wahudhurie kikao hicho saa 7.00 mchana leo katika Ukumbi Namba 227.

Mheshimiwa Anna Magareth Abdallah, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naye ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, leo Alhamisi terehe 2 Mei, 2013 saa 7.00 mchana, kutakuwa pia na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 231 Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala. Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, msikose katika kikao chenu cha Kamati. Tangazo hili limeletwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Nimepokea tangazo lingine kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa *Club* ya kulenga shabaha, Mheshimiwa Said Nkumba; anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge

wote kuwa, kutakuwa na zoezi la kulenga shabaha. Zeozi hilo litafanyika tarehe 19 Mei, 2013, katika Kambi ya Makutupora JKT hapa Dodoma. Waheshimiwa Wabunge wote wanaopenda kwenda kuhudhuria zoezi hilo la kulenga shabaha, wanaombwa kujiorodhesha ili taratibu za maandalizi ziweze kufanyika mapema. Sasa sijui taratibu hizo ni pamoja na mazoezi kabla ya kwenda huko. Mnaombwa mjiandikishe na kwa maelezo zaidi mnaweza kumwona Mheshimiwa Said Nkumba, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa *Club* hiyo ya kulenga shabaha.

Katibu, hatua inayofuata.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI**: Nimewaona Waheshimiwa Wabunge, nitawapa nafasi.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2013/2014
### Wizara ya Maliasili na Utalii

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, hoja zilizopo ni hoja za Serikali na majadiliano yanaendelea. Kwenye majadiliano ninayo orodha hapa, lakini ninaomba nisome yote kusudi kama kuna Wabunge wako nje ya Ukumbi wa Bunge, waweze kurejea ndani na shughuli ya kuchangia iweze kuendelea. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Maria Hewa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Prof. Peter Msolla ajiandae.

Sasa nikitaja orodha hiyo, mpaka hapo nadhani itanisaidia sana, kama kuna watu wako nje ya Ukumbi wa

Bunge waweze kuingia ili shughuli hii ianze. Nikiangalia naona Mheshimiwa Maria Hewa hayupo ndani ya Ukumbi wa Bunge, Mheshimiwa Luckson Mwanjale hayupo, namwona Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, kwa hiyo, naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa.

Waheshimiwa Wabunge, mnaoomba miongozo nimewaona, nitautazama muda wangu baadaye, tuanze kwanza kazi ya kuchangia halafu nitarudi tena kwenu. Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Hoja iliyoko mbele yetu ni hoja nyeti na kama tulivyosema kwenye Hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani, inailetea Taifa letu mapato makubwa sana; kwa hiyo, ni lazima ichukuliwe kwa uzito wa kipekee. Pamoja na mambo mengine ambayo tumeyazungumza kwenye Hotuba yetu, Wizara hii imekuwa na changamoto nyingi; kwa mfano, katika Pori Tengefu la Selous, tulikuwa na ndege sita, zote ziko *grounded* hazifanyi kazi. Tulikuwa na vyombo vya mawasiliano ambavyo ni *radio call,* zote hazifanyi kazi. Kwa hiyo, wale wote wanaolinda tembo wetu wanatumia simu za mikononi, kitu ambacho ni kigumu wanashindwa kutunza hawa tembo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapozungumzia hili kubwa ambalo kimsingi Mawaziri hawa wawili bila kushirikiana na Umma wote wa Tanzania, ni kitu ambacho hakiwezekani, kwa sababu vifaa vya mawasiliano havipo. Jambo kubwa ambalo linanisikitisha kama Wabunge ambao tunaishauri Serikali ni pale ambapo rasilimali hizi za Taifa zinatoweka. Takwimu nilizonazo mimi kwa siku ni karibu tembo 63 wanauwawa, ambao kwa mwaka ni karibu tembo 23,000 wanakufa. Hivi ninavyozungumza ni kama wiki tatu tu zilizopita, Iringa pale karibu na nyumbani wameuwawa tembo watano.

Jana tumesikia habari nyingine japokuwa wanasema tembo sijui wametoka Kenya, lakini wameuwawa. Kwa Kweli, tembo wanauwawa kwa kiwango cha juu sana.

Ukienda kwenye misitu, kwa siku tunakata misitu yetu karibu hekari 850 inateketea, tunatumia mkaa karibu tani milioni moja kwa mwaka. Kwa hiyo, rasilimali tulizonazo zinateketea kwa kiwango kikubwa sana. Kikubwa kinachonishangaza ni pale ambapo sisi kama Kambi ya Upinzani tunapojaribu kutoa mawazo yetu, kwa pamoja tujaribu kushirikiana, halafu watu wengine wanabeza.

Ningependa nijaribu kuzungumza jinsi ambavyo Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, ambaye yeye ni Waziri wa Mambo ya Ndani na nilitegemea yeye kama Waziri mwenye dhamana, angekuwa anasema Msigwa umetaja hawa watu hebu tuletee ushahidi, badala yake yeye ana-*defend*; ni kama vile kuna watu ambao huwa hawawezi kuwa wahalifu katika nchi yetu ya Tanzania. Nchi yetu ya Tanzania kila mtu anaweza akafanya uhalifu, hakuna mtu ambaye hawezi kufanya uhalifu.

Badala tushirikiane katika Wizara hii, Mawaziri wote wanakiri kwamba kwenye Wizara hii wahusika wakubwa ambao wapo, wanahusika hata kusaidia kuingiza silaha haramu. Wapo Polisi, Usalama wa Taifa, tumediriki kuona hata Jeshi linashiriki, ni mtandao mkubwa, ni *organised crime*. Kwa hiyo, ni suala ambalo linatakiwa litatuliwe kwa kina tukishirikiana kwa pamoja badala ya kuzomeana.

Sasa anapotokea Waziri anabeza, anasema niwaombee CHADEMA ni wahuni, nilishasema mimi kama Mchungaji, sikatai kuombea na tunaombea kweli, lakini hata majangili tunayaombea bila kujali ni nani.

Sishangai kwa malezo ya Mheshimiwa Nchimbi na nasikitika kwamba hayupo, ndiyo maana aliitwa *Doctor* kabla hata hajapata hiyo *Doctorate.* Kwa hiyo, hao ndiyo Viongozi tulionao katika Taifa hili, ambao wanaweza kubeza mambo ya msingi. Hapa tunatakiwa tushirikiane kwa pamoja tuweze kulitatua tatizo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mgogoro wa Loliondo na niwaombe Wamasai wanisikilize vizuri na

Wabunge wa humu ndani. Mgogoro wa Loliondo ulizalishwa na Ikulu ya Serikali hii. Kama kuna jambo ambalo linamtia doa Rais Mstaafu, Mheshimiwa Mwinyi, ambaye amefanya mambo mazuri ni mgogoro wa Loliondo, umekuwa kero kwa Taifa hili. Huu mgogoro ulizalishwa na Ikulu, ilivunja utaratibu wa namna hata ya kupata lile eneo. Ukaja ukalelewa na Awamu ya Tatu na umeendelea kulelewa na Awamu hii ya Nne. *(Makofi)*

Kinachonishangaza, hebu tujiulize Watanzania, badala la kurusha madongo na kutuita wahuni sisi watu wa CHADEMA tunapotoa mapendekezo yetu, hebu tujiulize; Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye aliyemteua Waziri wa Maliasili na Mawaziri wote; Rais huyo huyo wa Jamhuri ya Muungano ambaye ndiye Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ndiyo aliyemteua Abdul-rahman Kinana na Mwigulu Nchemba. Kuna tatizo Loliondo ambalo lipo; leo huyo aliyeteuliwa na Rais na amesema na naamini Mheshimiwa Waziri Balozi Khamisi Kagasheki siyo kichaa, ana akili nzuri na ameutangazia umma kwamba ametumwa na Rais na huyu Mwenyekiti wa CCM tena anamtuma Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Kinana waende kwenye mgogoro huo huo! Sasa hapo kuna mawaili mnayotaka kutuaminisha; aidha, sitaki kutumia maneno aliyoyasema Mnyika, labda kuna tatizo kwenye eneo la Rais, hilo sitaki kulisema maana mtasema tunamdhalilisha. Hilo la kwanza, pili, labda kuna udhaifu katika Ofisi ya Rais, kwa sababu hawezi kutuma watu wawili katika jambo moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, ninakuomba sana. Kwanza, naomba uketi. Nimekuelewa sana mchango wako una busara na una mantinki yote, nakuomba sana uwe mwangalifu katika kutumia jina la Rais kwa sababu Rais ni Taasisi. Kwa hiyo, nakuomba uwe mwangalifu katika kutumia jina la Rais. Naomba uendelee na mchango wako lakini naomba uchukue tahadhali kwa mujibu wa kanuni. Endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu wa dakika mbili uutunze.

**MWENYEKITI**: Hakuna neno zitazingatiwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali ambalo Watanzania wanatakiwa wajue kwamba, aidha kuna tatizo kwenye Taasisi ya Rais au wanataka kutuaminisha kwamba, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki anasema uongo au wale waliotumwa kupitia chama ndiyo waongo. Sasa mnatuacha Watanzania kwenye *dilemma* kwamba, Serikali hii ya CCM katika kutatua jambo hilo hilo, Kiongozi wa Nchi anatuma watu tofauti na maagizo tofauti.

Nataka niwaambie watu wa Loliondo na Wabunge mlioenda kusuluhisha hili tatizo ambalo hasa ni watu wa kule mmewatelekeza ndugu zenu, hamtaki kuwaambia. Mgogoro huu hauwezi kutatuliwa na Serikali ya CCM, ni ujanja wa kutaka kuchukua kura katika uchaguzi unaokuja, kwa sababu wao wenyewe wameuzalisha, wameulea na mtoto amekua sasa ameota meno na anaweza kula makande, wanazunguka kwa mlango wa nyuma kwamba wanaweza kuutatua.

**MBUNGE FULANI**: Hawa ndiyo wanasema watu wa Loliondo ni Wamasai wa Kenya.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Serikali hii muda wote imekuwa ikisema kwamba, Wamasai ni watu wa kutoka Kenya wanapodai haki zao! Imesemwa mara zote kwamba ni Wakenya!

**MBUNGE FULANI**: Mwangunga!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mwangunga aliwahi kusema, amezungumza wakati nyumba zinachomwa kwamba hawa ni Wakenya!

**MBUNGE FULANI**: Shamsa Mwangunga!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kwa hiyo, ninawasihi Wamasai, msikubali kuonewa katika eneo hilo, hilo ni eneo

lenu na sisi kama CHADEMA tunaoitwa wahuni, tumesimama imara kuwatetea, ni lazima mgogoro huu ufike mwisho. Naiomba Serikali isitishe mara moja, siyo kwamba suala litashughulikiwa, na huu mgogoro wa Loliondo ufike mwisho ili Wamasai wapate haki zao. Nasema Wabunge wamewatelekeza Wamasai kwa sababu gani?

Wamasai wametawanyika nchi nzima, kazi yao ni kulinda nyumba za watu, wamekuwa walinzi. Ardhi yao ambayo aliwapa Mungu imeporwa, wananyanyaswa, wanaletwa wageni. Hawa ni ndugu zetu ambao wanatakiwa walindwe kwa haki zote. Nawaambia Wamasai kwamba, *they are just using you*. Wanawataka tu wakati wa kura kama vile Wabunge wa Lindi na Mtwara walivyowatelekeza watu wao. Nawaomba Wamasai nao walikumbuke hili suala ili waweze kulinda ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza masuala yenye maslahi ya nchi ni vyema tukazingatia kwamba, tumepanda kwenye meli moja na ni vizuri tukaiacha Tanzania ikiwa bora kuliko tulivyoikuta; badala ya kuingiza ushabiki ambao kimsingi hautusaidii na hautuletei tija kwenye Taifa letu.

Mwaka jana nimezungumza hapa, nilisema na nirudie, maana wanasema labda urudie mara saba ndiyo wanaweza kueleweka. Nilisema Enigmatic Einstein alisema; *“Problems can not be solved by the same level of thinking that created them.”* Huu Mgogoro wa Loliondo mmeu-*create* wenyewe, ila ile *level* ya fikra iliyou-*create* huu mgogoro haiwezi kuutatua. Hamuwezi kwa sababu ni miaka zaidi ya 20 mme-*create* huu mgogoro halafu mnaingia upande wa nyuma, mnatuma watu wawili wawili. Mnamtuma Waziri halafu mnataka kumsulubu wakati alitumwa na Rais huyo huyo, ametumwa na Mwenyekiti huyo huyo, mnataka kuwahadaa Wamasai! *(Kicheko)*

Kiwango cha akili kilichosababisha ule mgogoro wa Loliondo hakiwezi kuutatua, inahitajika akili ya juu zaidi kwa sababu mgogoro huu umekuwa ni tatizo na mnawatesa

Wamasai na watu wa maeneo mbalimbali ambao kimsingi wanaonewa.

Kwa bahati mbaya sana niseme ndani ya Bunge hili, juzi baada ya kusema hotuba hii, nimepata vitisho; zaidi ya simu tatu zinakuja kwenye *private number*. Zinanitishia kwa sababu nasema haya maneno, kwa hiyo, naliambia Bunge na Taifa lisikie kwamba, tunaposema haya mambo wengine tunajihatarisha maisha, lakini Mawaziri wote wawili wanakili kwamba mgogoro na tatizo la tembo ni kubwa.

Kama Idara nyeti, Usalama wa Taifa, wamo watu wanahusika na ni Serikali yenu wenyewe, Polisi wanahusika; tunapowataja Viongozi wa Chama chenu kwa nini mnang'aka; kwa nini tusikae chini tukawachunguza wote kwa pamoja? Nilitegemea mngesema Msigwa umesema uongo lete ushahidi, lakini badala yeke mnapiga kelele na mnajaribu kuupotosha umma. Tukubaliane kwamba, katika suala hili na najua wengi yanawaumiza, hata Mheshimiwa Lukuvi nakuona unajisikia vibaya, lakini lazima niseme. *(Makofi)*

Hatupo hapa kutetea waovu, kila mtu ana *potential* ya kufanya wizi na kufanya ujangili. Kwa hiyo, kitendo cha ku-*cheat* na kutaka kumsulubisha mtu ni mgogoro wa Chama cha Mapinduzi na Serikali yake imeshindwa. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaendekeza ujangili katika nchi hii, kwa sababu ni mtandao mkubwa ambao unahusisha watu wengi ndani; ni kama sweta limefungwa unajizungusha humo ndani ndiyo maana mnalindana.

Watanzania wajue kwamba, tatizo hili Chama cha Mapinduzi hakiwezi kutatua kwa sababu Serikali yake inajuhusisha, kwa sababu wataalam waliotakiwa kulinda hawa tembo wamekuwa ndiyo sehemu ya tatizo hilo na Wizara inakiri, badala ya kusaidiana kwa pamoja tushirikiane imekuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia suala la misitu ambalo takwimu zinaonesha misitu yetu inateketea.

Kwa siku kama Taifa tunapoteza hekta 345.5, miti inakatwa kila mahali, lakini Wizara au Serikali haina mikakati ya makusudi ambayo inaendana na uhalisia wa miti hii tunayoikata.

Miti inakatwa inayopandwa haionekani, magogo yanakatwa yanayopandwa utaratibu mzima haupo. Badala ya kujadiliana kama Taifa, mipango mizima ya upandaji wa miti tunategemea wafadhili kutoka nje. Mazingira yetu hatuna mikakati ya makusudi ambayo inaweza ikasababisha tupande miti, tuweke mazingira mazuri ambayo ni kwa faida ya vizazi vijavyo.

Niliwahi kuwa na mwalimu wangu alisema, ukienda mahali popote ukipakuta, kama huwezi kupaboresha ni bora upaache kama ulivyopakuta. *(Makofi)*

Kizazi hiki tumekuwepo sisi, ni wajibu wetu na ni muhimu tukaiacha Tanzania bora kuliko tulivyoikuta badala ya kuiharibu. Tuna wosia wa Baba yetu wa Taifa, ambaye yeye alipoona hatuna uwezo, alisema tusichimbe madini kwa sababu hakutaka kuharibu Taifa hili. Ni masikitiko yangu, mitandao yote ya ukataji wa miti, uchomaji wa mikaa, ujangili, inahusisha Viongozi Waandamizi wa Serikali hii na Serikali hii imekaa kimya.

Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hoja, pamoja na maswali niliyouliza kwenye hotuba, naomba aje na majibu ya kutosheleza ni namna gani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, muda umepita.

Waheshimiwa Wabunge, nimesema miongozo yote nitaipokea baadaye, nisingependa kutumia muda wa kuchangia ndani ya Bunge kwa ajili ya miongozo tunapoteza wakati. Naomba nimwite mchangiaji anayefuata naye ni Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu ndani ya Bunge, kila mmoja ajiandae kwa muda wake aseme anachokiamini. Nisingependa mambo ya taarifa, nini, tunapoteza wakati na tunapoteza mwelekeo wa mjadala Bungeni.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nimpe taarifa, Mchungaji ambaye sijui ni Mchungaji wa kuku au mbuzi kwamba, sijawahi kutamka kwamba eneo hilo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu, naomba uketi. Unayo nafasi ya kutumia maneno yote ya kujenga hoja, lakini ninaomba sana tujiepushe na maneno ambayo yana kashfa ndani ya Bunge. Tumia maneno yote, lakini ninaomba sana tujiepushe na maneno yenye kashfa na ninaisema hii kwa kila Mbunge atakayechangia hapa ndani, nisingependa sana kutumia maneno ambayo yana kashfa.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi kwamba, kwa bahati mbaya sikuwahi kufahamu kama mbuzi au kuku ni neno la tusi. Ningependa tu nimtaarifu yeye kwamba, sijawahi kutamka kwa kinywa changu kuwa eneo hilo la Ngorongoro au kutamka Wamasai ni Wakenya, kwa hiyo, asahihishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa pia nimtaarifu yeye, Wabunge wa Lindi na Mtwara hawajawahi kuwaacha Wananchi wao, tunawawakilisha ipasavyo, kama ambavyo inatakikana. *(Makofi)*

Mara nyingi sana nimekuwa nikimsikia kwamba, akili ile ile iliyoleta tatizo haiwezi kutatua tatizo, siamini kama yeye anayo nafasi ya kuweza kulitatua hili tatizo, maana

angeweza kutushauri na kuweza kufikia mwafaka wa matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko hapa kuwawakilisha Wananchi wetu, lakini tuko hapa kwa ajili ya ustawi wa nchi yetu pia. Katika Hotuba ya Bajeti, ambayo Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha hapa, ameainisha mambo mengi sana. Moja kati ya mambo ambayo ameyazungumzia kwa uchache, amezungumzia maeneo ya vivutio vya utalii na ametoa tu kwamba, tutatumia utangazaji na kuishirikisha jamii katika kutunza maeneo ya vivutio vya utalii. Hili kidogo linanipa wasiwasi, kwa maana kwamba, yapo maeneo mengi sana ambayo hayajatamkwa na wala hayajawahi kuainishwa katika matangazo ya vivutio vyetu vya utalii.

Maeno kama ya Kilwa Kisiwani, sijawahi kuona sehemu yoyote ambayo inatangazwa, sijaona eneo ya *ruins* zile ambazo ziko kule Tanga, Bagamoyo, maeneo ya michoro ambayo umeyatamka pia, kuna maeneo ya kule Kondoa Irangi, kuna Isimira, Murongo, lakini bado hatujakua. Kwa sababu utalii wa sasa hivi, siyo watu wote ambao wanapenda kuangalia wanyama au kwenda kwenye mbuga za wanyama, kuna watalii wengine ambao huwa wanapenda kwenda katika *site scene*.

Kwa hiyo, ningependa Mheshimwa Waziri wakati anajumuisha, anieleze jitihada gani ambazo zinatumika, kuweza kuweka katika maeneo haya, yawe ni vivutio vya utalii. Nikirudi katika suala la utangazaji wa utalii, nimeona jitihada kubwa ambayo inafanyika kwa Serikali katika kutangaza vivutio vya utalii, kitu ambacho kinanishangaza na ninajua kabisa Mheshimwa Waziri na Naibu wake wanalifahamu; ni kwa nini tunaendelea kutumia *CNN* kutangaza utalii?

Wamarekani hawaangalii *CNN, CNN ni international. Most* wa Marekani wanaangalia *ABC, News Four, Fox;* kwa nini hatutumii vile vituo vya ndani vya utangazaji kwa nchi kama Marekani, ndivyo ambavyo watu wanatumia muda mrefu kupata taarifa zao? Kwa nini tunakwenda kutangaza

katika maeneo ambayo tunaamini kabisa hayataleta tija kwenye kutangaza utalii wetu?

Teknolojia ya utangazaji sasa hivi imebadilika, tunao Watanzania wengi sana ambao wako nchi za nje na wako tayari kushirikiana na nchi yao kuweza kutangaza maeneo haya. Tunaweza tukatengeneza *clip* tukaziweka kwenye *YouTube* au tukaweka katika *Websites* mbalimbali ambazo zinatembelewa na watu wengi zaidi na tukaongeza kuutangaza utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuutangaza utalii peke yake haisaidii, inabidi pia tuwe na miundombinu ya kuweza kuwapokea watalii wanapokuja hapa nchini. Tunalo tatizo kubwa sana ambalo kwa kipindi cha miaka yote tumekuwa tukilizungumza hapa; kwa nini hatujaweza ku-*rank* hoteli zetu katika ngazi ya nyota, hatuna idadi ya hoteli ambazo zunajulikana, hatuna *directory* ambayo inaonesha hoteli gani ziko mahala gani na zinafanya huduma zake ziko kwa kiwango gani? Hili ni jambo ambalo inabidi tuliangalie na tulifanyie kazi kwa haraka sana kuweza ku-*rank* hoteli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo ni kubwa sana kwa watalii kuja Tanzania ni *Visa*. Utakuta katika Kanda ya Ulaya nzima pale tunazo Balozi tatu, mtu ambaye yuko Spain, anatakiwa atembee zaidi ya saa nane au saa kumi kwenda kufuata Ubalozi wa Paris. Kwa nini tusianzishe mfumo wa *Electronic Visa* kwa zile nchi ambazo tunaamini kabisa hazina matatizo ambayo yanaweza yakaja; *I mean* watu wake kuja kuyaleta hapa kwetu? Kwa hiyo, hili nashauri kwamba, Wizara yako, pamoja na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, ikae kuangalia namna ambayo tunaweza tukaweka utaratibu wa kutoa *visa* za *electronic*. Kwa sababu *visa* peke yake ni tatizo na kikwazo kwa wageni kuja hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie katika suala la utangazaji wa vivutio vya utalii, tumeunda Bodi ya Utalii, ambayo kila mwaka inapewa kiasi kidogo sana cha kujiendesha, kwa nini sasa Taasisi zote ambazo zinafanya utangazaji wa Utalii; kwa mfano,

Ngorongoro na *TANAPA*, wangekuwa wanatoa kasma ya pesa kuwapa Bodi ya Utalii, halafu wao wakawa wanafanya kazi ya kutangaza vivutio vyote kwa pamoja, badala ya kugawanya fedha au kugawanya rasilimali zilizokuwepo kuzipeleka kila mahali kwenda kujitangaza kwa nafasi yake? Kwa hiyo, ningeomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni *Marine Parks. Marine Parks,* sasa hivi zinasimamiwa chini ya Idara ya Uvuvi. Jamani, hili jambo tunalizungumzia kila siku hapa, kwa nini hizi *Marine Parks* zisirudishwe Wizara ya Utalii na zikawa zinatangazwa, kwa sababu Watalii ambao wanakuja, ukiangalia katika nchi za jirani, yaani Msumbiji na Kenya; idadi ya Watalii ambao wanakwenda kufanya *diving* na kwenda kwenye hizo *Marine Parks* ni kubwa sana. Sasa hili ni jambo ambalo ni lazima mkae na kuliangalia kwa makini kwamba kila siku tutakuwa tunazungumza hapa, lakini utekelezaji bado haujafikia hatua ya kueleweka.

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, akae na Waziri wa Uvuvi, hili suala la *Marine Parks* zirudishwe katika Wizara ya Maliasili na Utalii na ni jambo la kimkakati katika kukuza utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni kuhusiana na suala la wanyama waharibifu au wanyama wa porini na maisha ya Wananchi wanaozunguka katika hayo maeneo. Suala la ulipaji wa fidia kwa wale ambao wanaathirika na wanyamapori, limekuwa ni tatizo sana. Ningependa kuishauri Serikali, badala ya kuweka mfumo huu wa kusumbuana kila siku, kwa nini wale ambao wanaishi jirani na zile Mbuga wasikatiwe Bima, ambapo wakiharibiwa mazao yao au wakiathirika, basi walipwe moja kwa moja badala ya kufuata mfumo huu wa uhakiki na nini ambao ni kero na usumbufu mkubwa sana kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie; Wananchi wa maeneo ya Pwani ambao

wanafanya shughuli za uvunaji wa chumvi, kila mwaka wanalazimishwa kulipa fedha kwa ajili ya kutunza mikoko. Mikoko ile ilishaondoka, ni maeneo ya majangwa, ambayo tayari mikoko ilishakuwa haioti. Naomba iangaliwe vizuri hii Sheria, ili Wananchi wa maeneo ya Kilwa na Pwani nzima ambao tunafanya shughuli hizo za uvunaji wa chumvi, tuweze kuwa na pumziko, maana kila siku tumekuwa tunalazimishwa kulipa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka niliseme ni Idara ya Uvuvi. Kipindi ambacho Idara hii ilikuwa chini ya Wizara ya Maliasili ilikuwa inafanya kazi vizuri sana, lakini leo hii imepelekwa kwenye Wizara ya Uvuvi, usimamizi wake umekuwa ni wa shida.

Jambo moja tu ambalo nilitaka nimwulize Mheshimiwa Waziri ni kwamba, miaka sita sasa hivi tangu umepigwa marufuku uvuvi wa kamba ili waweze kuzaliana. Kamba tangu anazaliwa mpaka anakuja kuzeeka na kufa, ni umri wa miezi tisa. Miaka sita sasa hivi mmezuia uvuvi wa kamba katika maeneo ya *Delta* na maeneo mengine ili kuweka kitu gani, kwa sababu miaka imeshapita na hawa kamba hawawezi kuzaliana tena kwa sababu kipindi chao cha maisha kinakwisha ndani ya miezi tisa. Hivi sasa ni miaka sita, kuna mahitaji makubwa sana ya kamba na Wananchi wale hawana shughuli nyingine mbadala za kufanya. Kwa nini wasiruhusiwe kuendelea na shughuli zao za uvuvi, tunaacha zinakuja *trawler* kutoka nje, zinavuna kamba zinaondoka bila kulipa gawio la aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie la mwisho ni kuhusiana na suala hili la ujangili, ambalo limekuwepo. Mimi naamini kabisa jitihada zikifanyika baina ya Wizara ya Maliasili kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi, tunaweza tukawatumia Vijana wa JKT ambao wako pale na hawana shughuli nyingi sana, tunaweza tukawapangia nafasi ya kuweza kuendesha Operesheni Maalum kuweza kukabiliana na huu ujangili.

Hili jambo la kuja kushutumiana tu hapa bila ushahidi, bila maelezo na watu wakabuni mambo yao, siyo la msingi sana kwa ustawi wa nchi yetu. Kwa hiyo, naishauri Serikali tuweke Operesheni Maalum kuweza kukabiliana na majangili na kudhibiti idadi ya wanyama ambao wanapotea kutokana na ujangili huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu, nakushukuru sana. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Msolla.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Nianze kwa kusema, mwaka jana wakati nachangia katika Wizara hii, nilieleza baadhi ya tuhuma zinazowakabili Watendaji wa Ngorongoro. Naomba Waziri atuambie ni hatua gani zimechukuliwa mpaka sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Bodi ya Ngorongoro tunajua imekwisha muda wake, ni lini Bodi hiyo sasa itaundwa upya; na nafasi ya Mhifadhi Mkuu wa Ngorongoro ni lini nayo itapatiwa mtu badala ya kukaimu kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze suala pia la migogoro iliyopo katika Hifadhi za Taifa na Wananchi wanaozunguka maeneo hayo. Waziri alitueleza mwaka jana kwamba, kuna Tume ameiunda ikishirikiana na Wizara mbalimbali; tungependa kuambiwa nini majibu ya Tume hiyo? Tumeendelea kushuhudia migogoro inayoendelea na ni vyema Wizara ikatambua kwamba, mipaka iliyoainishwa ni ya zamani sana, tangu enzi ya Ukoloni. Hivyo, ni vyema sasa mipaka hii ikaangaliwa upya, kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba, idadi ya wakazi katika maeneo hayo inaongezeka haiwezi ikalingana na wakati wa Ukoloni. Hivyo, ni vyema wakaangalia pia ongezeko hilo la watu.

Endapo pana mahusiano mazuri kati ya hifadhi na Wananchi wanaoishi jirani, ndivyo ambavyo pia tembo wetu wanaweza kulindwa, lakini kama hakuna mahusiano, ndivyo ambavyo tembo wataendela kuuwawa na watang'olewa hizo pembe na tutaendelea kupata hasara na kuona tembo wanaisha kabisa. Kwa hiyo, ni vyema Wizara ilichukulie suala hili kwa umuhimu na kumaliza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, unyanyasaji wanaopata Wananchi wa maeneo hayo; katika Wilaya ya Karatu, akina mama na Wananchi wanaoishi jirani na maeneo hayo wanapata manyanyaso makubwa sana; wakienda hata kuokota kuni, hawajafika kwenye *fire line,* wanakamatwa na Maaskari wanachapwa viboko, wanapigwa na wengine wanapelekwa kuwekwa *lockup* Loliondo. Ukiangalia umbali wa kutoka Loliondo mpaka Karatu ni karibu kilometa 500. Sasa hata kama ndiyo wanashukiwa na jambo lolote, kwa nini wasiwekwe *lockup* ya Karatu badala yake wanapelekwa *lockup* ya Loliondo, ambapo ni karibu kilometa 500, hawapati huduma, hawapati chochote?

Kwa hiyo, Maaskari hawa wameleta usumbufu mkubwa na manyanyaso makubwa kwa Wananchi wanaoishi jirani na Hifadhi ya Ngorongoro katika Wilaya ya Karatu. Tunaomba Waziri atuambie ni lini mahusiano haya yataimarishwa, kwa sababu ukiimarisha mahusiano ya Wananchi na Hifadhi, ndivyo ambavyo pia wanyama watalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni hapo juzi tarehe 29, wakati Mheshimiwa Waziri anasoma Hotuba yake, tembo ameingia kwenye makazi ya watu katika Kijiji cha Rhotia na ameua mtu mmoja anayejulikana kwa jina la Erro. Tunaomba kujua fidia ya mtu huyu inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema kwamba, uwekezaji katika Mamlaka ya Ngorongoro, mwaka jana nilizungumzia suala hili, lakini bado inaonekana suala hili *either* Wizara inalisukuma kwa kasi. Tunaomba mtathmini upya,

athari ya uwekezaji katika eneo la Ngorongoro hasa sehemu inayoitwa masalia ya tembo. Kwa hiyo, ni vyema sana mkaliangalia upya, uwekezaji huu ambao una athari badala yake leo tunawavutia wawekezaji, lakini baadaye kama kuna makazi, kuna shughuli zozote za uwekezaji kama ni *Hotels* za Kitalii, *automatic* kutakuwa na athari; ndivyo ambavyo kama tembo hawatakuwepo, wanyama hawatakuwepo, hata hawa watalii hawatakuwepo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni lazima pia muuangalie utaratibu huu. Naomba nizungumzie suala ambalo linataka kuanzishwa na Wizara, Mheshimiwa Waziri, ni vyema ukaangalia sana suala la kuanzisha utaratibu wa *double entry*. Mwanzo au mpaka sasa unatumika utaratibu wa *single entry* na kwa faida ya Watanzania, unaposema *single entry* ni kwamba, unapoingia katika Geti la Ngorongoro, unalipia kuingia kwenda kuona *attractions* zilizopo katika Ngorongoro. Ukitoka nje, ukitaka kurudi tena unalipia upya, lakini Wizara inataka kuondoa utaratibu na kuanzisha utaratibu kwamba mtu akitoka akitaka kurudi asilipie chochote. Huku ni kupoteza mapato makubwa ya Serikali, ni vyema utaratibu huu wa *single entry* ubaki, uendelee kama ambavyo unatumika hivi sasa, kwa sababu utakuwa unawafaidisha *Tour Operators*, Serikali inakosa mapato. Kwa hiyo, ni vyema sana wakaangalia suala hili na kwa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tena kwa kuitaka Wizara ituambie ni hatua gani zilichukuliwa kwa watu wa Ngorongoro ambao walikuwa wana tuhuma mbalimbali za ubadhirifu wa fedha? Tunaomba tuambiwe ni lini mahusiano kati ya mipaka ya Ngorongoro na Wananchi wa Karatu yataimarishwa ili kuondoa usumbufu ambao wanaupata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Msolla.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Nianze tu kwa kusema

kwamba, Wizara hii ni muhimu sana kwa sababu ndiyo imepewa jukumu la kutunza rasilimali zetu, hususan misitu, wanyamapori, ambao ni urithi wetu na urithi wa vizazi vijavyo. Kwa bahati mbaya sana kama walivyozungumza watu wengine, urithi huu unazidi kupotea kwa kasi hususan misitu na wanyamapori. *(Makofi)*

Haya yote yanatokea kwa sababu ya shughuli za mwanadamu za kiuchumi na za kijamii. Nijikite kidogo kwenye mambo ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapata Uhuru mwaka 1961, nchi yetu ilikuwa na eneo la misitu hekta milioni 48 na wakati ule idadi ya Watanzania tulikuwa milioni tisa. Kwa hiyo, kila Mtanzania alikuwa anamiliki eneo la misitu la hekta 5.5. Ilipofika mwaka 1990 eneo ambalo lilikuwa la misitu, ilikuwa ni hekta milioni 41.5 na wakati huo Watanzania walikuwa milioni 24.4. Kwa hiyo, kila Mtanzania alikuwa anamiliki eneo la misitu hekta 1.8. Ilipofika mwaka 2012, eneo la misitu ilikuwa ni hekta milioni 33. 4 na idadi ya Watanzania ilikuwa ni milioni 44.9. Kwa hiyo, kila Mtanzania kufikia mwaka 2012 alikuwa anamiliki eneo la misitu hekta 0.8. Hali hii inazidi kupungua na inapungua kama nilivyosema, kutokana na shughuli za mwanadamu za kiuchumi na kijamii.

Nchi yetu inazidi kuwa jangwa, sababu kubwa ni matumizi ya kuni ambayo asilimia 95 ya Wananchi wanaoishi vijijini wanatumia kuni. Wananchi wanaoishi mijini asilimia 85 wanatumia mkaa. Mathalani, Dar es Salaam peke yake kwa mwaka mmoja hutumia magunia ya mkaa 17,250,000, ambapo gunia moja ni sawasawa na uzito wa kilo 57. Kiasi hiki cha mkaa kinachotumika ni sawa na kukata eneo la hekta 156. Hiyo ni Dar es Salaam peke yake. Kwa nchi nzima ni eneo kubwa zaidi ambalo linafyekwa kwa ajili ya mkaa tu na shughuli nyingine.

Tazama miji mingine mikubwa kama Mwanza, Arusha na mingine yote, wote hawa wanatumia mkaa, lakini tunafanya nini? Eneo linalokatwa misitu kwa mwaka kwa nchi nzima ni kati ya 450,000 mpaka 500,000, sasa tuna juhudi gani

ambazo tunazifanya ili kusudi hali hii isiendelee kwa sababu tunakoelekea kwa kweli ni jangwa na itakuwa ni janga la Taifa?

Kuna njia nyingi, tumekuwa tukijaribu kupanda miti, lakini kwa mwaka kwa Tanzania nzima tunapanda hekta 160,000 tu wakati eneo tunalokata ni kati ya hekta 450,000. Kwa hiyo, kuna upungufu mkubwa katika kufidia hali hii. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, tutazame namna tunavyoweza kutumia taasisi zetu kwa ajili ya upandaji wa miti. Mathalani Shule za Msingi, tuna Shule za Msingi karibu 15,000 nchini, kama kila shule ingependa eneo la hekta moja, tungeweza kuwa na miti mingi. Shule za Sekondari zipo karibu 4,200, kama kila shule ingepanda angalau eneo la hekta mbili vilevile tungeongeza sana upandaji wa miti, lakini haya hayafanyiki na sielewi Sera ya Serikali ni nini.

Tusiende kwenye shule tu, hata kila mmoja wetu akipanda miti kumi kwa mwaka, kwa Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi, bado tungeweza kuokoa eneo ambalo linaelekea kuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie juu ya ulinzi shirikishi. Katika Wilaya ya Kilolo tuna Kata nne; yaani Kata ya Mahenge na Kata ya Ruaha Mbuyuni, Wananchi wa Kata hizi wanashiriki katika kulinda *Udzungwa National Park* na Milima ya Tao ya Mashariki *(Eastern Art Mountains)*. Katika Kata ya Ibumu na Kata ya Image wanashiriki katika kulinda misitu ya Milima ya Serebu, lakini watu hawa hawanufaiki na hizi juhudi ambazo wanazifanya. Wanahangaika hata madarasa hawawezi kumaliza, barabara ya kutoka Ilambo kuja Ibumu ni mbovu, barabara ya kutoka Udekwa kuja Mahenge ni mbovu, Zahanati pia ni duni, lakini hawanufaiki na ulinzi shirikishi ambao wanapewa. Ninaomba sana Serikali ione namna gani hawa Wananchi wananufaika na kazi hizo wanazozifanya na wanazifanya kwa uaminifu mkubwa ili kuokoa rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, napenda kuzungumzia juu ya makumbusho. Tumezungumza juu ya

makumbusho na utalii mbalimbali. Mkoani Iringa katika Wilaya ya Kilolo, Kijiji cha Lugalo, kuna kaburi ambalo Jemedari wa Kijerumani aliyepigana vita na Wahehe wakiongozwa na Jemedali Chifu Mkwawa alizikwa, alikuwa anaitwa Nyundo, kwa sababu yeye hakutaka kutumia mara nyingi risasi, akiwakuta watu alikuwa anawaua kwa kuwapiga nyundo kichwani.

Limejengwa kaburi miaka mingi na ni refu, lakini hakuna hata mtu mmoja anayeliangalia, hata rangi imefifia na majina mengine yaliyoandikwa hayasomeki, hata kusema watengeneze wapande maua tu inakuwa kama ni chombo ambacho hakina mwenyewe. Naiomba Wizara kwamba, eneo hili lipewe kipaumbele kwa sababu tumekuwa tukiwapata Wajerumani wanakuja pale kuja kuangalia sehemu hii ya kihistoria. Hivyo basi, kama Serikali itasaidia katika hili, nina hakika itakuwa ni moja ya vivutio kama inavyofanyika sasa, lakini kwa kweli hali yake siyo nzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo machache, napenda kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu ili Wizara hii iweze kupewa bajeti ambayo imeomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa Msolla, kwa mchango wako makini kabisa. Sasa namwita Mheshimiwa Paulina Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Sanya.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna usemi unasema kwamba, ukificha maradhi kifo kinakuumbua. Nasema usemi huu niki-*refer* au nikiangalia Hotuba ya Kamati ya Maliasili, Ardhi na Mazingira, ambao waliweza kutoa maoni yao chini ya Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Lembeli, kuzungumzia hali

halisi katika nchi yetu jinsi ambavyo wanyama hawa ambao tunawatunza katika hifadhi zetu wanavyotoweka na wameeleza kwamba, miaka saba ijayo tembo watakuwa wametoweka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yakizungumzwa na upande wa Kambi ya Upinzani, wenzetu upande wa Serikali wanaona ni kichomi. Hebu mtafakari pia hata hiyo Hotuba ya Kamati, kama miaka saba ijayo hapatakuwa na tembo katika nchi hii, maana yake Serikali ya Chama cha Mapinduzi mnataka kuondoka na tembo wetu mtuachie nchi ikiwa haina tembo; ndiyo kitu ambacho mnataka kufanya, maana mwaka 2015 kwa haya mnayofanya Watanzania watafanya maamuzi. Sasa maana yake miaka miwili baadaye nchi haina tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali isikinge kifua dhidi ya hao wahalifu na Mheshimiwa Waziri ni vizuri hao watu wakachukuliwa hatua upesi bila kujali kama ni Katibu wa Chama au ni nani. Haya yasingeweza kupuuzwa kama Serikali ni sikivu. Nami nashangaa, mara nyingi mnatuambia kwamba, Serikali hii ni sikivu, hata hilo hamlioni kwamba mna miaka saba tu wanyama wetu wanakwenda kupotea; hilo tu hamlioni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi siyo sikivu hata kidogo. Ninasema haya kwani katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwaka jana, nilieleza kwa kina jinsi ambavyo Wizara inatakiwa iangaliwe kwa makini na kufanya mabadiliko makubwa. Katika kitabu cha majibu ya hoja ya Wabunge ulitujibu kwa yale ambayo tumelalamika, kwa mfano, mimi Mkoa wangu wa Manyara tunaathirika sana na Hifadhi ya Tarangire dhidi ya Wananchi, kila siku navitaja vijiji na imekuwa ni wimbo Gijedabu, Ayamango na Mamire. Mheshimiwa Naibu Waziri, uliahidi ungefanya ziara pale, wale Wananchi wa Kata zote hizo hawana pa kuishi, hawafagii nyumba zao wala hawajengi, yaani ukifagia uwanja tu Askari wa Tarangire wameshafika pale na hifadhi ile mmeongeza mpaka. Tangu mwaka 2008

hadi sasa ni takriban miaka sita, mnasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu; masikio gani hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikio gani yasiyosikia dhidi ya kero za Wananchi? Tunapata shida tunapoielezea Serikali na Mheshimiwa Waziri katika kitabu kile umejibu kwamba, mnaunda Timu ya Wataalamu ambapo mnahusisha Wizara yako, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi. Ile timu imekwenda lakini ugonjwa mkubwa tulionao katika nchi yetu na asubuhi tumeona kwenye maswali na majibu; *report* zinaishia huko mnafungia kwenye makabati. Kamati nyingi zimekwenda, Wananchi wa Mkoa wa Manyara wanaopakana na Hifadhi ya Tarangire, Wananchi wa Vijiji vya Mwayamayoka, Mamire na kadhalika, wametembelewa. Tangu mwaka 2008 ni Kamati nyingi zinakwenda lakini hakuna *report* hata moja inayorudi. Je, hii Serikali ni sikivu? *(Makofi)*

Unajua tunatoa mifano ili mjue kwamba Serikali siyo sikivu na Mheshimiwa Waziri kama hiyo imeundwa na imekwenda kuangalia wale Wananchi wamekuwa wavumilifu kwa miaka minane; Serikali inapata kigugumizi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnarudisha majibu kwamba Mkoa uangalie na utenge eneo. Nilishazungumza humu ndani, kila eneo wanalokwenda kugusa wanaona ni *potential*, wao wanagawana na Wananchi wanaendelea na adha hiyo. Je, hii Serikali ni sikivu? Kama mna-*identify* maeneo mazuri, mnakwenda kugawana Serikali na watu wenu lakini Wananchi wale wanaendelea kuteseka. Serikali ya Chama cha Mapinduzi siyo sikivu hata kidogo! Labda siku ya leo Mheshimiwa Waziri unishawishi kwamba usikivu wenu unachukua miaka mingapi ndiyo muweze kuelewa halafu na sisi tusubiri kwa miaka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie jinsi ambavyo hata nilizungumzia kanuni. Mheshimiwa Waziri, nilisema zile kanuni ni kandamizi na Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake akasema kwamba, watarekebisha zile kanuni,

katika maswali unakumbuka Mheshimiwa Naibu Waziri unatingisha kichwa. Nikaeleza kabisa kwamba, ile mipaka mnapoongeza wale Wananchi wanapakana moja kwa moja na ile mipaka ya hifadhi, lakini kanuni inasema yule Mwananchi anayepakana na ule mpaka katika *zero point* yule hastahili fidia. Katika takwimu zenu hapa mmeonesha na bahati mbaya sana hata hamkuonesha wale ambao waliathirika, wale ambao ndugu zao walifariki vifo havikuoneshwa hapa. Mmeonesha katika takwimu zenu hapa kwamba Wananchi 776 mazao yao yaliathirika na ekari 1,896. Mazao yale katika ekari hizo yaliliwa na hao wanyamapori, lakini hawa ambao ekari zao zaidi ya 1,896 zinaathirika ndiyo wale wanaopakana na hifadhi moja kwa moja kwenye ile mipaka, kanuni imekataza hawalipwi! Je, hii Serikali ni sikivu? Kwa nini hii kanuni msiibadilishe?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Dakika tano zimepita. Atakayefuata ni Mheshimiwa Sanya.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutufikisha na sisi tuchangie kidogo kuhusu Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naweza nikasema moja katika nchi ambazo Mungu amezijaalia sana katika Bara la Afrika ni Tanzania. Ukija kwenye Sekta ya Utalii peke yake, tuna Mlima wa Kilimanjaro, mbuga za wanyama, fukwe za bahari zilizo safi na salama, majumba ya kale na utamaduni wa makabila mbalimbali katika nchi yetu lakini. Je, tunaitumiaje fursa hii?

Mimi ninaomba Serikali kama inaambiwa siyo sikivu sasa iwe sikivu, kwa sababu Serikali ni watu na sisi Wabunge ni watu. Sisi tumekuja hapa kuelekeza mambo gani yafanyike ili tuondokane na umaskini katika nchi yetu. Siku zote nasema kwamba, kama tungekuwa makini, mambo manne tu

yanatosheleza kabisa kuweza kuinua uchumi wa nchi hii. Moja ikiwa ni Sekta ya Utalii, Kilimo na Ufugaji, Uvuvi wa Bahari Kuu na Viwanda Vidogovidogo. Aidha, Sekta hii inachangia asilimia 17, hebu kabla ya uchaguzi wa mwaka 2015 tuipandishe ifike walau asilimia 25, tutakuwa tumefanya la maana.

Nataka niwaambie kwamba, hakuna kitu ambacho kitasaidia Sekta hii siyo tu kuhifadhi mbuga za wanyama, tukubali tusikubali kwamba mtalii anapotaka kutembelea nchi yoyote kwa hizi bidhaa nilizozitaja hapa ambazo tunazo zote, anataka usafiri wa uhakika. Tufufue Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania,* ile ndiyo *National Identity* yetu na ndivyo wenzetu wa Kenya wakalichukua soko la utalii wakawa wako kidogo mbele kuliko sisi kutokana na kwamba, wana *joint venture* na *KLM* na *Precision Air,* inasambaza watalii nchini Kenya na nchini kwetu Tanzania mpaka Zanzibar. *(Makofi)*

Hebu tuwe na *National Carrier* ya ndani na ya nje, mtalii unamtoa Dar es Salaam unampeleka Ruaha, *is more than 500 dollars,* wakati mwingine mtalii anatoka London mpaka Dar es Salaam kwa dola 600 au 700. Inakuwaje usafiri wa ndani kumpeleka kwenye mbuga za wanyama uwe ghali zaidi ya tiketi aliyoichukua kutoka Ulaya kuja Tanzania? *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi na tuitangaze nchi yetu na tuitangaze kwa njia ambazo tunaweza kutangaza utalii. Tuna Mabalozi wetu, tuna *Diaspora,* Watanzania wanaoishi nje ya nchi, tuna wanafunzi tunaweza tukawasaidia wakachukua *brochures* wakaitangaza katika vyuo wanavyosoma nchi mbalimbali za Asia, Ulaya na Marekani. *(Makofi)*

Sasa hivi utalii jikiteni zaidi Mashariki ya Kati, India, nendeni China na Thailand. Haya ndiyo Mataifa ambayo yanainuka na wana fedha nyingi na wanaanza kutoa watalii kwenda nje ya nchi. Chukueni vyombo vya ndani vya nchi zile kama television, badala ya kuchukua Vyombo vya Kimataifa kama *CNN* na *BBC*, gharama zinakuwa nafuu na

watu wengi watakuwa wanaangalia katika *television* zao za ndani. *(Makofi)*

Chukua mfano, nchi ya Morocco ipo Afrika, ina majumba ya kale, wanapokea watalii milioni nane kwa mwaka mmoja, milioni nne ni *diaspora* ya wanaoishi nje na milioni nne ni wa ndani kuja kuangalia pale. Wanapokwenda Marakeshi, wala hawana bahari, lakini kila hoteli ina *swimming pool.* Unapokwenda miji ya kale kama Hollywood wako pale wanachukua filamu, wanaingia mpaka kwenye *film industries.* Sisi tuna miji kama Mikindani, Tanga, Bagamoyo, Zanzibar na hata Dar es Salaam. Mji wa Dar es Salaam leo unapotea hadhi yake, una historia kubwa sana ya majumba yake, unachukua majumba marefu ya ghorofa tunaangusha miji yetu ya zamani.

Nenda London wana miji miwili tofauti; London ya Kisasa na London ya zamani, nenda Montenegro, Serbia au hata Sicily Italy, wana hadhi ya majumba yao na wanapata fedha nyingi sana watu kwenda kuangalia yale majengo. Sisi tunaihifadhi vipi hii miji? Ukienda imekaa inazidi kuzorota, haiangaliwi, matokeo yake matatizo na hizi ndiyo *site* zinazoingiza fedha katika nchi mbalimbali. Egypt peke yake utalii wao ni nini? *Pyramids*, basi. Greece kuna makuta tu yameinuka ya zamani, watu wanakwenda Greece, wanakwenda Italy Sicily; sasa kwa nini wasije kwetu? Je, sisi tunawa-*train* vijana wetu ili wawe ni mahotelia wazuri?

Tutakuwa tunapiga kelele tu kwamba Kenya wanachukua nafasi, lakini sisi hatuwaandai vijana wetu. Tunawaandaa kumaliza *form six,* tunawaandaa wamalize *degree*, halafu wanataabika wanasema hakuna kazi, kumbe tunatakiwa tuwaandae katika sekta ambazo tunazo ndani ya nchi; viwanda vidogovidogo, uvuvi, utalii, ndiyo utaona tija ya namna gani watu wanavyofanya kazi.

Mtu wa Kenya unaingia hoteli anakuona kule na begi anaanza kukupa *smiling face,* lakini sisi hatuna *tendency* hiyo. Kwa nini tusiwafunze na kwa nini wale wasichukue soko letu kwa sababu sisi hilo soko hatuna haja nalo?

Sasa ninachosema ni kwamba, tujikite kuutangaza utalii, *United Arab Emirates*, Waarabu wana fedha zao, lakini tunakaa tunapiga kelele kwamba, Mwarabu wee, Mwarabu kachukua nini, kachukua eneo gani! Wana fedha zao na sisi tunazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waarabu kuanzia Juni, Julai, Agosti, kwao joto, wanatafuta mahali pa kwenda, wanakwenda Indonesia, Malaysia, Iran na wapi, kwa nini wasije Afrika ambapo kuna *roots* zao hapa? Kwa nini tusijenge hoteli za kisasa tukaongeza vitanda, Waarabu wakaja wakatumia hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tu-*base* zaidi kwenye utalii wa fedha nyingi, siyo wanakuja watalii watatu wanagawana dafu moja, wanakula mshikaki mmoja. Tuchukue watalii ambao kila mmoja anakaa hoteli ambayo angalau akilala usiku mmoja asubuhi anaacha dola 500, 600 au 700, ndivyo wenzetu wanavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fukwe zetu ni safi na salama. Katika nchi ambayo ina fukwe safi na salama ni Tanzania kwa sababu hata hatuna viwanda vinavyomwaga taka katika *beaches* zetu. Ni *virgin beaches,* kwa sababu ndiyo kwanza tunafungua utalii. Watu wanaelewa Zanzibar *is a beautiful place*, unaweza kwenda ukaona mji wa zamani na ukaenda kwenye fukwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho natoa tahadhari ni kwamba, utalii wowote unaua mazingira na unaua utamaduni. Hivyo, tuwe makini na hivyo vitu. Watalii wa hapa watakwenda kwenye Mbuga, watakwenda kupanda Mlima Kilimanjaro, lakini wa Zanzibar watamalizikia kwenye Mji Mkongwe kwenye Jimbo langu ambalo na raia wanaishi hapo hapo. Atamalizikia kwenye fukwe ambapo raia anaishi hapohapo. Kwa hiyo, tusichanganye mambo, tukaja tukapoteza utamaduni wetu, silka zetu, tabia na historia yetu kwa sababu tu ya utalii. Tukiwa makini mambo mengine yanakuja yenyewe tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya maeneo ambayo kuna raia wanapiga kelele kwamba hawataki hili, hawataki hili, ni *compromise by government itself*. Serikali mkiwa makini, mkaenda kuzungumza nao, wale ni binadamu, ndiyo watakaokuwa walinzi wazuri hata kuliko wale askari wanaolinda katika zile mbuga, kwa sababu wao watajua tija ya utalii nao inawafikia. Wajengeeni zahanati, barabara, wapeni *shares* zao kwenye Kata na Wilaya zao, basi yamekwisha. Leo tukianza kugawa maeneo kwa makabila au watu hatuta-*boost economy* yetu kwenye sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutagawa nchi vipande vipande, tutaanza kuogopa watu wa nje na hatimaye tutaogopana sisi wenyewe. Kila tukikaa tunataja kabila hili, mtu huyu, kwa nini? *What is the reason?* Watu wana pesa, waache waje wawekeze, *whether* ni Chinese, Indians, Arabs, waache waje. Sisi haja yetu ni fedha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusigawane ndani mapande, tukaigawa nchi, halafu tukaja tukakosa huu utamu wa utalii. Tukiwa na uhakika wa usafiri, tukawa tunatoa huduma nzuri katika eneo la hoteli, tukawa tunazalisha na kuzipelekea hoteli kinachohitajika ili wale na walale salama, sisi ndiyo tutakuwa tunafaidika. Ndiyo sisi tunaopiga kelele hapa siku zote, posho ndogo, mishahara haipandishwi na Serikali haiko makini. Serikali makini ni ile inayotafuta vyanzo.

Vyanzo vikitafutwa mnaanza kupiga kelele; mnapiga kelele kwa Mwarabu wa Loliondo, lakini Mwarabu wa Oman amekuja ameleta dola milioni 100 ili kuinua *Air* Tanzania, yeye hamumpigii kelele. *Why double standards?* Kama ana fedha anakuja kuwekeza, *whether he is black, he is red, he is brown, he is green, let him comes in. Yes!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunachokitafuta hapa ni tija bwana, hatutafuti rangi ya mtu, wala kabila, wala dini ya mtu. Tunachokitafuta ni nchi kwenda mbele, kupata tija, kutoa ajira na kuinua uchumi. Hadi leo hii tunapiga kelele kwamba, hatuna maji, huku tunapiga kelele kwamba hili

eneo lisitwaliwe na huyu, tunachokitafuta ni *means of income* ili nchi yetu iinuke. Ukizungumza kwenye mazingira, Profesa amezungumza hapa...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwa kuwa na wewe pia ni Mwarabu!

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Haidhuru mie Mwarabu, mie Mhindi, ninachozungumza hapa ni kwa manufaa ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima naomba sana usiendelee na hicho unachokifanya.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuheshimiane ndani ya Bunge, mimi sizungumzii ukabila hapa. Kama kungekuwa na ukabila nisingechaguliwa nikaja katika hili Bunge. Hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wewe uwe Mwarabu, uwe Mhindi, unaingia hapa. Wanaingia mpaka Masingasinga kwa sababu wana haki ya kuingia. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanya kengele ya pili.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri endelea, tuko pamoja na wewe. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hii tabia ya kuropoka maneno ya kuudhi chini chini wakati Mbunge mwingine anachangia si njema. Mtu unaporopoka unahamasisha jazba kwa mchangiaji. Unapohamasisha jazba kwa mchangiaji, anaweza kutoka nje ya mstari na akasema kitu kingine.

Narudia sana kuonya tabia hii. Mheshimiwa Halima nisingependa urudie tena kwani unasikika kwa sauti na kiti changu kimekuona, si mara moja.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sana tuheshimiane. Kuropoka vitu ambavyo havina tija si tabia nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tabia hii, inatupelekea kuondoka kwenye utaratibu mzuri wa kuchangia na mtu mwenye jazba anaweza akasema jambo lolote, halafu akasikika ametukana kumbe chanzo cha kutukana ni kwa yule anayesema kichinichini zaidi ya yule aliyesema. (*Makofi*)

Sasa naomba nikupe nafasi Mheshimiwa Mkosamali na Mheshimiwa Mbowe ajiandae. Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi ni watu ambao wanapaswa kuwa na *focus* na maamuzi na si wanaongoza tu kwa muda wao ambao wako madarakani kwamba, wewe ukiwa Waziri miaka miwili, mitatu, unaongoza mambo yako kwa muda ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi ni mtu ambaye anafikiria nchi yake hata miaka mia moja mbele au miaka mia mbili nchi yake itakuwaje? Huyo ndiye kiongozi, haishi tu kwa kutazama muda mfupi, kutazama mambo kwa hali ya kawaida, huyu anakuwa siyo kiongozi mzuri. Ndiyo maana hata Mwalimu Nyerere alikuwa anakataa baadhi ya mambo kwamba, hebu tuache. Kwa mfano, madini alisema tuache, ilikuwa ni fikra ya namna fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninayasema haya? Namheshimiwa sana Mheshimiwa Kagasheki, najua ana uwezo, lakini nataka aniambie ana mkakati au mpango gani? Nataka wakati anahitimisha anijibu kwamba, hivi

nikimuuliza nchi hii miaka mia moja ijayo itakuwa na ndovu wangapi? *Will you give me that answer?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima anipatie jibu, kama ni kiongozi sahihi atatakiwa atwambie *after one hundred years* au baada ya miaka hamsini, nchi hii ambayo Kamati inatwambia baada ya miaka saba kutakuwa hakuna ndovu, wanaweza wakatwambia miaka hamsini tu ijayo, wana mpango tuwe na ndovu wangapi au hawana mpango wowote? Wapo wapo, wanaishi tu, liwalo na liwe, mazoea. Kama wanaishi hivyo, *they are not leaders* kabisa, wa siyo viongozi. Ni lazima wajue tutakuwa na misitu kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza hapa Profesa Msolla kwamba, hekta mia nne hamsini na kitu zinakatwa kila siku. Tunaongea kila siku, kwenye Wizara ya Mazingira tumezungumza hapa, lakini haya mambo ambayo tunayaongea hapa nimekuwepo na nimeangalia hotuba, watu wamechangia mwaka jana, mwaka juzi, watu wanazungumzia mambo haya haya, watu wameongea sana haya mambo, lakini huoni mkakati. *You don't see*, sasa hawa ni viongozi au akina nani? *Who are they?* Kwa sababu siwaelewi, ni kwamba hawana uwezo au hawajui tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wakati tukiwa kwenye semina ya maadili hapa, tulikuwa tunazungumza juu ya suala la viongozi, kwamba ni watu wa namna gani? Sasa wengine tunapata matatizo, nimechangia mwaka jana, nikawaeleza mambo mengi tu, wizi wa meno ya tembo na kadhalika. Nikawaambia huko kwangu kwenye Pori la Moyowosi juu ya mazingira, lakini hakuna kilichofanyika hata kimoja, *these people*, hata kitu kimoja!

Sasa ninyi ni Serikali ya namna gani? Mnaishi vipi? Yaani mnaambiwa, siyo kwamba hamjui, nyie Wabunge mlioko humu, siyo kwamba watu wameanza kuyasema hapa juzi. Haya mambo yameanza kuzungumzwa na watu muda

mrefu, lakini tunakosa watu wa kusimamia. Hatuna *leaders* au viongozi wa kusimamia haya mambo kwa umadhubuti. Watu wako hapa, wapitepite kwamba, nimekuwa Mbunge.

Tunajua mna *vision* sijui mpaka 2025, hivi tukiwauliza kwamba baada ya miaka mia moja nchi hii itakuwa na miti kiasi gani, mnajua, au mpo tu ili mradi mpo? *You don't care*! Yaani hatuwaelewi hata siku moja ninyi. Hivi hawa ni viongozi wa namna gani? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tuyazungumze. Naomba wananchi kwa kweli wawe *very careful*, msione tu watu wanakuja wanahutubia hutubia mkadhani ni viongozi, si kweli. Mtu ambaye hajui nchi yake, miti inakatwa, tupe mbadala, hii miti inakwisha, nchi itakuwa jangwa, mbadala ni upi *after ten years*? Hana jibu, hajui, haelewi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanakata miti na kuchoma tani za mkaa, unamuuliza wewe si tumekupa usimamie, una mkakati gani? Haelewi, yupo tu. Mkaa unachomwa, miti inakwisha, wanyama wanakwisha, watu wapo tu, *who are you*? Viongozi wa namna hii? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi ni mtu ambaye una uwezo, *focus* na unasimamia, siyo kuishi tu kirahisi. Zamani viongozi walikuwa wakija ukisikia Rais amefika Kibondo Kigoma, watu wako makini, ofisi zinasafishwa na nini, leo unasikia Waziri amepita sijui nani, anakwenda wapi? Anafanya nini? Ame-*deliver* nini? *Impact* ya kwenda huko ni nini? Eeh, ninyi watu, *be serious with this country!* Muwe *serious*, kama kuna mtu yuko huko amekaa tu anafanya shughuli zake na kusubiri mishahara na vitu vingine bora aache hii kazi ya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi ndiyo kazi ngumu kuliko kazi yoyote ile duniani. Uongozi ni kazi ngumu, ndiyo maana wewe ni kiongozi. Tuna-*expect* kiongozi hata kama hujasoma *medicine* ukielezewa na mtu wa *medicine* unaelewa kwa haraka. Hata kama hujasoma utalii, una

uwezo wa kuelewa, ndiyo maana wewe ni kiongozi, unajadili Wizara hapa, *everything*. *We are discussing here*. Tunajadili kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo *we are talking,* haya yaliyojadiliwa mwaka huu, ukiangalia na ya mwaka jana ni *the same,* tena inawezekana hata ya mwaka jana ni mengi zaidi ya haya, lakini hakuna kinachofanyika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye Jimbo langu la Kibondo. Kibondo ndiyo Muhambwe, wale Wabunge mnaonong'ona, yaani mimi naongoza Wilaya ya Kibondo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba. pale Kibondo kwenye pori la Moyowosi nilizungumza mwaka jana na nimeshaliuliza hili swali mara kadhaa, linasumbua Wabunge wengi sana wanaotoka maeneo ya hifadhi. Naibu Waziri anakuja hapa anatoa majibu ambayo hayaridhishi. Siyo mimi tu, Wabunge wengi wanamwambia kuna matatizo, wananchi wanazuiwa kufanya shughuli kadhaa ndani ya hifadhi. Anatoa majibu sijui anadhani wataalam ndiyo wana uzalendo wa wananchi kuliko sisi tulioko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishamwambia Waziri *face to face,* nilishamwandikia barua nikihoji ni kwa nini wanawazuia watu kuingia kuvua samaki ndani ya hifadhi? Kwa nini wamewazuia wananchi wa Kibondo kwa miaka mitatu wasivue samaki, wakati kwenye hotuba yake hapa anasema katika ukurasa wa pili kwamba, kuwezesha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi kunufaika na rasilimali za wanyama na misitu? Mmezungumza hapa kwamba ndiyo Ilani yenu hii ya CCM ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hii ndiyo Ilani yenu ya CCM ya mwaka 2010, nawaambia wananchi ni kweli wako hapa na mnanisikia kila mwaka nazungumza kuhusu Wizara hii, naomba muendelee vile vile kutowapa kura CCM kule kwangu. Kama mlivyofanya kwenye Ubunge na Urais, endeleeni kwa sababu wamewazuia miaka mitatu, *they*

*don't like you to go there*. Hawataki mfanye kazi, mnakaa na hifadhi, wanakuja watu wanawinda, wanafanya mambo mengine, nyie mmekaa tu, wamezuia kibali cha kwenda kuvua samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Afisa Uvuvi ameajiriwa pale Kibondo, wanamlipa fedha ya nini sasa? Maana ziwa haliko Kibondo, liko Kigoma Mjini, yule ameajiriwa kwa ajili ya kusimamia watu wanaovua kule, ana miaka mitatu analipwa fedha ya nini? Mnamlipa fedha, za nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaomba, tumezungumza, lakini hambadiliki, hamsikii na wala hamna nini. Tumewaambia kuna ng'ombe wako kwenye hifadhi, kuna maafisa wenu wanatoza fedha, nikamwambia Mheshimiwa Waziri mwaka jana twende nikamwoneshe, sasa ndiyo mnatunza hivi misitu? Tunawaambia rasilimali zinaharibika, hambadiliki, *you don't change* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Mheshimiwa Waziri awajibu watu wa Kibondo, vibali hivi vinapatikana? Siyo ku-*rely* tu kwenye majibu ya wataalam, wanapita pale haraka haraka, wajibu hili jambo kwamba inawezekana au haiwezekani ili tufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye hoja ya Kasulu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu. Nitajaribu kuelekeza mchango wangu katika maeneo matatu ambayo nafikiri ni ya msingi sana Serikali ikatafari iyafanyie vipi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza nitazungumza kuhusu Mlima Kilimanjaro. Mlima huu leo naweza nikaufananisha na yule bata anayetaga mayai ya dhahabu, kwamba sasa tunakubali tu kupokea mayai ya dhahabu kutoka kwa bata huyu, lakini mwishoni tunafikia hatua ya kumuua bata mwenyewe ili tupate mayai na nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna mpango wa Serikali wa kuutunza mlima ule, kwa mujibu wa tafiti ambazo zimefanywa, tunajua kabisa theluji ya Mlima Kilimanjaro itakuwa imekwisha katika muda wa miaka kama 10 au 15 ijayo. Mpaka sasa hivi hatujaelezwa au kusikia mpango wowote madhubuti wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi wa kujaribu kuiokoa theluji ya Mlima Kilimanjaro. Kwa bahati mbaya sana, jambo hili limeonekana kama ni mzaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ningependa Waziri na hasa Serikali itambue ni kwamba, asilimia 75 ya wageni wanaopanda Mlima Kilimanjaro wanapanda kwa sababu ya kwenda kuona barafu katika *tropics*. Hawapandi tu kwa sababu kuna *height* kubwa, wanapanda kwa sababu ya kwenda kushuhudia *snow fields* za Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mlima huu ambao unaiingizia Serikali hii mapato ya dola zaidi ya milioni 50 kila mwaka au kwa fedha za Tanzania zaidi ya bilioni 80 kila mwaka, tunaiona ile theluji inapotea na hatuchukui hatua yoyote ya kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inavuna fedha nyingi sana kutoka Mlima Kilimanjaro na kwa kweli kama inataka ku-*sustain* utalii wa Mlima Kilimanjaro, ni lazima iweze ku-*address* tatizo zima la *ecosystem* ya Mlima Kilimanjaro. Suala linalosababisha theluji kupungua ni mambo mengi ambayo yamechanganyikana kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, kumekuwa na uvunaji mkubwa sana wa miti katika

maporomoko yote ya Mlima Kilimanjaro na hata sehemu ya hifadhi ya mlima kule *KINAPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, vyanzo vya maji vimepungua kwa kiwango kikubwa mno kiasi kwamba, hata maji yanayopatikana sasa hivi pamoja na kwamba yanasimamiwa na watu wa Pangani *Water Basin* yanashindwa ku-*sustain* mazingira ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati kama huu ni lazima uwepo mpango wa makusudi ambao utakuwa unasimamiwa na Serikali kwa kushirikisha Halmashauri zote za Wilaya zinazozunguka Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sasa hivi *KINAPA* wanafanya kivyao, *TANAPA* wanafanya kivyao, hawaoni kama Halmashauri za Wilaya ni wadau muhimu na jamii inayozunguka Mlima Kilimanjaro, nao ni wadau muhimu sana katika kuhakikisha kwamba, wanaweza wakatengeneza ile *ecosystem* nzima ya Mlima Kilimanjaro, ikaweza ku-*sustain* biashara ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, amejitahidi sana maskini, kufanya programu ya kupanda miti, lakini programu hii haiwezi kufanikiwa kwa sababu haina *funds* za kutosha. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbali na kutokuwepo *funds* za kutosha ni programu ambayo upande wa pili inawalazimisha wananchi wasikate miti yao. Sasa wananchi wanapanda miti yao, wanahitaji kuvuna miti yao, wewe Serikali hupandi miti yako, ila unaweka amri kwamba watu wasivune miti yao, huu ni utaratibu ambao kidogo umewakwaza wananchi, tungeomba Serikali na Waziri muutolee tamko.

Njia pekee ya kuweza kui- *sustain* Kilimanjaro katika upande wa *forestry* ni kupanda miti zaidi, kuwa na *funds* za kutosha kupanda miti, kutunza vyanzo vya maji. Hili ni jukumu

ambalo Serikali inatakiwa ilifanye kwa sababu huu Mlima unawatagia mayai ya dhahabu, kwa hiyo, lazima muweze kutoa fedha nyingine ikapelekwa katika fungu hilo, bila kuwa na fedha hatutaweza kupanda miti katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za kupanda miti, zinafanywa na watu binafsi na Taasisi mbalimbali, lakini Serikali kama Serikali haijaonekana kama mtu anayevuna bilioni 80 kwenye ule Mlima kila mwaka. Kwa hiyo, naomba sana hilo jambo liweze kufanyiwa kazi na wananchi washirikishwe kwa karibu sana, hauwezi ukaulinda ule Mlima kama Halmashauri za Wilaya zinazozunguka Mlima Kilimanjaro hazitashirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanawaona watalii wanapanda Mlimani pale, wananchi hawashirikishwa kwa njia yoyote ile maamuzi mnafanya nyie, Halmashauri za Wilaya hazipo *involved*, hazihusiani na Bodi ya *TANAPA* au *TANAPA* kabisa, lakini ndiyo ambazo zinalinda ule mlima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunawaambia ndugu zetu kwamba kama mnataka ule Mlima uweze kuwa endelevu kuweza kuingiza mapato katika Serikali na kuweza kusaidia katika kujenga uchumi wa nchi hii, ni lazima sasa wananchi washirikishwe, Halmashauri zishirikishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mazingira yaboreshwe kwa fungu maalum kutoka kule kule kwenye mapato ya Mlima, msitegemee Halmashauri za Wilaya zitafute fungu lingine la kutengeneza mazingira ya Mkoa wa Kilimanjaro wakati kuna fedha nyingi sana zinazopatikana kutokana na vyanzo mbalimbali vingine vya Mlima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishamaliza kuongea habari ya Mlima, pengine niongee suala la ujangili. Hili suala ni *serious,* halafu naona watu wanalifanyia utani. Kwa bahati mbaya sana na watu wengi sana ambao wapo kwenye biashara ya ujangili, wapo *organized*, hii *organized crime* na kama kweli tunataka kupambana na ujangili katika nchi hii lazima tufanye maamuzi magumu, lazima tuweze

kutengeneza sheria ngumu, lazima tufanye mambo mengine ambayo tutapata lawama kwa wenzetu wa nje, lakini hatimaye tutaweza kuokoa rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia idadi ya ndovu ambao wanavunwa au wanauawa kijangili kila siku na kila mwezi, watafiti wanatwambia baada ya miaka saba nchi hii itakuwa haina tena tembo. Sasa katika miaka saba kama hatuna tembo na tunajua tembo ni *one of the big five* katika wale wanyama wakubwa wa pori ambao wanavuta watalii, tutakwenda kuwaonyesha nini watalii na tunakwenda kuiambia nini duniani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaposhindwa kuweka mkakati wa makusudi wa dharura wa kuokoa tembo wake, tembo wanapungua katika *phase* ambayo haiaminiki. Lazima pawe na mkakati wa makusudi. Pia watu wanaovuna vitu hivi wengi wanajulikana, lakini wengine wapo kwenye *system* wanaogopwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pengine tuweke na sheria ngumu vile vile kama mpaka leo katika nchi hii tuna sheria ya kifo, ni kwa nini watu ambao wanahusika na biashara ya ujangili wa tembo wasiweze kupewa adhabu ya kifo. Lazima tufanye maamuzi magumu ambayo yatawa-*scare* hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaona aibu, kama tunaogopa kuwanyonga watu ambao wanamaliza rasilimali ya nchi hii, tunasema eti sisi tunafuata mambo ya haki za binadamu, wakati tembo wanakwisha na hatuna kitu cha kuwaachia vizazi vijavyo. Ni lazima turekebishe sheria zetu siyo tu sheria za kufungana kifungo cha miaka miwili, mitatu wakati tembo wanakufa kama mchezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri alete mapendekezo hapa tuweke sheria ya kunyongana nchi hii kwa wale ambao wanavuna tembo katika utaratibu ambao siyo wa kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweka sheria kali kama hizi kuna watu watakuwa *scared* kufanya biashara hii. Biashara ya meno ya tembo Waheshimiwa Wabunge haifanyiki tena kama zamani walivyokuwa wanafanya. Zamani walikuwa wanabeba pembe nzima nzima au jino zima zima wanapeleka kwenye ma-*container,* sasa hivi watu wanasaga meno ya tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanasafirishwa kwenye *bags* kwenye ndege wala siyo kwa kutumia *containers* tena. Kwa sababu meno yanakuwa *granded* yanakuwa unga au wanatengeneza na *palettes.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Viwanda vya Kusaga meno ya tembo ndani ya nchi hii na vingine vinajulikana na vyombo vya usalama. Kuna viongozi wanashiriki katika biashara hii, kuna viongozi wetu katika vyombo vya ulinzi na usalama wanashiriki katika biashara hii, huu mtandao ni mpana na huu mtandao upo katika Tanzania nzima na viwanda vipo humu humu nchini vinavyosaga meno ya tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tembo wanaoondoka kwa siku ni wengi kwelikweli na siyo lazima waondoke kwa meli. Wengine wanaondoka kwa ndege kwa sababu sasa hivi meno ya tembo wanasaga na yakishasagwa wanaweza kuchukua katika *format* yoyote, katika *bag* tu la kawaida akaondoka nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilo moja ya jiwe la tembo sasa hivi ni kati ya *dollar* 3500 mpaka *dollar* 4500, ni biashara kubwa sana na kwa sababu ya ukubwa wa biashara hii unahitaji nguvu za ziada kuzuia biashara hii. Jeshi letu la Wanyamapori halina uwezo wa kuzuia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo kubwa siyo Jeshi la Wanyamapori kushindwa kuzuia, tatizo kubwa, ni *political will* na hii *political will* haipo kwa sababu viongozi na makada mbalimbali ambao wanahusiana na Vyama vya Siasa wanahusika katika biashara hii. Sasa tunamaliza tembo,

tembo wanakwisha Selou, tembo wanakwisha Katavi, tembo wanakwisha Ruaha, tembo wanakwisha Manyara, tembo wanavunwa mpaka ndani ya Serengeti na Serikali ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *game wardens* ambao tunafikiri wanaweza wakalinda tembo wale tunawaonea bure. Ni lazima pawe na *special operation* hata kama ni lazima kuomba nguvu ya ziada ya kutoka kwenye vyombo vingine vya ulinzi na salama *let this be a special operation* ku-*save our elephants*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendelea kuona tembo wanavunwa namna hii na Waziri mkakaa hapa, mkaomba bajeti mkaa chini. Huu lazima uwe mkakati shirikishi ambao Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Utalii na Serikali yote kwa ujumla ikae iweke mkakati wa kuwa-*save* tembo hawa. Ninyi mnajisikia namna gani kama Mawaziri mnapoambiwa *seven years* time hakutakuwepo na tembo katika nchi hii. *How do you feel*? Hiyo Serikali yenu ina *feel* nini mnapoambiwa kwamba in *seven years time* nchi hii haitakuwa na ndovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimeandikwa taarifa mbalimbali za kueleza ujangili katika nchi hii na ninyi wenyewe Mawaziri mnajua na Serikali yenu inajua, lakini mnaogopa kuchukua hatua na kwa sababu wahusika wakubwa ni watu ambao wana mahusiano ya karibu sana aidha Chama chenu ama na Viongozi ndani ya Serikali ama na vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Sasa kama hatutatunga sheria ya kunyonga hapa katika hili, hili tatizo la tembo halitakwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nilizungumzie hili *very clear*. Serikali ifanye maamuzi magumu, tutapata lawama kutoka kwenye Taasisi mbalimbali za Kimataifa kwamba Tanzania badala ya kuondoa sheria ya kunyonga watu inarudisha sheria ya kunyonga watu, lakini kama kweli tunataka ku-*save* maliasili yetu kwenye *particular* tembo, lazima tutunge sheria ngumu. Mtu ajue tu akiingiza mguu katika kukamata tembo anaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* kama tutakuwa na utamaduni huu huu tunaozungumza wa siku zote ni kwamba tunakwenda kulea tatizo ambalo litaua *tourism* katika nchi hii. Leo tukiua utalii, utalii ni *number one forest earn* katika nchi kwa sasa hivi. Halafu tunaona theluji ya Mlima inayeyuka, tunakaa kimya tunacheka. Tunategemea miujiza ya Mungu ama aje Mzungu atusaidie habari ya ku-*preserve* huo Mlima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona tembo wanakwisha tunacheka na tunajua kabisa tunahitaji wale tembo tuweze kutengeneza fedha za kigeni. Tunaona wanateketea tunasema sisi ni Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inalinda wanyama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, nakushukuru ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbowe.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya *Multi-Sectoral Land Use* kama ya Ngorongoro imeonesha mafanikio makubwa ambayo ni pamoja na *changes* mbalimbali kwa ng'ombe 24,000, aya ya 47 ya Hotuba. Aidha, kuna ushirikiano mzuri kati ya jamii, ng'ombe na wanyamapori na mapato yanapatikana takriban shilingi bilioni 47, aya ya 45 ya Hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Maswa Game Reserves na Controlled Areas* zina migogoro mingi kati ya wafugaji na *game rangers*. Migogoro hii inayohusu malisho ya ng'ombe imezaa mianya ya rushwa. Wafugaji wanatumia maeneo haya kwa malisho kwa malipo ambayo yanagharimu mamilioni ya fedha. Mapato haya yanaingia katika mifuko ya *game rangers* na Serikali haipati chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, dhana ya *Multi-Sectoral Land Use* ingetumika katika maeneo yanayopakana na vijiji, migogoro ingepungua na hata malisho yangepatikana kwa malipo; ni bora kuliko fedha hizi kuachiwa watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa jambo hili unawezekana kwa kutunga Sheria ndogo kudhibiti wanyamapori kuwindwa na ukataji wa miti kwa msingi ule ule wa Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Handajika kinafanya kazi nzuri ya uhifandhi wa Serengeti, lakini Barabara ya Handajika mpaka *junction* ya Barabara Kuu Seronera ni mbaya, haipati fedha ya matengenezo na wakati wa mvua barabara hii haipitiki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Gate* hili linafungua fursa ya watalii kutembelea *Western Corridor* ya Serikali ambayo ndiyo kipaumbele cha maeneo mapya ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Mwanza ni kiingilio muhimu sana katika kuendeleza *Western Corridor* ya Serengeti badala ya kutumia Arusha tu na *Kilimanjaro Airport*. Kwa mtazamo huu ni bora mtazamo wa Wizara ukaweka mkazo katika kuimarisha *Airport* ya Mwanza pamoja na kuhamasisha Hoteli za Kitalii Mjini Mwanza na Hoteli nyingi zaidi *Serengeti Western Corridor.*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Pori la Lwafi lenye ukubwa wa kilomita za mraba 2227 ambalo liko Wilaya ya Nkasi, Mkoa wa Rukwa, halina watumishi wa

kutosha na pia halina usafiri (gari). Naomba sana waongezwe gari, pori ni kubwa na uharibifu wa wavamizi ni mkubwa sana hasa wafugaji na baadhi ya wakulima na wawindaji haramu.

Pori la Lwafi linasaidia kuleta mvua, pia ni uhai wa Wakazi wa Namanyere kwa chanzo cha maji. Chonde chonde naiomba Wizara iongeze watumishi, pia nilikwishamwona Mheshimiwa Waziri Kagesheki kuhusu suala hilo. Ninategemea mtatutafutia hata gari kuu kuu mlipeleke Namanyere kupambana na wavamizi. Misitu au hiyo Hifadhi itakwisha kabisa, watu hawana aibu wala huruma, wanakata miti hovyo. Pia kuna makundi makubwa sana ya wachoma mkaa na wapasua mbao (Mninga), kama siyo Hifadhi tunaangamiza kabisa hilo Pori la Akiba. Wizara ilione hilo Pori kwa jicho la huruma kabisa.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara izingatie yafutayo:-

(i) Wapanda Mlima Kilimanjaro wanalalamikia Makampuni ya Kitalii kwamba malipo wanayowapa ni kiduchu, hayalingani na kazi wanayofanya. Naomba Wizara itangaze waziwazi kiasi cha malipo kinachopaswa kutolewa kwa wafanyakazi wanaotoa huduma hizo.

(ii) Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wanalalamika kwamba hawanufaiki na mapato yanayotokana na mapato ya utalii Mkoa wa Kilimanjaro. Ingefaa Wizara iseme Halmashauri za Mkoa wa Kilimanjaro zinanufaikaje.

(iii) Miaka mitatu iliyopita Serikali ilikuwa na nia ya kufungua njia nyingine ya kutoka Marangu ya kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia njia ya Kilema Kaskazini. Ningeomba Serikali itamke njia hiyo itafunguliwa lini kwani Serikali inakaribia kukamilisha barabara ya lami ya kutoka Marangu Mtoni kwenda Kilema Sokoni.

(iv) Nyumba zilizo kandokando ya Barabara ya Kitalii inayotoka Marangu Mtoni kwenda katika Ofisi za Kinapa

zimewekewa alama ya “X” inayoonesha kwamba barabara hiyo itapanuliwa na nyumba hizo zitavunjwa. Naomba ieleweke kwamba, barabara za kitalii zinazokwenda Mlima Kilimanjaro haziwezi kupanuliwa kama zilizo katika maeneo ya tambarare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itamke hatima za barabara za kupanda Mlima Kilimanjaro.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kuhusu ujangili wa wanyamapori uliokithiri. Suala la ujangili limezungumzwa kwa muda mrefu sasa na kadiri siku zinavyozidi kupita, ndivyo ukubwa wa tatizo unazidi kuongezeka. Kwa kuwa kuna ushahidi wa kutosha na wa mazingira kwamba, wahusika wa ujangili huu wanajulikana na wameshatajwa mara kadhaa tena kwa majina, nyadhifa na makampuni yao; ni kwa nini Serikali ina kigugumizi kikubwa katika kuwachukulia hatua majangili hawa?

Hivi ni kweli tuamini maneno yanayozungumzwa kwamba Serikali inawakingia vifua na kuwalinda? Kama sivyo, ni kwa nini haichukui hatua ya kuwafikisha kwenye vyombo vya Sheria kama kweli inalitakia mema Taifa lake?

Suala lingine ni silaha nzito na za kivita, tena za kisasa wanazotumia. Hizi silaha wanazipata wapi? Inafahamika kwamba ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania pekee lenye mamlaka ya kumiliki silaha za kivita na wala si Jeshi la Polisi. Kwa namna gani majangili haya yanapata silaha hizi bila JWTZ kuwa na taarifa?

Je, kuna utovu wa nidhamu kwa Wanajeshi wetu na hivyo kuuza silaha kwa majangili kinyemela? Kama sivyo, JWTZ wanafanya kazi gani kuhakikisha wanakamata silaha hizi? Kama zinaingizwa toka nje ya nchi, zinapitia wapi? Je, mipaka yetu haiko salama? Nahitaji majibu ya kina.

Kuhusu Sekta ya Utalii; ni aibu nchi kuwa na vivutio vingi vya utalii lakini hakuna uhamasishaji wa kutosha kwa Wananchi wa Tanzania kutembelea vivutio hivi. Si uhamasishaji tu pia gharama za kutembela vivutio hivi ni kubwa sana na hukatisha Wananchi tama ya kutembelea wao pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Siyo ajabu mtoto mdogo kumjua tembo, twiga, simba, chui na kadhalika kwenye *TV* wakati kuna *National Parks* nyingi ambapo watoto wangeweza kwenda kuwaona wanyama hao kwa macho. Ifike wakati mkakati uwekwe kwa Wananchi wa Tanzania ili waweze kutembelea vivutio vya nchi zao kwa gharama nafuu angalau mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mapato yanayotokana na Sekta ya Utalii, hayakidhi kiwango cha utalii uliopo. Kuna madai kwamba, watalii wanazidi kupungua badala ya kuongezeka kutokana na upungufu wa vyumba vya malazi na miundombinu mibovu kuelekea mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wawekezaji waliopewa ruhusa ya kujenga Hoteli za Kitalii hawakamilishi kazi hiyo kama mikataba yao inavyowataka? Kwa nini Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii isisitishe mikataba yao na kuwapa wawekezaji wengine ambao watakuwa waadilifu na kufanya kama mikataba inavyoelekeza? Mpaka lini Serikali itaendelea kupoteza mapato yake ya Utalii kwa uzembe wa wawekezaji wachache wasiotimiza wajibu wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vibali vya uwindaji; Sheria inataka mtu asipewe zaidi ya vitalu vitatu vya uwindaji. Inasadakika kwamba, kumekuwa na wafanyabiashara wasio waaminifu, wabinafsi, wanaoanzisha makampuni kwa majina tofauti tofauti ilhali wamiliki ni wale wale na wanaomba na kupewa vitalu zaidi na hivyo kuwanyima wengine haki hiyo. Kama hili lipo na linajulikana; kwa nini Serikali inawafumbia macho wafanyabiashara hawa wabinafsi? Kwa nini vitalu visigawiwe kwa haki kwa wote wanaohitaji na wenye sifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengi ambayo kama Serikali ikiyafanyia kazi inaweza kujiongezea kipato kupitia utalii. Mfano mzuri ni katika Mkoa wa Singida, eneo la Sukamahela (Manyoni), ambapo inasadikika ndipo msafara wa biashara ya utumwa ulikuwa ukipita. Wote tunatambua umuhimu wa biashara ya utumwa katika historia yetu *(Tanzania and EA),* hivyo ni vyema eneo hilo likafanyiwa utafiti wa kina na kuona ni namna gani inaweza kulitangaza kwa ajili ya utalii na kwa kuweka sawa kumbukumbu za kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote kwa utendaji katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera ya nchi kwamba, Wananchi wanaozunguka Mbuga za Wanyama washirikishwe katika uhifadhi na wathaminiwe na wathamini mali za kwenye mbuga kuwa ni mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujangili; yaliyotajwa na Kamati husika yazingatiwe, silaha zilizozuiliwa bandarini na *TRA* ziachiliwe ili ziweze kupokelewa Wizarani haraka na kutumika kupunguza ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii unakua kwa kasi ndogo hasa ukilinganisha na nchi majirani, lakini wenye vivutio visivyo bora kama vyetu. Ninashauri zifanywe jitihada za kutangaza vivutio vya maeneo yetu ya utalii.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeiandikia Wizara hii barua rasmi na kuikumbusha mara kadhaa kuhusu kupanua mipaka ya kijiji cha Lulanga, Kata ya Mgandu, Tarafa ya Itigi. Kijiji hiki hakipo mbali na Kijiji cha Doroto ambacho kilio chao kilisikika kwa kupanua mpaka wao. Hii imeleta tatizo kwa Kijiji cha Lulanga kwa kuona Serikali

imewasikiliza wenzao wa Doroto na wao kutosikilizwa. Naomba majibu juu ya tatizo hili; Serikali imefikia wapi katika kutatua tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Rungwa, Kintanula, Mwamagembe, Kalangali, Mitundu, Ipalalyu, Makale, Mtakuja, Kayui, Uswesanoni, Mwamatiga, Itagata, Lulanga, Doroto, Msisii, Kahomwe, Kitaraka, Kazikazi, Ibombeda, Itigi, Majengo, Damweru, Mgamboo, Mkajenga, Katumba, Ipande, Muhanga, Kiyanju; vipo kandokando ya Mapori ya Hifadhi ya Rungwa, Kizigo na Mhesi. Kwa bahati mbaya sana, havijapatiwa huduma muhimu za jamii kwa kiwango cha kutosheleza. Hakuna shule za maana, hakuna zahanati au vituo vya afya, hakuna huduma za maji ingawa mapori haya yanachangia kiasi kikubwa cha mapato kwenye Idara ya Wanayamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuna *open areas* za wawindaji kwenye mbuga hizi na Mbuga ya Chaya, lakini mapato yote yatokanayo na uwindaji bado hayajaweza kunufaisha vijiji hivi vilivyoko Jimbo la Manyoni Magharibi. Naomba kujua ni hatua gani za makusudi zinafanywa na Serikali kuvipatia huduma za jamii kutokana na rasilimali hizi za asili zilizoko maeneo yao? Wananchi wa maeneo haya wanashiriki katika hifadhi ya rasilimali hizi

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata majibu kutoka *TWPF* kupitia Wizara hii iko wapi ahadi ya miaka mingi sasa ya kulijenga upya Bwawa la Rungwa baada ya kuvunjwa na mafuriko? Mwaka 2007/2008, Serikali ilitenga shilingi 250,000,000 kukarabati na kulijenga Bwawa hili, lakini hadi sasa hakuna kazi yoyote iliyokwisha kufanyika kwa maelezo kwamba kunahitajika fedha zaidi ya hizo zilizotengwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ili Wananchi wa Rungwa ambako kuna Makao Makuu ya Pori la Akiba la Rungwa/Kizigo yapo. Bila bwawa hili lililokuwa linachangiwa na Wananchi na wanyama lilikuwa ndiyo kielelezo halisi cha

maisha ya Wananchi na mazingira yao. Mradi wa kisima unaojengwa na Serikali bado hautatosheleza mahitaji ya maji ya kijiji hiki muhimu. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, fidia ya maisha, mimea na mifugo bado haitoshi. Napendekeza kifuta machozi kiwe shilingi milioni tano kwa wafiwa. Kuhusu mimea na mifugo, thamani halisi ya mazao yaliyoharibiwa na thamani halisi ya soko la mfugo aliyeuawa vifikiriwe kulipwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza kwa kazi nzuri inayoendelea pamoja na mazingira magumu ya rasilimali chache za kutekeleza majukumu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kulaani yaliyojitokeza katika Ripoti ya Kambi ya Upinzani ya kumhusisha Katibu Mkuu wa CCM, Mheshimiwa Kinana na makosa mbalimbali wakijua wazi Kiongozi huyo hana nafasi ya kujitetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisisitize umuhimu wa Wizara kufanya kazi kwa karibu na Wizara nyingine ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na Wizara zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ni muhimu kwa utangazaji wa utalii kwa maana ya taarifa sahihi za maendeleo. Nashauri wafanye kazi kwa karibu na Wizara na Idara ya Maelezo na Msemaji wa Serikali ndani ya Wizara ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hasa katika hili tusaidiane, tuungane na *CCTV* China, wafungue *operation office* hapa nchini, ni *source* nzuri ya watalii. Katika hili la utangazaji lazima tufuatilie na tuhakikishe tunaungana. Pia kuwe na *Air Line* yetu *National* ndani na nje. Bado hili ni

muhimu, tusipokuwa nalo tutaendelea kuhangaika na kupishana na biashara mbalimbali za maendeleo yanayotokana na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya ulinzi shirikishi ni muhimu na kila mkoa tumepanga kufanya kazi nao kuhakikisha ulinzi shirikishi unabebwa vizuri na vijana. Nashauri Wizara yako itumie kwa karibu vikundi vya vijana kutoka sehemu zinazohusika walinde, kama ni mafunzo wapewe na vifaa pia. Hili pia litasaidia hata masuala ya ujangili. Wizara yangu inashirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kuwahamasisha vijana basi tusaidie vijana pia wafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia masuala ya utalii wa utamaduni na utalii wa michezo tufanye kwa ushirikiano wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Mchango wangu nauelekeza katika uhifadhi. Serikali isiogope kusimamia uhifadhi maliasili zote, wanyama na misitu wakiwepo nyuki, ni lazima Serikali iwe na msimamo isiyumbishwe na Wapinzani ambao wana ajenda ya siri ya kuiyumbisha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya maji muhimu katika Wilaya ya Lushoto vipo katika Misitu ya Hifadhi inayolindwa au inayosimamiwa na Serikali Kuu. Naomba Wizara isaidie katika kusimamia misitu hii kwa nguvu zaidi. Ikiwezekana misitu hii ilindwe na *TANAPA* ambao wana uwezo wa kitaalam na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iendelee kuwekeza kwenye upandaji miti isiyo ya asili katika maeneo ambayo yaliharibiwa na moto mwaka 1998 na imeonesha dalili kwamba uoto wa asili kutokana uharibifu wa mazingira

na mabadiliko ya tabia ya nchi. Naomba Wizara iongeze fedha katika upandaji miti katika Misitu ya Hifadhi Wilayani Lushoto.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kupongeza hatua zilizokwisha chukuliwa ili kukuza Sekta Ndogo ya Ufugaji. Hatua hizo ni pamoja na Maonesho Maalum ya Asili; kutoa mizinga ya kisasa na mavazi ya kinga kwa baadhi ya Wananchi; na kuzindua siku ya kutundika mizinga kila mwaka (tarehe 4 Machi, 2013).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hatua hizi zipanuliwe kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Maonyesho Maalum ya Asili yawe endelevu na yafanyike kila Wilaya.

(ii) Juhudi za kusambaza mizinga na mavazi ya kinga ziongezwe.

(iii) Siku ya kutundika Mizinga (tarehe 4 Machi, 2013) iadhimishwe katika kila Wilaya kila mwaka ili kuhamasisha utundikaji Mizinga nchini kote. Lengo la zoezi hili liwe kueneza ufugaji nyuki nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitajieleza kwenye Jimbo langu. Wenyeji wa Bukombe ni wafugaji wa nyuki toka zamani. Sisi tumezaliwa tukakuta babu zetu wakifuga nyuki. Ufugaji huo wa nyuki ulikuwa na matatizo yafuatayo; ufugaji huo ulitumia mizinga ya magome au magogo; na hakukuwepo mavazi ya kinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wananchi wa Bukombe ni wafugaji wa asili wa nyuki, naomba Serikali iwape msaada katika maeneo yafuatayo: Elimu ya kisasa ya ufugaji nyuki; mafunzo ya ufundi wa utengenezaji wa mizinga ya kisasa yaenezwe katika Tarafa au Kata zote; na mavazi ya kinga yatolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kuhusu ufugaji nyuki ni mpango mkakati wa utafiti wa ufugaji nyuki unaotajwa ukurasa wa 37 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri; mpango huu utakamilika lini?

Mwisho kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhamasisha ufugaji nyuki. Wizara izingatie ushauri wake kuwa umaskini wa kipato wa nchi yetu utapungua kabisa kama Wananchi watawezeshwa kufuga nyuki.

Sasa nitajielekeza kwenye jambo lingine, nalo ni tatizo sugu la madawati katika Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Rai yangu ni kwamba, Wizara ya Maliasili na Utalii, ikishirikiana na TAMISEMI, iandae Mpango wa kutatua tatizo la upungufu wa madawati katika shule zetu. Ni aibu kwa nchi yenye misitu mingi kama tuliyonayo kuendelea kuwa na tatizo hili. Nina imani kuwa hili linawezekana kama nia ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imebeba majukumu mazito ya kusimamia Maliasili na Utalii, mambo ambayo kwa mujibu wa tafiti za kitaalam kama yakisimamiwa kwa umakini yanaweza kuliongezea Taifa letu mapato makubwa kiasi cha kutukwamua kutokana na ufukara tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Waheshimiwa Wabunge wanaosema kwamba bila kupambana kwa umakini na changamoto zinazoikabili Sekta za Maliasili na Utalii, yaani usimamizi mbovu na hafifu, ufisadi, ujangili, utovu wa uzalendo, maendeleo katika sekta hizi yataendelea kusuasua au yatakuwa ya taratibu sana. Katika kuchangia hayo, nitajielekeza katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na suala zima la Utangazaji wa Utalii. Utalii ni biashara, haitoshi tu kuwa na vivutio vya kitalii. Lazima vivutio hivyo vitangazwe na wataalam wa matangazo ya biashara. Kwa kuwa soko

kubwa la biashara ya utalii bado liko katika nchi za nje, panahitajika mpango mkakati wa utangazaji utakaotumia mbinu za kisasa. Lazima Wizara iwekeze katika utangazaji wa kisasa na kitaalamu wa Utalii. Nchi zote zinazosifika kwa mafanikio katika Sekta ya Utalii (hata nchi jirani) zimewekeza sana katika utangazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo juhudi zinazofanywa na Wizara kutangaza Utalii. Tatizo la juhudi hizi ni kwamba, kwa kiasi kikubwa zinafanywa na watu ambao sio wataalam wa utangazaji wa utalii. Ifahamikie kwamba katika Ulimwengu wa kisasa wa utandawazi na ushindani mkali ambapo nchi mbalimbali duniani zinanyang'anyana watalii, mbinu za kisasa lazima zitumike na siyo zile za mazoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmoja wa juhudi wa Wizara kutangaza vivutio vya nchi yetu ni uanzishaji wa maonesho ya *Washington DC* yatakayofanyika kila mwaka. Maonesho hayo yanahusu vivutio vya Bonde la Olduvai na nyayo za binadamu wa kale. Hii ni hatua nzuri, lakini haitoshi kwa nini maonesho hayo yasipanuliwe ili yajumuishe vivutio vingine muhimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maonesho hayo yanafanyika *Washington DC* tu, kwa nini Serikali isipanue maonesho hayo kwa kuanzisha maonesho hayo Uingereza (London), Ulaya (Ufaransa au Ujerumani), Mashariki ya Mbali (Beijing), na kadhalika? Hakuna shaka maonesho haya yangeoneshwa sehemu mbalimbali duniani, vivutio hivyo vingefahamika zaidi na hivyo kuvutia watalii wengi kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisisitize kuwa kama Taifa, hatuna hiari katika suala la utangazaji wa Utali. Lazima tujitangaze na tujitangaze kitaalamu. Bila kujitangaza kitaalam hatuwezi kupata mafanikio mengi katika Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitajielekeza kwenye suala la kuendeleza misitu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa 20 hadi 21. Anaeleza juhudi za Wizara za

upandaji miti. Kwenye ukurasa wa 24 anataja maandalizi ya mpango mkakati wa kuboresha miti ya kupandwa katika eneo la Afrika Mashariki. Ni wazi kuwa, kwa kuzingatia maeneo makubwa yasiyo na miti nchini na kasi iliyopo ya uvunaji holela wa miti katika misitu yetu (ya Halmashauri na ya Kitaifa) juhudi zilizopo za kupanda miti hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara isisubiri mpango mkakati unaojumuisha nchi nyingine, bali Serikali ijipange ili iandae mpango mkakati usiotegemea nchi za kigeni wa kupanda miti katika maeneo yote yasiyo na miti. Mpango mkakati huu ukiandaliwa na kisha kuanza kutekelezwa kwa uhakika, maeneo yaliyo nusu jangwa yatakuwa na misitu. Hatua hii itasaidia sana pia katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitazungumzia migogoro iliyopo baina ya hifadhi ya misitu na vijiji vilivyo mpakani. Migogoro hii imeenea maeneo mengi katika nchi yetu. Hata hivyo hapa nitajielekeza kwenye eneo moja lililo kwenye mpaka wa Wilaya ya Bukombe na Wilaya ya Biharamulo mwaka 2012. Mwishoni kulikuwa na operesheni katika Mkoa wa Kagera iliyokuwa na malengo mahususi yaliyokuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, operesheni hiyo iligubikwa na uvunjifu wa haki za binadamu na udhalimu mkubwa hasa katika maeneo ya Nyamagana na Namagwangala (Wilaya ya Bukombe), Mpago na Kaniha (Wilaya ya Biharamulo). Vijiji husika ni halali kisheria, lakini wananchi walihangaishwa, wengine wakachomewa nyumba zao na mali nyingi kuharibiwa. Nashauri Wizara isahihishe dosari hii ili wananchi wa maeneo hayo waishi kwa amani.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Bodi ya Utalii kuwa na mkakati wa kutangaza Utalii 2012 – 2017; hivyo basi, katika suala zima la kutangaza utalii wadau muhimu wahusike katika zoezi hili. Kwa kuwa

mamlaka zingine zina fungu la kutangaza utalii ni vyema pawepo na ushirikiano wa karibu kati ya Mamlaka na Bodi katika suala zima la Utalii.

Tafiti zinaonesha kwa miaka mitano iliyopita, Mamlaka ya Ngorongoro imetumia zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa ajili ya safari za nje kutangaza utalii; hivyo basi, hakuna mahusiano baina ya mafanikio ya kukua kwa utalii na safari hizo za nje. Hivyo, inatia shaka kama kuna usimamizi au matumizi thabiti bila kuwepo na ufisadi. Wizara ilisimamie suala hili na kulitazama upya ili lengo halisi la kutangaza utalii lifikiwe kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ujangili limeendelea kuwa kubwa na hakuna mkakati wa dhati kujadili au kudhibiti suala hili. Hivyo, ni vyema kushirikiana na Wadau mbalimbali ili kukabiliana na tatizo la ujangili hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira katika Sekta ya Utalii hapa nchini limeachwa au kusahaulika, hivyo kuwafanya Wananchi walioajiriwa katika Sekta za Utalii kutaabika bila kuwa na stahiki sahihi za malipo, marupurupu na likizo wakiwa kazini. Hivyo, suala la ajira kulingana na hadhi ya hoteli husika ni vyema likaangaliwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumai Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira, watatatua matatizo yaliyopo katika Sekta ya Utalii.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa Hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alieleze Bunge ni lini Serikali itaondoa tozo ya asilimia kumi ya mapato ya Shirika la *TANAPA* kwa mwaka iliyowekwa 2009/2010? Kitendo cha Serikali kuweka utaratibu wa kuchota asilimia kumi za makusanyo ya Shirika hili kuingiza kwenye Mfuko wa Serikali kimedhoofisha sana Shirika hili ambalo lina jukumu kubwa la

kulinda na kuhifadhi Maliasili ya Taifa hili kwa niaba ya Serikali. Madhara yameshaanza kuonekana, ujangili unaongezeka na watendaji wanakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka mingi sasa tumeitaka Serikali kuongea na Wamiliki wa Hoteli za Kitalii ziliojengwa ndani ya Hifadhi za Taifa kuongeza *concession fees* kutokana na kile wanachokipata. Kwa nini leo bado kitanda kimoja kinalipiwa dola 8 – 10 fedha ambayo ilitolewa miaka kumi iliyopita wakati ililipa US dola 50 – 100 *prr day?* Leo kitanda kimoja kinalipiwa dola 500 – 1000 lakini *concession fee* bado haijapanda. Hawa wamiliki wana jeuri gani ya kukataa kulipa dola 25 – 30 iliyopangwa na *TANAPA?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa tumeunda Mamlaka ya Misitu Tanzania, bado misitu yetu iko hatarini sana kuteketea. Serikali imepiga marufuku kusafirisha magogo na mkaa wa miti ya asili tangu mwaka 2010/2011 baada ya vitendo vya ukataji magogo kuongezeka kwa kasi na kutishia uhai wa misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado magogo yanasafirishwa, mbao zinasafirishwa kwa kasi kubwa sana na misitu ya asili itabaki vichaka. Ni lini Serikali iliondoa zuio hilo; na ni utaratibu gani sasa mbadala umewekwa kudhibiti ukataji na usafirishaji wa magogo na mbao hapa chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ni lini itaanza matumizi ya makaa wa mawe kama nishati mbadala ili kuokoa misitu kutokana na uchomaji wa mikaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaacha lini kuweka siasa kwenye masuala ya msingi yanayogusa uhai wa Taifa hili? Kila siku tunaongea hapa mamilioni ya magunia ya mkaa yanasafirishwa mchana na usiku kwa ajili ya matumizi ya majumbani, Serikali inaona imetulia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeacha jukumu la kusimamia Mmaeneo ya Hifadhi za Jamii *(WMA)* kwa Wananchi wenyewe hasa suala la ulinzi. Huko nyuma Idara

ya Wanyamapori walikuwa na utaratibu wa kufanya doria kwenye maeneo ya WMA kila mwezi. Leo hakuna doria zile matokeo yake majangili wanajitanua kwenye hifadhi hizo. Rasilimali iliyotunzwa na kulindwa na Wananchi kwa miaka mingi inateketea, inaporwa na majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wa Vijiji *(VGS)* hawana uwezo wa kutosha kufanya doria za nguvu bila msaada wa Vikosi vya Kudhibiti Ujangili vya Idara ya Wanyamapori. Serikali ieleze ni utaratibu gani umewekwa kuona hifadhi hizi zinakuwa endelevu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Loliondo lisishughulikiwe kisiasa! Lile ni suala la kitaalam na kiutendaji. Kwa nini Serikali ilituma wanasiasa kushughulikia suala la Loliondo wakati wanasiasa hao hawana uelewa wowote wa Hifadhi ya Loliondo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imekosa mwelekeo; haiwezekani Waziri afanye maamuzi ya kitaalam kwa kushirikisha Wataalam wake halafu anakuja Katibu Mwenezi wa Chama anamkosoa hadharani! Hatuwezi kufika kwa mwendo huu. Nina wasiwasi kama hatatakiwa na utaratibu wa kuheshimu maeneo yaliyotengwa kwa hifadhi tangu huko nyuma nchi hii itakuwa jangwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilieleze Bunge ni nini hatma ya Wananchi wanaoishi Tarafa ya Ulyankuru, Wilaya ya Urambo, Kata za Kashishi, Uyowa, Sasu na Soleli, ambao wamekuwa wanasumbuliwa kila kukicha kwamba wapo hifadhini, wanashindwa kutulia na kufanya kazi zao za maendeleo, vijiji vyote viko kisheria na kuna mashule, vituo vya afya, masoko na kadhalika? Kwa nini wanansumbuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Kata ya Ujumbu, kilometa 90 na Vijiji vya Kombe, Shela, Maboha, Kata ya Usinge, nao wamekuwa wanasumbuliwa na hata kuchomewa nyumba zao eti wako hifadhini. Serikali itoe msimamo wake juu ya maeneo hayo.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la mipaka ya Wenyeji wa Vijiji na Hifadhi za Taifa. Suala hili limeathiri sana Wananchi kutoka pande zote nchini hasa vijijini. Bila Serikali kuchukua hatua za haraka, migogoro hii haitakwisha. Ni wazi hofu ya kutokea *internal conflicts* baina ya Askari wa Hifadhi na Wananchi vijijini inaweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo kama kupigwa risasi mifugo ya wafugaji kama ng'ombe na wenyeji wa vijiji kuchomewa nyumba na mali zao zote zikiwemo pesa kuchukuliwa na Askari Polisi na hakuna hatua yoyote ambayo Serikali inachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano dhahiri ni Kijiji cha Mapili kilichopo Tarafa ya Inyonga, Mkoani Katavi, ambacho Wananchi wapatao 250 hivi walichomewa nyumba na mali zao zote ikiwemo kuchukuliwa pesa zao na kuondoka mahali hapo katika Kijiji cha Mapili na kila mmoja kwenda hovyo popote kutafuta kuanzisha maisha mapya bila maelekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kuwa inawanyanyasa Wananchi na kuwafanya watangetange kama wakimbizi ndani ya nchi yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha anieleze Wananchi waliofukuzwa katika Kijiji cha Mapili Songambele, kilichopo Tarafa ya Inyonga Mpanda, walichomewa nyumba zao baada ya kuambiwa wahame katika eneo hilo na kwamba ni eneo la Hifadhi. Serikali imewapa eneo gani la kuishi; na nini hatma ya mali zao zilizoteketezwa? Kumchomea Mwananchi mali zake ni kumwendeleza au kumuua kabisa? Naomba Waziri anipe majibu ya ufafanuzi kama Serikali ilichukua jukumu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Katavi ni ya muda mrefu sana na ina wanyama wenye historia, kwani ina wanyama wakubwa na wanaopendeza kuwatazama,

ukubwa wake huwezi kuwafananisha na wanyama wa Hifadhi yoyote nchini, lakini *population* ya Watalii imekuwa ndogo katika Hifadhi hii ya Katavi kutokana na miundombinu mibovu ya barabara, pia uwanja wa ndege wa Hifadhi kujaa miti uliopo maeneo ya Kanyamkaa.

Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha inaitangaza Hifadhi hii muhimu ya Katavi na kutenga fedha kwa ajili ya kuiboresha Hifadhi hiyo ambayo hata majengo yake ya kufikia Watalii yamechakaa sana? Serikali itoe tamko ni lini itatangaza Hifadhi hii kama ilivyo kwa Hifadhi ya Manyara, Mikumi na Selous?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu na Wataalamu wa Wizara, kwa kuwasilisha Hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini. Pamoja na pongezi hizo, napenda kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejiwekea utaratibu wa kuwashirikisha Wananchi wanaozunguka Hifadhi katika Ulinzi Shirikishi na kuwawezesha Wananchi hao kunufaika na rasilimali hizo. Kwa bahati mbaya, katika Wilaya ya Kilolo, Kata za Mahenge na Ruaha – Mbuyuni, zinazoizunguka *Udzungwa National Park* na Milima ya Tao ya Mashariki, wakati Kata za Image na Ibovu zinashiriki Ulinzi Shirikishi wa Misitu ya Hifadhi ya Milima Serebu; lakini Wananchi hawa hawajanufaika na ushiriki wao! Je, Serikali itakuwa tayari kuona Wananchi hawa kama ilivyo sehemu nyingine wananufaika na rasilimali hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kilolo, kwenye Kijiji cha Lugabo, kuna eneo la Historia, mahali alipozikwa Jemedali wa Jeshi la Ujerumani aliyeuwawa na Majeshi ya Chifu Mkwawa wakati wa mapigano ya kupinga Ukoloni. Kaburi kubwa, refu, limejengwa hapo kama kumbukumbu na Wajerumani huja kutembelea eneo hilo la

Kihistoria. Jambo la kusikitisha ni kwamba, eneo hili halitunzwi na linapoteza umuhimu wake. Naomba Wizara iangalie namna ya kulitunza eneo hili ili libakie kuwa kivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwamba ipite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninashauri Serikali ifanye juu chini kuhakikisha rasilimali za nchi hii zinalindwa kwa manufaa ya watu wote. Nchi hii kwa sasa inakabiliwa na changamoto kubwa sana hasa kutokana na ongezeko la ujangili na uharibifu wa mazingira. Wanyama wanauwawa bila huruma kwa sababu ya tamaa ya kundi la baadhi ya Watanzania wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wanafanya shughuli la ujangili kuwa Janga la Kitaifa na kwa maana hiyo zinahitajika nguvu za ziada kukabiliana na ujangili kwani upo mtandao wa kihalifu wa matendo ya kijinai (*Organized Crimes*) na makundi haya yanaungwa mkono na majangili wenzao waliosambaa Dunia nzima na hususan Mashariki ya Mbali. Ni jukumu la Serikali sasa kuungana wa Mataifa mengine Duniani ili kupambana na uhalifu wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalifu mwingine ni uharibifu wa mazingira kwa njia mbalimbali kama ukataji miti kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile kukata miti ili kupata kuni, kuchoma mkaa, kupasua mbao, kuchoma moto misitu, kuvamia misitu na kujenga makazi na kuanzisha kilimo na hivyo kuendelea kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo upungufu mkubwa wa Watumishi na Walinzi, kwa maana ya *game rangers;* hali inayopelekea wanyama kuwa katika hatari ya kushambuliwa na majangili bila kupata upinzani kutoka kwa walinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pori la Akiba la Kigosi ambalo lipo katika Wilaya za Kahama, Bukombe na Mbogwe,

linakabiliwa na matatizo makubwa kutokana na ukubwa wa eneo la kilomita za mraba elfu tisa. Pamoja na ukubwa huu kuna watumishi thelathini tu! Hali hii ni hatari kwa hatma ya Pori hili la Akiba la Kigosi. Ni rai yangu kwa Wizara kuongeza fedha na kuwekeza katika miundombinu ya barabara na *Game Rangers Posts* ndani ya Pori la Akiba la Kigosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigosi imesahaulika, naomba Wizara izinduke na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupambana na ujangili. Pori la Akiba Kigosi liko katika hali mbaya sana, kinachogomba hapa ni hali mbaya ya miundombinu ndani ya pori hili ambayo ni duni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ichukue hatua madhubuti kuhakikisha barabara ndani ya pori hili inaimarishwa. Kuimarishwa kwa miundombinu ya barabara kutarahisisha upitaji wa magari ya doria hata vifaa mbalimbali vinavyohusiana na masuala ya uhifadhi wa wanyama, zikiwemo shughuli za utalii na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uhifadhi zinafanywa na Askari wa wanyamapori, lakini kwa bahati mbaya hakuna *Game Rangers Posts* zinazoweza kutumiwa na Askari wa Wanyamapori katika kuhakikisha ulinzi unaoweza kuzuia madhara kwa wanyama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ujangili katika Pori la Akiba la Kigosi ni kansa inayolikabili pori hili. Wanyama wanahujumiwa sana na majangili toka ndani na nje ya nchi. Kuwepo kwa Makambi ya Wakimbizi katika Mikoa ya jirani na pori hili kunachangia kwa kiasi kikubwa katika kukubuhu kwa vitendo vya ujangili ndani ya pori hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakimbizi toka nchi ya Burundi na Demokrasia ya nchi ya Congo wamekuwa wakiingiza nchini silaha za kivita zinazotumika katika ujangili ndani ya Pori la Akiba Kigosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa watumishi hasa Askari wa Wanyamapori ni changamoto ambayo

isipochukuliwa hatua wanyama wetu wataendelea kuuawa kwa kasi ya ajabu. Naiomba Wizara ya Maliasili na Utalii iliangalie eneo la Pori la Akiba la Kigosi kwa jicho la pekee. Wanyama Kigosi wanakimbia na kuuawa hovyo! Kigosi sharti iimarishwe na kuwa chanzo cha uvutiaji wa watalii kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji madini au utafiti hauruhusiwi kwa mujibu wa sheria, kwa nini utafiti wa madini ya shaba unafanywa kwenye Pori la Akiba la Kigosi. Naomba Mheshimiwa Waziri anijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa katika Kijiji cha Nsango bado halijakamilika. Ahadi ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya kutoa shilingi milioni 75 haijakamilika kwani ni shilingi milioni 25 pekee ndiyo iliyotolewa. Hivyo basi, milioni 50 bado inahitajika kukamilisha Bwawa hili ili wafugaji wasiendelee kupeleka mifugo yao ndani ya Pori la Akiba la Kigosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Taifa cha Utalii, kinapewa bajeti ndogo sana. Inategemewa Chuo kingepewa fungu la kutoka tozo la *Skilled Development Levy (SDC)*, ambapo kila mwajiri analipa asilimia 60 wakiwepo waajiri waliopo katika Sekta ya Utalii, lakini fedha hizi zinaenda *Higher Leaning Loan Board – Skills* za kuendesha utalii hazipatikani katika Vyuo vya Elimu ya Juu bali katika Chuo hiki.

Nashauri *Campus* za Arusha na Temeke zitoe mafunzo yanayofanana; na ili ziweze kufanya hivyo, *Campus* hizi zipate Bajeti ya kutosha. Kwa kuwa Chuo kina upungufu wa walimu, Serikali iingie mkataba na Taasisi za Nje ili kuendesha Chuo kama ilivyofanya Rwanda na Serikali ya Netherland.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iongeze bajeti ya Rasilimali Watu wa Wizara hasa Kitengo cha Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa na *Marketing Strategy* inatakiwa nchi iwe na Mkakati wa Maendeleo ya Utalii *(Tourism Development Strategy),* kwa ajili ya vivutio maalum kwa muda maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoka ghasia ya wanyama waharibifu wa mazao ya Wananchi na maisha ya watu, napendekeza kwamba, Hifadhi za Taifa *(TANAPA)*, iweke uzio *(Fence)* katika maeneo ambayo wanyama hao wanaingilia mashamba ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za *TANAPA* za ujirani mwema, suala la Wananchi wanaopakana na Hifadhi wapate sehemu ya malisho. Kuwe na mipaka ya wazi, *buffer zones.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wa Hifadhi wawathamini binadamu, wasiwe *brutal.* Kwa kutumia ujirani mwema, migogoro mingi itaepukika. Mapambano baina ya Jamii na *Rangers* wa *TANAPA* haitatupatia mafanikio yoyote.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hoja hii ya Maliasili na Utalii, sababu ni roho ya mali ya asili yetu, ni muhimu sana kwetu na vizazi vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujangili umekuwa mkubwa sana na unatishia amani ya wanyama hapa nchini, kama faru, tembo, twiga na kadhalika. Hivyo basi, hatuna budi kupingana na ujangili kufa na kupona. Hivi tuulizane ni nani anayewauwa tembo na kuchukua pembe, akasafirisha nje ya nchi yetu? Je, anapita bandari gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasoma kwenye vyombo vya habari, tunaona jinsi gani magari hayo yanabeba pembe za ndovu na meno ya tembo. Magari hayo ni ya Jeshi, kama ambalo lilipata ajali hapa Dodoma. Mengine ni ya Afisa Usalama. Kama hiyo haitoshi, yanapita bandarini kwetu na kuelekea Nchi za Mashariki ya Mbali ambako siyo rahisi raia wa kawaida akafanya biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema sasa kesi za ujangili zikifishwa Mahakamani, hukumu zitolewe. Kwa kuwa tayari vidhibiti au ushahidi ni meno au pembe, basi hakuna haja ya kucheleweshwa kwa kesi hizo, labda itasaidia. Pia ni vyema sasa Bandarini pakawa na *T-SCAN* ambayo inacheki makontena ambayo yanatoka ili kutambua nini ambacho kinatoka kama yanavyochekiwa yanayoingia ndani ya nchi. Ni aibu kila siku kusikia pembe na meno ya ndovu yanakutwa Nchi za Magharibi na yanatoka hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna magogo yalikamatwa China na yalipita Bandari ya Dar es Salaam kwa nembo ya chupa za maji; hivi ni lini tutaondokana na aibu hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Waziri atakapokuja kujibu anifahamishe ni lini Wizara hii itapeleka wanyama kama simba na wengineo katika Hifadhi ya Kisiwa cha Saanane pale Jiji la Mwanza ili kuongeza vivutio, kwani kama utaongeza vivutio ni ukweli usiopingika hata hoteli nazo zitapata biashara, kwani Watalii wa ndani wanalala majumbani, lakini Watalii wa nje wanalala hotelini, hivyo hata wafanyabiashara hao watapata biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo zamani kabla Kisiwa cha Saanane hakijapoteza umaarufu, wanafunzi wengi walikuwa wanakwenda kujifuza katika Kisiwa hicho. Siku za mapumziko wakazi wa Mwanza walikuwa wanakwenda kupumzika huko. Ni muhimu wanyama wakaongezwa ili kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Hotuba ya Waziri wa Wizara hii. Kwanza, kwa kuunga mkono hoja, nikitegemea yafuatayo yatazingatiwa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi yana migogoro katika ya vijiji na maeneo ya *TANAPA.* Kwenye Jimbo langu la Njombe Magharibi, nina tatizo na mpaka wa

*Mpanga Game Reserve* na vijiji hivyo ni Mambegu, Mpanga, Malangali, Ludingu, Igambo na Iyayi. Mara kwa mara Wananchi wamekuwa wanakamatwa bila sababu za msingi. Serikali iliweka mpaka na ikawahamisha Wananchi wa Mpanga, lakini yako malalamiko kuhusu namna fidia hiyo ilivyotolewa, wako watu hawajalipwa na wengine walilipwa. Isitoshe, mipaka hiyo baada ya zaidi ya miaka kumi toka wahamishwe, ilipita timu ya kutengeneza mpaka mpya. Huu mpaka uliorekebishwa, unaingia kuvimega vijiji hivi. Sasa hivi watu wameongezeka sana na ardhi waliyoachiwa imepungua haitoshi. Iko haja ya kutafuta maeneo haya ili Wananchi wasiwe wakimbizi kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni vizuri iweke mahusiano mazuri na Wananchi ili wawe sehemu ya ulinzi kwa kuzima moto na kuzuia au kutoa taarifa kwa majangili ili rasilimali hizi ziwe kwa manufaa ya Taifa.

**MHE. CHARLES H. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia njia ya maadishi, nichangie Bajeti ya Wizara ya Maliasili. Wizara hii ni muhimu kwa maendeleo na ustawi wa Taifa letu. Rasilimali zote ambazo Wizara imepewa dhamana ya kuzilinda, zikitoweka Tanzania haitokuwa Tanzania tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili, inakabiliwa na tatizo la majangili yanayoendesha shughuli za uwindaji haramu. Pendekezo langu ni kuitaka Serikali kwa ujumla wake, pamoja na njia nyinginezo za kudhibiti ujangili, waweke udhibiti mkali kwenye malango ya kuondokea. Kutokuwepo kwa *scanners* na Watendeji wa Wizara Bandarini na Viwanja vya Ndege, ni upungufu unaochochea ongezeko la ujangili. Serikali ikiwezekana siyo suala la kutowezekana, hili ni jambo la haraka na dharura; wakati umefika sasa mizigo yote inayoingia na kutoka ndani ni lazima iwe *scanned.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la maeneo ya Hifadhi na ardhi yote iliyoko chini ya Wizara hii, kwa sababu moja au nyinginezo uzembe umefanyika, Wananchi wakaingia na kuendesha makazi katika maeneo tajwa. Yapo maeneo ambayo Wananchi wameendesha shughuli zaidi ya

miaka kumi. Ushauri wangu ni kuwa, mipaka kwa kuzingatia wavamizi, iainishwe upya na kurasimishwa mipaka na eneo la wazi viwekwe wazi ili Wananchi wasiingie kwenye Hifadhi na kwa upande wa Serikali isije ikatokea kudai vijiji ni mali au sehemu ya Hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takriban asilimia 28 ya ardhi yote iko chini ya Hifadhi. Serikali itafakari ongezeko la watu na kumega sehemu kwa ajili ya shughuli za kibinadamu. Sehemu ya Hifadhi itakayobaki tuendeshe uhifadhi ya maliasili kisasa zaidi. Siyo busara kuwa na sehemu kubwa ya Mbuga ambayo miti imefyekwa, wanyama wametoweka na mazingira yameharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wa kuangalia maeneo upya, napendekeza na kuomba maeneo yanayopakana na Wilaya ya Muleba, eneo litengwe kwa ajili ya wafugaji. Wilaya ya Muleba, Kata za Rutoro na Ngege, zimekuwa na mgogoro na Ranchi za Taifa – *NARCO.* Kutoka katika Misitu na maeneo ya Hifadhi, *NARCO* ipewe eneo ili kupeleka wapangaji wake. Hali hii na uamuzi huu utawaacha huru Wananchi wa Kata tajwa hapo juu kuendeleza kazi zao za kujipatia riziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la mfumo wa malipo katika shughuli za utalii. Waendeshaji wa shughuli za utalii wanao utaratibu wa kuwataka wateja wao kulipa tozo zote ughaibuni. Watalii hapa huja mikono mifukoni ilhali fedha nyingi wameshalipa huko watokako. Ushauri wangu ni kuwa, uandaliwe utaratibu ambapo wanaoendesha shughuli watalazimika kuweka chumo lao katika fedha za kigeni katika benki za nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia Hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma tuna idadi ndogo sana ya Watalii, ukilinganisha na Mikoa mingine yenye

Mbuga mbalimbali, licha ya kuwa na Mbuga ya Gombe na Mahale, lakini uhaba wa usafiri kutoka maeneo mengine ya nchi kuja Mkoani Kigoma. Je, kwa nini *TANAPA* isiwe na ndege zao za kutosha ili kusafirisha Watalii kuelekea Kigoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makumbusho ya Mji wa Ujiji na *Livingstone Memorial* ni maeneo ambayo hayajulikani kwa kiasi kikubwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuyatangaza maeneo haya na kutusaidia kukuza uchumi wa maeneo husika ambayo ni Miji Mikongwe kama Kigoma Ujiji, Bagamoyo, Mtwara Mikindani, Kilwa na kadhalika?

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niseme kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyochangia kwa kusema juu ya matatizo ya vitendea kazi kwa watumishi wa sekta hii waliopo Nanyumbu, narudia kumwomba Mheshimiwa Waziri atupatie gari kwa ajili ya Idara ya Maliasili Wilayani Nanyumbu. Namwomba Waziri atamke waziwazi majibu juu ya ombi langu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri awajulishe wananchi wa Nanyumbu hasa wa Chimika na wa Masuguru, ni lini Wizara itapeleka fedha, Shilingi milioni 12 alizoahidi Mheshimiwa Waziri aliyetangulia (Mheshimiwa Ezekiel Maige) alipotembelea Wilayani Nanyumbu, ahadi ambayo haijatekelezwa hadi leo? Fedha hizi ni kwa ajili ya kuchimba visima viwili. Kimoja ni kwa ajili ya Kijiji cha Chimika na kingine kwa ajili ya Kijiji cha Masuguru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri awaambie wafanyabiashara wa mbao za kutoka Msumbiji ni jinsi gani atatatua matatizo yao kutokana na manyanyaso na dhuluma wanayofanyiwa na Afisa Huduma za Misitu Kanda ya Kusini? Hii inatokana na barua waliyomwandikia Waziri.

**MHE. REBECCA M. MNGODO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Kampuni ya *Ortello Business Corporation* kufanya shughuli za uwindaji katika eneo la Loliondo na hatuna uhakika kama wana kibali halali, bado kuna Makampuni mengine yanayojishughulisha na utalii wa picha katika eneo la Loliondo bila kibali cha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya Kampuni ni *Klein's Camp.* Kampuni hii imemilikishwa kiasi cha ekari 25,000 za Kijiji cha Ololosokwan kinyume cha sheria na wanakijiji. Aidha, Kampuni hii ina kiwanja cha ndege ambapo husemekana huingiza watalii nchini bila utaratibu uliowekwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifuatilie jambo hilo, kwani ni hatari sana kama watalii wanaingia nchini bila utaratibu uliowekwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa Kiwanja cha Ndege cha Kampuni binafsi, inawezekana kabisa wanyamapori wadogo wadogo wakaibiwa na kusafirishwa nje ya Tanzania kwa kukosa udhibiti imara wa Kiwanja cha Ndege kilichomo ndani ya Hifadhi ya Wanyamapori. Pia tunapoteza fedha nyingi za kigeni kwa watalii kuingia bila utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2013 watalii wa Kimataifa walioingia katika Hifadhi za Taifa walikuwa 750,797 na fedha iliyokusanywa ilikuwa Sh. 105,139,608,440/= zilikusanywa. Pamoja na hayo, watalii walioingia katika Hifadhi ya Ngorongoro hadi kufikia mwezi Machi, 2013 walikuwa watalii 507,984 na fedha iliyokusanywa ilikuwa Shilingi bilioni 47.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi hiyo ya watalii ni ndogo sana ukilinganisha na wingi na mvuto wa Wanyamapori wetu ambao kimsingi tungeweza kupata watalii wengi zaidi endapo tungeweza kutumia fedha nyingi kujitangaza na hivyo kupata pato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, machache naomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango ufuatao kuhusu utekelezaji kwa mwaka 2013/2013 na mpango wa bajeti wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kuhusu sekta ndogo ya wanyamapori, naomba mrejesho, hatua zilizochukuliwa katika Pori la Akiba la Pande *(Pande Forest Reserve)* katika Manispaa ya Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita, nilipendekeza Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania kufanya utafiti, kuweza kuongeza wanyama katika Pori la Akiba la Pande. Naomba maelezo ya hatua zilizochukuliwa mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ndogo ya Utalii mwaka 2012 kwa nyakati mbalimbali, Wizara ya Maliasili na Utalii iliniahidi kuboresha Pori la Akiba la Pande *(Pande Forest Reserve)* kuwa kivutio cha Utalii Jijini Dar es Salaam kama ilivyo kwa *Nairobi Animal Park.* Wizara ilieleza ingechukua hatua hiyo kwa kushirikiana na Bodi ya Taifa ya Utalii *(TTB),* hivyo naomba kujulishwa mchakato huo umefikia wapi na mipango gani itatekelezwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati na mpango wa Utalii Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki wakati wa mjadala wa bajeti ya mwaka 2012/2013, nilishauri Idara ya Misitu, Wakala wa Huduma za Misitu na Wakala wa Mbegu za Miti kushirikiana katika kuboresha Msitu wa Pande kwa kuongeza kiwango cha miti na pia kuboresha mfumo mzima, kuepusha pori hilo kuendelea kuwa eneo la mateso na mauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ndogo ya mambo ya kale, Wizara ya Maliasili na Utalii iboreshe mfumo wa Utendaji wa Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania ikiwemo kuhakikisha uteuzi wa Bodi unakamilishwa. Kwa

upande wa utaratibu, utawala na maendeleo ya watu katika mwaka wa fedha 2012/2013, niliomba kupatiwa nakala ya mkakati wa mpango ulioandaliwa kuhusu utalii katika Jiji la Dar es Salaam, lakini mpaka sasa sijapatiwa nakala ya nyaraka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mwaka 2011 na 2012 nilihoji kuhusu kiwanda cha *Tembo Chipboards* kilichopo Mkumbara Mkoani Tanga. Kiwanda hiki kilikuwa chini ya Maliasili na kubinafsishwa kwa raia wa kutoka Uholanzi. Ni hatua gani ambazo Wizara imechukua mpaka hivi sasa kuhakikisha kiwanda hicho kinarejea katika hali ya kawaida ya kufanya uzalishaji na nini hatua ya waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hicho?

**MHE. STEPHEN M. WASIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba Wizara ichukue hatua kwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo lote la Bunda linapakana na *Grumet Game Research*. *Game Reserve* hii pamoja na *Ikorongo Game Reserve* ni kitalu kimoja ambacho uwindaji katika eneo hili unasimamiwa na Kampuni ya *VIP* inayomilikiwa na *Tudor Johns* wa Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo makubwa wanayopata wananchi wa Bunda yanatokana na ujirani wetu na hifadhi ni kama ifuatavyo:-

(1) Hakuna manufaa yoyote ya kimaendeleo yanayopatikana ukilinganisha na huduma inayotolewa kwa Wilaya ya Serengeti. Wanachoambulia wananchi ni malipo ya Sh. 1,800,000/= kwa mwaka ambazo licha ya kuchelewa malipo, kiwango hicho miaka nenda miaka rudi.

(2) Wananchi wanaopatikana na hifadhi, wanapata huduma za maji ya mifugo yao katika Mto wa Rubana ambao ndiyo mpaka wa *Game Reserve* kwa kukosa chanzo cha maji ya mifugo yao, hawana namna ila kwenda kunywesha mifugo yao Mto Rubana. Wanapofika Rubana

na kwa kuzingatia kuwa ng'ombe hawana akili ya kujua mpaka, huvuka mpaka na kuingia upande wa hifadhi wenye mifugo, wakivuka hukamatwa kunyanyaswa na kutozwa fidia ya malaki hadi Shilingi milioni faini bila risiti.

Mbali ya kunyanyaswa, tembo wamekuwa wakiharibu mazao yao, lakini madai yakifikishwa Wizarani, hawalipwi hali ambayo inaleta mfarakano baina ya Serikali na wananchi. Wananchi lazima walipwe haki zao, vinginevyo ni ndoto kwa wananchi kushiriki katika ulinzi wa hifadhi.

(3) Wananchi wanaoishi katika eneo la *Speke Gulf* wanapakana na *Serengeti National Parks* bila mafanikio. Ni jambo lisiloeleweka kusikia kauli kwamba wananchi wanaoishi katika eneo la *Speke Gulf* eti ni wahamiaji! Swali; ikiwa watu hao ni wahamiaji, wenyeji wa hapo ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:-

(1) Bunda hatufaidiki na uwekezaji wa *VIP,* hivyo tunaomba Kitalu kigawiwe ili eneo linalopakana na Bunda apatikane Mwekezaji mwingine. Sisi wa Bunda tuko tayari kutafuta mwekezaji mwingine wa kushirikiana naye.

(2) Wizara ikomeshe unyanyasaji unaoendelea wa kupiga faini feki wanapokwenda kunywesha maji Mto Rubana.

(3) Grumet/Tanapa/Wizara wachimbe mabwawa katika eneo la Hanyari na Nyamatoka ili wafugaji wapunguze safari za kwenda Mto Rubana.

(4) Madai ya fidia kwa wananchi ambayo yako Wizarani kwa zaidi ya miaka mitatu walipwe mapema iwezekanavyo. Wananchi wa Nyatwali panapoitwa *Speke Gulf* wasibugudhiwe na badala yake *TANAPA* ishiriki katika kuwasaidia kupata huduma ukiwemo umeme kutokana na *Transformer* iliyo karibu na Kijiji cha Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa eneo la Grumet iwekwe *Buffer Zone* ili kuondoa unyanyasaji kutokana na wananchi kufuatia maji Mto Rubana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, kero ni nyingi, labda nimwalike Waziri kutembelea eneo la hifadhi linalopakana na Jimbo la Bunda ili kuwasikiliza wananchi na kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Bunda nikiwemo mimi Mbunge wa Bunda.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ishughulikie kero zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mamba wengi sana kandokandao ya miamba ya Ziwa Victoria Jimboni Mwibana hususan vijiji vya Kata ya Kisorya, Kata ya Nampindi, Kata ya Igundu, Kata ya Iramba, Kata ya Neruma, na Kata ya Namsimo. Wananchi wengi wameuawa na mamba hawa. Naomba Wizara ichukue hatua za kuwavuna mamba hawa, kwani uwepo wao kwetu ni maafa na siyo uhai.

Kuna viboko wengi sana kandokando ya mialo ya Ziwa Victoria Jimboni kuzunguka eneo lote la Jimbo ambao wanaua watu hasa wavuvi na kuharibu mazao na hivyo kusababisha balaa la njaa Jimboni. Nashauri hatua za kuwavuna viboko hawa zichukuliwe, kwani nimepiga kelele sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada ya utalii wa ndani imepandishwa kutoka Sh. 1,500/= kwa mtu mzima mmoja hadi Sh. 10,000/=. Kutokana na kiwango cha umasikini miongoni mwa Watanzania ambao wanaishi chini ya dola moja, nashauri ada ipandishwe hadi Sh. 3,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitendo vya unyanyasaji vinavyofanywa na Askari wa Kampuni ya Gurumeti, Ikorongo kwa kuwapiga wafugaji na kuua mifugo yao pindi wanapowakamata pembeni ya hifadhi ya Serengeti. Juzi ng'ombe 150 wa Kijiji cha Mariwanda Kata ya

Hunyovi Wilaya ya Bunda wametoswa Mto Rubana na kuchukuliwa na mafuriko. Suala hili limeripotiwa Kituo cha Polisi Bunda.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja. Mchango wangu katika hoja hii ni tatizo la wananchi wanaishi maeneo yanayozunguka Selou kunyimwa haki ya kuvua samaki walioko kwenye bwawa lililopo ndani ya hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je! Serikali ina mpango wa kuweka utaratibu wa kuruhusu wananchi wa vijiji jirani katika Wilaya ya Rufiji waweze kuruhusiwa kuvua japo wiki mara moja chini ya usimamizi wa uongozi husika. Hii itawapa fursa wananchi hao kupata mahitaji ya kitoweo na pia kupunguza samaki wanaozaliana ili kutoa nafasi kwa samaki hao kuendelea kuzaliana kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misitu; ili kupunguza uvunaji miti na ukataji miti kwa baadhi ya maeneo, nako pia kuwe na utaratibu ambao kwa baadhi ya maeneo unafanyika kwamba wananchi waruhusiwe kuokota kuni kwa ajili ya matumizi ya kifamilia na biashara. Hii itasaidia uharibifu wa misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri apange utaratibu ili tuende akaone hali ya Bwawa la Selou na kuweza kutoa uamuzi. Hili linawezekana na litaondoa kero kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu. Naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, Naibu Waziri Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ni muhimu sana kwa Taifa letu, ukizingatia kwamba nchi yetu ina maliasili ya kutosha kabisa. Tukiwekeza fedha za kutosha, ninao uhakika wa kuvuna mavuno ya kutosha. Naomba tuwekeze katika kujitangaza ndani na nje ya nchi. Hii itaongeza mapato kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo linasumbua sana wananchi ni suala la mipaka ya misitu. Kila mwaka huwa inafanyika *operation* ya kuchoma nyumba za wananchi. Hali hii haikubaliki kabisa. *Operations* hizi zimefanyika katika Wilaya ya Geita katika Vijiji vinavyozunguka msitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo Vijiji vyenye hati ya kuandikishwa chini ya Sheria Na. 7 ya 1982. Mfano, Kijiji cha Salagulwa kilichopo Kata ya Chigunga Wilaya ya Geita kimesajiliwa kwa No. M2/KIJ/715. Pamoja na kusajiliwa, bado kila mwaka wananchi wanasumbuliwa sana na Idara ya Maliasili kutaka kuwachomea wananchi nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara na Serikali itoe ufafanuzi wa changamoto hii ya mipaka hasa kwa vijiji vilivyosajiliwa ikiwemo Kijiji cha Saragulwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja hii. hata hivyo, ninazo hoja zifuatazo zinazohitaji kufanyiwa kazi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipaka ya *Forest Reserve* (Kihesi na Kizigo) ilirekebishwa mwaka 1995 kwa kuongeza eneo la hifadhi ya misitu. Hivi sasa 58% ya eneo la Wilaya ya Manyoni ni *Forest Reserves.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, baada ya miaka kumi, idadi ya nchi imeongezeka na ardhi imekuwa taabu; hivyo wananchi wa Vijiji vya Mpapa (Kata ya Iseke) Chisinjisa na Imale mpaka (Kata ya Sasilo) wameleta ombi Serikalini

kwamba mpaka wa *Forest Reserve* hizo urekebishwe urudi ulivyokuwa mwaka 1995 ili lipatikana eneo la nyongeza kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha ombi hili ili Wizara ije ikague eneo hilo kwa lengo la kulifanyia kazi ombi lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Urasimu wa malipo ya kifuta jasho na machozi; kutokana na eneo kubwa la hifadhi ya misitu na wingi wa wanyama, lipo tatizo kubwa la wananchi kushambuliwa mara kwa mara na wanyamapori, hivyo kupoteza mwisho au kuharibiwa mazao. Matukio haya yakitokea, wananchi walioathirika huchukua muda mrefu kulipwa kifuta jasho au machozi na wengine hawalipwi kabisa. Upo urasimu mkubwa katika utekelezaji wa suala hili. Naomba Wizara iingilie kati kuondoa urasimu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uanzishaji wa *Wildlife Management Areas (WMAs)* katika mbuga ya Manyoni, kuna vijiji takribani 29 vinavyopakana na hifadhi ya misitu ya Rungwa, Mhesi na Kizigo ambamo kuna vitalu vya uwindaji. Wanavijiji katika Vijiji hivyo ndio walinzi wa kwanza wa hifadhi hizo. Lakini utaratibu wa kuanzisha *WMAs* bado haupo Wilayani. Naomba wataalam wa Wizara waje watoe elimu kuhusu namna ya kuanzisha *WMAs* katika Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji nyuki, shughuli ya ufugaji nyuki ni moja ya fursa za kiuchumi katika Mbuga ya Manyoni. Vijiji vingi vimetenga maeneo ya misitu ya ufugaji nyuki na wananchi wengi tayari wametundika mizinga. Changamoto zilizopo ni bei kubwa ya mizinga ya kisasa, hakuna soko la uhakika na uchache wa viwanda vidogo vya kuchakata asali, kuiweka katika vifungashio pamoja na jitihada za Halmashauri za kuinua ufugaji nyuk,i naomba Wizara ituunge mkono katika kutafuta ufumbuzi, ni changamoto zinazoikabili sekta hii ya misitu na nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi ina Pori la Hifadhi ya Wanyama ya Lwanfi ambayo wananchi kwa hiari yao walilitoa pori hilo kwa *TANAPA* kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Changamoto kubwa iliyosababisha hali hiyo ni Halmashauri kukosa nyenzo za ulinzi wa maliasili zilizomo kwenye pori hilo wakimemo wanyama, ndege, miti na ardhi yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pori hili kutolewa *TANAPA,* mifugo imetapakaa pori zima na miti inafyekwa siyo kawaida. Wananchi wanahoji, hii maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwepo ndoa kati ya wafugaji na walinzi na wahifadhi wa pori hili, ambapo kwa sababu tusizozielewa wafugaji wameachwa kwenye pori na wanalima na kukata miti hovyo na mifugo ikichungiwa ndani ya pori. Hii imekuwa kero kubwa sana, kwani wenyeji wa eneo la Lwanfi ni wakulima na walikwishafukuzwa na wengine kufungwa. Inashangaza kuona wafugaji ambao ni wahamiaji, wakiachwa kwa kuwa wana uwezo wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* na Wizara naomba iliangalie jambo hili, kwani ni aibu na kero kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iharakishe mipango yake ya kuweka mipaka katika pori hili na kwamba eneo liachwe kwa ajili ya kuongezewa eneo kwa vile Halmashauri ilikuwa na mpango wa kurekebisha mpaka na ilikuwa moja ya makubaliano kuwa *TANAPA* wakichukuwa warekebishe mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Mbwendi, Mtapenda, China Ntunchi Wampembe Kasafa, Kala King'ombe, Nanansi, Ninde na vinginevyo hawana kabisa eneo kwa kilimo na kupata nishati (kuni)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshawishika kuchangia hoja hii kutokana na hali halisi ya maliasili na utalii ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunazo fursa za kuibua vivutio vya Utalii ndani ya nchi ambavyo havijatangazwa vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makumbusho ya Butiama, mbali na kuwa na makumbusho ya Butiama ijulikanayo kama Makumbusho ya Mwalimu Nyerere, bado haijachukuliwa kwa uzito unaostahili kisawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali, mbali na mambo mengine ya kumwenzi Baba wa Taifa, ilitenge jambo la uwepo wa Makumbusho ya Mwalimu Nyerere kama kivutio cha Utalii na ifanye *Butiama The Gate To Serengeti.* Mbali na kumuenzi Baba wa Taifa kwa kutangaza makumbusho pia ni vizuri kufanya Butiama kama *National Heritage* ili hata watalii wa nje wakipanga safari zao wawe wanajua kuna sehemu inayoitwa Butiama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama kuna Mbunge au mwananchi yeyote ambaye anaweza kupinga wazo hili labda lisifanyike kwa Serikali ya CCM kutopenda, lakini ni wazo ambalo kila mtu amekuwa akilisema na pengine wangependa kuona hili linafanyika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvunaji wa misitu, kumekuwepo na uvunaji wa misitu holela kwa njia ambayo vibali vyake vimekuwa na sintofahamu hadi kupelekea baadhi ya watumishi wa Idara kutuhumiwa na kuonekana pengine rushwa inakua na kupelekea vibali kutolewa hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendelea vibali vya mazao ya miti viwe na udhibiti wa kutosha na vipaumbele vya kibali hivi vitolewe kwanza kwa Halmashauri ili wawatumie wafungwa kutengeneza samani za Serikali na pia madawati kwa ajili ya shule zetu za msingi, sekondari na vyuo. Bado hatujawa na mkakati mahsusi wa kupunguza

matumizi ya mkaa na kuni katika Taasisi kama Magereza, mashule, Vyuo na majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupandisha bei mafuta ya taa ambayo ilikuwa nishati mbadala, imepelekea kuni na mkaa kuwa ndiyo suluhisho la nishati ya kupikia kwa walio wengi na hii imefanya kuvunwa kwa misitu kwa ajili ya nishati kuwa kubwa kila kukicha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa kujaribu kupunguza bei ya mafuta ya taa ikiwemo kuondoa kodi kwenye majiko ya gesi na kuondoa kodi kwenye mitundi ya gesi ya majumbani, ambamba na uhamasishaji matumizi ya gesi na mafuta ili kunusuru misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yakifanyika, tutaokoa sana misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utalii wa Ndani, bado ni tatizo kwa Tanzania walio wengi kutokana na gharama zilizopo. Mbali na kupunguza gharama, pia uwepo utaratibu wa kuhamasisha na kutangaza utalii ndani ya nchi hasa katika mabas,i ndege, daladala, radioni television na vipeperushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hapa Bungeni bado Waheshimiwa Wabunge wengi hawajapata fursa ya kutembelea vivutio vya utalii na kutumia fursa ya kuvitangaza kwenye hadhara zetu ili kuwafanya Watanzania kutembelea na kudhamini kazi ya Mungu katika uumbaji na kuisifu Wizara katika utunzaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na yote, lipo jambo kubwa hivi karibuni linalolisumbua sana Taifa hili na bado yawezekana halijapatiwa dawa, nalo ni uwindaji haramu wa tembo. Imewachosha Watanzania kusikia habari ya tembo wetu kuuawa kila kukicha. Pengine uelewa mdogo wa wananchi kuhusu wanyama hawa au hali ngumu ya maisha iliyopo miongoni mwa watu wetu ndiyo imepelekea watu wetu kujiingiza katika kulitia hasara Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ijulikane kuwa wapo watu wakubwa wenye fedha ambao ndio wafadhili wa vitendo hivi, lakini bado jinsi ya kuwabaini wakubwa hao, ndiyo imekuwa tatizo ikiwemo kuwakamata na kuwafikisha katika mikono ya sheria, hata kama ni wenye fedha na madaraka au majina makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata majibu ya mapendekezo na ushauri wangu kwa hayo ambayo nimeshauri sambamba na kuona utekelezaji wake katika kipindi kifupi.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeze Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii na timu yake kwa kazi nzuri wanazofanya kila siku na zinazoleta tija kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo Manyara, Serengeti, Ruaha, Mikumi, Ngorongoro, Saadani, Mlima Kilimanjaro, Selous tu ambazo ni maeneo ya vivutio kwa ajili ya utalii na siyo vivutio pekee vinavyoweza kuliletea Taifa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa nao ni miongoni mwa Mikoa ambayo ina maliasili na vivutio kwa ajili ya utalii. Mkoa wa Rukwa nao kama Serikali itajikita kutambua hizo fursa na kulingana na taratibu, zikashughulikiwa, zikaboreshwa, zikatangazwa watalii wa nje na ndani watatembelea vivutio vilivyoko Mkoani Rukwa. Mkoa utajiingizia fedha nyingi na kuinua uchumi wake, lakini na uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maliasili na vivutio vilivyoko Mkoa wa Rukwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa una misitu mikubwa, mizuri, misitu ambayo ndiyo chanzo cha mvua nyingi na za uhakika *(reliable)* lakini pia ni chanzo cha mito mingi Mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu minene hii imewasaidia wananchi wa Mkoa wa Rukwa kuanza Miradi ya Ufugaji wa Nyuki kwa ajili ya kuvuna asali na kuuza, kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda amekuwa mstari wa mbele kuhamasisha wananchi wa nchi hii ikiwa ni pamoja na Rukwa katika ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa Wilaya ya Kalambo una msitu wa Mbizi, mkubwa wenye miti mizuri. Msitu ulio na wanyama aina ya Mbega – Mbega hawa ni wekundu ni wa aina yake. Siyo kama wale tunaowaona kila siku weupe/weusi. Lakini msitu huu pia unao sokwe mtu wakubwa sana na wengi sana kama walivyo Mbega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijachukua hatua ya kuanzisha hifadhi na ulinzi kwa wanyama hawa na msitu, kwamba wananchi wanavuna kiholela misitu hii, wanyama wazuri hawa ambao wangetuingizia kipato wananchi wameanza kuwaua hovyo hovyo, uharibifu unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kalambo ina mito mingi ya Kalambo, Lwanji, Kibwe mito inayosababisha maporomoko makubwa *(Kalambo falls, Lwanji falls, Kibwe falls)*. Maporomoko haya ni vivutio vikubwa kwa utalii wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kalambo maeneo ya Kapozwe kuna chemchemi inayotoa maji ya moto sana, maji ambayo ukiweka kiazi kwa dakika chache kinaiva na kinaliwa. Lakini maeneo hayo ardhi yake ni tofauti, ukikanyaga inabonyea na kuinuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Rukwa kina chake ni kifupi sana kuliko maziwa yote duniani. Ziwa lina mamba wengi sana, lina samaki wa aina ya kambale ambao minofu yake ni mizuri, mitamu, na inasadikika inatibu ugonjwa wa kansa. Naomba Taasisi za Utafiti zilifanyie kazi suala hili. Dawa inaweza kupatikana ya kutibu ugonjwa wa Kansa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ilitupie jicho la pekee Mkoa wa Rukwa. Mkoa wa Rukwa una vivutio vikubwa sana.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naishauri Wizara kupitia Mameneja wa Mashamba ya Miti, kuongeza mgao kwa wavunaji wadogo wadogo wanaoishi jirani na mashamba yenyewe. Mgao huo uwe asilimia *(percentage)* ya *"harvest quota"* ya kila mwaka. Kwa namna hii, jamii jirani zitafaidika na mashamba haya kweli. Ndiyo yatakuwa chachu ya maendeleo ya wananchi hawa. Utaratibu wa sasa ambao kwanza huwapa kipaumbele wavunaji wenye mitaji mikubwa, haujengi na hauendani na Sera ya Uhifadhi Shirikishi ambao tunauhubiri.

Pia utaratibu wa kutorejesha sehemu ya maduhuli yanayopatikana katika mashamba haya kwa vijiji jirani, unasababisha wananchi kuzidi kutoona manufaa ya uwepo wa mashamba haya. Napendekeza mgao wa asilimia 25 wa maduhuli kama ilivyo kwa vijiji vyenye vitalu vya uwindaji utumike kwa vijiji vilivyo jirani na mashamba ya miti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchangiaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi unaofanywa na *TANAPA, TFS* na Taasisi nyingine hauna utaratibu maalum na kwa kiasi kikubwa umegubikwa na upendeleo. Napendekeza utaratibu utengenezwe ili kusiwe na mianya ya upendeleo na/au kulazimisha viongozi kwenda kubembeleza misaada kwa viongozi wa mashirika haya. Ipo mifano mingi ya ubaguzi na upendeleo kuhusu misaada hii.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nchi yetu imebarikiwa kuwa na vivutio vingi vya maliasili. Vile vile imebarikiwa kuwa na amani na utulivu, ambayo ni nyenzo muhimu katika kuendeleza utalii na maendeleo ya kiuchumi kwa jumla. Hivyo ni vyema kwa Wizara hii kushawishi wazawa (wananchi Raia) kuendeleza

na kuitunza amani yetu kwa Wizara kupunguza migogoro ya sehemu za Mbuga za Wanyamapori, misitu, na sehemu za ardhi iliotangazwa kama Eneo la Hifadhi (Hekta Milioni 13) mfano eneo la Loliondo ambapo jamii ya Wamasai wameporwa ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuchukua hatua mbalimbali katika udhibiti wa maliasili ya misitu, bado uuzaji wa mbao na magogo nje ya nchi hakujadhibitiwa vizuri, hivyo Serikali kukosa maduhuli halali ya biashara hiyo. Hivyo hivyo katika uvunaji wa misitu, kuna haja ya kuongeza nguvu ya kudhibiti hasa tukizingatia athari za tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali izidi kuboresha na kuongeza maeneo ya kale ili kutoka 118, yafikie 400 ambayo yameainishwa na Serikali. Serikali ikajifunze nchini Oman namna wanavyoendeleza mila na desturi wanazozifundisha Chuo Kikuu na namna ya utunzaji wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *Protocol* ya Tanzania na Oman eneo hili limo, nashauri fursa hiyo ya kuokota hazina hiyo Oman itumike, ikizingatiwa kuwa watu wa Oman na Tanzania wana historia ndefu ya udugu. Aidha, fursa za kujifunza kwa matumizi mazuri ya mambo ya kale; Egypt, Morocco, wako katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nashauri Wizara ijipange vizuri katika ukusanyaji wa mapato, kwani siyo mzuri. Hivyo, ni vyema Wizara ikasimamia eneo hili ili kuipatia Serikali mapato ya kutosha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangi kuhusu pesa kidogo inayotolewa na kukabidhiwa Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa, ili tunufaike na Sekta hii ya Utalii na kuongeza pato kwa Taifa, basi ni lazima tuwekeze na kuhakikisha kwamba vivutio vyetu tunavitangaza kwa nguvu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania lazima kwa umoja wetu tushirikiane kuvitangaza vivutio vilivyopo nchini kwetu kwa kushiriki utalii wa ndani ili kuvielewa kama fursa niliyoipata ya kupanda Mlima Kilimanjaro na kufanikiwa kufika *Gilman Point* na hivyo kuwa na uhakika na nini uzuri wa Mlima wetu huu maarufu kama *"the roof of Africa".*

Mheshimiwa Menyekiti ni jambo lisiloniingia akilini kwamba maporomoko ya pili kwa Afrika yaliyo Wilaya ya Kalambo hayatambuliwi na Wizara, kwani juzi juzi Naibu Waziri akijibu swali, alitaja vivutio vya kitalii bila kuyataja Maporomoko ya Kalambo yaliyo ya pili baada ya yale ya Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilitokea kwa bahati mbaya au kwa kutofahamu, basi tafsiri yake ije kwa vitendo kwa kuanza kuyatangaza kwa nguvu Maporomoko ya Kalambo ili kama Taifa, tufaidike na hazina hii tuliyonayo badala ya kuachia majirani zetu wa Zambia kufaidika na maporomoko hayo.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Tanzania kuna Wizara ambayo ni tegemeo la kuingiza mapato, basi Wizara moja inayochangia pato la Taifa ni hii Wizara ya Maliasili na Utalii. Hata hivyo, mapato yanayopatikana na Wizara hii yanalegalega kutokana na Serikali kutokuwa makini katika kusimamia sekta zitokanazo na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii unakwenda sambamba na suala zima la utunzaji wa mazingira jambo ambalo ni kivutio kikubwa cha watalii. Suala la kukata miti ovyo linapunguza hadhi na thamani ya misitu yetu na pia hutoa mwanya kwa majangili kushambulia wanyamapori kama vile ndovu (tembo) na kuchukua pembe na meno ya

ndovu na kusafirisha nje kwa nia ya kujinufaisha wao binafsi na kuikosesha nchi mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi iliyobarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii kama vile misitu ya asili, wanyama, Mlima Kilimanjaro, majengo ya kale, bahari, maziwa na hata utamaduni wa sanaa na utamaduni wa ngoma za asili na vile vile utamaduni wa mavazi ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba Serikali ya CCM haijawa mahiri na makini kabisa katika kusimamia Sekta hii ya Maliasili na Utalii. Katika hili, ziko sababu zinazopeleka Serikali kufumbia macho jambo hili, nazo ni kwamba wako Viongozi wa Serikali wanaonufaika na rasilimali hizi bila kuzingatia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii ingaliendelezwa kwa muktadha wa maendeleo ya Taifa, ni dhahiri kwamba asilimia 17% inayopatikana sasa hivi ingalikuwa ni zaidi ya mara tatu ya asilimia inayopatikana sasa, kwani sekta hii ingalitangazwa na kutumiwa ipasavyo ingalisaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza utegemezi wa bajeti kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri na ni wazi kabisa kwamba Serikali haijawa na utayari wa kuiendeleza Wizara hii na wala kupokea mapato makubwa yatokanayo na Sekta ya Maliasili na Utalii. Wizara imefanywa sawa na watoto wa Mitaani, inategemea zaidi kuomba misaada kutoka nje na ajabu zaidi hata kile ambacho kinapatikana hawapewi fursa ya kukitumia kuboresha sekta zitokanazo na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumejaliwa kuwa na sehemu kubwa ya hifadhi ambayo ingepatiwa wafanyakazi wa kutosha ili maliasili za nchi zisiibiwe na baadaye zitumike kunyanyua maisha ya wavuja jasho wa Tanzania ambao wameteseka kwa muda mrefu sasa. Wizara inahitaji walinzi mahiri wenye uwezo wa kutosha wa kupambana na majangili ambao hawapendi kuona Watanzania wanafaidika na rasilimali zao. Wafanyakazi sio

robo ya wanaohitajika katika sekta hii, lakini walinzi hawafiki hata thumni ya wale wanaohitajika. Hivyo Serikali ikiambiwa kwamba wanahusika na ujangili wa wanyamapori wanakataa kutokana na sababu zipi za msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalendo unahitajika zaidi katika kutunza, kuhifadhi na kulinda rasilimali za nchi. Siyo vyema kuingia watalii au viongozi wakahamisha rasilimali hizo kwenda nazo nje ya nchi na kama wako wanaofanya hivyo kwa maslahi yao, wajue kwamba kumbe Tanzania tulifanikiwa kuondoa utawala wa Mkoloni mweupe, lakini utawala wa Mkoloni Mweusi utakuwa ni mbaya zaidi, kwani umekosa hekima, busara na uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, penye nia pana njia. Ni matumaini yangu kwamba makosa ambayo yalijitokeza nyuma juu ya ujangili, wahusika watachukuliwa hatua na wale ambao walitajwa kuhusika na tuhuma hizo, wataendelea kuchunguzwa siyo kwa nia ya kuwakomoa, lakini kwa nia ya kuipa nguvu Sheria ili ichukue mkondo wake, ili iwe funzo kwa wengine wenye tabia za uhujumu uchumi wa nchi.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mkakati wake wa kupambana na ujangili maana hili limekuwa tatizo kubwa sana. Tumekuwa tukishuhudia kila mara pembe za ndovu zikikamatwa kutoka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na maoni ya Kamati ya Maliasili, Ardhi na Mazingira kuwa operesheni maalum ziendeshwe mara kwa mara ili kukabiliana na tatizo la ujangili wa wanyama pori hususani ujangili wa tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana pia na ushauri wa Kamati, tunahitaji kutangaza vivutio tulivyonavyo ili Mataifa mbalimbali yaone vivutio tulivyonavyo ili waweze kuja kuvitembelea na Taifa lipate pato kupitia utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iangalie, ni vipi itautangaza Mlima Kilimanjaro kuwa upo Tanzania? Kwa maana watalii wengi wamekuwa wakidanganywa kuwa Mlima Kilimanjaro upo Kenya. Naiomba Serikali iangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA A. CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali pamoja na kuongeza wafanyakazi wengi ambao ni Askari wa Wanyamapori, naomba Askari hao wapelekwe Jeshini wakapatiwe mafunzo kamili ya kijeshi pamoja na mafunzo ya kivita ili waweze kupambana na vita hii ya ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iruhusu Wizara kuingiza silaha za kisasa na kama itakuwa ni vigumu, basi iwape kibali ili silaha zao waagize kupitia hii JWTZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iagize silaha kama ndege, vifaru na kadhalika ili waweze kukabiliana na majangili hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuboresha utendaji wa Idara ya Wanyamapori Tunduru (wakati tunasubiri utekelezaji wa hatua ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa).

Vile vile kuna haja na umuhimu wa kuongeza idadi ya kuwapa uwezo wataalam katika ngazi za Halmashauri, Tunduru ikiwa ni mojawapo. Pia Kuwapatia vifaa/vitendea kazi watumishi ili kuwaongezea uwezo wa kutenda kazi zao. Je, kuna mpango gani wa muda mfupi wa kati na mrefu wa kuboresha hali hiyo kwa Wilaya ya Tunduru?!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mahusiano mema (ujirani) kati ya Serikali (Watendaji katika Wilaya na

mbuga, misitu na kadhalika) na wananchi wanaoishi katika maeneo hayo: Wanyama waharibifu na wanyama wakali: Serikali inajipanga vipi katika kushughulikia matatizo ya wanyama wakali wanaodhuru wananchi, na wale wanaoharibu mazao katika Vijiji vya Tunduru vikiwemo Ligunga, Kalulu, Ngapa, Tinginya, na Katete na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu namna bora ya kuwashughulikia wahalifu katika maeneo ya mbuga, misitu na kadhalika. Ni kwanini watumishi wa Wizara wanajihusisha na ukiukaji wa sheria na kuchukua sheria mkononi kwa kuwapiga na hata kuhusishwa na kuwaua wananchi bila kufuata taratibu na kuendesha mazoezi kwa njia za mkato na ukatili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali haifuati taratibu za kisheria na za kiutaalam katika kuwabaini wahalifu wa kweli ili kuepuka kuwadhuru wananchi waadilifu na watiifu kwa sheria na Serikali? Je, Serikali iko tayari sasa kupitia zoezi lililokamilika hivi karibuni Wilayani Tunduru ili kushughulikia kesi zilizopo kwa umakini na kuwaachia wananchi wasiohusika?! Hatua hii itairejeshea Serikali haki, heshima na hadhi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbao zilizokamatwa katika Wilaya ya Tunduru: Je, baada ya kukamilika kwa kesi husika na iwapo mbao zitakuwa mikononi mwa Serikali, Serikali itaharakisha zoezi la kukabidhi mbao hizo kwa Halmashauri ya Wilaya Tunduru ili itengeneze madawati kwa shule za msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Generator* la kuzalisha umeme linalotumika na Idara ya Wanyamapori – Kalulu – Tunduru: Je, Serikari iko tayari kudumisha ujirani mwema na wananchi wanaoshirikiana na Serikali katika kulinda maliasili ya Taifa kwa ku-*share* na Kijiji umeme unaozalishwa angalau katika Kituo cha Afya na sehemu nyingine muhimu? Ikumbukwe kuwa mafuta ya dizeli yatakayotumika hayataongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali iharakishe utaratibu wa kuipandisha hadhi *Selous Game Reserve* ambayo kwa sifa zake lukuki katika viwango vya kimataifa, ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali hadi sasa?

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na majangili ambao wanavamia mbuga za wanyama. Majangili hawa wamekuwa wanatumia silaha za kivita kuwaua tembo kikatilii na kuchukua meno yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mtandao wa kuua hawa tembo ni mrefu sana. Mtandao huu unawahusisha baadhi ya raia wa kigeni na baadhi ya raia wa Tanzania ambao ni wananchi waliozunguka Hifadhi ya Mbuga ya Wanyama pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa Wanyama Pori ambao si waadilifu. Mtandao huu ni mrefu kama wa madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ifanye operesheni maalum kwenye Mbuga zote za Wanyama na kuwafuatilia wageni ambao wanaingia nchini kwa ukaribu zaidi. Hata hawa wakandarasi wa Kichina, wanaojenga barabara wafuatiliwe kwa karibu, baadhi yao si waaminifu, mchana wanafanya kazi ya kujenga barabara usiku wanaingia kwenye kazi nyingine.

Vilevile hii biashara ya meno ya tembo soko kubwa lipo China, hata hizo silaha za kivita Tanzania hatuna kiwanda cha kutengeneza kwa mfano *SMG* na kadhalika silaha hizi zinatengenezwa China. Kama *TANAPA* hawana silaha za kukabiliana na majangili hawa ni kwa nini Serikali isiwashirikishe Jeshi la Wananchi washirikiane na *TANAPA* ili kukomesha ujangili uliokithiri katika Mbuga za Wanyama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *TANAPA* hawana silaha za kisasa za kutosha kukabiliana na majangili hawa, ni kwa nini silaha zilizoingizwa kukabiliana na majangili hawa zimezuiliwa bandarini mpaka leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ifanye mikakati ya kuwadhibiti majangili ambao wanawaua tembo, kwani kuna uwezekano wa tembo kutoweka miaka inayokuja kwa sababu tembo ni mnyama asiyependa bughudha. Vilevile uzazi wake unategemea chakula anachokula na kwa sasa hivi tembo wamekuwa hawana amani, kizazi chetu cha baadaye kitakuwa kinasikia kulikuwa kuna tembo Tanzania lakini tembo wenyewe hawaonekani vilevile pato la utalii litashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za wananchi waliozungukwa na Hifadhi (Mbuga za Wanyama). Kuna malalamiko kutoka kwa wananchi waliozungukwa na Hifadhi ya Mbuga za Wanyama. Wananchi hawa hawanufaiki na hizo Mbuga za Wanyama mfano Ngorongoro imeingia katika maajabu ya dunia (kuhusu wanyama na watu kuishi sehemu moja), wananchi ambao wanaishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro hawana maji safi, shule, hospitali na kadhalika. Ni lini Serikali itahakikisha wananchi wananufaika na rasilimali zao zilizowazunguka. Kama wananchi hawa watanufaika na raslimali zao, kutakuwa hakuna kero baina ya Serikali, mwekezaji na wananchi, rasilimali hizi zimekuwa zikinufaisha watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la makumbusho (vitu vya kale). Serikali imesahau sehemu hizi za makumbusho kwa mfano Bagamoyo na kadhalika. Majumba ya Mji Mkongwe Bagamoyo, yamesahaulika na wanaonunua sehemu hizi wanabomoa na kujenga majengo mengine wakati yale majumba ni kivutio kwa watalii. Majumba ya Mji Mkongwe ya Bagamoyo na Mji Mkongwe Zanzibar yamekuwa ni kivutio kwa watalii wengi sana. Aidha, bandari ya Bagamoyo ambayo ilikuwa inasafirisha watumwa ni chakavu vilevile na majengo pia ni chakavu. Ni lini Serikali itazienzi na kuzikarabati sehemu hizi za makumbusho ambazo ni kivutio kwa watalii wengi?

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia maeneo yafuatayo katika Hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, migogoro ya mipaka ya vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Taifa. Naomba Serikali ipate ufumbuzi wa kudumu na kuweka mipaka hiyo bayana kwa mfano Hifadhi ya Ngorongoro na vijiji vya Endamaghay, Mbulumbulu, Kambi ya Simba, Kitete, Lisitele na kadhalika. Usumbufu ni mkubwa sana hivyo hatua za makusudi zapaswa kuchukuliwa haraka na kwa upande wa *TANAPA* na vijiji vya Marang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, fidia kwa wale wanaoharibiwa mazao yao na wale wanaouawa na wanyama wakali. Ni kweli wanyama huharibu mazao ya wakulima na kusababisha njaa kwa familia hizo. Naomba Serikali iweke ulinzi wa kutosha kwa wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wananchi wanaodai fidia kwa muda mrefu bila mafanikio pamoja na kuwa tathmini ilishafanywa katika Halmashauri ya Karatu, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 29/4/2013 saa tatu usiku tembo waliingia katika kijiji cha Rhotia Juu Karatu na kumuua mtu mmoja aliyeitwa Ero Matlaà na anazikwa leo tarehe 2/5/2013. Je, Serikali inasema nini kuhusu mauaji yanayofanywa na wanyama wakali kila mara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Ziwa Manyara kukauka. Napenda kufahamu Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na mrefu ili kuokoa Ziwa Manyara na tishio la kujaa udongo na hata kukauka? Serikali itoe mkakati wa kuokoa Ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ujangili wa wanyama. Kutokana na Ripoti ya Mheshimiwa Waziri, ujangili unakua kwa kasi sana. Hivyo, naiomba Serikali kuimarisha ulinzi kwa hifadhi zetu hasa kwa kuajiri Askari wa kutosha na kuwa na silaha za kisasa. Pia naishauri Serikali kuwashirikisha raia (walinzi raia), ulinzi shirikishi na vijiji vile vinavyopakana na hifadhi zetu. Hii itawezesha kutambua majangili kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, naomba kuleta ombi la kijiji cha Qanded, katika Bonde la Eyasi kwa *TANAPA* kulinda hifadhi ya chanzo cha maji Qanded ambamo zamani kulikuwa na viboko na wanyama wengine. Ombi hilo likikubaliwa basi litakuwa limewasaidia kulinda chanzo cha maji na pia hifadhi ndogo ya wanyama pale na kurudisha uoto wa asili.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya watu wa Rombo, kutokana na ziara ya Mheshimiwa Naibu Waziri Lazaro Nyalandu aliyofanya Rombo mwaka jana. Ziara hiyo ambayo ilikuwa na lengo la kukagua uvamizi na uharibifu ambao umefanywa na tembo, imeleta nafuu kubwa ingawa tatizo bado lipo palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuu ambayo imepatikana ni kwamba Kituo cha Kupambana na wanyama hao katika Kata ya Ngoyoni kimefunguliwa, kina Askari lakini hawana silaha na hivi karibuni *KINAPA* wamekipa kituo hiki vitanda sita na magodoro sita. Kutokana na hali hiyo, tunaomba Kituo kipatiwe silaha na gari ili kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, hii ni sehemu moja tu inayovamiwa, sehemu nyingine ni Kikelelwa, Kata ya Tarakea na Mahorosha kata ya Kisale. Serikali iliahidi kujenga vituo viwili, kimoja katika kila eneo zaidi ya miaka mitano iliyopita. Wiki iliyopita, zaidi ya tembo mia tatu waliingia na kuharibu kijiji kizima, kati yao wanne waliuawa. Wananchi wanaomba ahadi ya Serikali kujenga vituo hivi izingatiwe katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni ombi la gari katika Idara ya Maliasili. Gari hili litaisaidia kupambana na majangili ambao wanaharibu mlima kwa kuvuna miti na kuharibu mazingira. Hali kadhalika itasaidia katika harakati ya kuhifadhi mazingira ya mlima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuchangia hoja ya makadirio ya matumizi ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha Hotuba yake aje na mkakati wa Serikali wa kudhibiti nyani wanaoharibu mazao na kula kuku wa wananchi wanaoishi Kata ya Msongole eneo la Kiboga A. Nyani hawa wanatoka kwa wingi katika msitu mkubwa wa Jeshi la Magereza na mashamba mwitu ya wananchi ambao hawayashughulikii mashamba hayo. Ni muda mrefu sana na vikao vingi kati ya wananchi na utawala wa Magereza vimefanyika lakini tatizo limeendelea kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndani unaweza sana kuiingizia Serikali fedha nyingi iwapo utapewa vipaumbele vifuatavyo:-

(i) Kupata taarifa sahihi na kwa wakati sahihi haswa wanapozihitaji. Kuna tatizo kubwa sana la kupata taarifa haswa kwa watalii wa ndani. Unaweza kwenda katika Ofisi za Wizara na kukuta taarifa zilizo nyingi zimeandikwa kwa lugha ya kigeni. Nashauri taarifa muhimu kuandikwa kwa lugha yetu ya Kiswahili.

(ii) Kuna tatizo kubwa la mawasiliano katika ofisi zenye mbuga za wanyama na vivutio mbalimbali, bado zinatumia simu za *TCCL* ambazo kwa muda mrefu tunapotaka kutembelea vituo hivyo ili kufanya maandalizi ya kupatiwa maeneo ya kulala na kujua gharama mbalimbali hazipatikani.

(iii) Katika vivutio vyetu kwa wananchi walio wengi bado gharama ni kubwa. Ili kuwawezesha wananchi wengi kutembelea maeneo hayo, nashauri Serikali kupunguza gharama ili Watanzania walio wengi waweze kutembelea vivutio vilivyopo nchini jambo litakalokuza pato la Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi za Taifa zenye migogoro na vijiji zihakiki mipaka yake na kurekebisha ili kumaliza migogoro kati yake na wananchi na kupunguza hasira ya wananchi dhidi ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ijipange na kulinda misitu ya asili na kuhifadhi *critical habitat* ya *wildlife* na *biodiversity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ione kuwa ufugaji wa asili ni *complementary* na uhifadhi na hivyo *alliance* kati hizi sekta mbili, maliasili na ufugaji uimarishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WMAs* zipewe *support* ili wanyama waishio katika maeneo ya vijijini wawe salama na ustawi wao uwe wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji jirani na hifadhi vishirikishwe katika ulinzi na hifadhi ya rasilimali zilizo ndani ya hifadhi zetu.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya utalii bado iko nyuma kwa sababu nyingi zikiwamo za kutotangazwa vya kutosha, ubovu wa miundombinu na uchache wa vyumba vya watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ielekeze zaidi mikakati ya kuliteka soko la utalii toka China. China ni nchi inayokuwa kwa kasi sana, kiuchumi, kiteknolojia na mabadiliko ya mila, desturi na tabia ambayo inaambatana na mambo ya Magharibi. Ni vyema sasa Wizara ijipange pia katika masuala ya lugha ya Kichina ili kurahisisha mawasiliano katika kutafuta soko hili la utalii toka China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika soko la ndani, nashauri Wizara na taasisi zake kuwekeza katika makundi

maalum yenye ushawishi kwa wananchi. Mfano Wabunge, ufanywe utaratibu maalum kuwapeleka katika hifadhi mbalimbali ili kuchochea utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ulanga Magharibi, kuna Hifadhi ya Bonde la Mto Kilombero, kwa mujibu wa mapitio ya Sheria ya Wanyamapori (2009), Kanuni zake zilielekeza iwekwe mipaka mipya ya hifadhi hiyo ikitiliwa maanani kuongeza au kuwaachia wananchi maeneo ya kilimo lakini badala yake zoezi hili halijaacha ardhi hiyo kwa wanavijiji jirani katika Jimbo la Ulanga Magharibi.

Naiomba Wizara kuliacha eneo la "*Buffer Zone*" kwa vijiji ili wananchi wapate ardhi hiyo kuitumia kwa ajili ya kilimo. Aidha, miradi ya Kitaifa ya *SAGCOT, FAMOGATA* na Program ya Kilimo kwa vijana zitatekelezwa vyema kwa kuitumia maeneo haya ya " *Buffer Zone*" ambayo yako katika mamlaka ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuipongeza Hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuutangaza utalii wa nchi yetu, kwa kupanua wigo wa aina za utalii, kwa kuendeleza utalii, huduma za utamaduni, mazingira na makumbusho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupitia hotuba nimeona Kondoa imekumbukwa na michoro ya kwenye miamba na kwa kuwa Kondoa ina historia hiyo, naomba angalau tupatiwe hoteli ya kitalii Wilayani hapo ili kuwavutia zaidi watalii ili waje kwa wingi Kondoa kuona chemchem na miujiza yake, mguu wa mtu wa kale huko Mogolo na Bonde la Ufa lililopita Kondoa, Mto Bubu na mambo mengi ya kuvutia ikiwapo Daraja ya Mnesoneso lililopo Kondoa Mjini. Pia kuenzi miji ya zamani kama Kondoa unaokaribia Karne moja kwani umetambulika mwaka 1926 na sasa 2013 kasoro miaka 13 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maeneo ya akiba pana madini na wapo wanaojiiba kuchimba. Hilo pia liangaliwe kwa haraka iwapo inaruhusiwa au hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi na rasilimali ya wanyamapori uwekwe lakini naomba nitamke mapambano ya wafugaji na Askari Wanyamapori busara itumike, tunapoteza watu kwa kuuawa na hasa Askari hao huwanyanyasa sana wananchi. Huko Kondoa ilitokea maeneo ya Mkongonero, kinachogamba hasa katika pori hilo, wakulima walikuwepo hapo kwa muda mrefu toka mwaka 1964 na mwaka 1995, Idara ya Ramani ikapima na kuwagawia eneo, mwaka 2006 ikatangazwa eneo hilo ni Hifadhi, wananchi hao wasiondoke sawa, wafungaji wanafuata nao maji huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wananchi wale waondoke, wapewe eneo lingine mbadala angalau na kifuta machozi kidogo kwani bila kufanya hivyo itawaonea wananchi na hao Askari wapunguze ukali kwa wananchi hao wa Kondoa na wale wanaochimba madini Serikali iharakishe Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri atuambie wakati wa majumuisho yake wakulima wa Wilaya ya Kondoa walioharibiwa mazao yao na tembo wamo kwenye malipo hayo? Mheshimiwa Waziri tunashuhudia mtu akiliwa na simba au kujeruhiwa wanalipwa lakini sidhani kama wote wanapata, naomba ofisi yake iwe inafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyoka ni sehemu ya utalii na anawekwa kwenye maonyesho. Sasa nyoka huyohuyo anapomgonga mtu akafa, je, Wizara inatoa fidia gani kwa wananchi wanaokutwa na maafa hayo? Kama ndivyo, tuelezwe ni kiasi gani cha fidia kinachotolewa na kama haina ulazima kwa nini Serikali na Wizara isifanye oparesheni ya kuwaua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina upungufu makubwa sana, tunashuhudia Askari wezi, tunashuhudia

wakiuza nyama, ngozi za chui na kadhalika. Risasi tu lazima wakaombe kwenye ofisi ya Mkurugenzi, je, ndiyo taratibu mbona hatuoni pesa iliyotengwa kwa matumizi hayo, hapohapo Mkurugenzi hahusishwi na lolote la maliasili, je sasa Serikali inaonaje mkazipa ofisi zote za Halmashauri kusimamia maliasili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, vitendea kazi hakuna kama vile magari, risasi na maeneo ya makazi ya Askari hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi ni watiifu, sioni sababu Askari kuwapiga mpaka kuua mtu ambaye ni wa kawaida. Ikibidi wapeni uhuru wananchi washiriki kuzoea wanyama kuliko inavyojitokeza kwa sasa.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maliasili na utalii, ni mhimili wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu kwani ina mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa kuchangia wastani wa asilimia 17. Japokuwa Wizara hii inachangia asilimia hizo lakini ni ndogo sana ukilinganisha na mali zilizopo kwenye maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii kuna fursa nyingi sana katika Hifadhi za Taifa wanyamapori na malikale. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri bado tuna imani nao, wasipunguze *speed* sanasana muongeze, msikate tamaa na endapo sekta hii watazidi kuisimamia vizuri na kuhakikisha inaendelea kupewa kipaumbele na Serikali katika kila kitengo, kwa kweli uchumi wa Taifa utaimarika kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya utalii. Ingawa takwimu zinaonesha kwamba idadi ya watalii wanaoingia nchini imeongezeka lakini ongezeko lake halilingani na vivutio vya utalii tulivyonavyo Tanzania. Kuna changamoto zinazosababisha uchache huo wa watalii, niiombe Wizara ifanye kazi ya ziada kushughulikia changamoto hizo ili kuongeza idadi ya watalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mmkono mapendekez ya Kamati yaliyotolewa, ni mazuri na yana mantiki, naomba Wizara iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niwazungumzie ndugu zangu wa Pangani – Tanga. Pangani kuna mbuga ya Saadani, tatizo kubwa lililoko kule ni tembo wanaharibu sana mashamba ya wananchi. Tembo wale wanaingia mpaka vijijini kama Mkwaja, Kipumbwi, Mikocheni na kadhalika, kwa kweli ni kero kubwa sana kwa wananchi kule. Wameng'oa minazi na mazao mengine na kuwaacha wakulima wakiwa maskini wa kutupwa. Naomba Wizara ilifanyie kazi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Nitaenda kuchangia katika sehemu kuu tatu ama nne. Kwanza, mauaji au ujangili wa wanyamapori. Pili, utangazaji wa utalii ndani na nje ya nchi. Tatu, suala la *concession fee* na nne, uimarishaji wa miundombinu katika sehemu mbalimbali za kitalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Ni sekta ambayo ikichukuliwa kwa umuhimu wake itakuwa ya kwanza kuogeza pato la Taifa na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu ambayo imebarikiwa sana na maliasili. Ukitembelea nchi za wenzetu, utashangaa jinsi mamilioni ya watu kutoka nchi za nje (wageni) na wenyeji wanavyotembelea sehemu mbalimbali za kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebarikiwa na milima midogo midogo ambayo ikijengewa miundombinu na kutangazwa itakuwa ya kipekee na kutuingizia fedha nyingi sana. Utashangaa jinsi nchi kama Afrika Kusini walivyoweza kuushinda mlima wetu wa Kilimanjaro kwa *table mountains* zao. Ukitembelea zile *table mountains* hazina maajabu zaidi

ya miundombinu iliyowekwa na kutangazwa hivyo kuvuta watalii kwenda, hapa kwetu mfano Milima iliyopo Morogoro, Tanga, Mwanza, Meru na kwingineko ingeweza kutuletea fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo miundombinu ni muhimu sana katika sekta hii. Tuna mbuga nzuri na kubwa sana lakini hazituletei faida yoyote ile yenye tija kama Taifa, bali tunapata pato dogo sana kama nchi na watu wachache ndio wanafaidika kwa kuuwa wanyamapori kwenye hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo katika kuhakikisha sekta hii inakuwa hatuna budi kwa maana ya Serikali (Wizara) kunuia kwa dhati katika kuutangaza utalii wetu wa Mbuga, Hifadhi, Milima yetu na makumbusho tuliyonayo ya Kilwa, Bagamoyo, Zanzibar, Mwanza, Dar es Salaam na kwingineko nchini. Suala zima la utangazaji wa utalii ni la muhimu sana na hasa nje ya nchi. Ukitaka kusikia aibu panda ndege kutoka nje halafu iwe ni *connection* ya kupita Nairobi utatamani kulia kwa jinsi ndege itakavyobaki tupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unashuhudia watalii au wageni wote wakishukia Nairobi na hata wengine huthubutu kusema tunaenda Nairobi ili baadaye twende Mombasa, halafu tukaone Mlima Kilimanjaro, *then* Serengeti na Maasai Mara. Hivyo, natoa rai kuwa ni wakati muafaka sasa utangazaji utalii nje uwe ni jambo la muhimu sana. Hivyo ni vizuri Serikali ikaangalia uwezekano wa kuwa na *Tourism Attaches* kwenye Balozi zetu nje ili waweze kutekeleza majukumu ya kutangaza na kuvutia watalii kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la utalii wa ndani ni muhimu kwa Serikali kuandaa mkakati maalum wa kuhakikisha utalii wa ndani ambao kwa sasa ni kama haupo kabisa ambapo tunabaki tunategemea zaidi wageni kutoka nje. Madhara yake ni kuwa matatizo ya kiuchumi yakitokea kwenye hizo nchi za wageni wanaoingia nchini, yanaweza kuathiri utalii wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia tena kwa mara nyingie juu ya suala zima la *concession fee.* Mwaka jana nilizungumzia na mwaka huu pia naomba kurudia kuzungumzia kesi iliyofunguliwa dhidi ya *TANAPA* na wamiliki wa hoteli wakipinga *TANAPA* kutoza tuzo mpya ya *concession.* Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kesi hii inaisha haraka kwani kwa hali ilivyo sasa, tunapoteza fedha nyingi sana na ni aibu kwa Taifa kuendelea kupoteza pato/fedha nyingi sana ambazo zipo wazi na dhahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu tuzo la kodi kwenye silaha zilizoingizwa nchini kwa ajili ya kupambana na ujangili unaoendelea kukithiri nchini na hapa tulipo tunatambua tatizo kubwa la ujangili lililopo nchini. Wakati sasa umefika Serikali itambue umuhimu wa silaha zinazoagizwa na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi zake kutokutozwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upitishwe Waraka/Sheria ya kusamehe kodi silaha hizi kama ambavyo silaha za Polisi zisivyotozwa kodi. Hii itasaidia kuondoa tatizo la ujangili nchini ambalo tumeshuhudia watu wasio na hatia kukamatwa kwa kuwa majangili lakini wakubwa hawakamatwi.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, napenda kupatiwa maelezo ya Wizara juu ya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kwa nini Wizara haiyapi kipaumbele Mapango ya Amboni – Tanga? Mapango ya Amboni yaliyopo katika Kata ya Kiomoni, Wilayani Tanga ni sehemu muhimu ya kujivunia na ya kihistoria kwa nchi yetu. Mapango haya yamekuwa yakivutia watu mbalimbali kutoka ndani na nje ya Tanzania. Inasadikiwa kuwa eneo la Mapango haya ni kilometa za mraba 23.4 ila inasikitisha kuona kuwa ni Mapango mawili tu kati ya 13 yanayopitika/yanayotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni kukosekana kwa watumishi wa kutosha na utaalamu utakaowezesha

kutumika kikamilifu kwa mapango haya. Mapango ya Amboni pia yanakabiliwa na hatari ya kuvunjika/kuporomoka kutokana na kuzungukwa na milipuko ya baruti inayotokana na uvunjaji wa mawe ya chokaa. Kwa ujumla mandhari na hali halisi ya Mapango haya si ya kuvutia watalii wa ndani na nje. Hivyo, napenda kupata maelezo ya Waziri, je, ni mikakati gani iliyowekwa kuhakikisha Mapango ya Amboni yanaboreshwa na kuvutia watalii wengi wa ndani na nje ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uhifadhi wa rasilimali za Malikale – Tongoni. Inasikitisha kuona kituo cha Malikale cha Tongoni, Tanga hakina mandhari ya kuvutia wakati kumekuwepo na watu wengi siku hizi hasa kutoka nje ya nchi wanaotembelea kituo hiki. Je, Wizara ina mpango gani wa kuboresha na kuendeleza kituo hiki? Naomba nipatiwe majibu, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya kituo cha Malikale Tongoni – Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuongelea Kilimanjaro *Ecosystem.* Uhifadhi wa Mlima Kilimanjaro hauwezi kuwa endelevu kama uhifadhi huo utalenga eneo la *KINAPA* peke yake. Yapo mambo kadhaa yanayochangia kujenga hofu ya uendelevu wa Hifadhi ya Kilimanjaro. Mambo hayo ni pamoja na:-

(i) Kupotea/kupungua kwa kasi kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro.

(ii) Kupungua kwa kasi kwa wingi wa maji katika vyanzo vilivyopo ndani na nje ya Hifadhi na hivyo kupungua sana kwa maji katika Mito inayoporomoka katika miteremko ya Mlima Kilimanjaro.

(iii) Kupungua kwa kasi kwa misitu ndani na nje ya Hifadhi na katika Mkoa mzima wa Kilimanjaro sambamba na uoto wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yote yamechangia kwa kasi kupungua kwa mvua za masika, vuli na hata ukungu na umande. Vilevile kumekuwepo na ongezeko kubwa la joto katika Mkoa na Mlima wa Kilimanjaro ambapo siku za miaka ya karibuni kumerekodiwa kiwango cha juu cha nyuzi joto 40°c ambacho ni cha juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya yote haya, ni ushauri wangu kuwa sasa kuna ulazima wa kuwa na programu *"Integrated Save* Kilimanjaro *Snowfields"* na program ambayo inaweza kuwa *funded* na watalii haohao wanaopanda mlima. Mpango huu ushirikishe Halmashauri zote zinazozunguka Mlima Kilimanjaro. Ni bahati mbaya hata katika Bodi ya *KINAPA* haina uwakilishi wowote kutoka Halmashauri hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuulinda Mlima na mazingira yanayouzunguka, Mfuko huu uchangiwe US$100 toka katika malipo yanayolipwa *KINAPA/TANAPA*. Kiwango hiki kitakusanya kati ya US$ 4 – 5 milioni na *fund* hii inaweza sana kuwa na *programm* pana ya ku-*adress* mambo yote niliyoyataja hapo juu na hivyo kuokoa mazingira, vyanzo vya maji, mvua na hatimaye barafu ambayo ndiyo kivutio kikubwa kinacholeta watalii kupanda Mlima Kilimanjaro. Ikumbukwe tukichelewa zaidi barafu itapotea na utalii wa Mlima huu utapungua kwa asilimia 80%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ujangili hususani wa meno ya tembo umekithiri. Biashara ya meno ya tembo sasa imepanuka sana na inashindana na biashara ya madawa ya kulevya kwa ukubwa wa faida. Utafiti unaonyesha sasa kilo moja ya *ivory* inauzwa kati ya US$ 3000 - $4000. Kibaya zaidi sasa meno ya tembo hayalazimiki kusafirishwa katika hali yake halisi (ya mfano wa pembe) bali kuna taarifa za meno haya kusagwa na kuwa "unga" au *"pellets*" na hivyo kurahisisha zaidi usafirishaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za ziada zinaonyesha kuwa hizi mashine za kusaga meno haya tayari ziko nchini,

kuna ukweli kuwa soko kubwa la meno ya tembo liko China na hata mashine za "ku-*process*" meno haya toka *its original form to powder or pellets* zinatoka hukohuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, kama nchi yetu haiko tayari kupata lawama tembo watakwisha miaka michache ijayo. Majangili yako *smart, well connected and networked, well funded, well equipped and well motivated*. Tuanzishe adhabu ya kifo kwa wote watakaohusishwa na biashara hii ya ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kikosi cha Wanyamapori kilivyo sasa hakiwezi kukabiliana na majangili. Tufikirie kuwepo "Vikosi Maalum" vya Jeshi la Wananchi (JWTZ) vitakavyokabidhiwa jukumu hili pamoja na *"appropriate" equipment and weapony*. Aidha, tu-*invest* katika *surveylance system* na *"elephants herds" tracking system*. Nchi ya *South Africa* inaweza kuwa mfano wa kuigwa kusaidia jambo hili pamoja na teknolojia yake.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Hamisi Kagasheki (Mb) na Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Lazaro Nyallandu (Mb) na Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu Mama Tarishi, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye kuonyesha kupiga hatua kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa watumishi wa Maliasili. Napenda kutumia nafasi hii kuiomba Serikali kutoa ajira kwa kuajiri watumishi zaidi wa Maliasili hadi ngazi ya Kata. Napenda kutoa sababu kwa nini natoa ushauri hili. Natoa ushauri huu kwa sababu uchumi kupitia Maliasili unakua sana mfano ufugaji wa nyuki, upasuaji wa mbao, kuchoma mkaa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote haya yanahitaji uangalizi wa karibu na kutoa taaluma ili uzalishaji wa nyuki uwe wa kisasa pamoja na kudhibiti biashara

haramu. Wataalamu walioko kwenye Halmashauri zetu ni wachache hata vyombo vya usafiri hawana kama ipo ni pikipiki moja tu. Nitashukuru kupata maelezo wakati Waziri anajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wananchi na Hifadhi za Wanyamapori. Napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuiomba Serikali kuangalia upya suala la mipaka ya makazi ya watu na maeneo ya ufugaji. Ni ukweli usiofichika kuwa Mbuga za Hifadhi zimeanzishwa wakati wananchi wanaishi kwenye maeneo yaleyale na vile vile ieleweke kuwa familia zinaongezeka kwa vile binadamu wanazaana na shughuli za kijamii zinakua sambamba na uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni vyema kuacha utaratibu wa kupanua mipaka ili tusiwasumbue raia wetu. Endapo wanyama wameongezeka ni vyema kuwapunguza kwa kuwahamishia kwenye Hifadhi zingine kama wanavyofanya nchi ya Kenya na nchi zingine au kutafutia raia makazi mengine. Nasubiri majibu ya Serikali yenye faraja kwa Watanzania kwa kuwa Serikali yetu ni sikivu haikuzoea fujo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubani unaotolewa baada ya mazao kuharibiwa au binadamu kuuawa na wanyama wakali. Kumekuwa na manung'uniko makubwa kwenye familia zinazopatwa na matatizo inapotokea mwanafamilia kauwawa na wanyama wakali au mazao kuharibiwa vibaya na wanyama kwani ubani unaotolewa kwenye familia hiyo ni fedha ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema suala hili liangaliwe upya ili ubani angalau uwe na kiwango cha kufariji familia ingawa thamani ya mtu halingani na chochote, lakini mazao yanaweza yakathaminishwa na fidia halisi ikajulikana na ikalipwa. Nasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa Mfuko wa Wafugaji Nyuki. Ni ukweli usiopingika kuwa sasa hivi ufugaji

wa nyuki umewaletea Watanzania uchumi mkubwa pamoja na Taifa kwa ujumla. Akinamama na vijana wameanzisha vikundi mbalimbali vya kufuga nyuki ingawa tatizo lao kubwa ni kukosa mitaji. Ninaishauri Serikali kuanzisha mfuko wa kukopesha vikundi vya akina mama na vijana ambao wameamua kujikita kujipatia kipato kupitia ufugaji wa nyuki. Nina hakika hata pato la Taifa litakua na wananchi wataendelea kiuchumi. Nasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuendelea kuibua vivutio vya watalii. Napenda kuhamasisha Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya wataalam kuendelea kufanya ziara Mikoani ili kuibua vivutio vya watalii ukiwemo Mkoa wa Singida ambao una vivutio vingi lakini havijulikani mfano:-

(i) Alama iliyowekwa na Wajerumani huko kijiji cha Sukamahela kata ya Sorly Wilaya ya Manyoni.

(ii) Maji ambayo daima huwa yamechemka joto la kuivisha mayai na chakula kwa ujumla, yako maeneo tofauti tofauti Mkoani Singida.

(iii) Mapango na maghofu ya Wajerumani huko Kisiriri Iramba na Mkalama ambayo inasemekana walifukia vitu vya thamani.

(iv) Michoro ya ajabu kwenye mawe makubwa mithili ya Malaika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la asali linaloaminika. Wananchi huko Manyoni wanajitahidi sana kuzalisha asali tena kitaalam kabisa lakini pamoja na asali ya Manyoni kuwa na ubora wa juu Afrika bado haina soko la kuaminika. Ninaiomba Serikali iwatafutie wananchi soko la asali la kuaminika ili akinamama na vijana ambao wameamua kujikita kwenye ufugaji wa nyuki wapate moyo zaidi wa kuzalisha zaidi. Ninasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujangili wa wanyamapori. Ni kweli tatizo la ujangili bado lipo kwenye misitu yetu, Hifadhi

ya Wanyamapori kwa sababu ya utajiri unaotafutwa na watu wachache. Ili kuondokana na ujangili huu ni vyema Serikali kufanya haya yafuatayo:-

(i) Kuajiri Askari wengi kwenye Idara ya Wanyamapori.

(ii) Wataalam kupewa vifaa vya usafiri yaani magari.

(iii) Watumishi kupewa silaha za kutosha.

(iv) Watumishi kuboreshewa maslahi yao zaidi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kituo cha Manyoni cha Askari wa Wanyamapori wanakabiliwa na upungufu wa hayo niliyoyaeleza hapo juu. Nitashukuru kupewa majibu yenye kuwatia moyo Askari hawa wa Manyoni wanaofanyakazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa magogo na mbao. Bado kuna wizi mkubwa sana wa magogo na mbao ambao huathiri uchumi wa nchi yetu hasa kwenye misitu ya tarafa ya Itigi, Wilaya ya Manyoni. Serikali imejipanga vipi kudhibiti tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumaliza mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii, nawatakia utekelezaji wenye tija chini ya Mtendaji Mkuu Mama Tarishi (Jembe).

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, utalii wa ndani uko chini sana (2/%). Ni vyema Serikali iandae utaratibu wa kuwaandaa Watanzania na kutunga Sheria ili kuhamasisha na kuongeza utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hoteli za Lobo na Seronera Lodges zirudishwe Serikalini na ziwe chini ya *TANAPA*.

Hii inawezekana hata kwa *TANAPA* kuingia ubia na Kampuni yoyote kisheria kwa ajili ya kuendesha na kusimamia mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, vivutio vya kiutalii vifuatiliwe na kubaini ili kupanua wigo wa Utalii hapa Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, matangazo ya utalii ndani na nje ya nchi. Utangazaji uko chini mno, ni vizuri Mabalozi wetu kupitia *"Economic Diplomacy"* wasaidiwe ili wasaidie kutangaza utalii hata kufanya maonyesho mbalimbali ya kiutalii huko waliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, makazi na maslahi ya watumishi wa Maliasili na Utalii ni duni sana. Hali hii iboreshwe ili kujenga morali kwa watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, hifadhi ya Serengeti ibadilishwe ili iwe Mamlaka kama ilivyo Ngorongoro (NCA) au Kilimanjaro *(KINAPA).* Hali hiyo itasaidia kusimamia mapato vizuri na kuboresha mazingira ya kazi na ya watumishi pia.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema. Pia nampongeza Waziri pamoja na jopo lake linalomwezesha kufanya kazi yake vema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee, nami napenda kuchangia bajeti hii ingawa kwa uchache. Katika Kata ya Nanganga, Wilayani Masasi, kuna bonde zuri lenye rutuba nzuri kando ya Mto Lukuledi. Bonde hili ndilo tegemeo la wakazi wanaolima kwenye bonde hilo. Katika Mto huu kuna viboko ambao wanaleta uharibifu wa mazao kiasi cha kuwafanya wakulima wayakimbie mashamba yao na kubaki wanahangaika kwa kukosa maeneo. Hivyo, naiomba Serikali/Wizara itafute njia ya kuwaondoa viboko hao na kuwanusuru na baa la njaa watu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na viboko hao, katika Mto huo wa Lukuledi kuna mamba wengi ambao kila

mwaka huwa wanaleta maafa, kwani wananchi hupata maji kwa matumizi ya nyumbani. Vilevile Mto huu unasaidia sana kwa kilimo cha umwagiliaji (bustani). Naomba Serikali ione umuhimu wa kutatua matatizo yanayojitokeza kutokana na mamba hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali, ukisoma ukurasa 7 - 8 unaelezea utekelezaji wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori na ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa kuna ujangili wa kutisha katika nchi yetu ambao pamoja na Askari wa Wanyamapori kufanya *operation* za mara kwa mara bado unaendelea. Nashauri Serikali iajiri Askari Wanyamapori wa kutosha kwa sababu idadi ya watumishi walio katika mapori yote ya akiba ni kidogo sana ukilinganisha na ukubwa wa mapori hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vivutio vingi vya kutosha kuweza kutoletea kipato kutokana utalii pamoja na vingine bado Serikali haijavitambua rasmi ili viweze kutumika. Nashauri Serikali kuwa na Kitengo cha Utafiti ili kiweze kugundua maliasili zilizopo katika nchi yetu ambazo tunaweza kutumia kuingiza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wachangiaji wote waliosema Balozi zetu ziwe na kitengo cha kutangaza utalii uliopo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupatiwa ufafanuzi kuhusu misitu iliyopo katikati ya Miji, sera yake inasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itakapokuwa inafanya majumuisho, inieleze kuhusu suala la msitu wa Kihesa, Kilolo katika Manispaa ya Iringa. Hatma yake

imefikia wapi sababu Halmashauri yetu imeshaleta maombi muda mrefu ya kuhamisha msitu ule ili waweze kubadilisha matumizi kuliko ilivyo sasa msitu huo ni hatari kwa wananchi wanaouzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka katika bajeti iliyopita nilizungumza na pia Bunge lililopita nilileta swali linalohusiana na msitu huo, majibu ya Waziri yalikuwa kwamba msitu huo tayari ulishakuwa *gazetted* na tayari maombi yalishakubalika. Nachotaka kujua ni taratibu gani zinazotakiwa kufuatwa ili sasa umilikishwe kwa Halmashauri ya Iringa Mjini? Halmashauri haiwezi kuwa na mamlaka ya kufanya kitu chochote bila kuwa na *document* ya umiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo ambalo napenda Serikali ilichunguze kwa makini. Kuna baadhi ya Askari Wanyamapori ambao huwalinda majangili na kuwasakizia wananchi kesi, wanapigwa na mpaka wengine hufungwa. Jambo hili limeshajitokeza katika Hifadhi ya *Ruaha National Park.* Tatizo hili ni kubwa na nilishalifikisha jambo hili kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu mwenye dhamana na wananchi wapo tayari hata kuleta ushahidi wa uonevu wanaofanyiwa na Askari hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki (Mb), Waziri na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu (Mb), Naibu Waziri pamoja na Bibi Maimuna Tarishi, Katibu Mkuu na Bibi Nuru Milao, Naibu Katibu, Wakurugenzi na Watumishi wa Wizara pamoja na Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kuendeleza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Nawashauri waendeleze jitihada hizo ili tufikie malengo tuliojiwekea kisekta na kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Misitu. Wakala wa Misitu *(TFS)* wanajitahidi sana kuendeleza maliasili ya misitu nchini pamoja na kushirikisha jamii inayowazunguka. Uongozi

wa Hifadhi ya Msitu wa Meru-Arusha unastahili pongezi kwa jitihada wanazofanya kuendeleza hifadhi sambamba na kushiriki kutekeleza miradi ya maendeleo ya jamii katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo, nashauri kuwa *TFS* ianzishe mpango wa kuwezesha jamii inayowazunguka katika Wilaya ya Arumeru kushiriki kuendeleza upandaji miti kwa lengo la kuhifadhi mazingira na kujipatia vyanzo ya mapato kwa kukuza miti na kuvuna kwa kuzingatia Sheria Ndogo zinazosimamia mazingira katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri kuwa utaratibu wa kutoa magogo kwa viongozi wa Kata na vijiji jirani na hifadhi ubadilishwe. Tunaomba Hifadhi itengeneze madawati na kukabidhi kwa uongozi wa Halmashuri ya Wilaya ambao watagawa kwa shule zenye mahitaji. Pendekezo hili linazingatia ukweli kuwa sio magogo yote yanayotolewa kwa viongozi wa Kata na Vijiji yanafika kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji nyuki. Wilaya ya Arumeru kwa miaka mingi ilikuwa ikitegemea kilimo cha kahawa ikiwa ndiyo zao pekee la biashara tokea enzi za utawala wa ukoloni. Kwa bahati mbaya kufuatia kuyumba kwa soko la kahawa Duniani imesababisha wakulima kukata tamaa na kutekeleza zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa hawana tegemeo lolote la kujipatia fedha, hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kupitia Idara ya Misitu na Nyuki kutoa elimu kwa wananchi wa Wilaya hiyo ili kwa kushirikiana na sisi viongozi wa wananchi tuwahamasishe ili waanzishe ufugaji nyuki kwa madhumuni ya kujipatia chanzo kipya cha mapato. Pamoja na elimu, naomba pia atusaidie kuchangia gharama za kuanzisha ufugaji wa nyuki ili wananchi hao wajikomboe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyamapori, nampongeza sana Bwana Allan Kijazi pamoja na timu yake ya wataalam kwa kazi nzuri wanayoifanya kuendeleza hifadhi zetu ingawa katika mazingira magumu sana. Napenda kuwahakikishia ushirikiano wangu binafsi na wapigakura wangu wote. Nawashauri waendelee na jitihada na ujasiri walio nao ili kuhakikisha kuwa maliasili waliokabidhiwa inaendelezwa kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwatia hamasa na kuendeleza moyo wa uzalendo alioonesha Mkurugenzi Mkuu na wasaidizi wake, nashauri kuwa Serikali ianzishe mfuko mahsusi wa tuzo kwa watumishi wa Maliasili wanaoonesha utendaji bora. Vilevile Wizara iwe ikipendekeza watumishi wanaofanya kazi nzuri kwa Mheshimiwa Rais kuwa wapewe Nishani kama inavyofanyika kwa Maafisa Jeshi, Polisi, Magereza na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii ili kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Wizara hii kwa uchapaji kazi wake ambao si wa kutilia shaka. Pamoja na mambo mazuri ya Wizara hii hasa kwa jitihada za Waziri wa Wizara husika, napenda kumuuliza Waziri maswali yafuatayo:-

(i) Serikali imefanya juhudi zipi ili kukabiliana na tatizo la ujangili wa nyara za Serikali hapa nchini?

(ii) Je, watumishi wasio waadilifu katika Idara ya Wanyamapori wamechukuliwa hatua gani?

(iii) Je, mapori ya akiba yaliyotengwa sehemu mbalimbali za nchi yetu yana faida na hasara zipi katika nchi yetu?

(iv) Wizara imefanya jitihada gani hadi sasa ili kuhakikisha kuwa inaondoa kabisa tatizo la migogoro baina

ya hifadhi zetu na wananchi au mapori ya akiba na vijiji vinavyozunguka mapori hayo?

(v) Je, mgogoro wa mpaka kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Serengeti (SENAPA) na wananchi wa vijiji vya Mrito, Gibaso, Gong'ora, Kitawasi, Masanga, Kegonga na Mangucha Wilayani Tarime utatatuliwa lini?

(vi) Ni hatua zipi zinazofuatwa katika ugawaji wa vitalu? Je, Wizara imetatua vipi malalamiko ya ugawaji wa vitalu vya uwindaji ambayo yanajiri kila kukicha?

(vii) Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo la wanyamapori waharibifu ambao ni kero kubwa sana katika vijiji vya Gibaso, Gong'ora, Kitawasi, Masanga, Kegonga na Mangucha?

(viii) Kwa nini Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imejichukulia na kujitwalia maeneo ya Kata za Kemambo, Nyarukoba, Gorong'a na Nyarungu bila ridhaa ya wananchi?

(ix) Je, bonde la Nyanungu lililopo Kata ya Nyamungu litarudishwa lini rasmi kwa wananchi?

(x) Je, Wizara imejipanga vipi kutoa elimu juu ya uhifadhi kwa wananchi wanaozungukwa na hifadhi za Taifa au Mapori ya Akiba?

(xi) Ni lini Serikali itarudisha *hotel* zake zilizo ndani ya hifadhi mbalimbali ambazo zimebinafsishwa kwa wawekezaji uchwara?

(xii) Serikali imejipanga vipi ili kuboresha miundoMbinu bora katika hifadhi zetu?

*(xiii)* *TANAPA*, Mamlaka ya Ngorongoro na *TTB* zimejipanga vipi kutangaza vivutio vya utalii hapa nchini? Ni kwa nini kila mamlaka isipewe jukumu lake la kutangaza kazi ya utalii peke yake badala ya mtindo wa sasa wa kuitegemea *TTB* katika jukumu hili la utangazaji?

(xiv) Misitu yetu ni hazina kubwa katika nchi yetu, je, misitu iliyopo nchini kwetu imeliingizia Taifa fedha kiasi gani kwa miaka mitano iliyopita?

(xv) Ni kwa vipi Halmashauri zetu zinashirikiana na Wizara ili kuhamasisha suala la utalii wa ndani hapa nchini?

(xvi) Je, utalii wa kiutamaduni (*Cultural Tourism*) una faida gani kwa nchi kama Tanzania? Kwa nini utalii wa aina hii usiendelezwe kwa hali na mali hapa nchini?

(xvii) Je, milima, mabonde, mito, maziwa na bahari vinasaidiaje kutangaza utalii wa nchi yetu?

(xviii) Serikali ina mikakati ipi ya kutangaza utalii wa Tanzania katika Mataifa mbalimbali duniani?

(xix) Watanzania wazalendo wamehamasishwa vipi ili kuwekeza katika sekta hii ya Utalii?

(xx) Kuna mkakati gani madhubuti wa kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya utalii katika ukanda wa Afrika Mashariki?

(xxi) Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha Mamlaka ya Utalii hapa nchini?

(xxii) Ni kwa vipi Serikali kupitia Wizara hii inawatumia Waasisi wa Taifa hili ili kuendeleza utalii wa kiutamaduni na kihistoria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri ujangili ni janga kubwa sana. Kwa vyovyote vile ni lazima kuhakikisha biashara hii inakomeshwa kwa kuharibu soko lake. Kitabu cha *Killing for profit Exposing the illegal*

*Rhino Horn Trade – Julian Rademeyer* kimeonesha kinagaubaga namna biashara ya pembe za ndovu *(Ivory)* inavyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima kuimarisha ulinzi kwenye hifadhi na mapori ya akiba kwa kupata ushauri wa makampuni yaliyobobea kwenye eneo hilo. *TANAPA* na Idara ya Wanyamapori ni lazima sasa wawekeze vya kutosha katika usalama na ulinzi wa Hifadhi na Mapori ya Akiba. Hata hivyo, kuua majangili hakuleti mafanikio yoyote. Suluhisho pekee ni kuua soko la biashara hiyo haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iingie makubaliano *(bilateral agreements)* na nchi zenye kununua meno ya tembo na pembe zingine ili kupiga marufuku biashara hiyo. Tanzania na China waingie makubaliano ya kushirikiana kupiga marufuku biashara ya Nyara za Taifa. Hii itasaidia sana kudhibiti biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutangaza utalii: Ni lazima sasa kutumia fedha za kutosha kutangaza utalii kwa nchi yetu. Bajeti ya Utalii bado ni ndogo sana. Hata tulipojaribu kuanza kutangaza mwaka 2007 – 2008 wanasiasa tulipiga kelele sana kuhusu gharama za matangazo. Tulikosea sana. Wizara na Taasisi za *TANAPA, TTB* na *NCAA* waweke mikakati ya kutangaza kwa nguvu sana utalii wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taifa *Stars*: hivi sasa nchi yetu ina nafasi kubwa sana ya kushiriki katika Kombe la Dunia nchini Brazil (TZBrazil 2014 ndio Kampuni yetu *twitter*). Hii ni nafasi adimu sana kwa nchi yetu kujitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Utalii lazima ishiriki kikamilifu katika kuhakikisha Taifa *Stars* inakwenda Brazil 2014. *TTB, TANAPA* na *NCAA* lazima wajipange kuchangia ushiriki wa Taifa *Stars* kwenye Kombe la dunia. Huu ni mkakati wa Kitaifa kujitangaza. Hii ni kampeni ya nchi ambayo tasnia ya utalii itafaidika nayo. Naomba Waziri atoe *commitment* hii na utayari wa Wizara yake kushiriki.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, migogoro inayojitokeza ya mipaka ya *WMAs* na Vijiji ama Kata zinazozunguka maeneo ya Hifadhi na Mbuga za Wanyamapori. Serikali iangalie upya namna a kutenga maeneo na mipaka hiyo, ikizingatiwa kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la watu ikilinganishwa na rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vema sasa *TANAPA* kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo husika ikaangalia upya mipaka hiyo ili kupunguza vurugu kati ya wananchi na *TANAPA*. Ni vema pia Serikali kupitia mamlaka husika ikatoa na kuendelea kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi husika katika maeneo yaliyohifadhiwa ili wananchi waone umuhimu wa maliasili hizo.

Pili, Sheria zinazotumika wakati wa kesi za ujangili:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza tatizo la ujangili Serikali inabidi iangalie uwezekano wa kuziangalia upya sheria zinazotumika kwa sasa, kwani inaonesha kwamba sheria hazina makali ya kutosha na ndio maana ujangili unazidi kuongezeka kwa kasi. Hivyo basi, ni vema Serikali ikaongeza adhabu na adhabu ziwe kali ili hao majangili waweze kukoma;

(b) Kesi zinazohusu majangili zimekuwa zikichukua muda mrefu na hivyo kuzifanya mamlaka husika kama *TANAPA* kuvunjika moyo na kuendelea na usakaji wa majangili. Hivyo basi, ni vema Serikali kwa kushirikiana na mamlaka husika kama Polisi na Mahakama kuharakisha kesi hizo na pia adhabu kali kutolewa kwa wale wanaobainika kuwa na makosa;

(c) Magari na vyombo vinavyopatikana na nyara za Serikali; Serikali iangalie namna ya kuyataifisha magari

hayo ili iwe fundisho kwa wanaofanya hivyo na hiyo itawafanya wenye magari kuogopa kufanya biashara na majangili;

(d) Serikali irejee mpango wake wa *operation* maalum ya kuwasaka majangili ili kuokoa tembo na faru pamoja na simba ambao wamekuwa wakiuawa kila siku na hivyo kuwa hatarini kutoweka kabisa. *Operation* hizo zinaweza kufanywa kwa kushirikiana na majeshi yote yakiwemo Polisi na Jeshi la wananchi (*JWTZ*); na

(e) Serikali na Mamlaka husika ni vema sasa ikashirikisha kikamilifu Usalama wa Taifa katika kufuatilia mtandao mzima wa ujangili nchini ili waweze kuubaini na kuuvunja kabisa kama si kuutokomeza kabisa. Lakini pia Usalama wa Taifa nao uangaliwe maana unaonekana kulegea au kusahau majukumu yake, hivyo Serikali iangalie na iwakumbushe Usalama wa Taifa wajibu wao ambao ni pamoja na kulinda rasilimali za nchi hii.

Tatu, kuhusu ukusanyaji maduhuli; katika kipengele hiki, Serikali kupitia Wizara hii iangalie utekelezaji wa ahadi zilizotolewa wakati wa Bunge la bajeti mwaka 2012/2013. Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya maduhuli ya Sh. 25,175,381,917/=, lakini katika mwaka 2012/2013, hadi mwezi Machi, 2013, Wizara kupitia Idara ya Wanyamapori imekusanya sh. 10,761,228,343 chini ya kiwango ilichokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua nini kilichopelekea au ni sababu zipi za kimsingi zimeifanya Wizara hii kupitia Idara ya Wanyamapori kutofikia lengo lake la makusanyo hayo?

Nne, ni kuhusu utalii wa ndani:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema sasa Serikali kupitia Idara ya Wanyamapori kuangalia uwezekano wa utaratibu wa kuwapa nafasi wananchi au vijiji vinavyozunguka mbuga waweze kutembelea mbuga zinazowazunguka, ikiwezekana

bila kiingilio chochote ili iwe chachu ya kuweza kushirikiana kikamilifu katika kuzilinda na kuzihifadhi mbuga zetu.

(ii) Ni vema sasa ujengwe utaratibu kupitia Idara ya Wanyamapori kuwa na utaratibu wa kuwinda wanyama kama swala na nyati ili kuwapatia au kugawa kwa wananchi angalau kila kaya ikapata kilo moja tu angalau mara mbili kwa mwaka kama kichocheo cha kuwafanya wananchi hawa waweze kuwa rafiki wa mazingira yanayozunguka mbuga za wanyama kama Mkoa wa Katavi.

Pia katika Mkoa wa Katavi wananchi kwa wakati husika waruhusiwe kupata kitoweo walichozoea hasa kabila la Wapimbwe (wadudu wanaitwa Madimu). Tunaomba wananchi hasa wa Tarafa ya Mpimbwe ama kwa kushirikana na *TANAPA* waweze kuvuna wadudu hao kwa kitoweo. Ombi hili maalum naomba lishughulikiwe ili kujenga mazingira rafiki na maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja katika Wizara hii kwa kuzungumzia kero zifuatazo kuhusiana na suala la mipaka, unyanyasaji wananchi unaofanywa na Askari wa Hifadhi ya Mikumi na Fidia ya mazao kutokana na wanyama waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipaka ya Hifadhi na Vijiji; kuna kero kubwa ya mipaka katika vijiji vinavyopakana na hifadhi na kupelekea usumbufu kwa wakulima na pia unyanyasaji wa Askari wa hifadhi dhidi ya wananchi. Ipo kero katika Vijiji vya Mkubilo, Kidudwe, Mzilia na Kunke. Hifadhi ya Wamimbiki inapakana na vijiji hivi na kupelekea migogoro, unyanyasaji wananchi. Naomba Wizara iingilie kati kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Hifadhi ya Mikumi chini ya *TANAPA* Askari pamoja na kuelewa mipaka mipya bado wanaingia Vijiji vya Maharaka na Doma na kupiga raia. Nimeomba kwa kuandika barua *TANAPA* na Wizara yako

kuwa askari hawa waache vitendo hivyo na pia *TANAPA* wafanye mikutano ya ujirani mwema na Vijiji vya Maharaka, Doma na Mkata ili kurejesha mahusiano mema kati ya *TANAPA* na wananchi wa vijiji hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia kwa uharibifu wa mazao; kumekuwepo na madai ya muda mrefu ya Wizara yako kuchelewesha malipo ya fidia za wakulima walioharibiwa mazao yao na tembo. Nimeandika barua Wizarani kwako kuhusiana na madai ya wakulima wa Vijiji vya Doma, Maharaka, Kata ya Melela na Dakawa. Naomba nipate majibu ni lini wakulima hawa watalipwa? Kinachosikitisha madai haya ni ya muda mrefu na pesa yenyewe ni kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvunaji mitiki Mtibwa; nimekuwa muda mwingi na ni kila mwaka tangu niingie Bungeni 2010, kuomba kuwapa kipaumbele wananchi wa vijiji jirani kupewa vibali vya kuvuna mitiki. Wananchi wa Vijiji vya Kumka, Lusage, Madizini, Dihiba wanasaidia kulinda mitiki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapokuja maombi ya wananchi wa vijiji jirani hawafikiriwi na badala yake hupewa Makampuni toka nje ya Mkoa na Wilaya. Ninachojua ni kweli Wizara hutoa vibali kwa njia ya *tender*, kwa njia hiyo je, vikundi vya wanakijiji watapataje? Naomba upendeleo wa wananchi wa vikundi vya vijiji jirani kupata vibali vya uvunaji mitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu na naunga mkono hoja.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Katika hotuba hii nitaongelea matatizo ya mipaka kati ya maeneo ya vijiji vinavyozizunguka au kupakana na Hifadhi, uvunaji haramu wa mbao katika maeneo ya Hifadhi (misitu ya hifadhi) na maeneo mengine, sekta ya uwindaji wa kitalii na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya mipaka; kwa muda mrefu kumekuwa na matatizo ya migogoro ya mipaka kati ya vijiji na maeneo ya hifadhi na taarifa za migogoro hiyo imekuwepo Wizara ya Maliasili na Utalii kwa muda mrefu sasa, bila Wizara hiyo kuchukua hatua za makusudi na za dhati za kumaliza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *records* za malalamiko hayo, Wizara inayo, ni mipaka gani inalalamikiwa Wizara ina *record*, hifadhi zipi zina migogoro, Wizara ya Maliasili inayo *records*. Je, ni kwa nini Wizara inashindwa kuchukua hatua stahiki za kusuluhisha na kumaliza matatizo au migogoro hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hadi lini Wabunge wa maeneo mbalimbali kila mwaka, kila *session* ya Bunge inapokuja wataendelea kulalamikia migogoro hii, kwa nini Wizara isifanye *crash programme* ya kumaliza migogoro hiyo yote ili migongano hii ya kimaslahi ya mipaka ikaisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa mpaka kati ya Selous *Game Reserve* na Kijiji cha Kikulyungu, Wilayani Liwale, umedumu zaidi ya miaka kumi sasa. Pamoja na kwamba Wizara ilikwenda kuhakiki mpaka, lakini haikufanya haki, Wizara ilipendelea upande wake wa Serikali na kuwaacha wananchi wakibaki na malalamiko mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo linalolalamikiwa ni dogo, Selous *Game Reserve* ni hifadhi kubwa sana. Ni vema sasa Serikali itumie tu busara kulirudisha eneo hili la bwawa la Kihurumila kwa wananchi, kama tangazo la Serikali la mwaka 1974 linavyosema ili kumaliza mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu ni vema uishe sasa kabla ya kuleta maafa kama yaliyotokea tarehe 23 Aprili, 2013 ya wananchi zaidi ya 20 Wilayani Liwale, kwa suala la stakabadhi ghalani zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa nia njema kabisa, imalize mgogoro huu na lakini niiombe tena

Serikali kwamba, eneo la Kihurumila katika Kijiji hiki cha Kikulyungu lirudishwe kwa wananchi na Serikali ya Kijiji cha Kikulyungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee tatizo la uvunaji mbao haramu, unaoendelea ndani ya misitu ya hifadhi iliyoko Wilayani Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na wimbi kubwa sana la uvunaji mbao haramu katika maeneo mengi ndani ya Wilaya ya Liwale. Cha kushangaza, Wizara ya Maliasili na Utalii, inafanya *operations* kila siku kila mara, ni kwa nini sasa tatizo hili la uvunaji mbao haramu haliishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa nyingi za kila mara na kila wakati zinazoashiria kwamba baadhi ya wafanyakazi wa Wizara ya Maliasili na Utalii na hasa wale wanaohusika na kitengo hiki cha misitu wanahusika kwa kiasi kikubwa na zoezi hili na wanashiriki katika vitendo hivyo huku wakidai wako kwenye *operation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Maliasili na Utalii hasa Mheshimiwa Waziri wa Wizara na *Management* yake ya juu, watengeneze timu ya kufuatilia suala hili na hasa Wilaya ya Liwale kwani kuna taarifa nyingi sana zinazohusu uvunaji huu haramu wa mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale kuna mbao ambazo zilikamatwa zipatazo kama 5000 *pcs* na watu wa Maliasili Kitengo cha Misitu. Ombi ninalolileta kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, zile mbao zilizorundikwa pale katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Liwale- Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ipewe zile mbao kwa ajili ya kutengeneza madawati kwa ajili ya Shule zetu za Msingi na Shule zetu za Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Wizara itukubalie mbao zetu zile watuachie tuchongee madawati, tutashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu kwa pori la akiba la Selous kubakiza asilimia 50 ya mapato yake *(retention)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuiomba Serikali na Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa *retention* kwa asilimia mia moja kwa pori hili la akiba la Selous. Mara nyingi, Idara ya Selous imekuwa ikishindwa kufanya doria na wakati mwingine kunapotokea wanyamapori kama vile simba, tembo na kadhalika kuchachamaa na kudhuru binadamu na mazao yao, Askari hawa wanashindwa kwenda au kuchukua hatua haraka kutokana na ama petroli au dizeli hawana, ama magari mabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja kubwa ya kurekebisha ugawaji wa mapato ya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa na kuleta bajeti yake hii nzuri iliyoandaliwa kwa umakini mkubwa ili kukidhi mahitaji ya wananchi katika sekta hii muhimu ya Maliasili na Utalii. Wizara hii ina umuhimu mkubwa sana katika kuliingizia pato Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza Serikali katika kuendelea kuipa kipaumbele wizara hii kwa kuzingatia umuhimu wake katika Taifa letu, pia kusimamia kikamilifu sekta ya misitu na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni kati ya nchi zenye vivutio vingi vya utalii Barani Afrika na duniani kwa

ujumla. Hata hivyo, japokuwa rekodi zinaonesha kuwa idadi ya watalii inaongezeka nchini, bado watalii wanaoingia nchini hawajakidhi kiwango kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo Serikali kutotoa kipaumbele katika kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hilo ndio husababisha kutokufikisha lengo la kupata watalii wengi kuja kutembelea nchini kwetu, ni vyema wizara na bodi ya utalii kwa kushirikiana na mashirika ya *TANAPA* na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA)* wakishirikiana na wadau wengine wakajiwekea mikakati ya kuvitangaza vivutio vya utalii vya nchi yetu katika sehemu mbalimbali duniani, badala ya kutegemea watalii wanaotoka katika nchi za Ulaya Magharibi na Marekani tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi kubwa zaidi zielekezwe katika masoko mapya kama vile ya Korea Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Brazil, India, Japan, Korea ya Kaskazini na nchi zilizokuwa chini ya himaya ya Urusi bila kusahau Soko la Nchi za Afrika Mashariki na Kusini. Kufanya hivyo kutasaidia vivutio vyetu kujulikana na kupata watalii wengi kutoka katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mkakati wa kuvitangaza vivutio vya utalii nchi za nje ukiendelea, ni muhimu pia Serikali ikatoa kipaumbele katika kukipa Chuo cha Taifa cha Utalii Dar es Salaam fedha za kutosha ili kiweze kutoa watumishi bora kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe chuo hiki kilijengwa kwa kiasi kikubwa cha fedha za ufadhili wa Serikali ya Ufaransa na hivi sasa licha ya kukamilika, kuwa na majengo bora, kinashindwa kufanya kazi kutokana na upungufu mkubwa wa Walimu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iangalie katika kuboresha vyuo vingine vinavyotoa fani ya utalii ili tupate wataalam wazuri katika fani ya utalii wenye kukidhi mahitaji ya wageni wajapo nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali iweke mkakati wa kukuza zaidi utalii wa ndani kwani kumekuwa na vikwazo kutokana na mahoteli mengi kumilikiwa na wageni na kutoza fedha nyingi za kigeni. Kufanya hivyo kunasababisha utalii wa ndani kutokukua kwa haraka kwa gharama kubwa kwa mwananchi wa kawaida. Naishauri Serikali kukaa na wawekezaji hawa na kuzungumza ili kuweka viwango tofauti kati ya mtalii wa ndani na wa nje ili kukidhi mahitaji na usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya tembo barani Afrika inazidi kupungua kutokana na kushamiri kwa ujangili. Taarifa za kitaalam zinaonesha kwamba hali ya ujangili wa tembo imefikia kiwango cha juu kabisa katika historia ya ujangili duniani ambapo tembo 42,800 wanauawa kila mwaka. Hapa nchini kati ya mwaka 2006 hadi 2009 Tanzania ilipoteza tembo 30,000 na sasa inapoteza takribani tembo 10,000 kila mwaka, wastani wa tembo 800 kila mwezi na 30 kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo yamebainika kukithiri kwa ujangili wa tembo ni ukanda wa uhifadhi wa Selous – Mikumi na ukanda wa uhifadhi wa Tanzania/Msumbiji wa Selous – Niasa. Kwa hali hiyo tunajikuta tukipoteza wanyama hawa muhimu na mwishowe wanaweza kupotea kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha ni ukweli kwamba, ujangili wa tembo unaongezeka kutokana na tofauti kubwa ya mahitaji halisi ya fedha za kudhibiti ujangili na fedha zinazotolewa pamoja na uhaba wa rasilimali watu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuchukua hatua za haraka iwezekanavyo ikiwa ni pamoja na kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kukabiliana na ujangili wa tembo na wanyamapori kwa ujumla ambao umekuwa tishio kubwa nchini kwetu. Pia kutoa kibali kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuajiri watumishi wa kutosha katika idara ya Wanyamapori na kurekebisha miundombinu katika mapori ya akiba ili

kunusuru kuangamia kwa tembo wa Tanzania kwa manufaa ya vizazi vya sasa, vijavyo na Jumuiya ya Kimataifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kukamilika kwa kanuni zinazosimamia Jumuiya za Hifadhi za wanyamapori na kuanza kutekelezwa, yamekuwepo malalamiko ya jumuiya hiyo hasa katika mgawanyo wa mapato ambapo jumuiya karibu zote zinadai kwamba mgawanyo huo haulengi kuziwezesha jumuiya hizo kujiimarisha na kujiendesha zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, mchanganuo wa mgawanyo wa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii unahusisha taasisi nne za *Tanzania Wildlife Protection Fund( TWPF)*, Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, Wilaya na Mamlaka ya Mapato *(TRA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi mgawanyo huu unaondoa kabisa dhana kwamba, maeneo hayo ya jumuiya ni mali ya vijiji na mapato wanayopata hayalingani na kazi wanayofanya ya kuyahifadhi maeneo ikiwa ni pamoja na kazi ya kuzuia na kudhibiti majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara kupitia upya kanuni hizo ili kukidhi matakwa ya wananchi. Hivyo, kuimarisha uhifadhi endelevu nje ya maeneo yanayosimamiwa na Serikali. Aidha, Wizara iwajengee uwezo wananchi wanaosimamia maeneo ya *WMAs* na kutoa ushauri na msaada wa kitaalam na kisheria kuhusu uhifadhi pale inapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mipaka limeendelea kuwa changamoto katika sekta ya maliasili na hivyo kuongeza migogoro kati ya jamii na hifadhi za Taifa na misitu. Naishauri Serikali kupunguza migogoro, wananchi wawe wanashirikishwa kwenye kuainisha na kuweka mipaka kati ya hifadhi na maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kutoa elimu ya kutosha na kuweka mikakati katika kuacha kutumia matumizi ya nishati ya mkaa na itafutwe nishati mbadala ili kulinda ukataji wa miti hovyo na misitu yetu. Pia itilie mkazo zaidi katika matumizi ya gesi, umeme kwa kushusha bei zake ili kupata watumiaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Idara ya Misitu na Nyuki imekuwa kitengo chini ya Idara ya Sera na Mipango baada ya kuanzishwa kwa Wakala wa Misitu na kwa kuwa suala la misitu na nyuki ni suala la kitaalam, kufanya hivyo imeonekana idara hii kuwa kitengo chini ya Idara ya Sera na Mipango ni kuua hazina ya utaalam wa watendaji wa misitu na nyuki na hivyo kupunguza ufanisi katika usimamizi wa Sera ya Misitu katika ngazi ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kupitia Wizara kuwa Idara ya Misitu na Nyuki ibaki kama idara inayojitegemea ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, napenda kuishauri Serikali iweke watumishi waadilifu, hususan katika maeneo ya mipaka ili kutoa huduma kwa watalii wanaoingia nchini kupitia maeneo ya mipakani. Hii itaondoa usumbufu kwa watalii katika vituo vya mipakani hali ambayo uharibu sifa nzuri ya Taifa letu katika nchi za nje kwamba ni nchi ya amani, watu wakarimu na yenye vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuajiri watumishi ikiwa ni pamoja na Wanasheria katika sekta za wanyamapori na misitu na malikale. Wizara iyatambue majengo ya kale/magofu ambayo yanafaa kuhifadhiwa na kutunzwa kwa mujibu wa sheria na yawe rasilimali ya Taifa na kutumika kama vivutio vya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maelezo; nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri

na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha Sekta ya Maliasili na Utalii inaendelea kuchangia pato la Taifa. Pamoja na pongezi hizo naomba kutoa ushauri katika mambo kadhaa kwa lengo la kuboresha ili Sekta ya Maliasili iweze kuchangia zaidi katika pato la Taifa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujangili wa tembo na wanyama wengine; kwa kuwa kumekuwepo na tatizo la ujangili wa tembo na uwindaji haramu wa wanyamapori, naomba kuishauri Serikali kuimarisha ulinzi katika mbuga zote za wanyama kuongeza Askari wa Wanyamapori katika mbuga zote za wanyamapori. Serikali ihakikishe kuwa inaongeza vitendea kazi vya kutosha kama vile silaha zenye nguvu, magari, rasilimali watu na fedha ili ulinzi uweze kuimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitalu; naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kuhakikisha vitalu vya uwindaji vinamilikiwa na Watanzania badala ya kuacha wageni peke yao ndio wawe wamiliki vitalu. Pamoja na pongezi hizi ningependa kujua, je, wanawake ni wangapi wamepewa vitalu hivyo kwa ajili ya uwindaji? Pia je, Serikali ina mkakati gani kwa kuhakikisha wanawake wanapata fursa na uwiano ulio sawa kati ya wanawake na wanaume waliokodishwa vitalu vya uwindaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hifadhi ya Taifa; Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha inakutana na wananchi wote wanaozunguka hifadhi ya Taifa kwa lengo la kuwasikiliza malalamiko yao na kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kuongeza maeneo ya utalii; pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali, ipo haja ya kuongeza maeneo ya utalii kama vile Maji Moto kule Siro Simba, Mkoa wa Mara, Butiama kwa Baba wa Taifa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mjusi *(dinasour)* wa Tanzania; niliwahi kwenda kumuona huyo Mjusi. Ana urefu sana na upana sana na uzito wa kilo 80. Huwezi kumuona Ujerumani mpaka ufanya *booking* ya miezi mitatu (3), ni utalii mkubwa sana. Anaingizia Ujerumani shilingi bilioni tatu (3) kwa mwezi. Kuna wafanyakazi 375 pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana na wa Ujerumani na tukaandikiana na *Memorandum of Understanding* hapo mwaka juzi na mazungumzo ya Mjusi huyo na Tanzania. Idara ya makumbusho walikuwepo na wanajua na pia Idara ya Malikale wote walikuwepo Ujerumani, kwa nini mpaka sasa hakuna maelezo yoyote tangu tulipokwenda na kuandikishana *memorandum* hiyo. Mambo kadhaa tuliyokubaliana yamefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo ya kina kuhusu:-

(1) Kurejesha Tanzania mjusi huyo; au

(2) Na sisi tupate pesa kiasi ili kuisaidia Tanzania kwa ujumla, pia na Mkoa wa Lindi ambao ni maskini, au

(3) Waje Lindi kutuwekea Mjusi mwingine ambaye wamesema kuwa, wapo Mijusi mingine huko Mipingo Lindi Milimani, waje wajerumani watutengenezee.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze suala la mipaka ya Hifadhi ya Selous na Vijiji vya Kata ya Mwaseni Wilayani Rufiji, limechukua muda mrefu sana na mgogoro katika Kijiji la Mloka na lenyewe limechukua muda mrefu. Naomba Serikali ishughulikie suala hili ambalo limesababisha hata vifo vya wakazi kadhaa ambao kutokana na mgogoro wa mipaka watu hao waliingia katika eneo ambalo ni la hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Jumuia za Uhifadhi za Wanyamapori kwa Kata za Ngorongo, Mwaseni, Utete na Kipogira ambalo mchakato wake umechukua zaidi ya miaka mitatu na kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi na viongozi wao ambao walishirikishwa katika zoezi ambalo limesimama bila ya maelezo yoyote. Naishauri Serikali iharakishe zoezi hili ili kuondoa malalamiko yote na kuwawezesha wananchi waweze kunufaika na maliasili inayowazunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuzisaidia Halmashauri mbalimbali ikiwemo ya Wilaya ya Rufiji katika kutenga maeneo ya uhifadhi wa misitu ambao utasimamiwa kwa ukaribu sana ili kupunguza uwezekano wa kuwepo kwa jangwa katika nchi yetu na mambo mengine yanayoendana na uharibifu wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza na naunga mkono hoja.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya Utalii ni vingi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, lakini bado Serikali haijaonesha nia ya makusudi kuimarisha Sekta hii ya Utalii katika Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara. Katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri imegusia kwa uchache maeneo ya Lindi na Mtwara kama vile Kilwa, Mikindani na kadhalika. Je, Serikali haioni umuhimu kwa kusimamia kwa karibu Sekta hii ya Utalii katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbuga ya Selous katika Wilaya ya Liwale ni kivutio muhimu kwa Utalii, lakini kwa muda mrefu Serikali ilikuwa ikitumia mbuga hiyo kwa kuvuna meno/ pembe za ndovu tu. Ni wakati muafaka kwa sasa kuanzisha utalii katika eneo hilo kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Lindi ni uwanja wa kihistoria katika Tanzania na Kusini mwa Jangwa la Sahara kwanza, Uwanja una njia sita (6) (*Running way*) na pili, ulitumika katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia 1939-1945.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam ni maeneo ya kihistoria, urithi wa Dunia. Imeonekana majumba mengi ambayo ni ya kihistoria yameanza kubomolewa na kujengwa mapya, kwa nini yale ambayo tumeyaainisha yasivunjwe tena na kuanza kuyakarabati.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu wake na uongozi mzima na wafanyakazi wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kusimamia sekta hii muhimu kwa uchumi na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumebahatika na kujaaliwa kuwa na utajiri mkubwa wa maliasili na vivutio vya utalii. Lakini ni dhahiri kuwa bado nchi yetu inakabiliwa na umaskini mkubwa na wengi wa maskini hawa wakiwa katika maeneo hayo yenye rasilimali hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ninavyoona mimi ni kutowafanya wananchi wa maeneo haya kuwa sehemu ya watekelezaji wa mipango ya Wizara. Tatizo lingine ni rushwa ambayo inafanya sekta hii kunufaisha watu wachache na hasa wa nje ya maeneo hayo na mwisho ni tatizo la elimu ndogo na uelewa mdogo wa wananchi na uwezo mdogo wa kuendesha shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kuhusu mapato, Serikali itenge Bajeti ya kutosha japo asilimia kumi (10%) ya mapato na fedha hii itokane kwanza na makusanyo ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kusimamia vyema ukusanyaji mapato, kuziba mianya ya wizi na rushwa kwa kuwashirikisha wananchi kuibua na kutoa taarifa za uhalifu unaofanywa kwenye maeneo yao na kwa vyombo husika kutoa zawadi kwa wapiga filimbi hao (*whistle blowers*) kwa usiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watalii, changamoto kubwa ni upungufu wa vitanda au mahoteli ya kukaribisha watalii. Tunashauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Uwezeshaji

na Wizara ya Fedha kutoa vivutio zaidi kwa wawekezaji wa utalii ili waweze kuruhusiwa kujenga mahoteli na *tented camps* bila kodi yoyote mwanzo hadi mwisho wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ujenzi unapoanza, basi mwaka wa kwanza alipishwe kodi ya asilimia 25, mwaka wa pili asilimia 50 na mwaka wa tatu asilimia 100. Hii itatuwezesha kupata mahoteli haraka na kwa hali hiyo kutuwezesha kupata watalii wengi watakaokuja kuona vivutio vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafunzo ya masuala ya huduma za kitalii; China na Ufaransa ina Vyuo vizuri sana vya Utalii. Kwa kiasi kikubwa wangeweza kutusaidia kufundisha wananchi wengi katika fani mbalimbali husika ili tupate wataalam zaidi wa kuja kuendesha mafunzo kwenye Vyuo vya Utalii nchini vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Vyuo vingi zaidi vianzishwe kwenye maeneo yote yenye vivutio ili wafanyakazi wenye ujuzi wawe wengi. Haya yote yafanywe na sekta binafsi na Serikali iwape motisha kwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wizara iunganishe huduma za utalii na utamaduni ili kutoa fursa kwa jamii mbalimbali kushiriki kwenye mahoteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu; kuna haja ya kuboresha miundombinu muhimu katika maeneo ya utalii na hii ikiwa ni pamoja na usafirishaji kama vile boti za kitalii, mabasi ya kuzungushia kwenye maeneo na kadhalika. Wizara itoe motisha kwa sekta binafsi katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama; suala la usalama na amani liendelee kupewa kipaumbele hasa sehemu ambazo Wapinzani CHADEMA wamekuwa wakisababisha vurugu na kutia wasiwasi watalii wanaotembelea Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Iringa na Kigoma, sehemu ambazo zina vivutio vikuu vya utalii, lakini

Taifa linakosa mapato kwa sababu ya usalama mdogo unaotokana na fujo za mara kwa mara zinazochochewa na viongozi wa CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanyamapori na usalama; Wizara ijitahidi kujenga Jeshi thabiti la Wanyamapori kuwapa mafunzo ya kisasa zaidi, kuwapa nyenzo za kisasa na kuwalipa vizuri ili wanyamapori wawe na ulinzi zaidi. Adhabu kali zitolewe kwa majangili ikiwemo ya kuwafunga maisha. Wananchi wanaowaficha nao pia wafungwe miaka mingi jela kwa kuchangia uhalifu. *Intelligential* izidishwe kwenye mapori yetu na mipakani kuwabaini majangili. Idara ya Usalama wa Taifa watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitalu vya uwindaji; hili limekuwa ni tatizo lisilokuwa na mwisho. Wizara itangaze wote waliopewa vitalu, muda wa umiliki na mapato waliyotozwa ili kuondoa utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malipo ya utalii; yalipiwe Tanzania kwa huduma zote zinazopatikana Tanzania.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaaliwa kuwa na wingi wa vivutio vya Utalii ulimwenguni na hivyo kuwa na fursa kubwa ya kiushindani katika sekta ya utalii. Taarifa mbalimbali zimekuwa zikiisifu Tanzania kwa kuwepo kwa vituo hivyo ikizidiwa tu na nchi kama Brazil.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo vivutio hivi vingetumika vizuri Sekta ya Utalii ingeweza kusaidia katika kutoa ajira kwa makundi mbalimbali wakiwemo vijana na hatimaye kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, pamoja na kuwa na fursa hii ya kimkakati katika kukuza Sekta ya Utalii nchini, ni jambo la kusikitisha kuwa kama Taifa tumeshindwa kutumia fursa hii hata kwa kufikia lengo dogo tulilojiwekea na kuwa na watalii milioni moja wanaotembelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwa muda mrefu Sekta ya Utalii ina nafasi kubwa ya kuendelea kuwa mhimili muhimu wa kukuza uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, kufanikiwa kwa hili kunategemea sana kufanya mambo muhimu kama vile kuongeza jitihada katika kutangaza vituo vya utalii vilivyopo kila kona ya nchi yetu, kuboresha miundombinu, kuboresha taaluma ya utalii ili kuwa na watumishi wenye elimu inayostahili na pia kuondoa urasimu katika maeneo mbalimbali ya sekta ya utalii na mikakati hiyo iende sambamba ya Serikali kuiwezesha *TTB* kifedha ili iweze kutangaza utalii ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfumo mbovu wa ukusanyaji wa mapato katika watalii wanaotembelea Mlima wa Kilimanjaro. Taarifa iliyokuwepo ni kuwa Kenya wanakusanya mapato mengi kwenye Mlima wa Kilimanjaro kuliko Tanzania. Hii inasikitisha sana kuwa Mlima wa Kilimanjaro upo Tanzania, kwa nini Kenya wawe wanakusanya mapato mengi kuliko Tanzania. Naiomba Serikali ilifuatilie jambo hili na ilipatie ufumbuzi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kudumisha amani ni wajibu wa Serikali na Watanzania kwa ujumla tudumishe amani itakayowafanya watalii wengi kuja kutembelea nchi yetu bila kuwa na amani, watalii hawatokuja kutembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada ya kutangaza utalii pia tuwahamasishe wawekezaji binafsi wawekeze kwenye utalii.

**MWENYEKITI:** Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Ole-Medeye nafikiri huyu atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa maana ya orodha na mgawanyo wa kiuwiano mlioupata hapa mezani leo.

Baada ya hapo basi tutaona utaratibu wa kufanya ama Mheshimiwa Naibu Waziri aanze, halafu akamalize kujibu

maswali na hoja hizo vizuri ili jioni tutakapokuja tuwe na kazi nyepesi ya kumalizia vifungu kwa muda wa kutosha. Mheshimiwa Ole- Medeye!

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na pia namshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amekuwa akituongoza katika majadiliano hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa ruhusa yako kurejea kwenye Kanuni zetu za Bunge, Toleo 2013 Kanuni 64(c) ambayo inatutaka kwanza kutojadili masuala yaliyo Mahakamani na Kanuni 64(d) inakataza kudhihaki jina la Rais na fasili ya (f) inatukataza kusema vibaya watu wengine na hasa wale wasio na uwezo wa kuja kujitetea humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikufurahishwa kabisa na kauli iliyotumiwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika hoja hii ya kutaja baadhi ya viongozi hususan viongozi wetu wastaafu ambao sisi na Watanzania wengine wote tunaamini wakati wa uongozi wao walifanya kazi nzuri sana ya kuliongoza Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu wa Awamu ya pili, mzee yule si kwamba tu alitufikisha mahali pa kuwa na uhuru tulionao leo hii wa kuwa na vyama vingi katika nchi hii bali ndiye aliyetufungulia uchumi wa nchi hii na kutufikisha hapo tulipo hivi sasa. Kwa hiyo, nimesikitishwa sana na kauli za Msemaji Mkuu wa Kambi katika hoja hii ya kumdhihaki Mheshimiwa Mzee Mwinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninalotaka kuzungumzia ni suala linaloagizwa na Katiba yetu sote tulioketi humu ndani ambao tumeapa kuilinda Katiba ya Taifa letu. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 27 inatuelekeza wajibu wetu sisi wa kulinda mali na rasilimali za Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani amezungumzia masuala ambayo alidai kwamba viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Serikali waliyafanya. Ninachojiuliza ni kwamba ni lini alipata taarifa juu ya kutendeka kwa vitendo hivyo na kama ni kabla ya Bunge hili kuanza kwa maana ya juzi alipowasilisha hotuba yake hapa Bungeni kwa nini hakutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Kwa sababu kwa kutokufanya hivyo amekiuka Ibara ya 27 ya Katiba yetu ya Jamhuri Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba Bunge lako Tukufu litafakari na kuona ni hatua ipi itachukuliwa dhidi ya viongozi ambao wanazo taarifa za uhalifu katika nchi hii lakini wakazificha kwa sababu wanazozijua wao. Hiyo inakwenda pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ambaye ametwambia hapa nchini kuna viwanda vya kusagisha meno ya tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba sana kwa maelekezo yako atupatie vielelezo na kutuongoza mahali viwanda hivi vilipo ili tuchukue hatua haraka sana ya kuwakamata wahusika na kuwachukulia hatua ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani amezungumzia sana suala la Wamasai na amegeuza Wamasai kama vile ni bidhaa ya kisiasa, alisema kwamba Wamasai hawana viongozi wa kuwatetea na alionesha kana kwamba kuna ombi lililowasilishwa kwake au Kambi yake kutoka kwa Wamasai ya kuomba msaada wa kutetewa eti kwa sababu viongozi waliowachagua wameshindwa kuwatetea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie hivi, viongozi wa Wamasai wapo imara, Wamasai siyo bidhaa, Wamasai ni Watanzania kama walivyo wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu lipige marufuku kutumia majina ya makabila kufanyia biashara humu Bungeni, kufanyia kampeni humu Bungeni. Wamasai wana viongozi imara wenye nia dhabiti ya kuwaongoza na kuwatetea wakati wote na hawajawahi kuomba msaada wa Kambi ya Upinzani katika migogoro au kero zinazowakabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kuwaambia kwamba *Roman* haikujengwa kwa siku moja na kwa sababu hiyo, nawahakikishia kwamba kero hizo ambazo wameita ni kero suluhisho lipo ndani ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake na watuachie hilo suala tutalimaliza sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijibu tu baadhi ya masuala ya Waheshimiwa Wabunge waliozungumza ambao masuala yao yanahusu migogoro ya maeneo ya mipaka katika nchi yetu baina ya vijiji na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia malalamiko au maelezo ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wameitaka Serikali kutoa maelezo. Tumemsikia Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka Mbunge wa Simanjiro na tumemsikia pia Dkt. Antony Mbassa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, maeneo ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge Serikali ilikwishapokea taarifa kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya zinazohusika na sisi tumekwishakaa na kutafakari juu ya hatua za kuchukua ili migogoro iliyopo ya mipaka baina ya vijiji pamoja na Hifadhi za Taifa kwa maana ya National *Parks* au *Conservation* zote pamoja na ardhi yote ya hifadhi kuweza kupata ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majuma mawili yaliyopita nilifika Kondoa, nilikwenda Kondoa kushughulikia masuala ya ardhi na katika taarifa ya Wilaya Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Timu yake waliwasilisha maelezo juu ya kero iliyopo ya mgogoro kati ya vijiji vya Wilaya hiyo na Hifadhi ya Mkungunero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wiki iliyopita tulikutana na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Juma Nkamia pamoja na Mheshimiwa Zabein Mhita ambao tulizungumza kwa pamoja juu ya migogoro iliyopo ya Hifadhi ya Mkungunero na Vijiji vilivyopo katika Majimbo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niliwasiliana na Waziri wa Maliasili na Utalii, tulizungumza na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na tulikubaliana kimsingi kwamba baada ya Mkutano huu wa Bunge kwa pamoja tutafanya ziara kwenye maeneo hayo. Pia tutafanya vikao vya pamoja na Viongozi wa Mikoa na Wilaya inayohusika wakiwemo na Waheshimiwa Wabunge ili tupate ufumbuzi wa kudumu ya migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imepokea maelezo ya Waheshimiwa Wabunge na kwamba tutayatafutia ufumbuzi bila kukawia kwa sababu tusingependa wananchi wetu waendelea kupata kero, tunataka washiriki katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuomba Bunge lako kwamba, kwa kuwa sasa imedhihirika wazi hasa kutokana na suala la usafirishaji wa meno ya tembo kwamba pengine huenda wenzetu waliowasilisha maelezo kupitia hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwamba huenda hawajui taratibu, sheria na kanuni zinazosimamia usafirishaji wa mizigo bandarini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ningeomba Bunge lako Tukufu litoe maelekezo kwa Wizara inayohusika kwamba

iandaliwe semina mahsusi ya kuelimisha Waheshimiwa Wabunge hao juu ya taratibu zinazotumika na Wakala wa Meli katika kupakia na kusafirisha mizigo bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nitamke wazi kwamba, naunga mkono hoja hii kwa dhati na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyokuwa nimesema orodha imeshakamilika ingawa naona Waheshimiwa Wabunge wengine wameingia, lakini nimeambiwa hawatachangia ingawa wapo kwenye orodha hii.

Kwa hiyo basi, naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri aanze kujibu hoja zilizowasilishwa na Wabunge. Makatibu wangu wataendelea kutunza muda kwa maana ya mgawanyo uliowekwa. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo ziliibuliwa wakati wa kujadili hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Nianze kutolea ufafanuzi hoja na mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati huu. Ufafanuzi huu umejikita katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa utalii, utangazaji wa utalii, mafunzo kuhusu taaluma za utalii, kuendeleza utalii wa ndani, kuboresha miundombinu na huduma za uendelezaji utalii na uhifadhi wa Mlima Kilimanjaro na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri muda utakavyoruhusu kuna mambo mengine ambayo nitayagusia. Katika eneo hili

Waheshimiwa Wabunge nane wamechangia au kwa kuongea au kwa kuzungumza. Baadhi yao wametoa mapendekezo na wengine wameshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira alipowasilisha Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Abuu Ahmoud Juma, Mheshimiwa Dustan Mkapa na wengine wamechangia wakisema Serikali iweke lengo jipya la idadi ya watalii ambao watatembelea nchi yetu kwa mwaka na ikumbukwe kwamba ilipofika mwezi Desemba, 2012 na kwa mara ya kwanza Serikali ilifanikiwa kufikisha lengo lake la kuweza kuwa na watalii nchini zaidi ya milioni moja na *to be precisely* ilikuwa ni 1,077,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya lengo hilo la awali kufikiwa, sasa lengo jipya la idadi ya watalii ni lazima lifanyiwe kazi kitaalamu, tuangalie na tuainishe masoko tuliyonayo. Moja ni yale masoko ya zamani ambayo ni *traditional markets* kama Jumuiya ya Ulaya, Amerika ya Kusini, lakini pia kumeibuka masoko mapya mengi moja likiwa ni soko la China na nchi za Mashariki ya Mbali ambalo Wizara inalifanyia kazi. Serikali italeta tamko hilo hapa Bungeni au katika vyombo vingine kuhakikisha kwamba tunaiambia dunia na Watanzania Azimio jipya la sisi kufikisha idadi ya watalii ambayo tunaikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuweka lengo jipya Wizara kupitia Bodi ya Utalii inaendelea kutekeleza mpango mkakati wa kutangaza utalii. Aidha, mkakati maalum wa kutangaza na kuhifadhi, Hifadhi za Kusini umewekwa na *TANAPA* imeweka kipaumbele katika uboreshaji wa miundombinu na kutoa maeneo ya uwekezaji kwa lengo la kuboresha huduma katika Hifadhi za Kusini na Kusini Magharibi. Aidha, *TANAPA* imefungua ofisi za utangazaji za Kanda ambapo kwa Kanda ya Kusini imefunguliwa katika Mkoa wa Iringa na Kanda ya Magharibi imefunguliwa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa miundombinu na huduma za kitalii. Kuhusu uboreshaji wa miundombinu na kuongeza huduma za malazi yaani hoteli na vitanda. Waheshimiwa Wabunge watano wamechangia na walianzia na Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili alikuwepo Mheshimiwa Abuu Hamoud Juma tena, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara tayari imeainisha maeneo ya uwekezaji katika hoteli katika Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na katika Mapori ya Akiba. Aidha, Wizara inaangalia utaratibu wa kisheria wa kutoa notisi kwa wawekezaji ambao hawajaendeleza maeneo ambayo walipewa kuwekeza kutokana na utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba katika kuwekeza kwenye hifadhi kunakuwa na utaratibu unaojulikana kama utaratibu wa kitaalam unaoonesha ni aina gani ya *lodge, camp* au hoteli, ukubwa wake, idadi ya watu, idadi ya vitanda ambavyo lazima viwekezwe katika eneo fulani. Utaratibu huu ndio unatoa mpaka, kwa mfano, Serengeti *National Park* tunaweza tukawekeza vitanda vingapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya nyuma kuna wawekezaji wengi sana wa ndani na wa nje kufuatana na ule utaratibu wa *General Management Plan (GMP)* ambao walipewa wawekeze. Kama walivyosema Wabunge wengi kutoka Chama Tawala na Upinzani wakizungumzia umuhimu wa sisi kuongeza utalii, hatutaweza kuongeza utalii kama watu ambao walipewa mahali pa kuwekeza wamekuwa madalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inatangaza rasmi kwamba, watu wote ambao tuliwapa maeneo ya kuwekeza wengine wamepewa miaka 10 iliyopita, wengine

miaka mitano, wengine mitatu, tutawapa notisi mara moja baada ya kikao hiki cha Bunge na Serikali imeazimia kuwanyang'anya yale maeneo na tutayatangaza upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawatangazia wananchi wote wazalendo walio tayari kuwekeza katika maeneo haya na wawekezaji wengine wa kigeni ili tuhakikishe kwamba tunaongeza uwiano wa vitanda sambamba na lengo letu la kuongeza watalii ambao tunataka waje hapa Tanzania kutembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuhamasisha utalii wa ndani tuna Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 11 waliochangia, naomba tu niende moja kwa moja na majibu. Wizara kupitia Bodi ya Utalii inaendelea kuandaa mkakati wa uendelezaji na utangazaji wa utalii wa ndani kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo wakati mkakati huo ukiandaliwa Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* limejenga na linaendelea kujenga malazi ya bei nafuu katika hizi hifadhi. Kama nilivyosema mwanzo tatizo kubwa tulilonalo ni malazi na hata sasa hivi maeneo mengi ya Ngorongoro na Serengeti wakati wa *high season* unaweza ukakuta maeneo haya yamejaa hadi miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu na tumekubaliana kwamba Mashirika yetu ya *TANAPA* wataendelea na wao kujenga malazi ya bei nafuu ili wananchi wanapokwenda kutembelea maeneo haya waweze kumudu gharama hizi na waweze kufaidi na utalii wa rasilimali zetu ambazo tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inahamasisha Mawakala wa Utalii kuandaa programu maalum za bei nafuu kwa ajili ya Watanzania kutembelea vivutio vya utalii na hizi tunaziita *incentive tours* kwa ajili ya wafanyakazi pamoja na kuhamasisha shule za msingi, sekondari, vyuo vikuu na

maeneo mbalimbali ya *academia* ili hawa vijana wetu waanze kuwa na ari na mwamko wa kutembelea hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu sote kwamba wanapoanza kuwa na ari ya kutembelea wakiwa wadogo, basi wataendelea kufanya hivyo watakapokuwa watu wazima. Aidha, gharama za kuingia kwenye Makumbusho na maeneo ya kihistoria pamoja na Hifadhi za Taifa ni ndogo kwa Watanzania na tunasisitiza Watanzania wote tuamke tujenge ile ari na mwamko wa kutembelea maeneo mbalimbali ambayo yana historia na kumbukumbu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taaluma ya utalii Wabunge wawili walichangia na Wizara kupitia Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii ikitathmini mtaala unaotumika kutoa mafunzo ya ukarimu na utalii kwa kushirikiana na wadau kwa lengo la kuuboresha mtaala huo. Kazi hii ya kurekebisha mtaala inategemea kukamilika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara itaweka mfumo wa kusimamia na kuratibu mafunzo na ubora wa utoaji huduma na kutoa ithibati kwa watoa huduma katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililojitokeza linahusu ufunguaji wa njia ya *Old* Moshi inayoanzia pale Kiboroloni, Kikarara na Kidia inayokwenda Mlima wa Kilimanjaro na kuimarishwa kwa usalama katika eneo hilo. Wizara kupitia *TANAPA* imepitia mpango wa usimamizi wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ambapo njia ya kupanda mlima kupitia njia ya *Old* Moshi sasa itafunguliwa rasmi na utaratibu huo wa kuifungua utawekwa na Shirika letu la *TANAPA*. Nikiwa pale pale Kilimanjaro naomba nikiri hoja ambayo aliitoa Mheshimiwa Freeman Mbowe kuhusu umuhimu wa Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua hatari ambayo Mlima Kilimanjaro inakabiliana nao. Moja ni hatari tu za mabadiliko ya tabianchi ambayo yanatokea duniani kote. Lakini la pili, ni ukweli kwamba miti katika Tanzania inakatwa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaangalia taarifa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana hapa wamelalamika wakisema kwamba, Wizara hii watu wakienda kuvua samaki hawaruhusiwi, wakiingia kukata kuni hawaruhusiwi. Kama Wizara haitachukua jukumu la kulinda hizi rasilimali za miti na kusimamia sheria zilizopo miti hii itatoweka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni kwamba, kuna misitu zaidi ya 160 inayosimamiwa na Halmashauri za Wilaya nchini kote. Misitu hii imepotea, misitu hii inaitwa misitu, lakini imekatwa yote, misitu ambayo sasa imebaki ni misitu ambayo bado inasimamiwa na Serikali Kuu na sisi tunasisitiza ushirikiano wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa narudia tena kusema kwamba, tutaongeza ushirikiano na Halmashauri katika kupanda misitu na kuhakikisha kwamba, watu hawajikiti kwenye kuvuna peke yake na mila hii ya kupanda misitu iwe ni sehemu ya kuendelea na mafanikio ya kuifanya Tanzania iwe ya kijani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika nikirudi kwa Mheshimiwa Mbowe kwa kipato ambacho Mlima Kilimanjaro inaendelea kuipatia Tanzania na wananchi ambao wanafaidika na (*numeracy)* biashara ambazo zinatokana na utalii wa Mlima Kilimanjaro, haiwezekani biashara hii ikawa endelevu, kama hatua za makusudi kama alivyosema Mwenyekiti wa CHADEMA, Mheshimiwa Mbowe hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hadi kufikia hapa tulipo tumeshajipanga na labda nitoe taarifa kwenye Bunge lako Tukufu, tayari Wizara chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe amekutana na Waheshimiwa

Wabunge wote wa Mkoa wa Kilimanjaro. Katika mkutano ule tumeazimia na Mheshimiwa Waziri amekubali kuanzisha mchakato maalum wa kuanzisha Mfuko Maalum wa kulinda na kuhifadhi *ecosystem* ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zitashirikisha wadau mbalimbali, hatua hizi hatimaye tutawashirikisha Wabunge na viongozi wote wa Mkoa wa Kilimanjaro na wadau kwa sababu *ecosystem* ni pana zaidi ya Mkoa wa Kilimanjaro wenyewe, inakwenda mpaka upande wa Kenya, inakwenda mpaka upande wa Mlima Meru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kulihakikishia Bunge lako Tukufu, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi na Wizara hii imeazimia kuhakikisha kwamba Mlima Kilimanjaro na *integrity* yake itabaki kwa kizazi hiki na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililoulizwa kwa hisia kali na Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Mbunge wa Lindi, ni suala la mjusi wa Tendaguru. Kuhusu suala hili Wizara imefanya majadiliano na Makumbusho inayohusika katika uhifadhi wa mjusi huyo nchini Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majadiliano hayo, Wizara imeandaa rasimu ya mapendekezo na utaratibu wa namna ya Watanzania wanavyoweza kunufaika na mjusi huyo. Wizara kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendeleza mazungumzo hayo kwa kuishirikisha Serikali ya Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo hayo yatalenga kuona fursa zinazoweza kuchukuliwa kwa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Wizara itaendelea kumshirikisha Mheshimiwa Mbunge na wadau wengine ili wajue kinachoendelea na hatimaye matokeo ya majadiliano hayo yatawasilishwa kwa wadau na tutakuwa na furaha ya kulijulisha Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba, baadhi ya vijifungu kukadiriwa kukusanya sh. 1,000/= ni

namna ya kuficha mapato kwa lengo la kufanya ubadhirifu. Naomba kutoa ufafanuzi kuwa makadirio haya yamewekwa kama *token* kwa ajili ya kushikilia kifungu kwa makusanyo ambayo Wizara haina uhakika wa kuyakusanya kwa mwaka huo kutokana na sababu mbalimbali. Hata hivyo, hali hii haizuii Wizara kukusanya fedha zaidi pale ambako fursa ya kukusanya itajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutoa vibali vya uwindaji wa kitalii kwa kampuni zenye madeni, napenda kutoa ufafanuzi kuwa, kwa msimu wa uwindaji wa mwaka 2012/2013, Kampuni zote saba zenye madeni ambazo ni Malagarasi *Hunting Safaris*, Mwanahuta *& Company Limited, Usangu Safaris Limited, Rana Tours and Safaris Limited, Coastal Wildness Tanzania Limited* na *Kilimanjaro Game Trade Limited,* hazikupewa vibali vya uwindaji wa Kitalii isipokuwa Kampuni ya *Saidi Kawawa Hunting Company* ambayo ilimaliza deni lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, imekamilisha makubaliano ya ukusanyaji wa tozo ya maendeleo ya utalii, hivyo Wizara inatarajia kuanza kukusanya tozo hiyo kuanzia Julai 1. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa maduhuli mbalimbali yakusanywayo na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ilianza kutumia mfumo wa kompyuta katika utoaji wa vibali vya uwindaji na ukusanyaji maduhuli yatokanayo na uwindaji wa kitalii. Mfumo huu umeonesha ufanisi mkubwa hasa kuondoa tatizo kubwa la madeni ambalo lilikuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha 2013/2014, Wizara itaanza kutumia mifumo ya kompyuta katika ukusanyaji wa tozo na ada mbalimbali zikusanywazo na Idara ya Utalii pamoja na ada za viingilio na uhifadhi ikusanywayo na Idara ya Wanyamapori kupitia utalii wa picha katika Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu, Mapori ya Wazi na Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya mfumo huu kuanza, Wizara itaongeza ufanisi na uwezo wa kukusanya maduhuli na pia itapunguza kiasi kikubwa cha mianya ya uvujaji wa maduhuli na madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kutolea ufafanuzi ni kuhusu kuvunjwa kwa iliyokuwa Idara ya Misitu na Nyuki na kuhamishia baadhi ya majukumu yake katika Idara ya Sera na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, baada ya kuanzisha Wakala wa Misitu Tanzania *(TSF)* muundo mpya wa Wizara ya Maliasili na Utalii ulioidhinishwa tarehe 3 Juni, 2011 umeiondoa Idara ya Misitu na Nyuki. Shughuli nyingi zilizokuwa zinatekelezwa na Idara hiyo pamoja na watumishi yaani wataalam wamehamishiwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Aidha, kwa mujibu wa muundo mpya wa Wizara Shughuli za Kisera kuhusu misitu na nyuki pamoja na wataalam husika zimehamishiwa Idara ya Sera na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mabadiliko haya ni kuleta ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Wizara. Hata hivyo, endapo katika utekelezaji wa muundo zitaibuka changamoto muundo huu utaangaliwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kukuhakikishia kuwa, maoni na mapendekezo yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ili kuimarisha Sekta ya Maliasili na Utalii tutayathamini, tutayaangalia na yote haya kwa pamoja tumeyaandalia bango kitita, tutahakikisha kwamba, kila Mbunge atajibiwa hoja zake moja moja kwa maandishi pale ambapo alituletea ama aliongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kipindi hiki kwa kusema kwamba, Serikali hii sio tu imejizatiti kuhakikisha kwamba, misitu itakuwepo miaka mia moja ijayo,

lakini watu wote ambao kwa sababu moja au nyingine wamejiandaa kuvunja sheria, wamejiandaa kuiba hii misitu, sisi tutaongeza nguvu, tutaongeza meno, tutaongeza ukali wa kusimamia sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali haitamuonea haya mtu yeyote ambaye kwa namna yoyote atahusika moja kwa moja au vinginevyo katika kuhujumu au katika kujihusisha na suala la ujangili na nitamwachia Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anamalizia alielezee vizuri suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipanga na sio tu tumejipanga, tumeomba na tumeruhusiwa katika mwaka huu wa fedha tunaajiri vijana 1,000 ili waweze kuingia katika mapori yetu, kama Maaskari wa Wanyamapori. Tunao vijana Pasiansi ambako nimetembelea na Mheshimiwa Waziri ametembelea. Tunao vijana pale Mweka, tunao vijana wanaomaliza *SUA*, tunao vijana wanaomaliza vyuo vingine wajiandae kwa sababu ajira inakuja kama mvua. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikumbushe jambo moja hapa, hadi kufikia sasa hivi tulikuwa na takribani watu 400 ambao wanafanya kazi kama Maaskari wa Wanyamapori katika misitu yote nchini, kuanzia Selous kwenda Moyowosi kwenda sehemu yoyote, lakini idadi hii sasa hivi tutaiongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alielekeza tunategemea kufikisha idadi ya Maaskari wa Wanyamapori 4,000 ili tuweze kufikisha kiwango ambacho kwa kweli kinastahili, kwa sababu sasa hivi nadhani wastani, askari wetu mmoja analinda zaidi ya kilomita 147 za mraba. Kwa kweli kwa mtu mmoja kuweza kusimamia ujangili katika eneo la kilomita za mraba 147 peke yake, ni jambo gumu sana na naliomba Bunge lako Tukufu lituunge mkono katika kuongeza vitendea kazi.

Ni rahisi sana wakati mwingine kulaumu lakini mimi na Mheshimiwa Waziri tumeenda katika mapori haya. Tumekutana na hawa vijana, hali ambayo wanayo, upungufu wa magari, upungufu wa vitendea kazi na bajeti hiyo inaendelea kuandaliwa na ninaomba Bunge lako Tukufu liendelee kuunga mkono hoja ambazo zinatoka katika Wizara hii, ikiwa ni pamoja na hoja hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameiotoa ili tuhakikishe kwamba tunainusuru nchi yetu na kupotea kwa wanayama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwahakikishie vilevile kwamba Serikali hii itahakikisha tembo wako miaka 2000 ijayo, miaka 3000 ijayo kwa mikakati ambayo tunaiweka. Mikakati hii ambayo tunaiweka haihusu kuongelea tu, kuna mikakati inaendelea ambayo hatuwezi kuizungumzia hapa kutokana na unyeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapopambana na majangili una pambana na mtandao, unapambana na watu wanaopanga kufanya uhalifu usiku, wanapanga wakiwa wamelala makwao, wanawasiliana katika mitandao mbalimbali, tunaendelea kuinasa hiyo mitandao, tunaendelea kuzungumza na *Interpol* Duniani, tunaendelea ku- *monitor* usafirishaji katika bahari kuu, tunaendelea kuwasiliana na nchi ambazo mali hizi zinapelekwa. Ndiyo maana moja ya jambo ambalo ningependa Serikali hii ipate *credit,* ni hatua ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamezisikia, majangili ambao wamekamatwa katika muda mfupi na wako katika vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme katika ziara yangu mimi binafsi nilipokuwa ninatembelea eneo la Serengeti, nilifika mahali ambapo nilikutana na majangili ambao wameuawa. Nilikutana na miili ya watu wanne ambao wameuawa ilikuwa inasikitisha lakini kazi ya kupambana na majangili itaendelea na ninaomba viongozi wa vyama vyote vya kisiasa, kwa hili kwa sababu ya unyeti wa maslahi ya Taifa, ninaomba wote tuungane, ninaomba tuilinde nchi yetu na maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maneno yako mazito kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, ile saa nne nilimwona Mheshimiwa Mnyaa akiomba Mwongozo lakini sasa simuoni, kwa hiyo, ninaondoa huo Mwongozo wake. Nilimwona Mheshimiwa Mnyika nitampa nafasi, nilimwona Mheshimiwa Mkosamali hayumo humu ndani ninaondoa Mwongozo wake na nilimwona Mheshimiwa Ole- Sendeka. Ninaomba hao niliowataja sasa wapate nafasi ya kutoa Miongozo yao.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 46 (1) kwamba Waziri ameulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa isipokuwa kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi, Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza kabla ya muda wa kujibu swali hilo haujafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema leo kulikuwa na swali la msingi ambalo nililiuliza, Namba 131 na swali hili nitasoma mstari wa kwanza tu wa swali kwenye ukurasa wa tatu, mstari wa kwanza mpaka wa tatu, je, ni hatua gani imefikiwa katika kuwarejesha wanafunzi waliofukuzwa na waliosimamishwa katika vyuo vikuu mbalimbali vya umma ikiwa ni pamoja na...

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali langu lilihusu vyuo vikuu mbalimbali vya umma, vyuo ambavyo nilivitaja, vilikuwa ni vyuo vya mfano tu kwa maana kwamba nimeweka msisitizo. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake hakugusa vyuo vyote ambavyo vilikuwa vinahusika na nilipomuuliza kwenye swali la nyongeza kwamba majibu haya siyo, hayajakamilika hata katika vyuo alivyovitaja takwimu alizozitaja siyo sahihi, Mheshimiwa Waziri

akajibu yeye ndiyo Serikali ndiyo ana takwimu sahihi. Wakati kimsingi jibu hili ni wazi kuwa halijakamilika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la ziada, nilipoomba kwa mujibu wa kipengele (b) la swali langu kwamba ile ripoti iletwe na Serikali Bungeni, Waziri akarusha huo mzigo tena kwenye Kiti cha Spika kwamba kama Spika ataruhusu ripoti iletwe wakati ni ripoti ya Serikali mwenye wajibu wa kuileta hapa Bungeni ni Serikali na tayari mimi kama Mbunge kama sehemu ya kusimamia Serikali nilishaomba ripoti iletwe Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba Mwongozo wako maana hata Mheshimiwa Mkosamali alipouliza swali lake la nyongeza la sehemu ya *means testing* hakujibu kabisa swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkosamali. Ningeomba Mwongozo wako ili swali hili liweze kujibiwa kwa usahihi, lakini pia hii ripoti iweze kuletwa Bungeni hapa hatua ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuomba Mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68 (7) na Kanuni ya 64(1)(e)(f)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kufuatia maelezo au mchango wa Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii ya Maliasili, Mchungaji Msigwa alipokuwa akichangia leo. Miongoni mwa maneno aliyoyasema ni kwamba Wabunge Wamasai wamewatelekeza wananchi wao, ni kauli ambayo kwa mujibu wa Kanuni ya 64 ni ya kuudhi. Siyo hiyo tu lakini kwa kiasi kikubwa Mchungaji wangu amepotosha ukweli ilihali akijua kabisa kwamba kwa miaka saba ya Ubunge wangu katika hotuba zote nilizozitoa na mchango wangu Bungeni kamwe sijawahi kuacha kuwasemea wananchi wa Loliondo na Ngorongoro. Kwa miaka saba ya Ubunge wa Mheshimiwa Telele, hata kama hakumbuki mengi, atakumbuka kuwa

Mheshimiwa Telele amezungumzia wananchi wa Ngorongoro kwa kiasi cha kutosha. Siyo hivyo tu alitoa maelezo ya Mbunge hapa Bungeni na mimi nikaunga mkono kupendekeza kuundwa kwa Kamati ya Ndugai na Bunge likaunda Kamati ya Ndugai kwa ajili ya mgogoro wa Loliondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha suala hilo ni kwamba hotuba yake, robo tatu ya maudhui yaliyomo katika suala la Ngorongoro na suala la Loliondo, ni nukuu halisi ya Ripoti ya Tume ya Mwigulu iliyokuwa na Wamasia wawili, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Sendeka wa Simanjiro lakini leo anasema Wamasai hawa, ananukuu yale yenye mvuto wa wapiga kura wa Loliondo na Ngorongoro ambayo yametokana na Tume ya Mwigulu iliyokuwa na Wamasai hao lakini baadaye anasahau ghafla anasema kuwa Wamasai wamewatelekeza Wamasai wenzao huku akitumia maneo yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiacha dhihaka kwa Rais na maneno ya kudanganya wananchi kuwa *OBC* anamilikishwa eneo na siyo kuwa ni mwindaji sawasawa na wawindaji wengine, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa pamoja na heshima yote ninayompa kama Mchungaji na rafiki yangu mpendwa, nilipenda tu nibainishe bayana kuwa tangu niingie Bunge hili, ukurasa mmoja wa taarifa ya Upinzani uliozungumzia Loliondo na Ngorongoro ni hii ya leo, ndiyo ya kwanza. Kwa hiyo, kama ni mapenzi kwa wananchi wa Ngorongoro na Loliondo, ni mapenzi ya dharura akitumia utafiti uliofanywa na Tume ya Mwigulu kuwashawishi Watanzania na ilhali anajua kabisa kwamba Mheshimiwa Kagasheki na Waziri Mkuu Pinda wanategemea kutoa kauli juu ya hatma ya eneo lile la Loliondo ili ionekane kuwa ni shinikizo la Upinzani na huku akijua kuwa Kinana aliunda Tume na Tume hiyo ndiyo anayonukuu ripoti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuomba Mwongozo wako pale Mbunge anapodanganya na kuongopea umma huku akijua kabisa kuwa sisi ni watetezi halisi na huku akidanganya kuwa yeye ni mtetezi wa Wamasai na akijua dhahiri kuwa hata kama anataka umaarufu kwa Wamasai,

Wamasai hawamtumi mtoto, wanamtuma mtu mzima na utoto kwa tafsiri ya Kimasai akawaulize hao, unaanzia wapi, unakomea wapi na utu uzima unaanzia wapi. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako kufuatana na Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ni chombo cha wananchi na kwa sababu Bunge hili ni chombo cha wananchi, ni wajibu wa Wabunge wa pande zote mbili kwa maana ya Chama Tawala na Wabunge wa Vyama vya Upinzani kutumia kikamilifu muda wa Bunge hili kufanya mambo ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika orodha za kazi zilizokuwa zimepangwa kufanyika ndani ya Bunge, ilipangwa Wabunge 18 waweze kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Maliasili. Katika Wabunge 18 waliopangwa kuchangia, Wabunge kutoka Chama cha Mapinduzi kwa maana ya Wabunge kutoka upande wa Serikali, Wabunge wengi hawakuchangia na katika idadi hiyo kubwa ya Wabunge wamechangia Wabunge wa nne tu na muda wa Serikali na muda wa Bunge umepotezwa bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza fedha nyingi kwa ajili ya kuweka vikao vya Bunge, vyama vingine vinaziba nafasi ya Wabunge wengine kuchangia halafu havileti wachangiaji hapa ndani, matokeo yake katika Wabunge 18 leo ambao walistahili kuchangia ndani ya Chama cha Mapinduzi wamechangia Wabunge wachache na tunapoteza saa nzima katika michango ya asubuhi ya leo bila kuwa na michango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako

ni kwa nini nafasi kama hizo zinapojitokeza, pale ambapo wenzetu wa upande wa pili hawaoni sababu ya kuchangia, nafasi hizo mkazitoa kwa Wabunge wa Vyama vya Upinzani tukaendelea kuchangia kwa faida ya nchi yetu, ahsante. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo utautoa lakini mimi ninatoa taarifa, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mbowe.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kutoafikiana na maaelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuwe watulivu, unajua kama mtu ana hoja atapata nafasi.

**MBUNGE FULANI:** Hajaruhusiwa.

**MWENYEKITI:** Nimeshamruhusu, Waheshimiwa Wabunge hebu tuwe watulivu.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu**.**

**MBUNGE FULANI:** Bangi!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumfahamisha Ndugu yangu Mbowe kwa sababu wakati tunapitisha marekebisho ya Kanuni yeye na mimi ni Wajumbe wa lazima katika Kikao hicho cha Kanuni, kwamba majina haya yanaorodheshwa kutokana na maombi ya wachangiaji wenyewe, Mbunge binafsi anaomba nafasi kwa kuonyesha nafasi ya kwanza ni ipi, nafasi ya pili ni ipi, nafasi ya tatu ni ipi. Kwa hiyo, Mbunge mwenyewe anao uwezo wa kuchagua

nini hotuba muhimu kuliko nyingine katika zile alizoziomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ambao hawakuja leo ambao wameorodheshwa na Bunge siyo mimi kama *Chief Whip,* wamechukua maombi yao katika hotuba ambazo walipendekeza ziwe katika chaguo la pili, la tatu na la nne. Kwa hiari yao ambayo wanaruhusiwa Kikanuni wamesema hotuba zao watazitoa kwenye Wizara nyingine ambazo walizipa umuhimu wa kwanza na siyo hii.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wangekuwa wanapitia, Mheshimiwa Mbowe anayo orodha ya wachangiaji na maombi yote, wote ambao hawakuchangia leo halikuwa chagua lao la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninataka kutoa taarifa kuwa, mimi ndio ningelalamika kwamba Wabunge wangu wa CCM hawakujitokeza. Aidha, nataka kutoa taarifa kuwa Wabunge hawa hawakujitokeza siyo kwa bahati mbaya ila wameamua kuchangia hotuba ambazo walizipa umuhimu wa kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamesimama wakiomba kupewa nafasi ya kuzungumza)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba mketi wote mliosimama, Miongozo imeombwa kwenye Kiti na haijaombwa kwa mtu mwingine zaidi ya kiti. Kwa hiyo, kwa mamlaka ya Kikanuni ninatakiwa kutoa majibu ya Miongozo kama Kiti na nitatoa kama ifuatavyo:-

Nitaanza na hili suala la mwisho la Mheshimiwa Mbowe, ninaomba niwaambie Watanzania, kwa mujibu wa Kanuni tulizonazo sasa, utaratibu wa uchangiaji ndani ya Bunge unakwenda kwa uwiano wa Vyama lakini vilevile unakwenda kwa mgawanyo wa dakika za uchangiaji ndani ya Bunge kwa kuzingatia uwiano huohuo wa Vyama. *(Makofi)*

Taarifa niliyoletewa hapa Mezani kwangu, ninafikiri Mheshimiwa *Chief Whip* alikuwa ametoka kidogo kuelekea kwenye Kikao cha Kamati ya Uongozi ya Chama, Wabunge watano wa Chama cha Mapinduzi wameziacha dakika zao zitumiwe na Mawaziri wa Serikali kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Hiyo ndiyo taarifa niliyonayo hapa Mezani. Ndiyo maana niliwaambia nitatoa Miongozo kwa sababu taarifa zote ninazo mie hapa kwenye Meza yangu. *(Makofi)*

Nalisema hilo kwa sababu gani? Kama zinabakia dakika za Chama cha Upinzani na mmeona hapa, juzi nilikuwa hapa Mezani Mheshimiwa Kasulumbayi hakuwepo, nilipokea ombi kutoka kwa *Assistant Chief Whip* wa Upinzani akiniambia kwa sababu Mheshimiwa Kasulumbayi hayupo, nafasi yake itatumiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya akigawana na Mheshimiwa Susan Kiwanga. Mheshimiwa Kasulumbayi ndio alikuwa kwenye orodha ya majina juzi lakini kwa kuwa hakuwapo nafasi ile ilitumiwa na Wabunge wa CHADEMA.

Kwa hiyo, utaratibu Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni ninadhani hata wewe unafahamu na tulipokuwa katika kikao cha Kanuni, tulikubaliana kuwa Mawaziri kama wanataka kutumia muda wa ziada hawataruhusiwa kutumia nyingine zaidi ya dakika za Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, wagawane na Serikali yao katika yao katika kujibu hoja na kusema lolote ambalo labda Mawaziri wangetaka kulifanya ndani ya Bunge. Kwa hiyo, huo ni mgawanyo ambao tulikubaliana wote katika kikao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba nikuambie Mheshimiwa *Chief Whip* kuwa huo ni utaratibu ambao nimeupokea hapa Mezani. Sasa na hilo lingine unalolisema inawezekana hawa Wabunge wameomba mara tatu, mara nne lakini utaratibu nilioupokea hapa Mezani ni huo. Mtaona dakika alizozitumia leo Naibu Waziri zimekiuka, siyo kwamba zimekiuka, ametumia nusu saa zaidi kwa sababu ameenda kupunguza dakika za wale wachangiaji ambao ni wa Chama cha Mapinduzi waliorudisha dakika zao kwa Serikali ili waweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huo ni ufafanuzi wa kwanza, uko Kikanuni na ninaomba niwathibitishie Watanzania kuwa kikao hicho tulikubaliana hivyo na ninakumbuka ilikuwa ni kazi ngumu sana mle ndani tukiulizana kama Mawaziri watataka kusema watumie dakika za nani? Tukakubaliana Mawaziri wakitaka kusema, watumie dakika za Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, hicho ndicho ninachotaka kusema.

Baada ya kutoa Mwongozo huo mimi sijaona kama tutakuwa tumepoteza muda na dakika hizi zilizobaki bado Serikali imeomba sasa itazitumia kufanya maandalizi ya kujibu hoja zilizobakia na baada ya kufanya maandalizi ya kujibu hoja hizo tutakapofika jioni wataendelea kushughulika na kujibu hoja hizo ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kiti kimekubaliana na hilo kwa sababu suala tunalolizungumza ndani ya Bunge la Hoja ya Maliasili siyo suala la mchezo. Wabunge mmezungumza sana kuhusiana na tatizo kubwa la kupotea na kuuawa kwa wanyama wetu katika mbuga zetu za Taifa lakini masuala ya ujangili yamezungumzwa kwa nguvu sana na tunaiomba Serikali kwa kutumia dakika hizi wakafanye kazi ya kutosha na kutuletea majibu ya kutosha ndani ya Bunge hapo jioni.

Mwongozo wa pili, ni Mwongozo wa Mheshimiwa Ole-Sendeka. Mheshimiwa Ole- Sendeka yeye amezungumza mambo mengi lakini akinukuu kuwa kauli zilizotumika humu ndani zilikuwa wakati mwingine ni kauli za kuudhi, lakini vilevile ametoa picha na kutoa maelekezo ni kwa kiasi gani Wabunge wanaotoka maeneo ya Wamasai walivyokuwa imara kuwawakilisha wananchi wao na siyo kweli hivyo ilivyoelezwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninamshukuru Mheshimiwa Ole- Sendeka pia ametoa taarifa ambayo ilikwishakutolewa na ninadhani Waziri mwenyewe pia ataisema kwamba tayari Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri mwenye dhamana mwenye dhamana anayo nafasi na amejipanga kuja kutoa maelezo kuhusiana na jambo hilo kwa ufasaha zaidi.

Sasa Mheshimiwa Ole- Sendeka pamoja na hayo

yote, hoja yake pia ilikuwa ni mjumuiko wa mambo mengi kwa hiyo Mwongozo wangu ni kama ufuatao:-

Kwa kuwa, kauli hii imeachwa kwa Serikali yetu kuishughulikia na Serikali ndiyo inayojua nini kinachoendelea na nani amefanya nini ukilinganisha na Wabunge hawa wa CCM na Wabunge wa Upinzani, mimi ninadhani Waheshimiwa Wabunge tuisubiri kauli hiyo ya Serikali, itatupa ukweli wa jambo hili kama Serikali haijafanya kazi au imefanya kazi. Kwa hiyo, hakuna haja ya kulumbana, Serikali itatoa maelezo hayo fasaha kwa mujibu wa utaratibu na jinsi hali ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mnyika, yeye aliuliza kwa nini swali lake halikujibiwa vizuri hilo la kwanza na ameulia kwa nini kauli ya Serikali isiletwe Bungeni ingawa Waziri aliomba Mwongozo wa Kiti changu kama anaweza kuileta kauli hiyo Mezani. Kwa hayo mawili, la kwanza Serikali ninawaomba wao wenyewe wakalitizame suala la ripoti hiyo kwa undani na kuona ni kwa namna gani wanaweza kutoa taarifa kwa Wabunge kuhusiana na kile kinachojiri kwa utaratibu ambao watakuwa wamepanga kupitia kwenye Meza ya Spika ama kadri watakavyoona inafaa watatutaarifu katika ofisi ya Bunge.

Kuhusiana na suala la kutofurahi kutojibiwa sawasawa, ninakushauri, unaweza kulileta swali hilo kwa namna nyingine likiwa *specific* sasa likiuliza katika eneo husika linalotakiwa na Mheshimiwa Waziri ninamwomba ajiandae kujibu swali hilo vizuri na ipasavyo na kama unaona hiyo haifai unaweza kutumia Kanuni zetu ambazo zinakuruhusu pia kufanya vinginevyo ama kuleta maelezo yako binafsi ama kuleta hoja binafsi, ama kufanya kitu kingine chochote ambacho Serikali itakuwa bado ina wajibu wa kusikiliza na kutoa majibu ambayo yatakuwa ni majibu yaliyokamilika ya kutaka kutoa maelezo ya kile ambacho ulikuwa unafikiria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa majibu ya Miongozo hiyo, ninaomba niiombe Serikali ikafanye kazi kama tulivyokubaliana ya kupitia hoja zote vizuri kabisa na kuja hapa na majibu ambayo Watanzania watapenda kuyasikia

kuhusiana na suala zima la Maliasili katika nchi yetu ya Tanzania.

Ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.20 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kipindi chetu cha jioni baada ya mapumziko ya mchana ambayo tumeyatumia kwa shughuli mbalimbali za Kibunge za kuwawakilisha Watanzania. Sasa tunarudi tena na tunaendelea na shughuli ya leo. Niwaambie tu Watanzania wote kwamba bado hoja iliyopo Mezani kwetu ni hoja ya Serikali ya kupendekeza makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na majadiliano ya mchana huu yanatupelekea moja kwa moja kumwita Waziri mtoa hoja ili aweze sasa kujibu hoja zilizowasilishwa na Wabunge katika mjadala huu na hatimaye tutaingia kwenye hatua nyingine. Waziri atakuwa na dakika sitini kwa maana ya saa moja. Waziri tafadhali!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaomba nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja mbalimbali ambazo zimewasilishwa na Wabunge wakati wa kujadili bajeti ya Wizara yangu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge wengi tumekuwa tunasema ni mahali ambapo wale wanaotutuma wanatutuma kwa dhamira ya kwamba tuje tuwawakilishe, tuje tuwatetee, ni mahali ambapo nachukulia kwamba panakuwa na mijadala wala si mahali ambapo panakuwa

na mvutano wa matusi ama mvutano wa kuwa na lugha ambazo kwa kweli siyo za Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nichukue muda huu kujibu hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la ujangili. Inavyoelekea katika kuweka hoja ndani ya Bunge hili, tumetuhumiwa sana kama Wizara lakini pia tumetuhumiwa sana kama Serikali na mbaya zaidi Chama ambacho kinazaa Serikali hii na chenyewe kimetuhumiwa. Tumelifanya hili likawa ni suala la kisiasa na tukalitizama katika mtizamo ambao nasema ni mtizamo finyu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujangili, ni sahihi lipo hakuna anayekataa, lakini ningeomba tukiri kwamba ni suala ambalo tusilitizame katika miwani ya Kitanzania kusema kwamba ni suala ambalo ni la Tanzania pekee. Nitakuja katika upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Desemba mwaka 2012, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani, Bi. Hillary Clinton, aliitisha mkutano *State Department* na ilikuwa ni muda mfupi tu kabla hajaondoka ofisini, akalitambua tatizo hili na akasema ni tatizo la kimataifa. Kubwa zaidi akakiri Mama Clinton kwa kusema kwamba katika nchi ambazo zinapokea na kununua nyara hizi ambazo zinatoka katika nchi za Kiafrika na nchi nyinginezo Duniani, Marekani ni nchi ya pili na akasema hii ilikuwa inatia doa katika nchi ya Marekani. Kwa maana hiyo, akasema wanaanzisha Mfuko wa Marekani ambao utasaidia nchi mbalimbali ambazo zinaathirika na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, nataka nitoe picha kidogo ambayo itaonesha ukubwa wa suala hili. Tarehe 27 Machi, 2013, uliitishwa mkutano wa nchi tatu za Central Africa Younde - Cameroun na hizo nchi ilikuwa ni Cameroun, Central African Republic na Chad. Ajenda yao ilikuwa ni moja kwamba tufanye nini kuhusu ujangili katika hizi nchi tatu. Katika mambo waliyokubaliana kubwa na la

msingi walikubaliana kuunda kitu kinaitwa *a One Military Command,* Jeshi moja la nchi tatu, ambalo kazi yake itakuwa kukabiliana la suala la ujangili. Kulitizama kimasehesabu, nchi ya Central African Republic, toka mwaka 2003 mpaka 2013 katika miaka 10, ndovu waliokuwa nao wakati ule ilikuwa ni ndovu 80,000 lakini kufikia mwaka 2013 walijikuta wamebakiwa na ndovu 20,000, hao ni Central African Republic. Gabon, wao walikuwa na ndovu 40,000 vilevile katika kipindi cha miaka 10 wamejikuta wamebaki na ndovu 20,000 na hivi sasa ninavyozungumza Rais wa Gabon ameitisha kikao cha kimataifa na hicho kikao mgeni rasmi atakuwa Prince Charles wa Uingereza kufuatana na kazi yake ambayo anaifanya katika mambo ya uhifadhi na Mheshimiwa Rais wetu Kikwete amealikwa na atahudhuria kikao hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ukilitizama ni suala ambalo linasukumwa sana na uhitaji *(demands)* na kwa kuwa *demands* inakuwa kubwa nitawapa picha ndogo tu ili Watanzania wanaosikiliza na Waheshimiwa Wabunge tuweze kuelewa ukubwa na upana wa suala hili. Kuhusu meno ya ndovu, hivi tunavyozungumza sasa hivi, kilo moja ya meno ya ndovu katika masoko ya dunia ni dola 1500 mpaka 1800. Ukitizama upande wa pembe za faru ni habari nyingine. South Africa na teknolojia kubwa waliokuwa nayo na uwezo mkubwa waliokuwa nao kuliko sisi mwaka jana peke yake wamepoteza faru 600 kwa mwaka mmoja. Hivi tunavyozungumza kuanzia Januari mpaka mwezi April, wamekwishapoteza faru 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kimoja ambacho South Africa walifanya mwaka jana wakidhani wakikifanya hicho kitawasaidia katika hii vita nzima ya kupambana na hili suala, la kupambana *'poachers'.* Mwaka jana South Africa ili kumnusuru mnyama aina ya faru wakaamua wawapige zile sindano za kulevya na kuwatoa nguvu na kila kitu, kwa hiyo, Serikali kwa hiari wakawakata pembe hawa faru, wakakusanya pembe ya faru 300 kwa maana ya kumsalimisha wale faru, ili iwe salama ya faru wale. Kilichotokea na hii naisema kwa sababu South Africa

wenyewe wanasikia na hii iko katika rekodi zao, kilichotokea zile pembe 300 ambazo walikata kwa maana ya kusema kwamba wanamsalimisha faru lakini watakuwa na zile pembe za faru na zile pembe za faru zikaibiwa kutoka katika *strong room* ya Africa. Hii mimi naisema tu ikupe picha siyo jamani tukae tuseme Tanzania iko hivi, hatufanyi, hapana! Hili tatizo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa hivi katika pesa za kimataifa pembe moja ya faru inakwenda mpaka dola milioni moja za kimarekani ndiyo bei yake. Ninachokizungumza hapa ni kwamba iko *demand* maana yake hii *driven by the demand* ambayo iko huko nje katika masoko ya Asia na masoko mengineyo. Kwa hiyo jitihada tunafanya na ukitizama hii naomba niseme ili muweze kuelewa ukubwa wa tatizo hili kwa nini tunazungumzia nchi kama South Africa na teknolojia kubwa waliyokuwa nayo na uwezo mkubwa waliokuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Uhuru Kenyatta hajakaa sana ameapishwa juzi tu, siku ile anaapishwa wale mliomfuatilia akiapishwa, katika matatizo aliyozungumza kwamba anakumbana nayo ni la ujangili, alilisema katika *inauguration speech* yake. Isitoshe juzi Jumapili alipokuwa katika *summit* Arusha, katika hotuba yake amelitaja hilo kwamba ni mojawapo ya changamoto alizonazo katika nchi ya Kenya. Sasa ukitazama unaona Marais wote hawa wakubwa wa nchi wanazungumzia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tukoje? Tanzania kweli tatizo tunalo lakini niseme hatujashindwa kiasi hicho na hii naweza kuisema kabisa kwa kujiamini. Ukitazama *trend* tuliyokuwa nayo, mwaka 1976 idadi ya ndovu tuliyokuwa nayo, population yake, *the peak* ilikuwa laki moja na elfu kumi, mwaka 1986 idadi ya ndovu ilishuka kwa sababu ya ujangili ikafikia mpaka elfu hamsini na tano, katika miaka miwili, mwaka 1989 idadi ilishuka mpaka elfu thelathini na pale ndipo iliingia *operation* uhai. Baada ya ile *operation* kubwa ya uhai mwaka 1989 idadi ilikuwa elfu thelathini, mwaka 2012 mwaka jana tulikuwa tumefikia idadi ya ndovu 62,000 tumepanda. Changamoto zipo na uwindaji huu

tunaouzungumza na matatizo haya makubwa, nakiri kwamba yapo, lakini bado nasema jitihada ambazo tunazifanya si jitihada ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete tayari amekwishatoa amri itakavyokuwa, tunakwenda katika operesheni nyingine tulikuwa na operesheni uhai na haya siyo maneno ambayo unataka kusema, maana yake hatutaki hawa watu wajiandae. Mambo ambayo yatafanywa katika mapori yetu na katika *National Park*s, nafikiri mpaka na vizazi vitahadithia kwa sababu ni operesheni ambayo itakuwa kubwa, lini itafanyika hatusemi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, Waziri wetu wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tumekwishazungumza na kuna mahali ambapo tumekwishafika. Siyo kwamba tumefunga macho, tupo katika utaratibu wa aina fulani lakini hatutaki ku-*publicize* ni kitu gani ambacho tutakifanya. Ninaomba Watanzania wawe na imani. Tunaposema kwamba tutafanya, tutafanya kweli. Wale ambao wapo katika biashara hii wanaotusikia sasa wajue kwamba ile operesheni iliyofanywa mwaka 1986 itakuwa ni cha mtoto, hii itakuwa ndiyo yenyewe kwa sababu hata utalaam na vyombo na kadhalika tayari tunajipanga na tutakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni suala la ujangili, kweli tunalipigia kelele lakini Rais analijua kama Amiri Jeshi Mkuu wa nchi hii, Waziri wa Ulinzi anajua, sisi wenyewe ambao ndiyo wenye mali kwa kweli hili tumekuwa tunafanya maandalizi ili kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ilikuwa ni hoja mojawapo ya ndugu yetu Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mchungaji Msigwa lakini pia amechanganya mle kuna Viongozi kawataja, kuna watu kawataja na kadhalika, lakini hilo waliotangulia wamekwishasema na mimi nitaizungumzia baadaye. Naomba nizungumzie suala la Ngorongoro na suala la Loliondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchungaji Msigwa katika hotuba yake ya kitabu hiki amefanya jitihada kubwa sana ya kumsifu Mkoloni kwa maana ya kusema kwamba alikuwa na huruma sana kwa Wamasai na amezungumzia juu ya ahadi ambazo Mkoloni aliziweka dhidi ya ndugu zetu wa Kimasai. Kwa kweli niseme kwamba Mchungaji baada ya miaka 50 ya uhuru katika nchi hii, kumsifu Mkoloni kusema kwamba alifanya mambo mazuri wakati wake, mimi nadhani kwa kweli Taifa hili hatulitendei haki na Watanzania hatuwatendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Mhehsimiwa Msigwa ukurasa wa 15 anasema kwamba *Governor Richard Turnbull* lakini *in actual fact* alikuwa ni *Richard Gordon Turnbull* alitoa ahadi kwa Wamaasai tarehe 25 mwezi April, 1956 kwa mujibu wa ukurasa wa 15 wa kitabu chake. Tarehe 25 Aprili, 1956 *Richard Gordon Turnbull* hakuwa *Governor* wa Tanganyika. *Governor* wa Tanganyika wakati ule alikuwa ni Edward Francis Twining na siyo *Turnbull*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kusema kwamba huyu *Turnbull* alitoa ahadi kwa Wamasai, Mchungaji Msigwa si kweli, kwa sababu wakati ule *Turnbull* alikuwa *Chief Secretary* Kenya lakini huyo ambaye unamsifu alikuwa katika mapambano makali sana na vita vya Maumau na alikuwa mstari wa mbele kuwafunga akina Mzee Kenyatta na wengine waliokuwa wanapigania uhuru, utamsifuje mtu wa namna hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo tuiache maana nazungumza kwa mujibu wa mtiririko tulivyopewa katika hotuba yao. Hata hivyo ukitazama ukurasa wa 16, anamzungumza Turnbull anasema kwamba ahadi aliyoiweka hiyo miaka miwili kwamba atawatizama na kuwajali Wamasai, alikuja kuirudia tena tarehe 14 Oktoba, 1958. Hii siyo sahihi kwa maana kwamba huyu anayemtaja ni Turnbull, ndiye aliwapa ahadi Wamasai na aliwapenda yeye alikuja Julai 1958 akitokea Kenya na kama nilivyosema huyu mimi siwezi nikamsifia hata kidogo, alikuwa ni mtu mbaya kwa sababu mambo aliyoyafanya Kenya huwezi ukaniambia vile alivyowafanyia Kenya katika Vita ya Maumau amekuja huku

sasa uniambie kwamba atawafanyia vizuri Watanzania na hasa ndugu zetu Wamasai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende katika historia na naona tuiweke sawa, Mheshimiwa Mchungaji anapomzungumzia *Governor Turnbull* alipokuja Tanzania nataka nimnukuu katika maneno yake yeye huyo *Governor* ambaye Mheshimiwa Msigwa anamsifu, walikutana na wazee wa Kimasai wakazungumza nao ili watoke katika eneo la Serengeti waende katika eneo la Ngorongoro. Wazee wa Kimasai (*the elders)* walikubali na wakasaini *document* na *Governor* tarehe 21 Aprili, 1958. Wazee wale wa Kimasai walichofanya katika kukubali ule mkataba, yale madai na haki zao za makazi ndani ya Serengeti walikubali kwa *Governor* wakasema kwamba sisi tutahama. Mtu huyohuyo Gavana Richard Turnbul, ambaye Mchungaji anamsifia kwamba alikuwa na huruma; baada ya wazee kusaini hiyo *document* yeye sasa anatamka baadaye, alitamka kwamba ahadi ambazo alizitoa zilikuwa *conditional.* Kwa Kingereza anasema:-

*"The promises were conditional on the Ngorongoro Masai behaving themselves and not needlessly interfering with the game."* Sasa haya yalikuwa ni maneno ambayo anayazungumza Gavana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwaka 1960, sisi tulikuwa hatujapata uhuru. Gavana huyu ambaye anasifiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani, walipokubali sasa wakatengeneza *Ngorongoro Conservation Area,* ilikuwa ina Wajumbe tisa. Katika Wajumbe tisa, mmoja ambaye alikuwa ni Mwenyekiti na alikuwa Mkoloni ni *DC* na wengine wa wanne pia na wenyewe walikuwa ni Wakoloni. Sasa katika utaratibu wakasema watakuwepo Wamasai watatu ambao watakuwa wanatoka katika eneo lile la Ngorongoro na Mmasai mmoja ambaye atakuwa anatoka katika *NCA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wao wa kwanza, Wamasai ndani ya hii *Ngorongoro Conservation Area Authority,* ambayo ilikuwa *created,* wakadai suala lao la maji

juu ya mifugo yao na maeneo ya malisho, wakataka yaeleweke vizuri. Hiyo ilikuwa ni ahadi ambayo walipewa na Waingereza kabla hawajatoka Serengeti. Kilichofuata, *Authority* baada ya Wamasai kuomba haki yao ambayo waliahidiwa na Gavana ambaye mnamsifia hapa, walikataliwa na baada ya kukataliwa kukawa hakuna tena vikao vilivyofuata vya hii *Authority.* Kwa hiyo, maamuzi yalikuwa ni ya *DC,* ndiye alikuwa anaamua, yanateremka yanakwenda chini. Hivi vitu vyote viko *documented,* wala sisemi hii kwa sababu nina nini, lakini ipo katika *history* na mimi siwezi kuamini kwamba, Mkoloni anaweza akawa mzuri, mzuri kwa lipi? Kwa lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sikiliza alivyosema Gavana. Baada ya kuwa vikao havikufanyika na kwa maneno yake alisema hivi na hiyo ndio mimi inaniumiza zaidi Mchungaji Msigwa, kwa sababu hapa unaye Gavana wa kikoloni. Ni Gavana huyohuyo ambaye alimsumbua sana Mwalimu Nyerere na kumtia ndani na kufamnya Mwalimu alale katika maficho, huyohuyo, katika harakati za kutaka uhuru sisi, halafu ukasema kwamba kuna watu katika Tanzania atawa-*favour,* atawa-*favour* kwa lipi? Sikiliza kauli yake. Gavana alivyoambiwa kwamba Wamasai wanadai haki yao ya kupata eneo la malisho na waweze kupata maji ya mifugo alisema hivi, kwa maneno yake; anasema:-

*"Masai attitude is conservative in the extreme with elders in particular being not enlightened but instead bigoted and conceited."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wewe, kweli, Mheshimiwa Mwenyekiti na Bunge hili Tukufu, haiwezekani mtu kama huyo uje umsifu, utamsifu kwa lipi? Anatukana huku watu na hata kama tunatafuta *political mileage,* mimi niseme Mchungaji, kwa kweli sio katika njia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema ni huyuhuyu Gavana Turnbul, ambaye alitusumbua sana katika uhuru wetu, ndiye alifungua makesi yaliyompata Mwalimu na ndiye huyuhuyu, nataka niwaambie na niwakumbushe,

najua wengine mtakuwa mnakumbuka, ni huyuhuyu mwaka 1960, tunapigana kupata uhuru akasema, *"Tanganyika is not ready for independence".* Akasema wanahitaji miaka mingine 50, huyuhuyu, leo tumo humu ndani eti anatwambia Watanzania kwamba, tumsifu alikuwa na huruma kwa Wamasai. Mchungaji, Mchungaji, Mchungaji, mimi nafikiri hapo... *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu Loliondo. Mchungaji katika Kitabu chake hapa, akiwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani, mbali ya yote, anayo sehemu kabisa ameandika Loliondo, Waarabu na CCM. Sasa mimi nasema kwa kweli, Mheshimiwa Mchungaji, hizi sio lugha nzuri. Waarabu ni watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni watu na hii ni lugha ya ubaguzi. Hii ni *discrimination.* Tanzania humu tunao Waarabu. Sasa Mwingereza ambaye unamsifu eti aliwasaidia Wamasai, nimekwishaeleza historia ilivyokuwa, hakuna alichowafanyia Wamasai na wala hakuna *favour* yoyote aliyowafanyia. Isipokuwa wao walikuwa na waliyoyataka, lakini baadaye waka-*abandon. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Loliondo kama wanavyosema wenzetu na ninaomba Watanzania waelewe, Loliondo haikuanza na *OBC.* Maana tunapozungumza tunasema ule mwaka 1993, Loliondo ndio ilipoanza. Kabla *OBC* hajaingia pale, katika eneo hilohilo alikuwepo Mmarekani anaitwa *Cotton Gordon, there was an American there,* lakini huwezi ukasikia mtu anamtaja popote kwa sababu ni Mmarekani. *There was an American and whatever defininition* mliyokuwanayo, lakini ndiye aliyekuwepo na tatizo lilianzia hapo Mchungaji *not anywhere,* sio mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kilikuwa ni Kitalu kama Vitalu vingine na wakati ule vilikuwa karibu Vitalu 50. Wakati huyu *OBC* anapewa Kitalu pale wako wengi walipewa, akina Pasenisi, alikuja hata yule *VIP* ambaye yuko Grumet, lakini hao ni Wazungu, akina Pesanisi ni Wafaransa yule Grumet ni

Mmarekani na wako wengine Wazungu, lakini hakuna anayewazungumzia. Suala linalozungumziwa hapa na huyo *Cotton Gordon,* maana baada ya kukosa kile Kitalu na ndio imekuja kutokea mpaka leo, ndio *head ache* niliyokuwanayo, wale waliokosa Vitalu wamekuwa ni tatizo. Sasa *OBC* aliomba na *OBC* tusidanganye watu, hamiliki ardhi na hatamiliki ardhi hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Loliondo Game Controled Area* lile eneo ni Kitalu na pale vipo Vitalu viwili, *Loliondo North* na *Loliondo South.* Ni kama mahali pengine katika *Selou. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nilivyosema huyu alipewa 1993, lakini *Grumet* pale *Reserve,* walipewa 1995 na mpaka leo bado wapo na hakuna kelele, sisikii mtu yeyote anasema chochote. Akina Pasenisi, ambao wao ni tangu 1978 mpaka leo lakini sisikii kelele yoyote; sasa kelele hii ya *OBC,* kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa *OBC,* kama nilivyowahi kutamka, tatizo kubwa tulilonalo hapa, ndani ya lile eneo kuna Kampuni moja hiyo ya *OBC,* lakini zimo Kampuni nyingine sita ndani ya eneo moja hilohilo. Katika hao, ziko kampuni tatu ambazo nataka niseme hapa ndani ya Bunge, *they are the most troubled,* yaani ndio wana-*cause a lot of problems*, ndio wana-*finance NGOs* na wenyewe wana *NGOs* na ndio wanatuletea matatizo. Ya kwanza kuna hii Kampuni inaitwa *And Beyond,* ambayo ni *Clens Camp,* ambao nafikiri hata Kambi ya Upinzani mnawajua na ukaribu wenu nao mnaujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni moja, lakini pia iko Kampuni nyingine ya *Dorobo Tours.* Hii ya *And Beyond* ni Kampuni ya *South Africa* na ndio *actually* unakuta vuruguvurugu zote hizi wanazi-*finance.* Kuna hawa *Buffalo Luxury Tented Camps,* ambao ni Wamarekani, halafu kuna hawa *Dorobo Tours. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi ninasema ngoja

tumalize, tunakwenda *one thing at a time.* Kwa sababu, mimi ninasema Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya CCM, haiwezi ikaendeshwa na *NGOs* hata siku moja; *it will never happen* na hii naisema wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NGOs* wanaweza waka-*influence* watu wengine, wanaweza watu wengine wakachukua *position* kwa niaba yao, lakini ninataka nikuhakikishie safari hii, katika *round* hii, wamefika na tutakula sahani moja. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi mwenyewe binafsi nilikwenda Loliondo mara nne. Mchungaji Msigwa, anasema kwamba, nilitumwa na Rais Kikwete. Ndivyo ulivyosema, umesema katika Hotuba yako na hata leo asubuhi umesema, umesema kwamba Rais Kikwete alinituma; nataka niseme katika Bunge hili, Rais Kikwete hajanituma. *That is what I am saying,* ninachozungumza ni kwamba, Rais Kikwete, aliniteuwa katika Wizara na hii Wizara ina majukumu yake na kazi zake. Kwa hiyo, unaposema kwamba Rais huyohuyo amemchagua Waziri kaenda Loliondo na Rais huyohuyo ambaye ndiye Mwenyekiti wa Chama, akapeleka Tume ya Chama hukohuko; mimi ninasema hiyo ni ku-*mislead the public,* sasa *take it from me,* mimi ninasema sijatumwa na Rais, mimi nilikuwa ninafanya kazi zangu na nitaendelea kufanya kazi zangu kwa sababu iko katika *mandate* ya Wizara yangu. Nilikwenda Loliondo mara nne kwa shabaha ya kumaliza mgogoro huu wa Loliondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sakata la Loliondo, kumekuwa na Tume nyingi ambazo zimekwenda. Kumekuwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kumekuwa na Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kumekuwa na Kikosi Kazi ambacho aliunda Waziri Mkuu na kadhalika. Mimi mwenyewe nimekwenda mara nne na shabaha ya kwenda kule ni kutaka kupata suluhu na kupata ufumbuzi wa mwisho lakini na yote ambayo tulifanya na sitaki kwenda kwa undani, kama nilivyosema katika Hotuba yangu sikuingia katika undani wa suala hili kwa kuzingatia kwamba,

ndugu zetu kutoka Loliondo walikuja hapa, walionana na Waziri Mkuu, walieleza kutoridhishwa na mambo jinsi yalivyokwenda. Niseme kwamba Waziri Mkuu hilo suala analo kwa hiyo, sioni kwamba kuna sababu gani hasa ya kulishabikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi niseme Mchungani, hata kama tunafanya siasa, kusimama hapa ndani ya jengo hili ukasema kwamba, Wamasai ambao ni Wabunge wamo ndani humu, wamewatendea ubaya na unasema kwamba, wamewasaliti, maana ndio neno ulilotumia; mimi nafikiri kwa kweli, hukutenda haki. Kwa sababu, hawa wamekuwa ni wawakilishi wao, wamekuwa ni watetezi wao, wamekuwa ni watu ambao wanasimama nao, pamoja na Mbunge wao, ambaye anatoka Ngorongoro na tumekuwa tunafanya kazi na yeye. Hata kama tunataka umaarufu, usiwe umaruufu wa kuumizana kiasi cha kusema kwamba miaka yote ambayo kazi kubwa wamekuwa wanafanya katika kuwawakilisha Wamasai. Mheshimiwa ndugu yangu, wewe umekuja Bungeni jana, eeh. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kuna mambo mengine kidogo yanatia simanzi na yanatia uchungu kwa sababu, tunapojaribu kutengeneza, watu wanapokuwa wapo katika matatizo, tukajaribu kusema kwamba tunafanya siasa ndani yake kwa kweli, inakuwa si jambo jema. Mchungaji Msigwa amesema hivi, tunapoongea sisi tukasema kwamba, wapo Wamasai kutoka Kenya na mifugi yao, tunasema uwongo. Tunachosema ni kwamba, wale ni Wamasai wa pale. Mimi ninachokisema pale kuna mdogo wangu Christopher Ole-Sendeka na pale yuko Mzee mwenzangu Laizer, yuko Telele mwenyewe; unapokuwa kule Loliondo, maana pale Loliondo katika mpaka wa Masai Mara, yaani mpaka wa Kenya na Tanzania, maana hii ni Masai Mara na hii ni Loliondo. Pale ziko koo kubwa mbili ambazo ni Purko na Loita, ni wengi maana na wao ukiwauliza watakwambia. Kuna wakati ule mwaka 2009 kilikuwa kiangazi kikubwa Kenya, mifugo mingi na wale Wamasai wengi walikuja huku Tanzania na ni wengi na wengine wapo mpaka leo wanakaa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hii ni ajabu. Leo mtazungumza kwamba mipaka yetu mnaacha watu wanaingia, ghasia zinafanyika. Leo, watu wanaingia unasema hapana, sasa jamani, hatuwezi kuwa na *contradictions, either* tunakuwa *consistent* ama tunakuwa vingine. Kitu tunachokisema, Kenya ni ndugu zetu, tumo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, wala hatuna haja ya kusema tuna ugomvi na wao, isipokuwa ukweli ni lazima usemwe. Ninasema na mimi nimekwenda katika maeneo hayo, Wamasai wa Kenya katika eneo lile la Tanzania wapo wengi na mifugo yao ipo mingi, hiyo tu na ni ukweli usiopingika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumalizia hili suala la Loliondo. Suala la Loliondo sisi tunalitizama kwa upande wa uhifadhi. Tunapozungumzia ile *ecosystem* ya pale, itakuwa na itaendelea kuwa pale na watu wa Loliondo wanajua, niliwambia *okay,* kama tatizo lenu ni kuwa na *OBC,* lile eneo halijabadilishwa chochote, *TANAPA* itabidi mipaka yake iongezwe, hii ni katika mazungumzo ambayo tumekuwanayo. Nachosema kwa kuwa suala hili limeshafika kwa Waziri Mkuu sasa, kama mnavyosema, mimi ninasema tusubiri na hapo tutaweza kupata majibu mazuri lakini suala la uhifadhi hatuwezi tukaliacha lakini pia na maslahi ya watu wetu. Mheshimiwa Ole-Medeye, ametukataza sana hii kusema Wamasai, Wamasai, maana pale kuna watu kuna Wasonjo, kuna watu wengine, sasa anasema hii kwa kweli si katika mwenendo uliokuwa mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumwambia Mheshimiwa Msigwa, CCM kuunda Tume ama Kamati kwenda Loliondo si dhambi, ni jambo la kawaida. Tume hiyo imekwenda pale, imetizama iliyoyaona, imetengeneza ripoti yake na hiyo ripoti ni *pre-mature,* wewe huwezi ukaja hapa ukaanza kusema kwamba, tunaijadili. Ile ripoti itapita katika vikao vinavyohusika mpaka kwa viongozi wa Chama, halafu itaweza kutolewa maamuzi lakini kusema kwamba unaweza ukaitumia hapa kwa kusema kwamba, Rais amefanya hivi, amefanya vile, mimi nasema kwamba, sio sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, katika tuhuma ambazo zimesemwa kuhusu haya masuala, kumekuwa kuna suala ambalo Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ameuliza kuhusu *Game Frontier,* Kampuni ambayo anasema kwamba ilikuwa inachimba *urani* na kusema kwamba hatuna, sasa mimi ninasema, jamani Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasikilizana vizuri. Hili suala nililieleza na sasa kuligeuza kusema bado tu ni swali, mimi kwa kweli, inanisikitisha. Nilieleza yafuatayo; hili suala sio la Maliasili kwa maana ya kusema kwamba eneo ambalo wamekwenda ku-*operate* ni eneo ambalo ni la Vijiji, ambalo sisi kama Maliasili hatuna *jurisdiction* nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mikataba iliyokuwepo ni kati ya *Game Frontier* pamoja na watu wa Kijiji cha Mbarang'andu ambacho kiko katika Jimbo la Mheshimiwa Vita Kawawa. Kwa hiyo, yeye atakuwa anaelewa zaidi kwa sababu ni katika Kijiji chake, wameweka mkataba na huo mkataba wala hautuhusu kwa sababu mle hakuna masuala ya wanyamapori. Masuala ambayo yako mle ni masuala haya ya kuchimba urani na sanasana ambao wanaweza kuhusika na hilo, kama ni kweli lipo, itakuwa ni Wizara ya Nishati na Madini. Niombe tafadhali, msililete tena katika Wizara yangu suala hili kwa sababu, halituhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la tuhuma ambazo zimekuwepo kuhusu Mkutano uliofanyika Bangkok na kusema kwamba kuna Mtanzania, Muhsin, ambaye imeonekana kwamba yuko katika ujangili na kadhalika. Sasa kitu ambacho amekosea Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ni pale anaposema kwamba *Environmental Investigation Agency,* ndio iliyotoa taarifa hiyo; hii si kweli, si kweli kabisa hata kidogo, wao hawajatoa. Waliotoa hizi taarifa ambayo ilikuwa ni *side event* katika Mkutano wa *CITES – Bangkok,* walikuwa ni *NGOs. NGO* moja ni *the Green Line Foundation* na nyingine ilikuwa ni A100. Ni kama vile kuwa na *NGO* hapa, ikaenda katika Mkutano, ikawa na *side show,* ikaonesha *clips* zake na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi hatusemi kwa sababu ni *NGO* zimefanya vile tunaichukulia kwa urahisi, hapana. Hiyo ni lazima tuangalie kuona kwamba kitu ambacho anakisema kweli kinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwishamwambia Mheshimiwa Msigwa, na ninasema kwa nia nzuri, mnaweza msituamini, lakini tunavyokwenda hatuogopi kitu chochote. Mahali ambapo tunaona kwamba kuna makosa, tutasema hapa kuna makosa; kama ni mtu amekosa, tutasema huyu amekosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kwa kweli jinsi mnavyoichukulia sivyo na kusema kwamba sisi kama Serikali ya CCM, kama Chama tunawafichia makosa, hapana. Hata kidogo! Hiki, wameonyesha ile nanii yao, na sisi tunataka kutazama *the authenticity of that* na tumekuja nazo, siyo kwamba hatukuja nazo. Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori amekuja nazo, kwa sababu alikuwepo kwenye Mkutano. Tunataka kui-*follow backward* kutazama hili jambo ni kweli? Kama tukikuta lina ukweli, lazima itabii tuchukue hatua. Tukikuta kama hakuna ukweli, ni mambo mengine, basi itakuwa haina sababu. Wala sioni kama ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyemkiti, sasa mambo mengine ambayo najaribu kwenda haraka haraka, katika ripoti yake Mheshimiwa Msigwa amewataja watu kama Mheshimiwa Mohamed Khatib, anasema yupo katika hii biashara. Mohamed Khatib ni kweli alipewa kitalu, lakini Mohamed Khatib amekwishaandika Wizarani barua karibu tatu, anasema kitalu alichopewa, hakina manufaa naye, kwa sababu hakina hata wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu kwenda kuzungumza watu kama *family* ya Hayati Sokoine, mimi nataka niseme kitu kimoja; jamani, hii *democracy* ambayo tunakuwa nayo na *it is good* kwamba *we are democratic,* lakini naomba ndugu zangu tujifunze hata katika Mataifa makubwa. Watu wanapokuwa viongozi, kuna lugha wanatumia, lakini pia kuna *respect* kwa sababu huyu alikuwa ni kiongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawapa mfano; mkubali, msikubali. Katika historia ya Marekani, *America* ni nchi kubwa, kubwa tu. Mwaka 1974 Richard Nickson alikuwa Rais pale, *Water gate* ikawa kubwa kiasi kwamba hakuweza kuihimili. Walikaa viongozi wa *America* wote; kitu kimoja walichokisema na unaweza uka-*chek* katika *record,* katika *record* zozote unaweza uka-*check* walisema yafuatayo: Walisema Amerika ni nchi kubwa duniani, wakasema Amerika ina heshima yake, tunakiri Rais wetu amekosea.

Kitu ambacho hatutafanya, kwanza hatumshtaki (hii ni wenyewe Wamarekani wanasema); pili, hili suala yeye kujiuzulu na ndiyo utakuwa mwisho wa suala hili. *That is it!* Tangu ametoka, *ofcourse* watu watasema, lakini ninachosema hapa, sikatai, lakini unapoanza ku-*attack family* za viongozi, *I can assure you* hakuna *any country that will respect your country.* Taswira ya nchi, ni viongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala hii sisemi kwa nia mbaya hata kidogo, tujifunze katika Mataifa makubwa hawa ambao tunajifunza *democracy* kutoka kwao. Sio Waingereza, sio nani, viongozi wao wanakuwa *caught into so many scandals.* Helmut Schmidt wa Ujerumani hakumaliza muda wake, *he resigned.* Ni kwa sababu Chama chake cha *Christian Democtratic Party* sijui, waliwakuta wamechukua pesa za makampeni kinyume na utaratibu. Kitu gani kilitokea? Ali-*resign, and that was the end of the story!* Huwezi ukasikia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, unapomzungumzia Hayati Moringe Sokoine, lazima ujue kwamba *you are talking about* mtu ambaye ameweka mchango mkubwa katika nchi hii *and and he was a very respectable man* na unakuja sasa unazungumza kitu... *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiyo nasema, siyo kwamba nina-*argue,* natoa ushauri. Unapotoa ushauri, *some can take it and others can reject it. It is democracy.* Lakini huko mbele ya safari, sisi ni watu wazima, tutakuja kujua.

Najua Watanzania wanajua wanavyomwenzi Sokoine. Kitu kilichotokea, huwezi ukasema kwa sababu Sokoine alikuwa Kiongozi hapa, *family* yake haiwezi ikaomba kitu chochote katika nchi hii. *Why?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa amechukua kwa wizi, ama kwa ujambazi, *that is another story!* Lakini amekwenda *through the procedures and through the* utaratibu akapewa. *What is wrong with that? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema vitu vingine jamani, twende vizuri. Hii kuhusu kwa mfano Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, wengi wameielezea, hata Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye najua kwamba, *ofcourse others were not happy* lakini ameielezea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitoe mfano mdogo tu. *Precision,* tunamjua *owner* wa ndege ya *Precision*, ama *owner* wa *Air Tanzania* tunamjua. Sidhani kama ana *control* na *passangers* wanaoingia katika ile ndege ambao wanasafiri. Kwa hiyo, *passenger* akiingia mle katika ile ndege anasafiri na akienda kule akakamatwa labda amenyajua sijui vitu gani ambavyo ni *contrary to the law,* leo utaniambia kwamba yule *owner* wa *Precision* kwa sababu ile ndege ni mali yake na ile bidhaa iliyokamatwa mle kwa hiyo, anahusishwa! Mimi sidhani. Nafikiri tujaribu kutazama vizuri na tujaribu kuwe na mwelekeo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchungaji mimi namheshimu sana na yeye mwenyewe anajua, kanipiga makombora mengi na mashambulizi mengi, lakini mimi nasema hiyo ni sawa sawa, *that is politics,* lakini ni *politics* ambazo sidhani kama zinasaidia sana. Kikubwa twende katika hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bada ya kusema hayo, kuna suala ambalo limejitokeza sana na lenyewe ni suala la misitu. Misitu sijakataa, imekuwa inavamiwa na mambo ambayo yanafanyika katika mambo ya misitu yetu ni mambo ambayo

yana athari kubwa. Lakini naomba pia mtambue jitihada za Serikali. Sasa hivi Serikali ilichokifanya na hii imekuwa ni katika mwaka mmoja, tumeweka mamlaka ambayo inasimamia.

Ni mamlaka pekee na kwa sababu hili suala tumelitoa Wizarani na tumeweka mamlaka ambayo itasimamia misitu Tanzania na nishukuru kwamba Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kweli wamesaidia sana kiasi kwamba katika suala la ajira na kadhalika, na sasa tumepata ajira ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo asubuhi yupo mchangiaji mmoja, Mheshimiwa Mkosamali amesema kwa jazba kubwa na ametumia muda mrefu sana, wala haina haja hata ya kuyarejea; lakini kubwa ni kwamba mamlaka hii imewekwa na kusema kwamba hakuna mikakati siyo kweli, ina Bodi yake na Bodi imeanza kufanya kazi. Lakini pia tunashukuru kwamba tayari tumepata ajira ya watu ambao watafanya kazi pale. Kikubwa ambacho kinajitokeza katika masuala haya Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba kila tunapojitahidi kusimamia sheria lakini Waheshimiwa Wabunge wenyewe mmekuwa wagumu na wazito, maana yake kwanza mtatuambia kwamba waacheni watu; maana yake siasa kwa kweli zinaingia katika mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kweli tufanye siasa, lakini pia katika masuala kama haya iko haja kubwa kwamba tuweze kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha misitu yetu ambayo ni kweli inateketea kwamba tunakwenda katika njia ambayo itakuwa nzuri, kwa sababu kuteketea kwa misitu ni kuleta jangwa na kuleta jangwa ndiyo haya mabadiliko ya tabianchi na kufanya mambo mengine yanakwenda visivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo uhifadhi na usimamizi wa misitu ni jambo la muhimu sana na kuweza kujenga uwezo katika Taasisi mbalimbali lakini pia na jamii, lakini pia zile sheria na kanuni ambazo tunaziweka jamani, ningeomba Waheshimiwa Wabunge tujaribu hata huko katika maeneo yetu katika Majimbo yetu, tuwakumbushe wananchi kwamba upo umuhimu wa kufuata Sheria na wa kutii zile sheria ambazo zinawekwa na tusiwe wa kwanza

katika uchochezi wa kuona kwamba zile sheria zinakwenda sawa au visivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu hapa kwamba jamii kupitia vijiji vyao vimeweza; na hii ni katika hatua ambazo tumezichukua. Tumeweza kuanzisha hifadhi za vijiji zenye ukubwa wa hekta, kwa mfano, sasa hivi ndiyo tumeanza. Hii naomba tupate ruksa kwa maana ya kusema kwamba uelewa wa watu, kwa sababu hii ni shirikishi; watu pia wanashiriki, kuwauliza watu na watu waweze kukubali. Maana yake hili ni zoezi, mambo yamebadilika ya kusema kwamba Serikali inaweza ikaja na jambo tu kwamba inatekeleza, haiwezekani. Kwa hiyo, inabidi twende katika mtiririko ambao utahusisha wanavijiji na kuona kwamba tunakwenda katika njia iliyokuwa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamekuwepo masuala mengi ambayo yamejitokeza, lakini mimi ninadhani makubwa ambayo yalikuwa ni ya muhimu ni hii hotuba ambayo aliitoa Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambayo nimefanya kila jitihada ya kuweza kuielezea, *ofcourse* mengine yaliyokuja kujitokeza, ni suala la ujangili ambalo na lenyewe ningeomba wananchi na wenyewe watuunge mkono, tujitahidi kwa pamoja kwamba tunakwenda sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na suala la migogoro ya mipaka. Hili suala la nataka nilisemee kwa ujumla wake. Tume ambayo ni kikosi kazi, lakini ambacho kilijumuisha Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Ardhi; na hii hata Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi amelisemea. Mimi niseme kwamba tu, ni kama kazi yao imekamilika. Tutakalolifanya sasa linalofuata ni utekelezaji. Hiyo naona karibu inamgusa kila Mbunge katika kila eneo. Tutajaribu kadiri tuwezavyo tuweze kuyafanyia maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yako maeneo ambayo yana utata unaotokana na historia, yako maeneo ambayo utakuta wenzetu wameweza kuwashawishi watu, lakini inasema kwamba ripoti tuliyoipata ni nzuri, na baada ya Bunge tutakapokuwa tumemaliza, tutaanza utekelezaji

wake katika maeneo mbalimbali na haya yote tutawahusisha wanavijiji na Waheshimiwa Wabunge na kadhalika ili tuweze kupata muafaka ambao utakuwa ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mlima Kilimanjaro; Naibu Waziri Nyalandu alilizungumzia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlima Kilimanjaro ni kivutio muhimu katika Afrika. Mlima Kilimanjaro wako watu wengi ambao wako nje ya Tanzania, nje ya Afrika ambao wanafanya *saving* zao wanasema kwamba waende wakatazame Mlima Kilimanjaro. Nakiri kwamba umekuwepo upungufu inapokuja katika ushirikishwaji, yaani kushirikiana na zile jamii. Lakini hayo tumeyapokea na nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika maeneo husika tutashirikiana vizuri tu na Halmashauri za maeneo yale, tutashirikiana vizuri na Wabunge na nina uhakika tutafika mahali tutapata muafaka mzuri wa kuhakikisha kwamba kitu tunachokisimamia ni kitu chetu sote, lakini ni kitu ambacho tukiweke katika hali ambayo hata vizazi vitakavyokuja wajue kwamba wale waliotutangulia walikuwa ni watu wenye maarifa na busara kwa kuona kwamba wametuwekea kitu ambacho kipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlima wa Kilimanjaro ni kweli, na hii ningeomba hata Watanzania wazingatie kwa umakini, ni ile theluji yake, siyo ule urefu wake wa kwenda juu. Ile theluji yake ambayo imekuwa juu, maana watu wanashangaa kwamba theluji imekuwa ni kitu ambacho kinaonekana katika nchi za Ulaya ambako ni baridi na kadhalika, au nchi za Urusi huko au nchi za Uchina na kadhalika ambako ni baridi sana. Lakini sasa inapokuja katika *tropics* na inakuja katika ikweta maana yake ni karibu ikweta inakopita pale, unakuta kuna Mlima Kilimanjaro na juu kuna theluji hapa kubwa, ni katika kuhakikisha kwamba tunahifadhi ile theluji ambayo inakuwepo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine ambalo tutakuja nalo, ni katika sheria hii ambayo tunataka kuileta juu ya Mamlaka ya Wanyamapori. Mamlaka ya

Wanyamapori ni kitu ambacho kipo, kilipitishwa na Bunge, lakini kilikawizwa na nilisema hata juzi wakati nikijibu swali hapa, nikasema tulikawia lakini haina maana ya kusema hakitafanyika. Ahadi tuliyowapa ni kwamba itakapofika Bunge la mwezi wa Kumi na Moja tutaweza kuipitisha hiyo Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwaombe Waheshimiwa Wabunge zile adhabu ambazo tutaziweka mle, tunaomba kabisa tushirikiane. Tatizo kubwa ambalo tumekuwa nalo, wakati mwingine tunatengeneza sheria tunakuja hapa sisi wenyewe tumekuwa katika mkakati kujaribu kuzi-*waterdown* tunasema kwamba hizi adhabu ambazo zimewekwa zimekuwa ni kali. Lakini ningeomba kwamba tungeweza kushirikiana, maana kwa kweli nimemsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Freeman Mbowe hapa, alivyosema kwamba sasa wale ambao watakuwa wanakamatwa katika mambo ya ujangili, tuweke adhabu ya kifo. Sasa hilo ni pendekezo ambalo ameleta na shabaha ni kuona kama inaweza ikawa kama *deterrence* kuweza kuwafanya watu waweze kuogopa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba itakapokuja katika masuala ya Sheria, Bunge lituunge mkono, tuweke sheria ambazo zitakuwa na nguvu kidogo ama zenye meno ili kuhakikisha kwamba ujangili unatoweka na wanyama wetu katika mapori yetu wanakuwa na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hayo, kwa kuwa naona muda wenyewe umekwenda, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa nitamuita katibu atuongoze utaratibu unaofuata.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

## FUNGU 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Kamati ya matumizi ya Bunge zima naomba sasa nimwite Katibu aweze kutuongoza.

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*..............................Tshs. 5,336,897,960/=

**MWENYEKITI:** Haya, dakika moja kidogo Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, katika fungu hili mnafahamu kwamba tunakwenda kwa uwiano ule ule na kwa mujibu wa kanuni ni lazima utaratibu wa wachangiaji majina yao yapitie kwenye Kamati za Vyama. Basi, nimemwona Mheshimiwa Kuruthum, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Sendeka, Mheshimiwa Telele na Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi katika majibu yake na maelezo mazuri ya Waziri ninakusudia kuzuia Shilingi. Nilitaka nipate maelekezo katika utendaji wake wa kazi; kwa mujibu wa sheria baada ya Sheria ya Wanyama Pori ya mwaka 1974 kufutwa, Sheria ya Na. 5 ya mwaka 2009 inamtaka Waziri atangaze mapori tengefu, lakini mpaka sasa Mheshimiwa Waziri hajatangaza. Anafanya kazi kwa mujibu upi na ni mapori yapi tengefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa kutosha, ni *GN* ipi iliyotangaza mapori hayo tengefu? Maana yale mapori tengefu yalikufa mara tu ile Sheria ya mwaka 1974 ilivyokuwa imekufa. Kwa hiyo, ningeomba nipate ufafanuzi wa kina, ni lini hayo mapori tengefu yalitangazwa? Kama hayakutangazwa, anapata wapi mamlaka kwamba tuna

mapori tengefu? Kwa sababu kwa uelewa nilionao, baada ya Sheria ya mwaka 1974 kufa hayo mapori tengefu hayakutangazwa. Kwa maana nyingine ni kwamba hatuna mapori tengefu sasa hivi kwa mujibu wa hiyo sheria. Naomba nipate ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Huvisa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niliarifu rasmi Bunge lako Tukufu kwamba, mabonde au mapori tengefu yote yako chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na tuna mikataba ya kimataifa Bonde la *RAMSA* na lilishatangazwa. Kwa mfano, Bonde la Kilombero liko chini ya Mkataba wa Kimataifa la *RAMSA*. kwa hiyo yalishatangazwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema mabonde, mimi nimeulizia mapori tengefu. *I am talking about game controlled area.* Siyo mabonde!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa naomba uheshimu Kiti. Hata kama hujaridhika, upo utaratibu wa kusimama na kutoa hisia zako za kutokuridhika, lakini siyo kusisimama tu bila kupewa idhini halafu unaendelea kutoa hoja yako. Naomba uendelee kuheshimu Kiti.

Mheshimiwa Waziri naomba urejee maelezo yako fasaha katika jibu la swali la msingi lilotolewa na Mheshimiwa Peter Msigwa. Mheshimiwa Huvisa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Labda nimwelimishe maana na tengefu. Tengefu maana yake ni oevu. Kwa hiyo, oevu ni pamoja na mabonde, mapori, mabonde yote chepechepe, tengefu, oevu yako chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na yalishatolewa mkakati maalum wa Kitaifa. Tumeshatangaza na mengine yako chini ya Mikataba ya Kimataifa.

**MWENYEKITI:** Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapori tengefu kwa kadri alivyoeleza Mheshimiwa Waziri na kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri anayehusika na Mazingira, Ofisi ya Rais, yamekwisha kutangazwa. Katika sheria zote ambazo zimefuata, hakuna sheria yoyote ambayo ilishawahi kuyafuta mapori tengefu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli!

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** *Order*, *order,* tafadhali! Waheshimiwa Mawaziri naomba utulivu! Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli!

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nipo kwenye mshahara wa Waziri. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kidogo, kwamba tunatambua kwamba *WMA* zinatoa ushirikiano mkubwa katika kuhifadhi maliasili zetu, hasa katika maeneo ambayo yanazunguka. Lakini kwa kipindi cha nyuma wale Askari wa Vijijini, walikuwa wanapata nguvu kutoka Idara ya Wanyamapori, kwenye maeneo yetu, kwa kwenda na silaha zile za kisasa kwa ajili ya kufanya doria zidi ya ujangili katika maeneo yale.

Kwa sasa utaratibu ule unaonekana kufifia, kwa hiyo, unawafanya wale majangili waone kama *WMA* ni sehemu za kwenda kuvuna kwa urahisi. Kwa sababu wale askari wetu wana silaha za asili; wana marungu, mishale; kwa hiyo, wanashindwa kupambana na wale majangili ambao wana silaha za kivita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza fungu kwenye hizi Idara za Wanayamapori, ili sasa Askari wa

Idara za Wanyamapori waweze kwenda kwenye zile *WMA* kuongeza nguvu kule ili sasa hawa majangili wasiende kuvuna kirahisi kama wanavyo vuna sasa hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu waziri, Majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa mwenyekiti, tunashukuru kwa swali la Mheshimiwa Kuruthum. Kinachofanyika sasa hivi, Serikali inatoa asilimia 25 ya mapato yote yanayotokana na *WMA* katika vijiji husika, na asilimia 25 katika Halmashauri ya Wilaya. Hali kadhalika, tunatambua kwamba ushiriki wa Maaskari walio katika *WMA* ni muhimu. Kutokana na upungufu mkubwa sana tulikuwa nao wa Maaskari wa Wanyamapori na kutokana na ukweli kwamba tumekuwa na Maaskari wa Wanyamapori 400 nchi nzima, imekuwa ni vigumu sana kuwa nao. Sasa hivi kama tulivyosema katika *speech* ya Waziri, tunaajiri Maaskari wengi na tunategemea kwamba tutashirikiana ikiwa ni pamoja na kuongeza ushiriki wetu katika *WMA*.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Christopher O. Ole- Sendeka!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekitri, nashukuru sana kwa kuniona. Nilimwelewa sana Mheshimiwa Waziri katika suala la Loliondo alivyoelezea kwamba, hoja ile ilikwishapelekwa kwa Waziri Mkuu na viongozi wa Wilaya ya Ngorongoro wenyewe waliokuja hapa kumwona Waziri Mkuu na viongozi wa Chama waliokuwa wamekwenda kule Loliondo na kwamba jambo hili uamuzi wake unasubiriwa, baada ya Waziri Mkuu kushauriana na Waziri mwenye dhamana na vyombo vingine ili wananchi wa Loliondo waweze kupewa kauli ya Serikali katika hili. Mimi ndivyo nilivyokuwa nimemwelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mahali ambapo Mheshimiwa Waziri amenitatanisha na ninataka maelezo. Kwamba katika kueleza juu ya nia ya matumizi ya eneo lile ambalo sasa linatumika kwa uwindaji wa *OBC,* kuna mahali Waziri alisema, kama basi siyo *OBC,* basi eneo lile sasa

litaweza kubadilishwa matumizi, likaingizwa ndani ya *Serengeti National Park*.

Kama nitakuwa nimemwelewa vibaya, basi nitamwomba a-*clarify*, kwa sababu *Serengeti National Park* siyo tu kwamba ina migogoro na Vijiji vya Lolosokwan na Swetisambu katika Wilaya ya Ngongoro kwamba imeingia ndani ya eneo la Vijiji, lakini ukweli pia ni kwamba ukiondoa eneo lile, maana yake wananchi wa Tarafa ya Loliondo na Sale wanabaki na kilometa 265 kwa ajili ya ufugaji, na kwamba hakuna maisha ya wananchi wale bila kilometa 1,500 kutumika kwa ufugaji na wanyapori katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *massage* tano nilizopokea hapa, Mheshimiwa Waziri amewachanganya wananchi zaidi, na ndiyo maana nimelazimika kusimama tena japo hakuacha hata hoja niliyotaka kuuliza, ili aweze kuweka bayana juu ya suala hili. Maana sasa ni moto mwingine juu ya moto, kwamba suala lile la Loliondo halipatiwa ufumbuzi, tena nia ya kumega na kuingizwa kwenye *TANAPA,* imeweka balaa tena katika eneo hili. Kwa hiyo, naomba msimamo wa Serikali katika hili ili Bunge lako na Watanzania waweze kuelewa, maana huko wanazidi kuchanganyikiwa zaidi na mimi mwenyewe nimechanganikiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Uratibu na Bunge)!

**MHE. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwa niaba ya Waziri Mkuu ambaye anatajwa sana; ni kweli kwamba jambo hili kama alivyosema vizuri sana Mheshimiwa Waziri wa Sekta, limeshughulikiwa sana. Mheshimiwa Waziri wa Sekta mwenyewe kama alivyosema amekwenda mara nne, na ni kweli Chama cha Mapinduzi na chenyewe kwa uamuzi na kujali wananchi, kimetuma *delegation*, imekwenda kule na maoni yao yapo sasa hivi katika mchakato wa vikao mbalimbali vya maamuzi ya Chama.

Nataka nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Christopher Ole-Sendaka kwamba, kama alivyosema Waziri Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, uamuzi kutokana na ziara iliyofanywa na viongozi wa Loliondo, wanaotoka katika lile eneo na ziara iliyofanywa na viongozi wa Chama na hasa viongozi wa Loliondo waliofika kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Dodoma, ndiyo maana Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, uamuzi juu ya jambo hili utatangazwa na Waziri Mkuu Mwenyewe. Narudia hapa kusema, kwamba uamuzi wa jambo hili sasa uko mikononi mwa Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwatoe wasiwasi wananchi wa Loliondo na Serengeti na maeneo yote hayo kwamba, inawezekana Waziri amesema jambo hapa, lakini nataka niwatoe wasiwasi kwamba kama walitafakari au walifikiri kwamba kuna uamuzi mwingine wa kumega hili eneo kwenda *TANAPA* bado Serikali haijafikia uamuzi huo. Wajue tu kwamba uamuzi wa mwisho utakaofikiwa ni ule ambao utatolewa na Waziri Mkuu.

Kwa hiyo, nataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Kaika Telele na Waheshimiwa Wabunge wote wa maeneo hayo kwamba, uamuzi wa jambo hili la Loliondo ni kama ule uliotangazwa na Mheshimiwa Waziri anayehusika na kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelekeza, jambo hili limsubiri yeye na atalitolea uamuzi. Hakuna uamuzi mwingine uliotolewa, tunasubiri uamuzi wa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka tunakuomba uvute subira, Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa majibu ya mwisho juu ya Loliondo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felix F. Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati nachangia nilihoji juu ya sera za wananchi kuingia kufanya baadhi ya shughuli ndani ya mapori ya akiba. Nikasisitiza juu ya pori ya Moyowosi ambako kuna mabwawa saba na Kasulu kule ambako kuna mashamba ambyo pia

wananchi walikuwa wanalima zaidi ya miaka 30, sasa wameambiwa ni eneo la hifadhi.

Sasa katika haya mabwawa ya Kibondo, walikuwa wanavua mpaka mwaka 2003, kulikuwa na kijiji pale kinaitwa Ilunde baadaye Serikali ikaamua kukifuta na ile shule ikananii. Sasa nilitaka ufafanuzi wa Serikali; kwa nini isiwawekee wananchi utaratibu kama ule wa zamani? Kwa sababu samaki wapo wengi, hawavuliwi, sana sana tutawaona tu wanauzwa Mitaani kinyemela tu, hatujui wanatokaje kule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini Serikali isiweke utaratibu kama ule wa zamani, Wawe wanaingia kuvua kwa misimu ili na wao weweze kunufaika na pori lile ambalo wanalitunza? Vile vile nilisisitiza kuhusu Afisa Uvuvi ambaye yuko pale hana kazi, amekuwepo pale muda mrefu, anasimamia hao wavuvi; lakini pia kuna Mto Malagarasi ambao unakatiza katikati ya Hifadhi pia wanatakiwa wapite kwenda kuvua, lakini hawaruhusiwi tangu mwaka 2009; kwa nini Serikali isiwawekee utaratibu wananchi hao?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi ni uamuzi ambao nchi inauchukuwa. Ni suala la kupanga na kuchagua. Sheria ya msingi inayosimamia uhifadhi wa mapori ya akiba ni sheria ambayo imeweka bayana kwamba maeneo haya ambayo ni hifadhi ya mapori ya akiba, maeneo haya ambayo ni *National Parks Systems*, maeneo haya hayaruhusu shughuli za kibinadamu ikiwa ni pamoja na uvunaji wa miti, samaki au uvunaji wa shughuli zozote zile. Sheria hii Mheshimiwa Mkosomali na kwa wakati tofauti nilipozungumza naye nilimweleza, anaifahamu na kuna namna mbili tu ambazo tunaweza tukatatua hili jambo.

Moja, ni kama Bunge hili litaleta sheria liibadilishe, kwa sababu kazi ya Serikali ni kusimamia sheria kama ilivyo *to the later* , na sisi tutaendelea kusimamia sheria hii ili tuwahikishie

wananchi na vizazi vijavyo kwamba uhifadhi na *integrity* ya uhifadhi itakuwepo katika miaka yote ijayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Mwijage!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri, *sub vote* 1001. Nimesikiliza kwa makini hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hoja za Waheshimiwa Wabunge na mimi nalijua Taifa hili kuanzia daraja la Mkapa mpaka kufika Karagwe. Mazingira yote yameharibiwa; tumesikia ushuhuda wa wanyama waliouawa.

Hoja yangu na nasimamia mshahara huu kikweli; ningependa kujua, sera ya kuanzisha *operation* inaanza lini? Kwa sababu *operation* ya hii sera siyo suala la kushitukiza, siyo kulenga *target* na kuipiga, wananchi watahusika. Tunamshitukiza nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri anasema ni mtandao, hatuujui. Sasa unasubiri mtandao uujue lini? Tunaanza lini? Ningependa Serikali iseme sasa tunaanza lini? Nchi imekwisha, vilima vyote vya Morogoro vimekwisha, vimebaki vipara; nchi imekwisha, mkaa unalundikwa barabarani, maliasili imekwisha, watu wanaendelea kulia katika nchi yao; ningependa kujua, tusimwogope adui, tutangaze leo adui ajue kwamba sisi tuko tayari kupambana naye. Kwa sababu hata hivyo, yeye anatudhulumu, na sisi tuko tayari kupambana naye.

Mheshimiwa mwenyekiti, bado nimesimamia mshahara wa Mheshimiwa Waziri!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kumjibu kwa heshima kabisa Mheshimiwa Charles Mwijage kwamba Wizara na Serikali inasimamia msimamo ambao kabisa yeye anao. Tunatambua kwamba tatizo hili la uharibifu mkubwa

unaoendelea wa rasilimali, tatizo kubwa la kutoweka kwa misitu ambalo kila mtu anaona kwa macho, tunaliona na tunalitambua.

Suala la *operation* ni suala ambalo ni endelevu na Serikali imeanza na inaendelea na *operations*. Kuna *operations* ambazo zitakuwa zimetangazwa, lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mwijage, *operations* nyingine ni lazima zifanyike wakati adui mhusika hajui. Adui mhusika ana watu ambao anashirikiana nao. Ana watu miongoni mwetu. Ndiyo ile wanayosema, *there is an enemy between.* Kuna adui aliye ndani yate sisi wenyewe, na ni lazima tuhakikishe kwamba tunapofanya hizo *operation,* siyo wakati wote tutamshirikisha kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *operations* ambazo Mheshimiwa Waziri alikwenda kuzifungua baada ya hitimisho katika Mkoa wa Lindi na Mtwara ambazo zilifanikiwa sana, tuliwashutukizia na tuliweza kukamata bunduki zaidi ya 300. Tuliweza kukamata magobore na *pistol*. Haiwezekani mtu anakaa nyumbani kwake na silaha za kivita, akasema hizi ni siliha za kujihami. Hili tatizo ni kubwa, tutaendelea kufanya hivyo na mwisho tunaanzisha Mamlaka inaitwa *Tanzania Wildlife Authority* ili iweze kutatua suala la kimuundo, kimfumo na kiuendeshaji katika Mamlaka ya Wanyamapori.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kaika Telele!

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nianze kwa kusema kwamba sisi Wabunge ambao tunatokana na jamii ya kifugaji, kamwe hatuwezi kuwasaliti ndugu zetu, wala hatuwezi kuwatelekeza katika kutetea maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niseme kwamba suala la Loliondo limejadiliwa sana kwa mapana na marefu. Lakini naomba leo hoja hii ya Loliondo ifikie mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu hili suala limemfikia mara kadhaa, na viongozi wa jamii kutoka Tarafa ya Loliondo kutoka Sale, Tarafa ya Ngorongoro wamekuja Dodoma, wamemwona, amewapa matumaini, naomba matumaini hayo Waziri Mkuu kwa kweli atuhakikishe na atoe kauli ya Serikali mara baada ya kumaliza Bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kama hapana, kwa sababu simwoni ndani ya Bunge, atatoa kwa wakati wake muafaka, lakini itakuwa ni vizuri akatoa kauli ya Serikali kabla ya Bunge hili kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo tarehe 2 Mei, 2013, jambo hili lifike mwisho, tupate ufumbuzi na namwomba Waziri Mkuu kama nilivyosema, lakini naomba niseme hivi, bila kigugumizi, wanachotaka wananchi wa Ngorongoro ni kurudishiwa ardhi yao yote, na ikiwapendeza wataanzisha *WMA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa katika suala la sera lifanyiwe mabadiliko haraka sana ili wananchi wa Ngorongoro na Loliondo waweze kupata matumaini juu ya ardhi yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Uratibu na Bunge)!

**MHE. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri naye Mheshimiwa Kaika S. Telele, ametoa maoni yake ambayo nadhani ni sahihi na amependekeza kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe kauli katika Mkutano huu. Nataka kuhakikisha kwamba nitafikisha salamu hizo na kumhakikishia Mheshimiwa Telele kwamba nitamshawishi Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe kauli katika Mkutano huu kama alivyowaahidi wananchi wa Loliondo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**MHE. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Nazungumza kwa niaba ya Waziri Mkuu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lukuvi anajibu kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu na hiyo ni Serikali kwa ujumla wake. Kwa hiyo, hakuna kitu cha ajabu. Mheshimiwa Peter Msigwa!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza kabisa, nitaomba mwongozo wako kwa sababu Waziri wa Mazingira amelipotosha Bunge. Neno Oevu kwa Kiingereza inaitwa *Wetlands* na neno tengefu, tunapozungumzia kwenye maliasili kuna *game controlled area,* ndiyo nilikuwa nauliza kwa Waziri wa Maliasili. Kwa hiyo, amelipotosha Bunge kwa kusema kitu ambacho siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba mwongozo wako.

Pili, swali langu nimesema, Sheria...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, nenda moja kwa moja kwenye hoja!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nakwenda kwenye hoja, maana yake sijajibiwa, ndiyo maana nasema nang'ang'ania Shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema Sheria ya Wanyamapori Na. 5, ya mwaka 2009, inatangaza kabisa katika kifungu cha 16. Napenda ninukuu. Inasema: "Kifungu cha 16 kinamtaka Waziri wa Wanyamapori kuyatambua maeneo hayo na kuyatangaza upya. Nimesema ile Sheria ya mwaka 1974 ilivyokufa na ikazaliwa hii mpya, inamtaka Waziri atangaze. Kama hayo mapori tengefu, yaani *game controlled area* hayajatangazwa, maana yake mpaka sasa katika nchi hatuna mapori tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, Waziri ana-*operate* vipi wakati hajalitangazia Taifa kwamba

kuna mapori tengefu? Namwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi, anafanyaje kazi wakati hajatangaza hayo mapori tengefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayo ndiyo yalikuwa maswali yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, halafu Mheshimiwa Waziri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingilie kwenye mabishano haya. Ni kweli kwamba Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 katika kifungu cha 16, inasema hayo ambayo Mheshimiwa Msigwa anayasema. Lakini maneno yanayotumika, nitasoma kwa Kiingereza: "*Subject to Section 4 (2) of the Land Act, the Minister may after consultation with relevant Local Authorities and by Order in the Gazette, declare any area of Land in Tanzania to be a Game Controlled Area*."

Sasa Sheria ambayo unairejea iliyofutwa, ilikuwa na kitu kinaitwa *serving provision.* Yale mapori unayoyaita tengefu ambayo ni *game controlled areas,* hayakufutwa, yalirithiwa na sheria hii. Kama ukiangalia pia kifungu cha 122(3) cha sheria hiyo Na. 9 ya mwaka 2009, ambayo ni *serving provisions*, kinayatambua mapori tengefu yote yaliyotangazwa chini ya sheria iliyofutwa, mpaka hapo yatakapofutwa. Kwa sababu hayajafutwa, bado yapo. Huo ndiyo ufafanuzi wa kisheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona kuna waliokuwa wanashangaa, kwa nini Mheshimiwa Msigwa nampa ruhusa tena; kwa mujibu wa Kanuni, Mheshimiwa Msigwa alishatoa nia ya kuondoa Shilingi. Kwa hiyo, baada ya kuwasilikiza wote, tunamrudishia nia yake ndiyo anayoisema na waliosimama kuchangia hoja ya Mheshimiwa Msigwa walikuwa wawili tu, Mheshimiwa *AG* na Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, nikishamaliza hapa, basi tutaingia kuhoji, kama hiyo Shilingi ya Mheshimiwa Msigwa iondoke amala.

Waheshimiwa Wabunge tutahoji baadaye. Mheshimiwa Waziri, kama kuna majibu ya nyongeza, karibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina majibu ya ziada isipokuwa kumwambia Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba, baada ya *Attorney General* kujibu kama alivyojibu, ni kwamba *Game Controlled Areas* hazijafutwa kisheria, bado zipo. Kumekuwa na *succession of laws* lakini zimekuwa bado zipo na *Attorney General* ameeleza vizuri tu. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, bado Shilingi unaing'ang'ania? Ama umeridhika!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya Taifa, ngoja niridhike. *(Makofi/ Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance And Accounts..........Tshs.* 2,031,520,880/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning..............Tshs.* 1,674,809,410/=
Kif. 1004 - *Govern't Communication......Tshs.* 442,861,600/=
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit ...............Tshs.* 595,924,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Procurement Mgt Unit.............Tshs.* 759,308,120/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi katika kifungu kidogo cha 410200 - *Acquisition of Vehicles and Transportation Equipment*, zimetengwa Shilingi milioni 70. Napenda kufahamu hizi fedha ni kwa ajili ya kununua gari la namna gani kwa Shilingi milioni 70?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo fedha Shilingi milioni 70 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa magari ambayo yatanunuliwa katika kifungu kingine.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007- *Legal Unit..............................Tshs.* 323,043,500/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 - *Mgt Information System...........Tshs.* 585,651,600/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza, kwenye kifungu 1008 ile 210100 - *Basic Salaries*, hakuna mshahara mwaka huu, lakini kuna posho pale chini yake za kuwalipa watu. Sasa ni vibarua au ni nini? Je hao watu wamefukuzwa kazi au kilichotokea ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho mishahara yake imekasmiwa katika Idara ya Utawala.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001- *Wildlife............................. Tshs.* 19,163,099,730/=

**MWENYEKITI:** Taratibu Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Cecilia, Mheshimiwa, Kangi, Mheshimiwa Eugen, Mheshimiwa Bura. Haya, Mheshimiwa Cecilia.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuuliza katika kifungu kidogo 410200 - *Acquisition of Vehicles and Transportation Equipment*, imetengwa Sh. 1,110,000,000/=. Naomba kupata ufafanuzi,

ni magari ya namna gani na ya aina gani yananunuliwa kwa hizi Shilingi bilioni moja?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Mawaziri, ngojeni tuwachukue wote kwanza kwa sababu wako wengi katika kifungu hiki. Mheshimia Kangi!

**MHE. ALPHAXARD .K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 410700 - *Feasibility Studies, Project Preparation and Design,* ile Sh. 33,641,600/=, nilitaka kujua kama huu upembuzi yakinifu na hii miradi inahusu ile miradi ambayo niliulizia ya uvunaji wa mamba ambao wanaua watu ndani ya Ziwa Victoria; na nikasema Kata ya Igundu na ya Kisorya, sasa nilitaka kujua hizi fedha: Je, zinahusu pia hiyo miradi ya uvunaji mamba wanaoua watu?

**MWENYEKITI:** Haya, kutoka Tembo mpaka Mamba. Mheshimiwa Bura!

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu kidogo 220500 -*Military Supplies and Services.* Fedha zimetengwa hapa Shilingi milioni 50, lakini tumeambiwa kwamba kuna...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bura, naona hiyo *microphone* yako ina matatizo, husikiki kabisa. Tungeomba uhamie kwenye *microphone* nyingine, tumia hiyo ya jirani yako hapo.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu kidogo 220500 - *Military Supplies and Services.* Zimetengwa Shilingi milioni 50, lakini pia tumeambiwa kwamba kuna silaha ambazo ziko bandarini kwa ajili ya shughuli za kuzuia ujangili, lakini silaha hizo bado hazijatoka mpaka sasa.

Ningeomba kujua kwamba hizi fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kugomboa silaha zile zilizozuiliwa bandarini au ni kwa ajili ya kununua silaha mpya wakati kuna silaha ambazo zimezuiliwa bandarini? Naomba maelezo.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu kidogo 220300 ambacho kinahusiana na *Fuel, Oils and Lubricants.* Kifungu hiki katika kipindi cha fedha cha mwaka 2012, hiki ambacho tunakimalizia kilitengewa Sh. 1,201,700,000/= lakini katika kipindi hiki sasa ambacho tunaingia cha fedha 2012/2013 kimetengewa Sh. 483,350,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka tu ufafanuzi kwamba, kuna upungufu mkubwa ukilinganisha fedha zilizotengwa kipindi kilichopita na cha sasa hivi, kiasi cha Sh. 718,350,000/=. Kwa hiyo, nilikuwa tu nataka ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Haya, Waheshimiwa Mawaziri, maswali yamekamilika. Sasa, tunaomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na swali alilouliza Mheshimwa Lugola, na jibu lake ni kwamba; *yes,* fedha hizo zinahusisha na shughuli za uvunaji wa mamba, kama tulivyofanya sensa ya mamba kwa kipindi kilichopita cha mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali linalofuata ilikuwa ni kifungu 220500 ambacho kiliulizwa na Mheshimiwa Bura, na tofauti kile kiasi cha fedha ambacho anakiuliza Mheshimwa Bura, kinatolewa mahususi kwa ajili ya ununuzi wa silaha.

Swali la mwisho, ilikuwa ni kifungu 220300 na jibu lake ni kwamba, fedha hizo ambazo ziko katika ongezeko, zinatokana na ongezeko lililopo katika Watumishi...

**MWENYEKITI:** Mheshimwa Naibu Waziri, kifungu gani hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 220300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, imepungua. Kumradhi! Imepungua kutokana na upungufu wa idadi ya

Watumishi ambao wanakwenda likizo pamoja na posho zinazohusiana na kazi za ziada.

**MWENYEKITI:** Ile 210700, ameshajibu? Aliyeuliza anasema amelidhika?

Hebu Waheshimiwa Wabunge samahani, taratibu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijapata swali la jibu langu nililouliza.

**MWENYEKITI:** Kilikuwa ni kifungu gani? *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Kilikuwa ni kifungu 410200.

**MWENYEKITI:** 410200 Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko ambalo analiulizia Mheshimiwa Mbunge ni kwa sababu ya magari ya kupambana na haya matukio ya ujangili.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001- *Forestry and Beekeeping….. Tshs.* 15,330,404,720/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika fungu hilo nilikuwa nataka kupata ufahamu tu kwenye kifungu kidogo cha 220900 ambapo kitengo hiki ndiyo kinahusika na ukuzaji wa misitu na nyuki, lakini hakikutengewa mafunzo ya aina yoyote. Sasa tunapohamasisha wananchi wetu kufuga nyuki, sijui wenzetu wamepanga vipi kuweza kuhamasisha hilo!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo hicho kinachohusiana na nyuki, fedha zake zimehamishiwa katika *Tanzania Forest Service (TFS)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001-*Tourism*.............................. *Tshs*. 12,060,764,280/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Sabreena na Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niko kwenye kifungu kidogo 270300 - *Current Grant to Non-Financial Public Units-(Academic Institutions).* Ukiangalia kifungu hiki, kimepungua kwa takribani Shilingi milioni 182, ukilinganisha na mwaka 2012 na ninaelewa kwamba Tanzania tuna tatizo kubwa sana la wanafunzi wanaosoma masomo ya utalii. Sasa nilikuwa naomba kupata maelezo kutoka kwa Waziri au Naibu Waziri, ni kwa nini kumekuwa na punguzo hili hasa ukizingatia kwamba Tanzania kwa sasa hivi tuna mahitaji makubwa sana ya wanafunzi wanaosomea masuala ya Utalii na *especially* suala zima la *hospitality* ambalo tumelikosa sana hapa nchini?

**MHE. JOHN. J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niko kwenye kasma 270500 - *Current Grant to Non-Financial Public Units-(Boards)* na ninaamini kasma hii ndiyo inahusiana na ruzuku kwa ajili ya Bodi muhimu ya Utalii. Kiwango cha fedha kimeporomoka, mwaka wa fedha uliopita kilikuwa Shilingi bilioni 5.6, sasa hivi kimeshuka mpaka Shilingi bilioni 5.4, lakini taarifa za ndani nilizonazo vilevile hata huu mwaka wa fedha uliopita, walipewa kiasi kidogo tu cha Shilingi bilioni 2.9.

Sasa ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, na iwapo ufafanuzi hautaniridhisha nitaomba nafasi ya kuondoa Shilingi. Ningependa uhakika kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kuwa mwaka 2012 *Tanzania Tourist Board* iliahidi kupitia kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni, kwamba ingefanya utaratibu wa kuboresha lile pori la akiba la Pande kwa ajili ya kuwa kivutio cha utalii, naomba hakikisho kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba kushuka huku kwa kiwango cha

fedha kutoka Shilingi bilioni 5.6 kwenda Shilingi bilioni 5.4, hakutaathiri ile mikakati na vikao vilivyopaswa kufanyika kwa ajili ya kuboresha lile pori la akiba la Pande. Ningependa kupata uhakika kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**MHE. SUBREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nipo kwenye kifungu cha 221400, kwenye *Hospitality Supplies and Services.* Ukiangalia mwaka 2012 kilitolewa kiasi cha Sh. 65,920,175/=, lakini mwaka huu tuna Shilingi milioni 100 na kidogo. Ongezeko hili ni kubwa. Nilitaka tu kujua ni kwa nini kiwango hiki kimeongezeka kwa kiwango hicho? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Mawaziri, mmeiona hiyo? 221400, ile ya tatu kutoka juu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, niko kwenye kifungu kidogo 411000. Hapa kuna *Rehabilitation and other Civil Works*, imetoka Shilingi milioni sita kwenda Shilingi milioni 38.6. Ningependa kujua kuna ukarabati gani ambao umefanya ongezeko hili kuwa kubwa kiasi hicho.

**MWENYEKITI:** Waheshimwa Mawaziri, mko tayari? Hiyo ya mwisho, nadhani mmemwelewa eee! Haya.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza na kujibu swali la Mheshimiwa Lyimo. Tofauti ya fedha katika kifungu 270300 imetokana na Bajeti halisi ya mwaka huu, na Serikali imeazimia kwamba tutajitahidi kuhakikisha kwamba kiwango cha fedha ambacho tunakipanga kutokana na mapato kinatolewa. Kwa hiyo, pungufu ya hiyo fedha imetokana tu na majukumu mazima ya changamoto tulizonazo katika Serikali.

Swali la pili ameliuliza Mheshimiwa Mnyika, kifungu 270500, hii inahusu *Tanzania Tourist Board.* Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mnyika kwamba Wizara na Serikali kwa ujumla imefanya mjadala mkubwa sana kuhusu

umuhimu wa *Tanzania Tourist Board* na kuhusu umuhimu wa kazi ambayo wamekasimiwa ya kutangaza utalii wa Tanzania duniani kote na tunaridhika kwamba kiasi hiki cha fedha ambazo kimepangiwa *TTB* ni kidogo na Serikali imeazimia katika michakato ambayo inaendelea sasa hivi kuhakikisha kwamba *TTB* tutawaongezea fedha katika jukumu la kuendelea kutangaza utalii wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyalandu katika hiyo ya kuendelea kutangaza utalii, lipo pori ambalo limeulizwa kwamba je, fedha hiyo pia itahusika?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niongeze, kumradhi kwamba nimesahau lile pori muhimu ambalo Mheshimiwa Mnyika siyo tu kwamba ameongea na mimi kwa wakati tofauti, lakini tunatambua mchango wake kwenye hili pori. Tutaendelea katika mchakato wa kuongezea fedha *TTB,* itahusiana pia na wao kuweza kuliendeleza hilo pori kama ambavyo waliazimia.

Kwa hiyo, ikumbukwe *TTB* wameazimia kwa kushirikiana na Chuo chetu cha Utalii cha Dar es Salaam *campus* ya Bustani kuweza kufanya utalii katika Jiji la Dar es Salaam. Itakuwa ni pamoja na kuwapeleka maeneo ya karibu ikiwa ni pamoja na hili pori ambalo Mheshimiwa Mnyika amelitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ambalo linafuata lilikuwa ni namba 221400 ambalo aliliuliza Mheshimiwa Sabreen na ukarabati huu umepanda kwa sababu ya kuongezeka kwa gharama za vifaa na ujenzi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4002 *Antiquities Unit* ............................ Tshs. 5,729,292,400/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu na Mheshimiwa Betty Machangu. Mheshimiwa Machangu!

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *sub vote* 270800 - *Current Grant on Non Financial Public Unit.* Naomba *clarification* kwamba hizi fedha zina-*include* na fedha ya ku-*redesign* Makumbusho kwa sababu niliona juzi walipiga marufuku kwamba Makumbusho inataka irudie kama ilivyokuwa kwa ajili ya kivutio cha watalii. Je, hizi fedha zipo pia na kwa ajili ya ku-*redesign*? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki cha 270834 cha *National Museum of Tanzania* kinahusu shughuli zote za *National Museum* na ni pamoja na ukarabati wa namna yoyote ambazo hizi fedha zitamudu katika hicho kijiji cha Makumbusho.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka kujua kwenye kifungu kidogo cha 270200 kwamba hizi pesa zimeongezeka kutoka Shilingi milioni 82 kwa mwaka uliopita mpaka Shilingi milioni 100 kwamba hizi *International Organisations* ambazo tunazipa *grants* ni zipi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni *member* wa *organisations* mbalimbali. Kwa mfano, kama *sites,* yaani ile *membership* yetu katika *organisations* mbalimbali, tunalipa *fees* katika uanachama wetu. Yaani uanachama katika shughuli mbalimbali, hii ndiyo *fee* ambayot unalipa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIRADI YA MAENDELEO**

**FUNGU 69**

**Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1002 *Finance and Accounts* ................ Tshs. 162,250,000/=
Kif. 20012 *Wildlife* ....................................... Tshs. 2, 860,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 *Forestry and Beekeeping*............. Tshs 7,207,426,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Limbu na Mheshimiwa Machali. Haya, Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nakwenda kwenye *item number 4628 - Participatory Forestry Management.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba ni Sera ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi ambao wanaishi kandokando ya hifadhi ambazo zimetajwa kuwa ni za mapori, nao wanaendelea kupata haki zao ikiwemo suala la kuweza kubadilisha matumizi ya maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Sasa nitoe mfano mmoja tu kwamba kule kwetu Kasulu Mjini na Vijijini kumekuwa na mgogoro mkubwa sana baina ya Serikali pamoja na wananchi ambao wamekuwa wakilima kwa zaidi ya miaka 30 bila Serikali kuwaingilia. Lakini miaka ya hivi karibuni Serikali ilianza kusema kwamba yale maeneo ni maeneo ya hifadhi. Naomba ufafanuzi kwa kuwa fedha zimetengwa hapa, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuweza kufanya ziara na sisi Wabunge wa maeneo hayo ya Wilaya ya Kasulu ili kwenda kutatua mgogoro ambao umedumu na wananchi hawa wamekuwa wakifukuzwa na

wengine wakipigwa na kufunguliwa kesi na kunyang'anywa raslimali zao kama pikipiki, baiskeli na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi iwapo Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari twende tukafanye ziara hivi karibuni ili kuweza kumaliza tatizo ambalo linawakabili. Kama Mheshimiwa Waziri ataniambia hapana, basi nakusudia kutoa Shilingi. Naomba nitangaze rasmi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, kwanza yaani hata unachokisema hakihusiani kabisa na kifungu hiki. Fungu hili wala halizungumzii ziara. Wewe bora ungejenga hoja tofauti na kumwomba Waziri kuja kwenye ziara kwenye Jimbo lako. Lakini kwa sababu ni mwaliko ambao ni mwaliko mwema wa kujenga mahusiano na kutatua matatizo ya wananchi, basi Mheshimiwa Naibu Waziri nikupe nafasi, lakini swali la fungu lililotajwa ni vitu viwili tofauti kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima tu nimjibu Mheshimiwa Machali kwamba Wizara kwa kupitia *TSF* na kwa kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania tuna azma ya kushirikiana na jamii katika kuhakikisha kwamba misitu na majirani wanaokaa katika misitu kwa maana ya *catchment areas* wote wananufaika na wote wanakuwa sehemu ya uhifadhi. Naomba hapa nikubali kwamba Mheshimiwa Waziri atafanya ziara hiyo kwa wakati muafaka katika Jimbo lako.

**MWENYEKITI:** Haya Bwana. Mheshimiwa Machali, Waziri atakuja! Mheshimiwa Suzana A. J. Lyimo!

**MHE. SUZANA A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye kifungu 4629 na 4641.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzana ni kifungu kimoja tu!

**MHE. SUZANA A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, okay, 4629.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kilio cha Wabunge wote kwamba misitu yetu imekuwa ikikatwa hovyo sana na tumekuwa tukishuhudia mikaa maeneo yote nchini. Lakini jambo linalosikitisha, nimeangalia katika kitabu hiki, hakuna hata Shilingi moja iliyotengwa kutoka fedha za ndani. Sasa naomba kujua au ufafanuzi, kwa mfano, kama fedha hizi za wafadhili zitachelewa na kimsingi fedha zao huwa zinachelewa, ni kwa nini Serikali haija-*commit* hata Shilingi moja kwa ajili ya tatizo kubwa hili la mkaa hapa nchini na ukataji hovyo wa misitu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tumjibu Mheshimiwa Suzana Lyimo kwamba pamoja na kwamba haijaonekana kwamba kuna fedha za maendeleo za ndani, lakini kuna fedha nyingine ambazo Serikali imepanga zinazopitia kwenye kasma ya *OC* ambazo zinatumika katika shughuli za maendeleo.

Hapa ningeweza kumpa mfano kidogo tu katika fedha ambazo zimepangwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania katika shughuli mbalimbali; tumepanga Shilingi bilioni tano na nusu, kazi yake ni kuwezesha ulinzi wa misitu na hifadhi ya nyuki ikiwa ni pamoja na kukidhi vigezo vya ubora wa asali vinavyohitajika katika soko la nje. Tumepanga Shilingi bilioni 6.4 kama pesa ya maendeleo kwa ajili ya kusimamia misitu ya hifadhi ya uzalishaji na mashamba ya miti ya kupandwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye kifungu kidogo *4628 - Participatory Forestry Management.*

**MWENYEKITI:** Dokta Limbu, hicho tayari kimeshaulizwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Tourism* ....Tshs. 1,000,000,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa. Mheshimiwa Peter Serukamba!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote 4001* kifungu kidogo cha 6367, *under tourism,* naomba kuuliza kwa sababu sijaona hapa, ukisoma kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kuna kazi kubwa ya kutangaza utalii imefanyika hasa kule Uingereza kwenye viwanja karibia vitano, Tanzania inatangazwa. Lakini nashangaa hapa sioni pesa kwa ajili ya kazi hiyo. Ama kuna mtu amejitolea kutufanyia huo utangazaji?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna shughuli za utangazaji ambazo zinaendelea, lakini ni kweli vilevile kasma za mashirika mengine yanayojitegemea kama vile *Ngorongoro Conservation Area, Tanzania National Parks (TANAPA)* ambao wanachangia kwa kiasi kikubwa kwa kushirikiana na *TTB,* hesabu zao hazijafika hapa lakini ni shughuli ambazo zinafanywa na Serikali kwa ujumla wake na hizi kazi zinaendelea kufanywa kwa uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, fungu hilo lina kifungu kidogo kimoja tu. Kwa hiyo, hatuwezi kurudia tena kwa watu wawili; na utaratibu uliowekwa na Mheshimiwa Spika ni kwamba fungu moja ukiachia sera haya mafungo mengine, fungu moja halitaulizwa na Wabunge wawili.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4002 - *Antiquities Unit*…………………. Tshs. 418,490,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya na Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Niko kwenye kifungu kidogo cha 5201 - *Integrated Preservation at Kilwa Kisiwani.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna mradi wa ku-*rehabilitate* majengo ya Kilwa Kisiwani ambayo yalikuwa ni kivutio kikubwa kwa Watalii na majengo yale, na kwa kweli yapo kwenye hali mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ni kwa nini Serikali haijatenga fedha hata kidogo za ndani, inategemea fedha za nje wakati sasa hivi yale majengo likiwepo soko la Kilwa Kisiwani, yanaishia mwishoni sasa hivi.

Serikali ina mpango maalum kwa ajili ya kuhakikisha kwamba majengo yale yanakarabatiwa ili yaweze kuwa kivutio kwa watalii kama ilivyokuwa mwanzoni?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna jitihada kubwa zaidi ambayo inahitajika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba eneo hili la Kilwa Kisiwani linakarabatiwa na Serikali inaendelea kushirikiana na Washirika wa Kimataifa kama *UNESCO.* Lakini halikadhalika Serikali imejitahidi na inajitahidi kuongeza utalii wa ndani kwa kuongeza pato linalotokana na utalii unaotokana na maeneo ya kale na tunaamini kwamba ongezeko la mapato litaendelea kutupa nguvu ya kuweza kutumia pesa za ndani katika kuendelea kuboresha na kukarabati Mji huu muhimu wa Kilwa Kisiwani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirejea)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2013/2014 kifungu

kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba ya Mheshimiwa Spika niwapongeze sana Wizara na kiujumla niipongeze Kamati iliyofanya kazi ya kujadili makadirio haya, tuwapongeze na Kambi ya Upinzani katika maeneo yale waliyotoa ushauri ambao una manufaa kwa Taifa letu. Yale ambayo yana manufaa kwa Taifa letu, yatachukuliwa. Lakini yale ambayo kwa namna moja ama nyingine, basi Serikali itapima wenyewe namna ya kuyatekeleza.

Mheshimiwa Waziri, tukuombe sana wewe na Serikali yako na Wizara, basi mjitahidi kupambana zaidi na hizi changamoto zilizopo katika Wizara yenu, kwa kweli ni kazi nzito sana lakini tunawaombe *inshallah* Mwenyezi Mungu awasaidie. Taifa hili linawategemea sana katika kusaidia katika kuboresha hizi rasilimali za Taifa kwa manufaa ya Watanzania.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufikia hapo, sina hoja nyingine hapa mezani, ninaomba sasa niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi katika Ukumbi huu.

*(Saa 1.00 jioni Bunge liliahirishiwa Mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 3 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*